

1 NOVEMBA, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 1 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya
Afrika Mashariki Ziliimbwa**

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama wote tujuavyo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipata msiba, kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi ambaye alifariki siku ya Alhamisi tarehe 13 Oktoba, 2022 nyumbani kwake Zanzibar.

Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, alizikwa siku hiyo hiyo ya Alhamisi, tarehe 13 Oktoba, 2022 Kijiji kwake Bwejuu Zanzibar. Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa hamkuwepo, nilituma salam za pole na rambirambi kwa familia Jimbo la Amani na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi huyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima naomba sasa tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka mwenzetu na kumuomba Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzisha kwa amani.

*(Hapa Wabunge Walisimama kwa muda kumkumbuka
Marehemu Mhe. Mussa Hassan Mussa)*

1 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mahali pema peponi Amina.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumapili, tarehe 2 Oktoba, 2022, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alimteua Mheshimiwa Angellah Jasmin Kairuki kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia nafasi za kuteuliwa na Rais.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 68 ya Katiba inaelekeza kuwa kila Mbunge kabla ya kushiriki katika shughuli za Bunge anatakiwa kuapa kiapo cha uaminifu. Vilevile Kanuni ya 30(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeelekeza kwamba Mbunge kabla ya kuanza kushiriki shughuli za Bunge ataapishwa na Spika kiapo cha uaminifu. Aidha, Kanuni ya 30(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020 inanitaka baada ya kumuapisha Mbunge aliyeteuliwa wakati hakuna Mkutano wa Bunge unaoendelea kutoa taarifa Bunge kwenye kikao cha kwanza cha Mkutano wa Bunge unaofuta.

Hivyo, napenda kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, aliaapa kiapo cha uaminifu siku ya Jumatatu ya Tarehe 3 Oktoba, 2022, katika Ofisi Ndogo ya Bunge Jiji Dar es Salaam. Kwa niaba yenu nampongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki na kumkaribisha tena katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu aliyoaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada minne ya Sheria ifuatayo:

- (i) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022;
- (ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 2 Bill, 2022)*;
- (iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management Amendment Bill, 2022)* na;
- (iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 *(The Written Laws Financial Provisions Amendment Bill, 2022)*.

1 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili tukufu kuwa tayari Miswada hiyo Minne imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Sheria hizo za nchi sasa zinaitwa:

- (i) Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sheria Na. 6 ya Mwaka 2022;
- (ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2, Sheria Na. 7 ya mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act, No. 7 2022*);
- (iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 8 ya Mwaka 2022 (*The Water Resources Management Amendment Act, (No.8) 2022*) na;
- (iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha, Sheria (Na. 9) ya Mwaka 2022 (*The Written Laws Financial Provisions Amendment Act. (No.9) 2022*).

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo taarifa ya Spika. Katibu!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Maelezo ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022.

MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Maelezo ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022.

1 NOVEMBA, 2022

MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, sasa aulize swali lake.

Na. 1

Kumaliza Ujenzi barabara ya Manyinga hadi Madizini- Mvomero

MHE. JONAS V. ZEELAND aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kumaliza barabara ya Manyinga hadi Madizini kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland Mbunge wa Jimbo la Mvomero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 500.00 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa urefu wa kilomita 0.54 ambapo ujenzi huo umekamilika.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* itaendelea na ukamilishaji wa kipande kilichobaki kulingana na upatikanaji wa fedha ili wananchi wa eneo la Madizini na sehemu zingine katika tarafa ya Turiani waweze kufanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa ufanisi.

SPIKA: Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali la moja la nyongeza; kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mvomero, Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kutupa fedha nje ya bajeti ya TARURA.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuiongezea TARURA bajeti ya matengenezo ya barabara, kwa kuwa barabara nyingi zilizoko vijijini ambako kule yanapotoka mazao ya wakulima wetu, barabara zile ni mbovu.

Je, Serikali ni lini itaongeza fedha za bajeti ya TARURA ili barabara hizi ziweze kutengenezwa vizuri na kwa wakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Jimbo la Mvomero kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza ofisi ya Rais – TAMISEMI, tunapokea pongezi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini suala la pili la msingi ni kwamba nimhakikishie tu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu kipenzi, Mama yetu Samia Suluhu Hassan inazingatia jambo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amezungumza hapa la kuongeza bajeti kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nimuondoe shaka tu kwamba fedha bahati nzuri iliyopo ipo na tutaendelea kuifanyia kazi na nyongeza yoyote tutaendelea kuileta kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy John Sabu swali la nyongeza.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga, barabara ya Maswa – Kadoto, kupitia Mnadani kwa kiwango cha lami? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Sabu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba bahati nzuri maeneo aliyoyataja yapo katika mipango yetu na kadri

1 NOVEMBA, 2022

tutakavyoweka fedha maana yake tutayajenga na yatakamilika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph George Kakunda, sasa aulize swali lake.

Na. 2

Hitaji la Shule za Msingi Mpya – Sikonge

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga shule mpya za msingi katika maeneo ya Mbirani, Makibo, Kiyombo na Tutuo – Sikonge?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inakamilisha tathmini ya upembuzi yakinifu wa Shule zote za msingi kupitia mradi wa *Boost* ili kubaini taarifa za eneo shule ilipo, hali ya mazingira shule ilipo, umbali kutoka shule moja hadi nyingine, umbali kati ya shule na makazi ya watu na idadi ya watu (*School Mapping*). Lengo lake likiwa ni kuandaa mpango endelevu wa uboreshaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhuishaji huo, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia mradi wa *Boost* Serikali imetenga Shilingi Bilioni 230 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi katika Halmashauri zote 184 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na pia napongeza majibu mazuri ya Serikali hasa hiyo tathmini ambayo inaenda kufanyika ni tathmini nzuri ya *school mapping*.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili. Swali la kwanza, hivi karibuni kuanzia miaka ya 2017 kumekuwa na ujenzi wa madarasa, mabweni na kadhali na hiyo ni miundombinu ya shule. Je, tuna uhakika gani kama hizi Shilingi Bilioni 230 nazo zitaendeleza tu utaratibu huo wa kujenga madarasa badala ya shule mpya?

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye taarifa ya jana ya sensa, katika Wilaya ya Sikonge, wananchi wameongezeka mara mbili, maana yake ni kwamba hata idadi ya wanafunzi imeongezeka mara mbili.

Je, kwa nini Serikali isiweke kipaumbele ya kujenga shule mpya Nne katika Wilaya ya Sikonge kwenye hayo maeneo ambayo nimeyataja kwa mwaka huu wa fedha? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika tathmini tunayoifanya ya ujenzi wa shule mpya za msingi na katika fedha ambayo imetengwa sehemu ya hiyo fedha itakwenda kujenga shule mpya sehemu nyingine tutakwenda kukarabati maboma ya madarasa ambayo yamekwisha muda wake, na maeneo mengine tutabomoa kabisa na kuanza upya ujenzi katika mabwawa ambayo yamekwisha kabisa. Kwa hiyo, huo ndiyo mpango wa Serikali ambao upo, kwa hiyo nimuondoe hofu kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lake kuhusu shule nne mpya za msingi, nikuhakikishie tu fedha ipo kwa sababu mradi peke yake wa *BOOST* ambao tunautekeleza kwa miaka mitano, thamani yake ni trilion 1.15. Kwa hiyo ni fedha ipo ya kutosha ambayo tutahakikisha changamoto ya elimu msingi tunazimaliza nchini. Ahsante

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 3

Maeneo Yaliyotambuliwa Kuwa na Madini – Iringa

MHE. DKT. RITTA E. KABATI aliuliza: -

Je, ni maeneo gani yametambuliwa kuwa na madini Mkoani Iringa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati (Mbunge wa Viti Maalum) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi yake ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), ilifanya utafiti wa awali na kuanisha madini yanayopatikana katika Mkoa wa Iringa. Miongoni mwa madini yanayopatikana katika Mkoa wa Iringa ni dhahabu katika Kata za Sadani, Ikweha, Malengamakali, Mlolo, Ifunda, Kalenga, Idodi na Pawaga; shaba katika kata za Mahenge, Kiwele, Pawaga, Nyang'oro, Malengamakali na Kihongota; madini viwanda aina ya chokaa katika Kata za Kiwele, Idodi, Inyigo, Ifunda na Kihongota; udongo wa mfinyanzi (*ball clay*) katika Kata za Ifunda na Rungemba; *kaolin* katika Kata za Mbalamaziwa, Nyanyembe, Nyololo na Ifunda; *kyanite* katika Kata ya Mlowa; *bauxite* katika Kata ya Rungemba; chuma katika Kata ya Mawindi; na vito katika Kata za Isimani, Idodi na Kiwele.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa wetu wa Iringa na sisi tuna madini ya kutosha. Mkoa wetu wa Iringa tunao Mgodi wa Nyakavangala uko katika Jimbo la Isimani. Na kwa kuwa taarifa ya jiorojia na utafiti, inaonesha kwamba eneo hilo limeshaonesha. Je, ni hatua gani sasa inayofuata ili wachimbaji wa eneo hilo waweze kuchimba kwa tija na ili Mkoa wetu wa Iringa uweze kupata mapato kutokana na madini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nipongeze sana wanawake waliothubutu kuanza uchimbaji wa madini nchini, na sasa wameanzisha chama cha TAWOMA. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha wanawake wengi zaidi waweze kuchimba madini nchini na ukizingatia sensa inaonesha kwamba wanawake tuko wengi zaidi na Mheshimiwa Waziri alisema tunalipa vizuri?

Nimpongeze Mheshimiwa Rais alifungua uwekezaji mkubwa sana wa mwanamke pale Geita, Sarah Masasi, ili wanawake wengi tuweze kuchimba madini na kuwekeza katika madini nchini. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kama ifuatavyo: -

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali lake la kwanza kwamba kwa kuwa utafiti wa awali umeshafanywa na taasisi zetu kubaini uwepo wa madini ya dhahabu katika eneo la Nyakavangala, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua zinazofuata sasa ni kufanya utafiti wa jiofizikia ambao ndio unaohitajika kwa sasa ili usaidie kutambua mikondo inayoweza kuwa na mashapo ya dhahabu, na kwa njia hiyo wale wachimbaji waweze kuchimba kwa tija. Aidha, GST kwa kushirikiana na STAMICO sasa wamepanga kwenda kuendelea na utafiti katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali lake la pili, ni kwamba Serikali ya Mama Samia kwa kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unaotutaka tuwape wachimbaji wadogo wakiwepo wanawake maeneo ya kuchimba madini imetuagiza sisi tuendeleo kuwa walezi wa sekta ndogo ya wachimbaji wakiwepo wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kutekeleza hilo sisi Wizara ya Madini, kwanza tumeteua mabalozi wa madini ambao Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ni moja wa mabalozi na vinara wa madini hapa nchini, kazi ambayo anaifanya kwa dhati, na mpongeza kwa kuleta swali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi mamia kwa maelfu ya wanawake wanafaidika kupitia mnyonyoro wa sekta hii ya madini. Zaidi ya leseni 20 zimeshatolewa kwa vikundi mbalimbali vya wachimbaji wa madini. Na wanawake hawa wamekuwa wakichangia pia katika kukusanya maduhuli ya Serikali. Kwa mfano kikundi kimojawapo cha TAWOMA mshikamano kilichopo katika eneo la Nyamisiga, Halmashauri ya Msalala kule Kahama wamechangia ujenzi wa zahanati. Hizo ni juhudi kuonesha kwamba Wizara imezingatia suala hili la uchimbaji wa wanawake wadogo, na ninampongeza sana Mheshimiwa kwa kuleta swali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuwaomba wanawake popote walipo Tanzania kwenye madini wajiingize katika biashara hii maana ina tija na Serikali inawatambua na itawa-support.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 4

Ajali zinazosababishwa na Bodaboda

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya ajali zinazosababishwa na bodaboda kwa kutoa *sight mirror*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Fakharia Shomar Khamis Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya usalama barabarani Sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, Kifungu 39 (1) inayotumika Tanzania bara, na sheria ya usafiri barabarani Sura ya 7 ya mwaka 2003, Kifungu cha 22 inayotumika Zanzibar zinatamka kuwa ni kosa kisheria kwa mtu yeyote kuendesha chombo cha moto barabarani ikiwemo gari na pikipiki bila kuwa na vifaa kamili ikiwemo *sight mirrors* kwani chombo hicho kitahesabika kuwa ni kibovu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kuwa, mtu yeyote anayeendesha chombo cha moto zikiwemo pikipiki za biashara (bodaboda) kufuata sheria na kutotoa *sight mirror* kwenye pikipiki. Kitendo cha kutoa *sight mirror* ni kukiuka sheria na mhusika atapaswa kukamatwa na kutozwa faini ya papo kwa papo au kufikishwa mahakamani na chombo chake kuzuiwa hadi akirekebishe.

SPIKA: Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kujua *TANROADS* pamoja na polisi wanashirikiana vipi ili kuweka usalama wa raia barabarani?

Mheshimiwa Spika, la pili, baadhi ya bodaboda, pamoja na wapakia wateja wao wanapopita barabara huwa hawavai *helmet*.

Je, Wizara yako inaangalia vipi sheria wakati askari wa barabarani hawawajibiki na kutenda majukumu yao wakati wanatembea watu bila *helmet*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

1 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, namna tunavyoshirikiana na *TANROADS* kudhibiti usalama barabarani ni pamoja na kuimarisha miundombinu, ambayo ni shughuli ya *TANROADS* kwa pande barabara kuu za mikoa na barabara kuu za kitaifa, lakini kwa upande wa *TAMISEMI* ni *TARURA*, na hawa wote ni wajumbe wa Baraza la Taifa la Usalama Barabara. Na Naibu Waziri, wa Wizara yenye dhamana na uchukuzi ni Makamu Mwenyekiti wakati ni Naibu Waziri Mambo ya Ndani ni Mwenyekiti. Kwa hiyo tuna ushirikiano mkubwa sana kuhakikisha kwamba kwa pamoja inapotokea ajali tunafanya uchunguzi kujua sababu na kama sababu ni za kimiundombinu, *TANROADS* wanahusishwa, kama sababu ni za kisheria basi polisi kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani inachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, bodaboda kutokuvaa *helmet*, hili nalo ni moja ya makosa ambayo vyombo vyetu vya usalama barabarani hususan askari wa usalama barabarani *traffic police* wanawaelimisha hawa vijana wanaoendesha bodaboda mara kwa mara kwa sababu kwa kweli kutovaa kofia ngumu ambazo ndizo zinaitwa *helmet* ni chanzo kikubwa cha vifo ambavyo vijana wetu wanaoendesha bodaboda wanapata. Kwa sababu wanapogongwa au kichwa kikigonga barabara ya lami hupasuka, au kinapogongwa na chombo kingine ama gari na kadhalika. Kwa hivyo, kuepusha madhara mkubwa haya tunawahimiza wazingatie sheria pamoja na kuvaa hii *helmet*.

SPIKA: Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, na kwa changamoto za matumizi ya barabara kwa bodaboda kuongezeka na kuhatarisha Maisha kila siku; sasa Serikali haioni leo kutoa tamko kwamba bodaboda wote wanaopita kwenye taa nyekundu, *no entries* pamoja na kupakia mishikaki wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba Abbas kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni kosa kubwa sana si bodaboda tu hata magari kukatisha wakati taa nyekundu zimewaka, zikawazuia kwenda wao wakapita; kwa sababu wakati taa nyekundu zimekuzuia wewe

za kijana zimeruhusu gari nyingine kupita. Kwa hiyo, unapojaribu kukatisha kwa kweli unajiweka kwenye hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba polisi wetu wa usalama barabarni huchukua hatua, lakini mara nyingine imekuwa changamoto kwa upande wa viongozi wa kisiasa kuwatetea vijana hawa. Kwa hiyo, niombe tushirikiane sote. Elimu tunatoa, sheria huchukuliwa, lakini wote tuwe na utashi wa kisiasa, kwa maana ya mabaraza ya madiwani, ngazi zetu sisi Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ili wote tuzungumze lugha moja kuhusu usalama wa barabarani, hususan hawa vijana wa boda boda nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo sasa aulize swali lake.

Na. 5

Kufanya Utafiti Kuhusu Biashara na Hali ya Uchumi

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kufanya utafiti kuhusu hali ya biashara na uchumi wa wananchi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kupata matokeo ya tafiti zinazolenga kuboresha biashara na uchumi wa wananchi pamoja na kuwaunganisha wananchi na fursa za masoko kupitia maonesho ya mifuko na programu za uwezesaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na hiyo mikakati mingine ni kutoa tuzo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya tafiti bora kwenye masuala ya uchumi na biashara.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza Malapo swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, nataka tu kujua Serikali ilipofanya tafiti

1 NOVEMBA, 2022

imegundua ni kwanini wafanyabiashara wengi hasa wadogo wadogo wanafunga biashara zao hivyo kupelekea hali ya uchumi kudolora hususan Mkoani kwetu Mtwara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka tu kujua mkakati wa Serikali ukoje kuhakikisha unawaunganisha wananchi wa mkoa wa Mtwara na fursa ya masoko katika nchi ya Comoro?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, moja ya mikakati tunayoifanya ni kuhakikisha tunafanya tafiti mbalimbali. Moja kwa kuwashirikisha taasisi za umma lakini pia na wadau wa maendeleo ambao wanafanya tafiti hizo kuhusiana na hali ya uchumi lakini pia na namna ya kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya matokeo ambayo yanaonesha pamoja na kwamba kuna udolora wa wafanyabiashara wadogo lakini ni changamoto za maeneo. Ndiyo maana Serikali imekuja na mpango wa kuwapanga katika maeneo mahususi ili wawe na maeneo ambayo ni mazuri na rafiki kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao mara nyingine wakikaa maeneo ambayo si rafiki kunakuwa na ile changamoto zak ukimbizwa na baadhi ya mgambo na taasisi zingine ambazo wafanyabiashara wadogo wanakuwa wamevamia na kufanya biashara zao katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli tunaendelea kutafuta, moja ya changamoto yao ya mitaji ambayo tunaifanyia kazi ili wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kupata mitaji kwa njia rahisi. Lakini zaidi pia tutaendelea kuwatafutia maeneo ya kufanyia biashara katika Mkoa wa Mtwara kama ulivyosema lakini pia na maeneo mengine nchini, ili wafanyabiashara wadogo kwanza wapate mitaji lakini pili wawe na maeneo mahususi ya kufanya biashara bila kusumbuliwa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita Mbunge wa Kiteto sasa aulize swali lake.

Na. 6

Ujenzi wa Barabara ya Arusha – Simanjiro – Kiteto – Kongwa

MHE. EDWARD K. OLELEKAITA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Arusha – Simanjiro – Kiteto hadi Kongwa kilometa 430 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi (CCM) 2020 – 2025.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mnamo tarehe 27 Juni, 2022 ilitangaza zabuni kwa ajili ya kuonesha nia (*Expression of Interest*) kwa Makampuni ya Ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Arusha – Simanjiro – Kiteto – Njiapanda ya Kongwa yenye urefu wa kilometa 453.42 kwa utaratibu wa EPC + Jumla ya Makampuni kumi na moja (11) yalikiidhi vigezo na tarehe 22 Novemba, Zabuni hizi zitafunguliwa.

SPIKA: Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD K. OLELEKAITA: Mheshimiwa Spika, sana, na niseme wazi kabisa kwamba nashukuru sana majibu ya Serikali ni mazuri sana sana. Pamoja na hayo Mheshimiwa Waziri natarajia kwamba hiyo barabara mtaanza kujenga kutoka Kongwa, Kwenda Kiteto mpaka Arusha. Swali la nyongeza, ni lini hasa kwa mipango yenu, baada ya hii process ya kufungua tenda, ninyi mmepanga lini sasa ujenzi huu uanze, ni Novemba, Desemba, Januari? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kuipongeza Serikali kwa hatua ambazo inaendelea kuzichukua. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kwamba taratibu zimeshaanza, na kama makampuni haya mojawapo litakidhi vigezo, litapewa hiyo zabuni, kwa hiyo taratibu za manunuzi zitaanza ili kuanza ujenzi huo kwa kiwango cha lami. Ahsante

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa barabara ya Mlowo Kamsamba, ina umuhimu mkubwa sana wa kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi pamoja na Momba. Naomba kufahamu sasa, ni lini ujenzi wa kiwango cha lami utaanza katika barabara hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mlowo Kamsamba, imeshafanyiwa usanifu wa kina na Serikali inatafuta fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Sale kuelekea Mto wa Mbu kwa kiwango cha lami, ukizingatia barabara hii ni muhimu kwa shughuli za utalii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Valentine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo hadi Sale ni barabara ambayo tumeanza kujenga kipande cha Waswaswale na kipande kilichobaki tayari usanifu umekamilika na Serikali sasa inatafuta fedha ili kujenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza; barabara ya Makofia – Mlandizi – Manarumango mpaka Vikumburu, ni lini itaweza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa ujenzi na uchukuzi, majibu.

NAAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Makofia – Mlandizi – Mzenga hadi Vikumburu ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango wa lami.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza, Serikali imefikia wapi maandalizi ya ujenzi wa barabara kutoka Lumecha – Kitanda – Malinyi – Kilosa - Kwa Mpepo hadi Ifakara kwa kiwango cha lami? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ambayo inaanzia Lumecha – Malinyi kuja Ifakara, ipo kwenye Mpango kama nilivyojibu kwenye swali la msingi; na jibu lake ni hilo hilo kwamba tayari wazabuni wameshaoneshwa, hiyo barabara, nayo imewekwa kwenye mpango wa EPC+F. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba.

Na. 7

Ujenzi wa Barabara ya Mwandiga Hadi Kagunga

MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MHE. ASSA N. MAKANIKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mwandiga – Chankele – Mwamgongo hadi Kagunga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assa Nelson Mekanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwandiga – Chankele-Mwamgongo hadi Kagunga yenye urefu wa kilometa 65 ni barabara ya

wilaya. TANROADS wanaendelea kuifungua kutoka njia panda ya Chankele hadi Kagunga kilometa 47 na tayari kilometa nane zimeshafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.85 kuendelea kuifungua barabara hii kwa kiwango cha changarawe. Baada ya kuifungua barabara yote, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab Katimba, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali yanayotia faraja. Nina swali moja la nyongeza. Naomba kufahamu na kauli ya Serikali kuhusiana na kukamilika kwa ujenzi wa barabara hii ifikapo mwaka 2025.

SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi tunayoitekeleza sasa hivi na imeeleza wazi kwamba lazima tuifanyie usanifu wa kina. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mekanika ambaye amekuwa akiifuatilia sana hii barabara kwamba tutahakikisha tunaifungua yote na baada ya hapo tutaanza kuifanyia usanifu wa kina baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu wa barabara hii.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kipande cha barabara kinachotoka Uvinza kuelekea Malagarasi ujenzi wake unasuasua sana kwa muda mrefu. Napenda kujua nini tatizo la Serikali kufanya kipande hicho cha barabara kisikamilike?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilikuwa inasuasua, lakini sasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ya Uvinza hadi Malagarasi yenye urefu wa kilometa 51, kasi imeongezeka baada ya

kuondoa changamoto zilizokuwepo. Ni matumaini yetu kwamba Mkandarasi huyu atakamilisha barabara hii ndani ya wakati. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itafanya upanuzi wa barabara ya Moshi – Arusha kuanzia Tengeru – USA – Moshi Mjini – Himo mpaka Holili?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Priscus Tarimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii imetengewa fedha kujenga, kwa maana ya kuikarabati, ikiwa ni pamoja ya kujenga daraja la Mto Karanga. Kwa hiyo, taratibu zinaendelea ili kuanza kujenga hii barabara ikiwa ni kuikarabati sasa kwa kiwango kikubwa kwa mwaka huu wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako, kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo sasa aulize swali lake.

Na. 8

Tatizo la Maji Safi na Salama Mtwara

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kumaliza tatizo la maji safi na salama Wilaya za Newala, Tandahimba na Nanyumbu Mkoani Mtwara?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji 26 ambapo miradi 14 imekamilika na miradi 12 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa mradi wa maji wa miji 28, ambapo Mkoa wa Mtwara miradi inayotekelezwa ni mradi wa maji Makonde na Nanyumbu. Utekelezaji huu unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2024 na utanufaisha

wananchi zaidi ya 500,000 wa Wilaya za Newala, Tandahimba na Nanyumbu.

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES J. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi 2022, idadi ya watu imeongezeka: Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mawanda ya mradi huo ili kuongeza idadi ya watu watakaonufaika na mradi huo?

Mheshimiwa Spika, pili, chanzo cha maji cha Chiwambo na Maratu havitoi maji kwa sasa kutokana na deni kubwa la bili ya TANESCO. Serikali ina mpango gani wa kusimamia jambo hili ili kuwawezesha wananchi hao kupata maji safi na salama?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Hokororo kutokana na kazi kubwa anayoifanya hasa kupigania wananchi wake kwa ajili ya kupata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Wizara ya Maji kutokana na takwimu hii ya ongezeko la watu, tumejipanga kutumia kwanza vyanzo toshelevu kwa maana ya mito na maziwa ili kuhakikisha kwamba tunawafikia watu wengi ili kuendelea kutoa huduma ya maji. Mathalani, huu Mradi wa Nanyumbu, tunatoa maji ya Mto Ruvuma ili kuhakikisha wananchi wengi wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ipo mamlaka ambayo ina deni na TANESCO. Namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge tukae ili kuona namna gani tunaweza kuisaidia mamlaka hiyo kwa haraka ili huduma iendelee kwa ajili ya upatikanaji wa maji.

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuitembelea Kata ya Kihurio na Kata ya Bendera na kujaribu kutatua matatizo. Mheshimiwa Waziri, nikwambie kwamba umetatua matatizo ya Kata ya Bendera, lakini matatizo ya maji kwa Kata ya Kihurio yamezidi kuwa mabaya zaidi na sasa wananchi wengine wamekuwa wakidanganywa na kupewa maneno ya kuichafua Serikali na kumchafua Mbunge:-

Je, Waziri utaniambia nini kuhusu maji Kata ya Kihurio ninapotoka mimi? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Kwa kweli nimefika katika jimbo lake na tumekwenda katika kata inaitwa Bendera, hapakuwa na mradi wa maji kabisa na tulitoa maelekezo na sasa watu wanapata maji pale Bendera. Huu ni utatuzi na Mheshimiwa Mama Anne Malecela, wewe ni mkombozi hasa katika eneo lile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Kihurio, nitoe maelekezo ya haraka kwa Meneja wa RUWASA wa mkoa na timu yake, hivi tunavyozungumza kesho wawe Kihurio, nami Mheshimiwa Mbunge naomba tukae tuzungumze kwa pamoja ili tuoneshe msukumo wa pamoja kukamilisha mradi huu na wananchi waweze kupata maji.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa namna anavyopambana na changamoto inayoendelea Nkasi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayotukumba kama Taifa ni kwa sababu ya miradi tunayoitumia ni mabwawa ambayo yanategemea kupata mvua. Inapotokea mabadiliko ya hali hewa, ndiyo changamoto inaonekana kama hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hatuna shida na vyanzo vya uhakika...

SPIKA: Mheshimiwa Aida, swali.

MHE. AIDA J. KHENANI: Je, Serikali ni lini mtaanza kutumia Maziwa makuu badala ya hivi ilivyo sasa inapotokea mabadiliko tunapata changamoto? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli sisi Wizara yetu ya Maji Mheshimiwa Rais alishatupatia maelekezo mahususi kwamba yeye ni mama, hataki kusikia wamama wa nchi hii wakiteseka juu ya adha ya maji. Wizara ya Maji itumie rasilimali toshelevu na yeye yupo tayari kutoa fedha kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata huduma ya maji safi

na salama. Kwa hiyo, ndiyo uwelekeo wa Serikali hii ya Mheshimiwa Rais Samia Hassan kutumia rasilimali toshelevu hususan maziwa na mito mikubwa ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Rukwa, Ziwa Tanganyika ndiyo mkombozi kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya maji. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni finyu sana, pongezi na shukrani zisiwepo kama sehemu ya swali. Mheshimiwa Hamis Tabasam.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sengerema kuna mradi wa maji ambao unasubiri kuwekwa kwenye tangazo kwa ajili ya *tender*. Hili jambo limechukuwa muda mrefu sana. Sijui Waziri anasemaje mradi wa Kata ya Mabiru, katika Kata ya Igalula? Ni mradi wa siku nyingi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, miradi ya maji pamoja na ujenzi wake unakuwa na taratibu zake, hasa katika eneo la manunuzi. Nataka nimhakikishie, tunakamilisha hizi taratibu, lakini huu ni mradi mkubwa na nimhakikishie, saina yake nitaishuhudia mimi mwenyewe pale Sengerema. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 9

Kutekeleza Miradi ya Maji – Msalala

MHE. IDDI K. IDDI aliuliza:-

Je, ni lini Miradi ya maji Halmashauri ya Msalala itaanza kutekelezwa baada ya Serikali kutenga Shilingi bilioni 4.8 kwa ajili ya miradi hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Msalala. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya

miradi mitano ilikamilika. Katika mwaka 2022/2023, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi 12 ambapo miradi miwili imekamilika na miradi 10 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa mradi wa maji wa Mhangu – Ilogi awamu ya kwanza umekamilika na tayari unatoa huduma katika Kijiji cha Ilogi. Utekelezaji wa awamu ya pili unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2022. Mradi huu ukikamilika utakuwa na bomba lenye urefu wa kilomita 37.5, matenki manne yenye jumla ya ujazo wa lita 440,000 na vituo 32 na kunufaisha wananchi wapatao 24,436.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa sababu umetuzuia kutoa pongezi, mimi nimpe pole Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa unayoifanya lakini pia watendaji wake wanamwangusha huko chini, mfano ni mradi wa Izuga.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, wewe unavyofikiri unajenga picha gani? Uliza maswali ya nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza: Mchakato wa ununuzi wa mabomba ambao ulikuwa unasimamiwa na Wizara na baadaye kurudishwa mkoani, sasa ni lini Serikali itaharakisha mchakato huo wa manunuzi ili wakazi wa Busangi waweze kutumia maji katika eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Mkandarasi anayejenga mradi unaotoka Mangu – Ilogi bado ameendelea kuchelewesha malipo ya wafanyakazi: Ni lini Serikali itamhimiza mkandarasi huyo ili aweze kuwalipa watumishi wake fedha hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji imeangalia namna ya kutatua tatizo la maji hasa maeneo ya vijijini. Tumeanzisha Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na Bunge lako Tukufu tunalishukuru. Tunapoanzisha taasisi yoyote tunakuwa na mikakati. Tumeweka kwa ajili ya manunuzi wizarani, sasa yameshuka mikoani. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara yetu itaendelea kufanya marekebisho ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maji inafanyika kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, malipo ambayo mkandarasi amekuwa akichelewesha kulipa watumishi wanaofanya kazi, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa baadaye saa 7.00 Bunge litakuwa limeasitishwa,

1 NOVEMBA, 2022

tukutane ili tuzungumze na Mkandarasi moja kwa moja kwa ajili ya malipo ya watumishi wake. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 6/6/2022 Serikali yetu iliingia mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma kuja Mji wa Mangaka, miezi minne imefika. Naomba kupata kauli ya Serikali, ni lini mkandarasi atakuwa *site* ili kutekeleza mradi huo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kweli eneo la Nanyumbu ni eneo ambalo limekuwa na changamoto sana ya maji. Tumesaini mradi huu tarehe 6/6/2022 kama alivyoeleza, kwa sasa tuna-*process advance payment* kwa Mkandarasi ili kuhakikisha kwamba anakwenda kutekeleza mradi kwa haraka na wananchi wake waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilikubali kutoa Shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa tenki la kuchujia maji: Je, ni lini pesa hiyo itatolewa ili ujenzi huo uanze?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tulitoa ahadi na ahadi ni deni. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge ndani ya mwezi huu tutaoa pesa kwa sababu tumeshapokea pesa za Mfuko wa Maji na tutawapa kipaumbele katika Jimbo lake.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, mwishoni hapo umesemaje? Umezima *mic* mapema ili *Hansard* zishike maneno yako.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nasema kupitia Mfuko wa Maji, Wizara yetu ya Maji inapookea fedha kila mwezi. Tumeshapokea Shilingi bilioni 14, tutampa kipaumbele kwenye pesa hii Shilingi milioni 200 ili kuhakikisha kwamba ujenzi unaanza mara moja.

1 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 10

Kuwezesha TTCL Kuunganisha Wateja Wengi Kwenye Mkongo

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuiwezesha TTCL kuunganisha Wateja wengi kwenye Mkongo wa Taifa kwa punguza gharama za kuunganisha?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2021, Wizara iliingia mkataba wa ushirikiano na TANESCO kwa ajili ya matumizi ya pamoja ya miundombinu inayojengwa. Kupitia mkataba huo, miundombinu inayojenjwa kwenye nguzo za TANESCO nchi nzima zinazojumuisha nyaya za mawasiliano zitatumiwa kwa pamoja. Hivyo, kupitia ushirikiano huo, utawezesha TTCL kuunganisha wateja maeneo ya biashara na nyumbani (*fiber to X*) kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa gharama nafuu kwa kuwa gharama za uwekezaji zitapungua. Aidha, Serikali inaongeza uwezo wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano kutoka kiwango cha 200G hadi 800G. Kuongezeka kwa kiwango hiki kitasaidia kupunguza gharama, hali itakayopelekea kuwaunganisha wateja wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine wa Serikali ni kuondoa Wizarani shughuli zote za mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kupeleka TTCL. Suala hili litawezesha TTCL kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya kibiashara kwa haraka zaidi inayojumuisha masuala ya kuwaunganisha wateja kwenye mkongo huo. Aidha, Serikali inaongeza kiwango cha *internet band width* kinachotumiwa na taasisi 312 za Serikali, taasisi za utafiti na elimu ya juu kutoka 2.1G kwenda 20G. Hii itapunguza gharama za *internet* kwa taasisi hizo pamoja na nyingine zitakazounganishwa.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini niseme, tumejua kwamba uwekezaji

kwenye *TTCL* unaweza ukageuka kuwa ni mkakati mzuri wa kuongeza mapato ya Serikali. Tatizo la kuunganisha watu linatokana tu na gharama hizo, njia mojawapo ya kupunguza gharama hizo ni kuiwezesha *TTCL* kupata mtaji au kupata mkopo kwa kupata dhamana au kwa kutumia dhamana ya Serikali ili iweze kuwaunganisha watu na kuwachaji polepole, kidogokidogo kwa miaka miwili mitatu, hizo gharama zitakuwa ndogo na watu wataomba kujiunga kwenye mkongo huu ambao ni cha msingi sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba siku za karibuni tumesikia kwamba *TCRA* inataka kugawa masafa ya *spectrum* za *5G* na tunajua kwamba nchi hii zama hizi ni zama za *internet of things* na ni *Artificial Intelligence* tunaingia na inahitajika sana *5G*...

SPIKA: Mheshimiwa Kimeji, swali.

MHE.DKT.CHERLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, naomba niulize Serikali, je, imejipanga namna gani kuiwezesha *TTCL* kupata masafa ya kutosha ya *5G* katika ugawaji wa *spectrum* hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

WAZIRI WA HABARI MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dkt. Charles Stephen Kimeji, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anauliza Serikali kama iko tayari kuliwezesha Shirika la Mawasiliano (*TTCL*) kupata mtaji. Majibu ni kwamba pamoja na kwamba tumeendelea kuwekeza hata Bajeti hii iliyopita hapa Serikali imetenga zaidi ya bilioni 150 kwa ajili ya kujenga mkongo. Huu mkongo tunaukabidhi sasa kwa *TTCL* ili waweze kuuendesha kibiashara ikiwemo kutafuta fedha kwenye vyombo vya fedha kwa ajili ya kujenga, kuimarisha na kuwahudumia wateja wao. Uamuzi huu utaboresha huduma na kuipa mtaji *TTCL*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kama tuko tayari kutoa upendeleo maalum kwenye umiliki wa *spectrum*. Ni kweli kwamba *internet of things* ndio dunia inakokwenda na ni kweli kwamba *5G* itakwenda kubadilisha matumizi hayo, lakini kama Serikali mauzo ya hizi *spectrum* tunayauza kwa uwazi na tunataka kila mmoja akashiriki na hatuna mpango wa kumpendelea mtu. Hivi juzi tumefanya mnada, tukapata zaidi dola milioni 187 kwa sababu mnada ulitenda haki, kila mmoja aliingia sokoni, akashindana akapata ambacho alikuwa anastahili kupata.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunashukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

1 NOVEMBA, 2022

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 11

Ujenzi wa Chuo cha Veta Kalambo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Wilayani Kalambo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo, kiasi hiki pia kitatumika katika ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, Kalambo ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa Vyuo vya Ufundi Stadi katika mwaka huu wa fedha. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kutenga na kuanza kujenga vyuo vya ufundi ni jambo jema, lakini ipo haja ya kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinaanza kufanya kazi. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba vyuo vinapomalizika kujengwa na vifaa vya kufundishia vijana vinakuwa vinapatikana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu wananchi wa Kalambo wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu ujenzi wa chuo, je, ujenzi huu utaanza lini?

1 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikamilisha au tunakamilisha ujenzi wa vyuo 25 katika wilaya 25 pamoja na vile vya mikoa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweza kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa pamoja na samani ili vyuo hivi viweze kuanza kufanya kazi mapema iwezekanavyo. Tunatarajia kama mambo yote yatakwenda sawasawa kunako Januari vyuo vile ambavyo vitakuwa vimekamilika au tunavyokamilisha hivi sasa vitaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, kwa upande wa kule Kalambo, tayari Serikali tupo katika mchakato wa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chuo hicho. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi, ndani ya *quarter* hii ya pili tutahakikisha tunapata fedha hizi ili ujenzi wa Kalambo uweze kuanza mara moja. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mbunge wa Kwahani, sasa aulize swali lake.

Na. 12

Ahadi ya Ununuzi wa Meli za Uvuvi

MHE. YAHYA ABDULWAKIL AHMED aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ununuzi wa meli nane za uvuvi itatekelezwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI aljibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Abdulwakil Ahmed, Mbunge wa Kwahani, kama ifuatavyo:-

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali, naomba nifanye maboresho madogo sana katika aya inayosema katika mwaka wa fedha 2023/2024, badala yake isomeke katika mwaka wa fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, baada ya maboresho hayo, naomba niendeleo sasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea na hatua mbalimbali za ununuzi wa meli nane (8) za Uvuvi katika Bahari Kuu kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo Serikali itanunua meli nane kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) chini ya Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo-IFAD kwa awamu mbili ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, meli nne na vifaa vyake zitanunuliwa. Meli hizo zitagawanywa Tanzania Bara meli na Zanzibar meli.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba baina ya Serikali na IFAD ununuzi wa meli hizo unatakiwa kukamilika baada ya kufanyika kwa tathmini ya athari za kimazingira na kijamii pamoja upembuzi wa kina wa uendeshaji wa meli za uvuvi. Hata hivyo, taratibu za kufanya Upembuzi huu yakinifu zinaendelea. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, swali la nyongeza.

MHE. YAHYA ABDULWAKIL AHMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na ya kutia moyo katika ununuzi wa meli hii, naipongeza Serikali kidogo, nina swali moja la nyongeza.

Kwa vile ununuzi wa meli hizi utashirikisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, watafaidika wa meli mbili na mbili itafaidika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo Tanzania Bara, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshirikishwa katika hatua hizi za awali za manunuzi haya? Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Naomba arudie swali.

SPIKA: Mheshimiwa Abdulwakil hujasikika, rejea swali lako maelezo ya mwanzo yote ameyasikia, rejea swali lako.

MHE. YAHYA ABDULWAKIL AHMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafaidika na ununuzi wa meli hizi mbili, je, ushirikishwaji upi uliofanywa kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili suala hili likae sawa kwa pande zote mbili? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar upo wa kiwango kikubwa kabisa na jambo hili linaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais upande wa Zanzibar na Wizara zetu pia vilevile ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Uchumi wa Bluu lakini na Mashirika yetu vilevile ya TAFCO na ZAFCO yote yanafanya kazi hii kwa pamoja. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Abdulwakil kwamba Serikali inashirikishwa ipasavyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

MHE. SALMA RASHID KIKWETE: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naipongeza Serikali kwa mpango kabambe wa ununuzi wa hizo meli nane na wataanzia na meli nne. Je, Serikali ina mpango gani kwa mikoa yetu miwili Mikoa ya Mtwara na Lindi juu ya upatikanaji wa meli hizi angalau moja ukizingatia kwamba kule kuna samaki wengi. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba meli hizi kwanza zitamilikiwa na Shirika letu la TAFCO kwa ubia na mashirika binafsi na kwa upande wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na kwingine kote ambako shughuli za uvuvi zinafanyika, Serikali imekuja na mpango madhubuti wa kukopesha wavuvi ambapo boti zaidi ya 150 zitakopesha nchi nzima katika maeneo ambayo shughuli za uvuvi zinafanyika na tayari maelekezo na maombi mbalimbali tumekwishayapokea ili harakati na utaratibu wa kuweza kuwapata wenye sifa za kukopa mikopo hii zifanyike na hatimaye waweze kupata mikopo isiyokuwa na riba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ussi Salumu Pondeza Mbunge wa Chumbuni, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zahor Mohamed Haji.

Na. 13

Hitaji la Mahakama ya Rufaa Zanzibar

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA
aliuliza:-

Je, ni kwa nini kusiwe na Mahakama ya Rufaa Tanzania Kanda ya Zanzibar badala ya kesi kusikilizwa kwa mwaka mara moja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Rufaa Kanda ya Zanzibar ipo kwa sasa na inaendesha shughuli zake kupitia Masijala ndogo iliyopo Jengo la Mahakama Kuu ya Zanzibar. Hata hivyo, Serikali inaona umuhimu wa kuwa na jengo la Mahakama ya Rufani Zanzibar na inaendelea kulifanyia kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

MHE. ZAHOR MOHAMED HAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba niongeze swali moja la ziada.

Wanasema *justice delayed is a justice denied*, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, Serikali iko tayari sasa kuongeza uharaka wa jambo hili kwa sababu wananchi wamekuwa wakipata matatizo kwa muda mrefu? Nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, sikuelewa anataka nini?

SPIKA: Anataka kujua kama Serikali inaweza kuongeza kasi ya utekelezaji wa hicho ulichokisema

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu pale Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli uharaka upo na kwa sababu ni sehemu ya mchakato wa kupatikana kwa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo hayo, naomba Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi tu na muda wa kutosha

na ataona kinachoendelea kwa sababu kimsingi Mahakama ya Tanzania iko kwenye mabadiliko makubwa sana katika uwekezaji wake, kwenye majengo ya kutolea huduma. Kwa hiyo hata hili ndio maana tumelitolea maelezo kwamba tunalifanyia kazi na kazi itakwenda kwa kasi sana. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 14

Hitaji la Ofisi ya Mamlaka ya Mapato - Halmashauri ya Kibondo

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI aliuliza:-

Je, ni lini Ofisi ya *TRA* itajengwa katika Halmashauri ya Kibondo ili kuzuia biashara holela katika masoko ya ujirani mwema kati ya Tanzania na Burundi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, *TRA* ilifanya utafiti katika maeneo yote nchini yenye uhitaji wa ofisi za kudumu za usimamizi wa kodi ikiwemo Halmashauri ya Kibondo na kubaini kuwa gharama za usimamizi wa kodi katika Wilaya ya Kibondo zitakuwa kubwa ikilinganishwa na kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa. Kwa muktadha huo, *TRA* itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi na ukusanyaji wa kodi katika wilaya hiyo ili mara tu itakapokidhi vigezo, *TRA* itafungua ofisi za kudumu. Aidha, *TRA* itaendelea kuimarisha mfumo wa sasa wa kuhudumia walipakodi wa Wilaya ya Kibondo ili kuwawezesha kulipa kodi bila usumbufu wowote. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, swali la nyongeza.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, halmashauri hii makusanyo yake ya mwaka 2021 ilikuwa bilioni 5.3 kwa mwaka na Jimbo hili la Muhambwe liko mpakani ambapo tuna biashara za ujirani mwema kwenye Masoko ya

Mkarazi na Kumshwabure. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kujenga TRA ya kudumu lakini pia na kujenda ushuru wa pamoja mpakani ili kudhibiti biashara holela za mpakani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wananchi wa Muhambwe wanafuata huduma za leseni Mkoani Kigoma ambapo ni kilomita 240 kutoka Jimbo la Muhambwe. Je, ni lini Serikali itaanzisha huduma za leseni katika Jimbo la Muhambwe ili kuwaondolea adha wananchi hawa wa Muhambwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, Serikali imelichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba ikimpendeza Mheshimiwa Mbunge niambatane naye kwenda kuona hali halisi ya Wilaya ya Kibondo, tuone namna gani tunaweza tukatatua usumbufu huu ambao wanapata wananchi wetu wa Kibondo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 15

Vifo kwa Akinamama Wanaojifungua kwa Njia ya Upasuaji

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA aliuliza:-

Je, nini chanzo cha vifo kwa akinamama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji siku chache baada ya upasuaji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa vifo vitokanavyo na uzazi uliofanywa na Wizara ya Afya kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 umeonesha kuwa vifo ambavyo vilisababishwa na matatizo ya dawa za ganzi (nusu kaputi) na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni ni 58 yaani 3.3% mwaka 2018; vifo 80 yaani 4.8% mwaka 2019; vifo 65 yaani 4.0% mwaka 2020; na vifo 65 yaani 4.1% mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu za vifo hivi ni nne ambazo ni ajali ya dawa za ganzi/nusu kaputi, kupoteza damu wakati au baada ya upasuaji, tatizo la damu kuganda na maambukizi ya bakteria baada ya upasuaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma inatekeleza mkakati wa kuwajengea uwezo watumishi wa vituo vya huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za Taifa katika eneo la utoaji ganzi (nusu kaputi) na upasuaji kwa usalama kwa kuzingatia miongozo ya Wizara ya Afya. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante, namshukuru Naibu Waziri wa Afya kwa majibu yake.

Kwa kuwa, umesema kwamba Wizara imekwishafanya ufuatiliaji wa hivyo vifo na sababu zake. Moja ya sababu ni kutokana na matatizo ya dawa za ganzi (nusu kaputi).

Je, kuna watumishi wa kutosha wa kutoa dawa za nusu kaputi katika vituo vyetu vya afya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa mwaka 2021 ni asilimia 4.1 ya akina mama walipoteza maisha baada tu ya kujifungua kwa oparesheni. Je, kuna utafiti wowote ambao Wizara imeufanya ili kubaini sasa ni dawa gani ambazo zinasababisha akina mama wanapoteza maisha? (Makofi)

SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, moja, anauliza kama tuna uhakika wa kuwa na wataalam wa kutoa dawa ya nusu kaputi kwenye nchi. Juzi mlimsikia Mheshimiwa Waziri wa Afya akieleza kuhusu mkakati wa Rais wetu Samia

Suluhu Hassan, ametoa Shilingi Bilioni Nane kwa ajili ya kusomesha wataalam 524 kwa mwaka huu. Mojawapo wa eneo lililoangaliwa ni eneo hilo ambalo kwa kweli kuanzia kwenye hospitali zetu za Wilaya kushuka chini kumekuwapo na wataalam wachache lakini kwa wanaomaliza chuo mwaka huu tutaenda kupunguza hilo tatizo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili baada ya uchunguzi wetu kwamba imegundulika nini na tunatakiwa kufanya nini kwenye eneo hilo la kupunguza vifo vya akina mama. Moja, ndiyo maana unaona kuna eneo hili la kusomesha, imefanyika kazi kubwa sana, lakini baada ya Serikali yetu kutoa zile fedha za tozo, vituo vya afya 238 vimejengwa kwa mwaka huu tu peke yake. Pia mwaka huu *ambulance* 663 zinaenda kununuliwa, nazo mnajua zitakavyokwenda kuweza kupunguza kwenye eneo hilo suala la vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, labda nimalize kwa kumjibu namna hiyo.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, sasa aulize swali lake.

Na. 16

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mfumo wa Stakabadhi Ghalani hautekelezwi kikamilifu kiasi cha kuwawezesha Wakulima kupata fedha wanapohitaji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unawezesha wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya ushindani, wanunuzi kupata mzigo wenye ubora pamoja na Halmashauri kupata takwimu halisi za mauzo na mapato. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba zao la kahawa, ufuta na korosho ni baadhi ya mazao ambayo huuzwa kupitia mfumo huo. Mfumo huo, umekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo baadhi ya wanunuzi kuchelewesha malipo kwa wakulima.

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo Serikali itaimarisha usimamizi wa mwongozo unaoainisha muda maalumu wa kuwalipa wakulima kwa kuchukua hatua za kisheria kwa wanaokiuka taratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali moja la nyongeza.

Kama Serikali inaamini kuwa Ushirika ndiyo njia bora ya kufikisha huduma za kilimo kwa wakulima wadogo wadogo, ikiwemo huduma za Stakabadhi za Ghala na pembejeo hasa mbolea. Je, kwa nini Serikali katika msimu huu haikuona haja ya kutumia Vyama vya Ushirika ili kufikisha mbolea za ruzuku kwa wakulima kwa njia ambayo yenye tija zaidi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mhagama, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, siyo kwamba tumeviacha vyama vya ushirika, sasa hivi Bodi ya Mazao Mchanganyiko ndiyo inachukuwa mbolea kwa wingi na kukabidhi Vyama vya Ushirika. Sasa hivi tumeanza utaratibu wa kutambua maghala ya Vyama vya Ushirika na Chama cha Ushirika cha Tumbaku cha Mkoa wa Ruvuma kimepewa jukumu la kuanza kupeleka maeneo ambayo sekta binafsi imeshindwa kuyapeleka.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufanya hivyo, Mkoa wa Rukwa tutashirikiana na Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Rukwa kwa ajili ya wakulima wa mahindi, Kanda ya Ziwa tunashirikiana na Vyama vya Ushirika vya zao la pamba kwa ajili ya kuongeza usambazaji wa mbolea ya ruzuku.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 17

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kibaha

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua migogoro ya ardhi kati ya Wananchi na Wawekezaji wenye mashamba makubwa Kibaha Vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 17 la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua jitihada za kutatua migogoro ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji katika maeneo mbalimbali hususan katika Jimbo la Kibaha Vijijini. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kufanya ukaguzi wa ardhi iliyomikishwa kwa wawekezaji ili kubaini iwapo masharti ya umiliki yanazingatiwa.

Pili, kuchukua hatua za ubatilisho kwa wawekezaji waliobainika kukiuka masharti ya uwezekaji; na Tatu, kupanga upya ardhi iliyobatiliwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kulingana na mahitaji halisi ya sasa hususan hazina ya ardhi, huduma za kijamii na makazi. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii na wawekezaji kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na miongozo ya sekta ya ardhi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

SPIKA: Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza niikumbushe Serikali kwamba, kuna eneo la Soga kwenye shamba la Mohamed *Enterprise* tayari kulishakuwa na maelekezo ya ekari 500 kurudi Serikalini. Kwa kuwa, kuna changamoto mbalimbali zinazoendelea kusababisha kutokutekelezwa kwa agizo hilo.

Je, Waziri atakuwa yupo tayari kuambatana nami mara baada ya Bunge kwenda kusaidia kuondoa hizo changamoto zinazosababisha utekelezaji wa agizo hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, pale Kata ya Kikongo kuna mwekezaji anaitwa *Trans-continental* na shamba moja la UFC ambalo lipo mikononi mwa Serikali, kuna wananchi ambao wapo pale muda mrefu, wana miaka mingi, karibu 15 mpaka 20, na wawekezaji hao hawajaendelea.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuwaruhusu wawekezaji hao kuendelea na shughuli zao? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusiana na suala la Soga kwenye shamba la *Mohamed Enterprise* naafikiana nawe Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kutatua kero hizi maana tunaambiwa yanayoendelea huko siyo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusiana na jambo la *trans-continental* kule Kikongo na Waya mifugo, Mheshimiwa Mbunge nataka nikuhakikishie utayari wa Serikali, kwenda kushirikiana nawe kutatua kero hizi. Pili, katika Shamba la Waya, tutashirikiana na Wizara ya Mifugo kuhakikisha kwamba hatua zinazostahiki kufuatwa ili kukabidhiwa shamba hilo kama ambavyo Serikali iliamua nazo pia zinafuatwa. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 18

Kuanza kwa Umeme wa Upepo na Jua

MHE. ABEID R. IGHONDO aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa kufua umeme wa upepo na jua wa MW 100 utaanza rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwekezaji aitwaye Upepo Energy alifanikiwa kushinda zabuni ya kuendeleza miradi miwili ambapo *Megawatt* 100 za umeme zitazalishwa kwa nguvu ya upepo na *Megawatt* 45.08 zitazalishwa kwa nguvu ya jua.

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa sasa majadiliano baina ya TANESCO na Mwekezaji kuhusu bei ya kuuziana umeme (PPA) yamekamilika. Majadiliano kuhusu mkataba wa utekelezaji (*Implementation Agreement-IA*) yanaendelea. Ipo changamoto ya mwekezaji kuhitaji "*Government Guarantee*" kinyume na Sera ya Serikali na masharti ya zabuni kama ilivyotangazwa. Iwapo mwekezaji atakubali kutekeleza mradi huu bila masharti mapya aliyoweka, mradi huu utaanza kutekelezwa mwezi Januari, 2023.

SPIKA: Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia fursa. Pamoja na majibu haya ya Serikali ningeomba kujua, kwa kuwa mradi huu ni muhimu sana katika nchi yetu, pia umechukuwa muda mrefu sana bila kukamilika. Je, Serikali sasa ina mkakati gani mahsusi na wa ziada wa kuhakikisha mradi huu unaanza uzalishaji mara moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema Mkandarasi tayari amepatikana kwa ajili ya majadiliano lakini tumepata changamoto ndogo ya yeye kuhitaji vitu ambavyo havikuwemo kwenye masharti ya tenda ya zabuni. Tumeshafikia mwisho na msimamo wa Serikali ni kwamba hakutakuwepo na *Government Guarantee* kwenye mradi huu, bali akubaliane tufanye vile tulivyokubaliana tangu mwanzo.

Mheshimiwa Spika, akikubali Januari tutaanza kufanya kazi hii na asipokubali, Serikali sasa ishaamua kuendelea mbele na Zabuni hii mpya ili tuweze kuhakikisha tunampata Mkandarasi wa kufanya kazi hii kwa wakati. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 19

Hitaji la Umeme Vitongoji vya Jimbo la Kyerwa

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vitongoji ambavyo havijafikiwa na huduma ya umeme katika Kata za Businde, Bugara na Kibale?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati ambaye ni Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa ina jumla ya kata 24. Kati ya Kata hizo, kata 21 tayari zina umeme na kata tatu ambazo ni Businde, Bugara na Kibale zenye vijiji 11 zitapata umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II). Kwa sasa, mkandarasi yupo kwenye Kata hizo anaendelea na kazi ya kusambaza umeme katika vijiji 11 kati ya vijiji 29 vilivyopo kwenye wigo wa mradi huu kwa Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, Kata hizo zina jumla ya Vitongoji 62 na tunategemea Vitongoji 33 vitafikiwa na umeme awamu hii na Vitongoji vitakavyobaki vitafikiwa umeme kupitia miradi ya ujazilizi.

SPIKA: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kyerwa tuna Vitongoji 670, Vitongoji ambavyo vina umeme ni vitongoji 170, vitongoji 500 vyote havina umeme sawa sawa na asilimia zaidi ya 75.

Je, nini mkakati wa Serikali wa kupelekea vitongoji vingine ambavyo havina umeme? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la Pili; Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa Mikoa ambayo tunapata adha kutokana na umeme unaokatika mara kwa mara. Je, nini mkakati wa Serikali wa haraka kuunganisha Mkoa wa Kagera na gridi ya Taifa? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme katika maeneo ya vitongoji ni katika maeneo matatu. Kwanza ndiyo hii ambayo tunaifanya saa hizi ya *REA III Round II*, ambayo inafikisha umeme katika vijiji lakini katika vitongoji pia. Kama tulivyosema kwenye jibu la misingi Vitongoji 33 vitapata umeme.

Mheshimwa Spika, kuna mkakati wa pili ambao unafanyika wa umeme jazilizi (*densification*) na Mkoa wa Kagera kwenye eneo lake la Kyerwa *densification* katika two B na C zimo na kuanzia Januari tutaongeza wigo wa kupeleka kwenye maeneo hayo.

Mheshimwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta pesa sasa nyingi zaidi kwa ajili ya kumaliza vitongoji vyote nchini takribani kama elfu 30 na zaidi ambavyo havijapata umeme, inahitajika karibia Trilioni Sita na Bilioni Mia Tano kuweza kukamilisha eneo hili lote na jitihada za Serikali kutafuta hizo pesa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, mwezi huu, Mheshimiwa Rais amezindua kituo cha kupooza umeme cha pale Nyakanazi ambacho ndiyo sasa kimeingiza Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma na katika Wilaya mbili za Mkoa wa Kagera ambapo ni Ngara na Biharamulo. Jitahada za kuhakikisha kwamba Mkoa mzima wa Kagera unapata umeme kutoka katika chanzo hicho unaendelea na tayari mradi wa kuanza kupeleka umeme kutoka Benako kwenda Kyaka umeshatangazwa na Mkandarasi anatafutwa ili sasa Mkoa wa Kagera na wenyewe uweze kuingia katika Gridi ya Taifa hivi karibuni.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Hai maeneo mengi yamekuwa na miundombinu ya umeme ambayo ni chakavu sana, jambo ambalo ni hatari. Katika Kata ya Uroki, Masama Kusini, Machame na maeneo mengi yamekuwa na miundombinu ambayo kwa kweli ni chakavu sana. Tuliwasilisha maombi maalum ya kupewa vifaa kwa ajili ya kufanya marekebisho.

Je, ni lini Serikali itatuletea vifaa hivi ili kutuondoa kwenye hatari ya miundombinu ambayo imekuwa chakavu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kurasimisha na kurekebisha miundombinu yake ya umeme inayowapelekea wananchi nishati hiyo. Katika Mwaka huu wa Fedha, Serikali imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 500 kwa ajili ya kurekebisha Gridi ya Taifa katika maeneo ya umeme mkubwa pia imetenga Bilioni 300 kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ya umeme kwenye maeneo madogo madogo ambayo tunaziita ni *project* mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na yeye atapata mgao huo kwa ajili ya kurekebisha miundombinu yake chakavu ili huduma hii iweze kuendelea kupatikana katika eneo lake la Hai. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Sumbawanga Mjini, Kata ya Malangali, TANESCO waliweka kipooza umeme kwenye Kata hiyo.

Je, ni lini sasa Serikali itawalipa wananchi wa kule fidia? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikimaliza maswali nikapate eneo maalum, eneo ni eneo gani na fidia ni fidia gani ili niweze kulishughulikia na kujua kwa nini halijafanyiwa kazi kama changamoto hiyo bado ipo.

SPIKA: Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, swali lake litauliza kwa niaba yake na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

Na. 20

**Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kupooza Umeme
Wilaya ya Mbinga**

MHE. BENAYA L. KAPINGA K.n.y. MHE. JONAS W. MBUNDA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo Kikuu cha Kupooza katika Wilaya ya Mbinga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuimarisha Gridi ya Taifa uliopewa jina la 'Gridi Imara' kwa kujenga miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme pamoja na vituo vya kupooza na kudhibiti umeme.

Mheshimiwa Spika, mpango huu una miradi zaidi ya 40 na utatekelezwa ndani ya miaka Mitano (5) kuanzia mwaka huu wa fedha 2022/2023 ambapo Serikali imekwishatenga jumla ya Shilingi Biloni 500 kwa ajili ya kugharamia miradi yenye vipaumbele vya kwanza.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *kilovolts* 220 yenye urefu wa kilometa 93.5 kutoka Songea hadi Mbinga na ujenzi wa kituo cha kupooza umeme cha ukubwa wa *Megawatt* Mbili mara 30, *kV* 220 kwenda 33 utatekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja na nusu tangu utakapoanza. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, nina swali moja la nyongeza lenye sehemu (A) na (B).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *lane* iliyopo sasa ni hiyo ambayo inayotumika Songea, inatumika Mbinga pia inatumika Nyasa. Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa sana la utumiaji wa umeme kutokana na uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe pale Mbinga, viwanda vikubwa vya kubangua kahawa, viwanda vya kusaga sembe na viwanda vya maji ni vingi hali inayopelekea umeme kuwa wa *low voltage* au kukatikakatika.

SPIKA: Swali lako Mheshimiwa.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Je, Serikali iko tayari kurudisha mpango wake nyuma badala ya mwaka 2024/2025 uwe 2023/2024 ili kuwafanya wananchi nao wapate nafasi ya kutumia umeme ambao sasa haukatikatikati.

Mheshimiwa Spika, ikiwa hili haliwezekani, je, Serikali itaisaidiaje Mbinga kuondokana na hali hii ya kukatika katika kwa umeme? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikweli kwamba Mkoa wa Ruvuma umekuwa na changamoto ya maeneo kuwa na matatizo ya *low voltage*, na kwa sasa kwenye bajeti ya mwaka huu, kama tulivyosema tumeiweka Mbinga, kuna line ya kujengwa inayotoka Songea kwenda Tunduru ambayo ina kilometa kama 211. Serikali ilifanya uhakiki wa matatizo na ikagundua kwamba hapo kuna changamoto kubwa zaidi, na wako wale wenye changamoto kidogo na ambao hawana changamoto zaidi. Kwa hiyo eneo la Mbinga limewekwa kwenye wale wasiokuwa na changamoto sana kama hao wengine.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuifanyia marekebisho na matengenezo ya mara kwa mara hii line ya kutoka Songea kwenda Mbinga na tuone uwezekano wa kuvuta mapema kabla ya ule muda uliopangwa kulingana na bajeti itakavyokuwa imewekwa.

SPIKA: Mheshimiwa Hhayuma, swali la nyongeza.

MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Wilaya ya Hanang tunachangamoto kubwa sana ya umeme kukatika mara kwa mara, na suluhu ya tatizo hili ni kujengwa kwa kituo cha kupooza umeme pale Mogitu. Serikali iliahidi kutoa zaidi ya shilingi bilioni mbili ili ujenzi huo ufanyike.

Je ujenzi huo utanza lini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye maswali mengine, Serikali imefanya utafiti na kubaini maeneo yanayohitaji kujengwa vituo vya kupooza umeme kwa ajili ya kuhakikisha huduma inawafikia wananchi, na eneo hilo ni mojawapo kati ya maeneo ambayo yametengewa na muda utakapofika huduma hiyo itatekelezwa kwenye jimbo lake.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

1 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Ezra naomba ukae, Mheshimiwa Mnzava naomba ukae.

Ninayo matangazo hapa mbele, matangazo ya wageni waliotufikia siku ya leo, kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika; tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nape Nnauye ambaye ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ndugu Dkt. Jim Yonaz, karibu sana; na yupo pia Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) Mhandisi Othman Khatibu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; wageni watatu wa Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale kutoka Mkoa wa Geita wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Nyang'hwale, Ndugu Kaswahili Enock, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka makanisa mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 47 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Kwaya ya Uvuke kutoka Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu Dayosisi ya *Central Tanganyika* Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Revocatus Gwihangwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Ester Matiko, Mbunge, ambao ni mama zake wadogo kutoka Tarime, Mkoa wa Mara wakiongozwa na Ndugu Chaboka Mantago, karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo la wageni tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Nilimwona Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, alisimama na Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesu pia alisimama. Mheshimiwa Mnzava.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 53(1).

Mheshimiwa Spika, nimeuliza swali namba 15 kwa Wizara ya Afya, na katika swali langu la msingi nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Katika

swali la pili la nyongeza, nimeuliza kitu kingine lakini kimejibiwa kitu kingine. Naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa.

HOJA YA JAMBO LA DHARURA

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) inayosema; Baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivoorodheshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi na la dharura na muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, sasa nimesimama kutoa hoja ili Bunge lijadili jambo muhimu na la dharura katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunajua vyuo vimefunguliwa *weekend* hii iliyopita lakini watoto wengi sana kwenye Taifa hili wamekosa mikopo. Baada ya kupitisha bajeti yetu katika Bunge hili tukioneshana kwamba Bodi ilikuwa imeongeza fedha na watoto wengi wangeweza kupata mikopo lakini watoto wengi hawakupata mikopo, kwa hiyo, ni jambo la dharura katika Taifa. Hivyo naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako lijadili jambo hili la dharura ili hatimaye tupate majibu kutoka hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Usitoe hoja, bado.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Dkt. Christine Christopher Mnzava, ametumia Kanuni ya 53 ambayo inataka maswali yajibiwe kikamilifu. Ameeleza kwamba kwenye swali lake la msingi namba 15 aliuliza maswali mawili ya nyongeza kama ambavyo kanuni zetu zinamruhusu. Yeye kwa namna alivyouliza swali lake la pili la nyongeza na namna Naibu Waziri alivyojibu, Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava anasema Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu swali lake kikamilifu.

Sasa kwa sababu swali hili la msingi lilikuwa ni la kwake, tutakwenda kutazama Taarifa Rasmi za Bunge, halafu tuone alivyouliza swali na namna Naibu Waziri alivyojibu. Kama atakuwa hakujibu lile swali aliloulizwa tutaoa fursa ya kujibiwa upya swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama pia Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa kwa Kanuni ya 54, akitaka kutumia kanuni hii kwa jambo ambalo amelisema. Kanuni zinataka akishasema hivyo, kwa sababu ameshasema, ni kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kanuni zinanitaka mimi kama

naona kwamba hilo jambo alilolisema ni la dharura nimpe fursa sasa ili awasilishe halafu ndipo atoe hoja, ndivyo kanuni yetu inavyosema.

Sasa nitakupa nafasi ya dakika tano uwasilishe hilo jambo lako halafu na Wabunge wataweza kupewa nafasi ya kuunga mkono au kutokuunga mkono hoja hiyo. (Makofi)

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kukubali jambo hili na kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja yangu hii ya Bodi ya Mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu tulimwona Waziri wa Elimu katika vyombo vya habari akisema kwamba aliunda tume maalum ya kuchunguza Bodi ya Mikopo, lakini Waziri akawa analalamika kwamba ile tume aliyoiunda imeshindwa kupata ushirikiano. Kwa hiyo, maana yake Bodi na Serikali haviko pamoja ndiyo maana Waziri ameunda tume na tume haijaweza kutoa ushirikiano kwa Serikali. Kwa hiyo jambo lile likanishtua kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini *weekend* yote hii baada ya majina kutoka na wanafunzi kuanza kudahiliwa na wengine kuripoti mimi nimepokea simu nyingi sana kutoka jimboni kwangu, wazazi wengi wanafunzi wao wamekosa mikopo, wote wanakimbilia kwa Mbunge. Sasa *solution* hata mimi nikawa naona nikirudi kwa Waziri yule ambaye nilimwona kwenye vyombo vya habari analalamikia tume, sidhani kama ningeweza kupata jibu la haraka, ndiyo maana nikasema Bunge ndicho chombo cha wananchi hivyo nilete hoja katika Bunge ili Bunge liweze kujadili hatimaye tupate majibu na tutoke na maazimio ya Bunge ili tuweze kuelekeza Serikali nini ifanye kuweza kuwakwamua watoto hawa ambao wamekwama katika maeneo haya. (Makofi!)

Mheshimiwa Spika, niki-refer ukurasa wa 49 wa hotuba ya Waziri wa Elimu aliyotoa humu Bungeni, tumeona alikuwa anasema kwamba katika mwaka huu uliopita wa fedha, tumetoa mikopo ya takribani Shilingi bilioni 569. Tukaona ni jambo zuri, na katika mwaka huu wa fedha ambao tunaendelea nao wa 2022/2023 tulikuwa tunategemea kwamba fedha ilikuwa inaongezeka. Alikuwa pia na shilingi bilioni 200 kutoka NMB ambazo zingeenda kukopesha wafanyakazi na watu wengine ambao wanao uwezo wa kukopesheka kutokea huko, mpaka na watu wa *diploma* waweze kupata huo mkopo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza, niko na fomu hapa ya mtoto wa mkulima ambaye ameandika, mama ni *farmer* na baba ni *farmer*. Mtoto huyu ni miongoni mwa watoto *reference* katika Taifa hili ambaye amepata *division 1.7 O'level*, Msalato Sekondari (shule ya Serikali). Akiwa na "A" saba mtoto wa kike, *form five* na *form six* akabaki Msalato palepale. Mtoto huyu wa kike akapata *division 1.7* tena. Mtoto huyu amechaguliwa kwenda

kusomea udaktari Chuo cha KCMC. Ajabu ni kwamba alichokipata, anapewa ile fedha ya kujikimu lakini hajapewa ada.

Mheshimiwa Spika, ada ni shilingi 5,600,000. Mtoto wa mkulima ambaye amesoma Msalato miaka yote sita, anapata wapi ada hii ya kuweza kusomea udaktari? Maana yake tunachokiona ni nini? Hata watoto wadogo walioko pale waliomwona kama *role model* wao aliyepata *division one* ya pointi saba watakata tamaa ya kusoma maana ndoto zao zinakatizwa kwa sababu hawana uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kigezo ambacho nashindwa kukielewa kipindi wanachambua. Katika masharti yaliyowekwa humu kwenye *Loan Board* hapa, kipo kigezo ambacho, baada ya viongozi wa Serikali ya kijiji kusaini fomu ya mtu huyu, tumeambiwa kwamba endapo itakuwa wametaja taarifa za uongo, watatozwa faini ya shilingi milioni moja na nusu au kifungo cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja. Sasa tunajiuliza, kama watu wanasaini fomu na zinapita kwa viongozi na sheria mmeweka, sijasikia kama kuna kiongozi wa kijiji hata mmoja ambaye amepelekwa mahakamani kwamba alijaza fomu za uongo na akashtakiwa, *that means* taarifa za watoto hawa ni sahihi lakini watoto hawa wananyimwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako lipokee hoja yangu na lijadili hili jambo ili tuone jinsi ya kuwakwamua hawa watoto ambao wamekwama na wengine bado wako majumbani na hata walioripoti vyuoni bado hawajapewa fedha hiyo pia bado wanahangaika mtaani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa fasili ya Nne ya Kanuni yetu ya 54 inasema, iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na linamaslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano, ambazo nilimpa Mheshimiwa Mbunge, na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja alikuwa ameshaeleza Mheshimiwa Ezra mwanzo kwamba inahusu mikopo, nikampa nafasi ya kutoa hoja. Ametoa hoja na imeungwa mkono, sasa watasimama wale wanaotaka kuchangia na hawataweza wote kupata nafasi lakini nitatoa muda mfupi kwa ajili ya kuchangia hoja hiyo kwa wale Wabunge wanaotaka kuchangia, halafu Mbunge mtoa hoja atapewa fursa ya kuhitimisha hoja yake, ndivyo kanuni zetu zinavyosema.

Waheshimiwa Wabunge watakaopata fursa ya kuchangia hoja ni Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Kigwangalla, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Charles JMwijage, Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Kwezi, Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Profesa Mkenda halafu tutahitimisha hoja. Katika hawa wachangiaji niliowataja, kila mchangiaji atapewa dakika tano. Mheshimiwa Judith Kapinga.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ambayo iko mezani.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu kwa nchi yoyote ama kwa jamii yoyote ndiyo mkombozi wa mtoto wa masikini yeyote katika taifa lolote. Elimu ndiyo imani ambayo mzazi anaweza kuiweka kwa mtoto wake, ndio urithi pekee ambao mzazi wa kimasikini wa Kitanzania anaweza kumpatia mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuipongeza Serikali. Sasa hivi elimu msingi katika nchi yetu ni bure. Mtoto anaanza darasa la kwanza mpaka darasa la saba, anafuata *form one* mpaka *form four*, *form five* mpaka *form six*. Mazingira ni wezeshi kwa mtoto wa Kitanzania kuweza kupata elimu yake kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha sita. Kwa kweli napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambazo imefanya kwa ajili ya haya mazingira wezeshi.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu ya Kitanzania mtoto yupo katika elimu kwa miaka takribani 16 hadi 17. Baada ya hapo mtoto huyu anategemewa kwenda elimu ya juu. Pale kwenye elimu ya juu kama atapata nafasi, au kama mkopo atapata ama asipopata, baada ya hapo anaenda mtaani. Tayari tuna-*frustration* kubwa ya changamoto ya ajira mtaani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mtoto anakaa kwa takribani miaka 14 katika elimu, ile miaka mitatu ambayo inabidi amalizie, bado inakuwa kizungumkuti. Kwa hiyo tunakuwa tunavunja imani kwa watoto wetu kuweza kumaliza.

Mheshimiwa Spika, kwa Afrika Mashariki, ukitoa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo imejiunga sasa hivi, Tanzania ni mojawapo ya nchi ambayo ina-*population* kubwa ya watu. Ukilinganisha na nchi kama Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, Tanzania iko hapo juu lakini kwa kipindi kirefu Tanzania siyo amabayo inaongoza kwa idadi ya wanafunzi ambao wanamaliza katika elimu ya juu. Inaongoza kwa idadi ya *population* lakini haiongozi kwa idadi ya wanafunzi ambao wanamaliza katika vyuo vikuu vyetu.

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nchi zetu jirani kwa mfano, idadi ambazo zinamaliza ni laki moja mpaka laki na ishirini; nchi ambazo zina-*population* ndogo, lakini sisi idadi zetu ni *sixty thousand*, elfu hamsini, elfu arobaini na tano, hatuvuki hapo. Sababu ni nyingi lakini sababu mojawapo ni uwezeshaji wa wanafunzi kuweza kujiunga na elimu ya vyuo vikuu. Mikopo imekuwa changamoto kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, elimu ndiyo *advantage* ambayo tunaweza tukaitumia tukiwa tuna-*population*. Ukiwa na idadi kubwa ya watu walioelimika, ndipo hapo unaweza ku-*explore opportunities* nyingi kwa wananchi wa taifa lako. Sasa tukiwa tuna namna ambazo zinasababisha watoto kupata vizingiti vya kuendelea na elimu ya juu hapo kunakuwa kizungumkuti, na hapo ndipo ambapo tunajitahidi huku ngazi za chini tunakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi ambao sasa wanakaa mtaani, wanakuwa *frustrated*, wanajiunga na wale ambao tayari wanachangamoto ya ajira, tunakuwa na taifa la vijana ambao wako *frustrated* kwelikweli.

Mheshimiwa Spika, elimu kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni haki ya msingi kabisa. Kwa hiyo ni jukumu la Serikali kuhakikisha fedha inapatikana kwa ajili ya wanafunzi kusoma, hususani masuala ya sayansi. Sayansi ndiyo ambayo inakomboa taifa lolote duniani kwa sasa masomo ya sayansi ndiyo msingi wa maendeleo ya sayansi na teknolojia kwenye taifa lolote lile; na hapa ndipo ambapo vijana wengi wataweza kuajiriwa. Hatuwezi kutatua changamoto ya ajira taifa hili kwa kazi *physical*. Changamoto za ajira zinatatuliwa kwa uvumbuzi unaotokea kwenye maendeleo ya sayansi na teknolojia. Sasa tusipoweka mikopo watoto wakasoma kwenye masomo ya sayansi mpaka ngazi ya juu, sasa ubunifu tutatoa wapi?

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali i-*dedicate* kwenye kuhakikisha fedha zinapatikana. Ukiangalia bajeti yetu ya Wizara ya Elimu 60% ni Bodi ya Mikopo. Hata hiyo Bodi ya Mikopo imewekwa kwenye *list* ya miradi ya maendeleo, lakini si mradi halisi wa maendeleo huu. Ilitakiwa iwe ina-*vote* yake tofauti, peke yake. Ndiyo maana ukiangalia Wizara ya Elimu unaona Bodi ya Mikopo inafedha kubwa lakini haina fedha kubwa. Imekaa kwenye bajeti ya Wizara, ilitakiwa iwe na *vote* peke yake. Ndiyo maana tukiona bajeti hapa tunaona bajeti ya Wizara ya Elimu ni Bodi ya Mikopo ina fedha kubwa lakini siyo fedha kubwa, ni 60% ya bajeti ya Wizara ya Elimu; lakini sio fedha kubwa. Tunashauri iwe na *vote* peke yake ili tuweze kui-*monitor*. Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Cosato David Chumi ajjandae.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, hali ya kiuchumi ya familia nyingi za kitanzania zinafanana sana na kesi ya mtoto aliyetolewa mfano na Mheshimiwa mtoa hoja. Pia kesi ya mtoto ya mtoa hoja inafanana sana na kesi za watoto wengi ambao wapo katika majimbo yetu. Hii imenifanya nisimame hapa kwa sababu nimejitazama mimi mwenyewe ninatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtoto wa Katibu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi enzi hizo, na ninakumbuka kipindi hicho wakati mimi nafaulu vizuri sana *Form Six* masomo yangu ya *PCB*, mama yangu mzazi ndio alikuwa mlezi wangu pekee na alikuwa hajalipwa mishahara yake ya karibu miaka miwili hivi.

Mheshimiwa Spika, nikitafakari hali ya mtoto ambaye amefaulu kwa *Division One*, kama ambavyo mimi nilikuwa nimefaulu kwa *Division One* kipindi namaliza na mzazi wangu hana uwezo; na nikitazama mazingira ya watoto wengi wa kitanzania; naona kuna haja ya suala hili kutazamwa kwa umakini zaidi kuliko linavyotazamwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Tunaelewa Wizara ya Elimu wanafanya kitu kinaitwa *means tests* ili kuwapata watoto ambao watapata sifa za kupewa mkopo na Serikali. Tunafahamu kama Taifa, tunapata changamoto ya kuongezeka kwa wahitaji wa mkopo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo kila mwaka, kwani kila mwaka wanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, sasa hatutarajii siku moja *population* itashuka kwa sababu ukitazama namba zilizotangazwa jana za sensa utaona pengine miaka 30 ijayo idadi ya jana itakuwa ime-*double*. Pengine tukawa na watu zaidi ya milioni 120. Sasa nini Serikali ifanye kama suluhisho la kudumu? Ni lazima ufanyike mchakato wa wazi wa njia za kupata wahitaji na wanufaika wa mfuko huu wa Bodi ya Mikopo, pia ipatikane namna ya kuwasaidia hawa ambao wanafikisha zile sifa ambazo zinahitajika. Vinginevyo, tutatengeneza bomu kubwa sana la watoto pamoja na wazazi wao ambao watakuwa wanailaumu Serikali maisha yao yote.

Mheshimiwa Spika, *you can imagine* mtoto ambaye amefaulu kwa *division one* kama ambaye ametolewa mfano na mtoa hoja, akikosa fursa ya kwenda kusoma Udaktari kama ambavyo alikuwa ametamani, *you can imagine* hiyo *scenario crisis* ambayo inajitokeza kwake na familia yake, lakini namna ambavyo watoto wengi watakufa moyo kutokana na hiyo. Pia yatatokea maswali ambayo tutapaswa kuyahoji kwamba je, tunatenda haki kwa watoto wa Taifa letu? Kwa sababu elimu ni haki ambayo inatolewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia kupata mkopo ni haki ya watoto ambao wamefaulu na wanakidhi vigezo. Tusipotoa haki hiyo kama Taifa, maana

yake tunatengeneza kundi la watu ambao wataacha kuamini katika Katiba, wataacha kuamini katika Sheria, wataacha kuamini katika Serikali, wataacha kuamini katika Bunge, wataacha kuamini kwenye kitu chochote kile ambacho kiko *morally right*. Kwa sababu kama nimefanya kila kitu vizuri, nimefanya kila kitu sawa, nisipopata haki, kuna haja gani ya kuwa mtu mwema katika dunia hii? Ndiyo maswali ambayo watoto wengi na wazazi wengi watajiuliza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wewe ni msomi wa Sheria, anaisema vizuri sana Mwanafalsafa Tom Tyler kwenye kitabu chake cha “*Why People Obey the Law*” ambacho alikiandika mwaka 1990, kwamba uhalali wa maamuzi yanayotolewa na viongozi, uhalali wa sheria zinazotungwa na Mabunge ya Mataifa utapatikana tu endapo sheria hizo, endapo Serikali zao, endapo Mabunge yao yatatoa haki kwa wananchi na wananchi wataona haki imetolewa na wata-enjoy matunda ya haki ambayo inatolewa na sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili mifumo yetu ya Utawala Bora, ili Katiba yetu, sheria zetu ziendeleo kuaminiwa, kuthaminiwa na kutumainiwa, ni lazima tutoe haki kwa watu wa Taifa letu. Haki ya msingi kabisa ambayo mwanadamu yoyote anapaswa kuipata, basi ni haki ya kupata elimu. Kuna haja gani ya kuzaa mtoto ukamlea vizuri, ukampa miongozo, akaenda shule, akasoma vizuri, na akafaulu, akakosa fursa ya kwenda kusoma masomo ya Chuo Kikuu kwa sababu nchi yake imeshindwa kumwekea mfumo mzuri wa namna ya kupata msaada wa kulipiwa ada na gharama nyingine za masomo yake?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kwamba tunaelewa Serikali ina mzigo mzito wa kukidhi gharama za kusomesha watoto wa Taifa letu, ni lazima tuweke mfumo kwanza wa wazi; pili, unaokubalika; tatu, unaotekelezeka, wa kuwafikia wahitaji na wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya kati na hata elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ilivyo sasa, mfumo tulionao hautoi haki kwa watu wengi na hivyo ninaunga mkono hoja ya mtoa hoja kwamba jambo hili liangaliwe upya na mwisho wa siku tupate suluhisho la kudumu, ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Eng. Ezra na imenifanya kufikiri sana. Hivi huu ni msaada, mkopo, huruma au upendeleo? Kwa sababu unashindwa kuelewa uiweke kwenye *position* gani?

Mheshimiwa Spika, mimi ninao watoto zaidi ya 100, acha hao waliosoma Msalato; amehangaika kwenye shule zetu huko vijijini, akafanikiwa kupata *Division One*. Ameomba mkopo mwaka wa kwanza, amekopa; wa pili amekosa, akija kupata, anapata asilimia 30. Sasa swali langu hapa bado najjuliza, huu ni mkopo ambao mtu ni haki yake kupata? Ni huruma, upendeleo au ni zawadi? Maana yake kama ni mkopo, imani yangu ni kwamba kila mwenye sifa ambaye amekuwa *admitted* kwenye *university*, na anaomba mkopo kwa sababu atalipa, ndiyo maana ya mkopo. *Otherwise* tukubaliane hapa, tubadilishe jina la hili fungu

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye anaomba kukopa, atalipa. Halafu anayemkopesha, anasema sikukopeshi, nakupa asilimia 10. Je, huu ni mkopo, huruma, upendeleo au zawadi? Tutafute jina ambalo litafiti kwenye hili fungu, badala ya kulipa jina kubwa halafu kumbe hatuna uwezo wa kulisimamia jambo hili halafu tukakuta watoto wengi wanakosa haki ya kusoma.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana kama wanne walikuwa wanasoma *UDOM*. Mwaka wa kwanza wakaomba mkopo wakakosa. Nikamfuata Naibu Katibu Mkuu nikamwomba anisaidie, naye akaniambia nipe majina. Akapeleka kule kwenye Bodi ya Mikopo naye akakosa. Mwaka wa pili wakaomba, wakakosa, wakaacha shule. Mwaka huu tena nimempelea Naibu Waziri kwenye simu yake.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niko Bungeni, Mbunge mwenzangu nimemwomba awasaidie hawa Watoto, nawajua ni masikini, akaenda na yeye akaniambia waambie wa-*appeal*, wakimaliza waniambie. Waka-*appeal* wakakosa. Sasa najjuliza hii *means test*, ina-*test* nini? Kama amejaza fomu, imepitia *process* zote, ni *authentic form*, lakini bado sifa za kupata hiyo fedha hana.

Mheshimiwa Spika, na kama kweli Mheshimiwa Naibu Waziri alichukua yale majina akapeleka na amethibitisha kwamba wame-*appeal* na bado na yeye aliwapeleka wakakosa, sasa nilitaka nikushauri, kwanza turudi kwenye *Hansard*. Tulishauri hapa wakati wa bajeti tukasema, inawezekana kweli kwamba tumeweka utaratibu ambao watu tunajikuta tunashindwa kujua nani anahitaji. Mimi hata unaposema tusomeshe watu wa sayansi peke yake, mimi sikubaliani nayo. Nchi hii haiwezi kuongozwa na watu wa sayansi peke yake. Kuna watu wamesoma sheria, wamesoma masomo mengine, wana haki ya kupata mkopo na wana haki ya kuitumikia nchi hii na wana haki ya kuongoza nchi hii, hatuwezi kusema tuwape wanasayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuweke utaratibu ambapo itakuwa ni haki ya kila mtoto aliyesoma. Bado nashawishika kwamba utaratibu wa kupima vigezo vya kuwapa watoto mkopo, hautusaidii kuwapata watu wenye shida. Mtoto

wangu akiomba mkopo, najulikana Kanyasu, utaninyima kwa sababu ni Mbunge. Nina Diwani wangu ambaye mtoto wake aliomba mkopo akanyimwa, kwa nini? Eti Diwani. Hivi Diwani ana uwezo wa kusomesha mtoto kwenye ada ya Shilingi milioni nne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Ezra, nadhani tuna shida ya kuutaza upya mfumo mzima wa ukopeshaji, na pengine inawezekana fedha tunazozitoa tunadhani ni nyingi kumbe siyo nyingi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge lililopita tulipitisha bajeti hapa. Mtoto wangu anasoma Chuo Kikuu cha Mweka, akaniambia baba, hivi mbona ninyi wanasiasa wote ni waongo? Nikamwambia kwa nini? Mmepitisha Shilingi bilioni 500, huwa mnampa nani? Hapa nina watoto karibu 20 hawajapata mkopo. Sasa inaonekana wanasiasa wote waongo.

Mheshimiwa Spika, tufumue upya, tuangalie namna bora ambayo kila mtoto mwenye haki ataweza kusoma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Francis Mtinga, ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra. Kwanza napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kuwa na *scholarship* maalum kwa ajili ya watoto ambao wanaenda kusoma sayansi.

Mheshimiwa Spika, kuna *scholarship* zimetolewa kwa ajili ya watoto zaidi ya 600, ni jambo jema nami kwa mawazo yangu na uelewa wangu nimeona kwamba kama Taifa tuna miradi mingi inayoendelea. Tuna mradi wa SGR, tuna mradi wa Bwawa la Umeme na juzi tumeona uwekaji wa jiwe la msingi katika kiwanja kikubwa sana cha Kimataifa cha Msalato na viwanja vingi vinaendelea kujengwa kikiwemo kiwanja cha Iringa pale ambacho kitapanua wigo sana wa utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi vitu vyote ambavyo tunavijenga, hii miundombinu yote baada ya kuwa imekamilika, itahitaji huduma katika kuiendesha miundombinu hii. Vile vile itahitaji wataalamu na utaalumu na nadhani kwa sababu hiyo ndiyo maana Mheshimiwa Rais akaona atoe *scholarship* kwa ajili ya watoto ambao baadaye watakuja kutumika katika kusimamia miundombinu na miradi mbalimbali ambayo tunajenga sasa hivi kwa fedha nyingi ambazo ni za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, suala la mikopo ni suala ambalo siyo la hiari tena kwa Taifa letu, ni suala la lazima. Tukitoka huko nje kwa wananchi sisi kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi, katika mikutano yetu ya hadhara, katika vikao vyetu vya ndani tumekuwa tukijinasibu kwamba tumeongeza fedha kwa ajili ya mikopo ya watoto wetu. Sasa inapotokea kwamba watoto na waliokuwa na ufaulu wamekosa, maana yake ni kwamba tunajichanganya sisi wenyewe na wananchi, kwamba tumeongeza fedha kama alivyosema Mheshimiwa Kanyasu, kijana anauliza hiyo shilingi milioni 570 sasa iko wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa kama tumeongeza fedha na watoto hawapati, kwa kadri ya matarajio na kwa kadri ambavyo tumewaaminisha kwamba tumeongeza fedha, maana yake ni kwamba tunakuwa tunawachanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niseme jambo moja, maana tayari hii ni *crisis*, hili ni tatizo. Sasa je, tatizo hili ni namba moja, ni tatizo kama hivyo walivyokuwa wanasema wenzangu namna ya kuwatambua wanaostahili mikopo au tatizo ni ufinyu wa bajeti?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kuwa tumetambua shida ni nini, tatizo ni nini, basi kama Bunge ambao tunaishauri na kuisimamia Serikali, ni wajibu wetu kuona tunatoka na suluhisho gani?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tulipokuwa tuna shida ya ongezeko la bei ya mafuta kutokana na ongezeko la bei ya mafuta duniani, Serikali yetu tunaipongeza sana ilikaa chini, ikaona kuna umuhimu wa kutoa ruzuku kupunguza makali ya bei ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa na kilio hapa cha mbolea, Serikali yetu ikafuata ushauri wa Wabunge, imekuja imetoa ruzuku ya mbolea. Mwaka 2021 au mwaka 2020 wakati tulipokuwa na *crisis* ya bei ya mahindi, tulikaa na Serikali; Wabunge wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Serikali ikatafuta fedha ikawezesha hifadhi ya chakula, ikatoa fedha mahindi yakanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, kama hili ni tatizo basi kama ni la kibajeti, hebu tukae chini tuone tunafanyeje, fedha ipatikane watoto wapate mikopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Mtinga na Mheshimiwa Kwezi ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, kuhusu hili suala la malipo wanayolipa wanafunzi wanapokuwa katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra na naomba niichambue kiuchumi na kisiasa. Dira ya Taifa 2025 ina malengo Matano. Mojawapo ya malengo ni kujenga jamii ya watu walioelimika na wenye uchu wa kujifunza. Kwa hiyo, mtu akikuuliza kwamba 2025 tutafika, kwa speed hii tutakwama, lakini kwa sababu tumeona, naona Mheshimiwa Ezra ametusaidia tunakwenda kukwamua ili tuweze kujenga jamii ya watu walioelimika na wenye uchu wa kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kiuchumi kwa haraka haraka nimeangalia kipato cha Mtanzania, *income per capita*, najua kinachomsumbua Mheshimiwa Ezra, mkoa wake ndiyo ambao una pato dogo. Kwa hiyo, wakuu wa vyuo mkoa wa Mheshimiwa Ezra ukumbukwe sana, ndio una pato dogo. Ila *per capital income* ya Watanzania ni Dola 1,040. Sasa Dola 1,040 angalia mwanafunzi anayekwenda kusoma shule ya milioni tano kwa mwaka, ataweza vipi na mzazi huyo ana watoto nne mpaka watano?

Mheshimiwa Spika, lengo la Taifa ni kuelimisha watu bila kubagua, lakini kuna fani zinazopendelewa. Ninachoshauri, hapa kuna suala la haraka la kuokoa hii hali na suala linalohitaji mchakato wa miezi mitatu, minne, mpaka sita tufanye maamuzi. Suala la haraka kama walivyodokeza wenzangu, kama mjomba Chumi alivyosema, tutafute namna ya haraka, hawa wenye sifa tuwabebe wote kama walivyo waende wasome, waendeleo na shule. Wanapoendelea sisi huku tuweze kwenda kutafuta mpango wa muda mrefu, nami mpango wa muda mrefu kwangu ni miezi sita.

Mheshimiwa Spika, kisiasa nimekwazika, kama mfumo huu tukiendelea nao ambao tuliutengeneza kwa nia njema, lakini umekwama; nami sioni tatizo, unatengeneza *formation*, inakwama unabadilisha, unatengeneza *formation* nyingine, unatoka na magoli. Mfumo huu kwenye Chama cha Mapinduzi umekwama, tunakwenda kujenga matabaka wana-CCM wenzangu. Huu mfumo unakwenda kutupeleka kwenye matabaka, hawa wapate hawa wasipate.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kanyasu amebahatika mwanaye yuko chuo kikuu wakamwambia, kuna mzazi hana mtoto chuo kikuu, atasemewa na nani? Kwa hiyo, nawasihi, tuweze kutafuta wepesi wa haraka kuwakomboa wote hao wenye sifa waende chuoni, halafu turudi tuje tutengeneze mipango ya muda mrefu. Mojawapo ya sababu za kufanya, naweza nisishiriki kwenye mchakato huo, hizo fani mnazotaka kupeleka watoto za Shilingi milioni tano, hebu fikiria vyuo vya namna hiyo mvipe ruzuku. Yaani *course* inapewa ruzuku kabla ya mtoto, kwamba ukienda

kusoma udaktari wewe, ni shilingi milioni moja au ni laki saba, kusudi watu waende kule. Ukienda kwenye u-pilot ni shilingi laki tatu, kusudi wale watoto wanaomudu waende kule.

Mheshimiwa Spika, langu ni kuunga mkono hoja kwa sababu wanaolia ni wengi, Mheshimiwa Chiwelesa alilolisema ametusemea wote, amewasemea Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati nikiendelea kuita majina hapa ya wachangiaji, michango ni mizuri na hoja ni nzito sana, lakini niwakumbushe hoja kama hizi hazina uhusiano na uchaguzi. Isionekane kwamba Serikali inaposhauriwa, inashauriwa ifanye ili ishinde uchaguzi. Serikali haina uchaguzi wowote, chenye uchaguzi ni chama na mambo ya chama yajadiliwe huko kwenye vyama vyetu.

Waheshimiwa Wabunge, humu ndani tunaishauri Serikali, tunazungumza mambo ya wananchi, wananchi hawana vyama huko, wako wenye chama hiki, wako kwenye chama hiki, kila mtu anachagua chama chake. Tukisema saa hizi tunataka kujitisha na uchaguzi ahaa jamani! Tujadili tu hii hoja ya msingi kabisa wala isielekee huko kwenye uchaguzi, kama mtu atachaguliwa au hatachaguliwa hiyo sio hoja, hoja ya msingi ni kwamba tunataka watoto wetu ambao wamefaulu vizuri wapate mikopo, hiyo ndiyo hoja ya msingi. (Makofi)

Mheshimiwa Francis Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kwezi na Mheshimiwa Mwakasaka ajiandae.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jambo hili muhimu sana ambalo linajenga mustakabali wa kujenga nchi yetu miaka inayokwenda mbele na miaka ya sasa. Naomba nianze kwa kuunga mkono kabisa hoja nzuri ambayo Mheshimiwa Ezra ameileta, hoja ya kukomboa kizazi chetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa ni nchi ambayo inajiunga na *forum* mbalimbali ikiwepo *East Africa* na nchi zinazidi kuongezeka ndani ya *East Africa* na wenzetu wanasomesha watoto wao kwa nguvu kabisa. Katika nchi yetu mkombozi pekee aliyebaki katika suala la ajira ni kujijiri. Sasa tunataka vijana wetu wajijiri lakini tunataka kuepuka kuwasomesha, sasa sijui watajiri kwenye ajira gani? Nasema hivi kwa sababu wanashindana na wenzao katika *East Africa* ambao wamesoma sana na mipango ya kujijiri lazima watu wawe wamesoma, kwa hiyo hiki ambacho kinatokea sasa tunakokwenda vijana watakuwa ni wafanyakazi sijui wafanya kazi za ndani sijui za mashambani? Maana yake tutakuwa hatuna wasomi ambao wamesoma ili waweze kujijiri na kuajiri wenzao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala hili, naomba kabisa Bunge lako tuje na *solution* ya haraka ili vijana wetu ambao wamefaulu vizuri waende wakasome. Huu utaratibu jinsi gani wanapata mikopo ya asilimia mbili, asilimia tatu pengine umefeli. Baada ya hao kuondoka, naomba Bodi ya Mikopo waje hapa watueleze *formula* hizi wanazitumia vipi, wanachagua vipi watu hawa. Tuwasaidie mawazo ikiwezekana, kwa sababu inaonekenana wamelemewa na huu mzigo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Kanyasu, huu ni mkopo wa aina gani? Mbona ni kama hisani. Wapo watoto wana *division one* mwaka jana hawakupata mikopo, wamekaa mwaka huu ndio wamebahatisha asilimia ndogo, wengine ndio wamefaulu na *division one* mwaka huu, hawajapata kabisa, afadhali hata yule aliyetolewa mfano ana viasilimia kidogo, wako wengi kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe suala hili kwa kweli tutoke na muafaka hapa jinsi gani watoto wetu hawa ambao wamefaulu vizuri wanakwenda shule. Vinginevyo nchi yetu hii tuna idadi kubwa ya watu ndani ya *East Africa*, ukiacha Congo, lakini sasa sijui ndio tutaanza ku-*provide* wafanyakazi wa ndani kwa wenzetu. Kwa kweli inabidi sasa tuliangalie jambo hili kwa makini sana. Bajeti imeongezeka tulisikia hapa, bado marejesho yanafanyika, lakini sijui kitu gani kinatokea katika jambo hili. Jambo hili ni *serious* sana, hatuna urithi mwingine wa kuwarithisha vijana wetu na watoto wetu zaidi ya elimu, tukishampa elimu tunamwambia ardhi ile pale, mifugo hiyo hapo, nenda kajijiri, lakini elimu wanayo, hivyo, atajua ata-*convert* vipi hiyo ardhi ili iweze kumpatia maslahi. Sasa hili atalifanya vipi kama hana elimu kichwani? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningepomba niunge hoja suala hili na tulichukulie kwa makini, kwa u-*serious* mkubwa, hawa waende lakini Bodi ije hapa itueleweshe vizuri *formula* wanayotumia, tuwasaidie mawazo ili usawa upatikane. Watoto wengine wakishasoma *private* ndio kibali cha kunyimwa mkopo tayari. Pengine amesaidiwa huko wengine na *compassion*, wengine wamesaidiwa na Mbunge na wengine wamesaidiwa na mjomba. Mjomba ameshafariki, eti kwa sababu kasoma *privatae* tayari anaambiwa wewe huna sifa ya kuwa na mkopo. Kwa hiyo ningepomba hii *formula* iangaliwe upya kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache kwa uchungu sana naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kwezi, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze tu kwa kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ezra.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niwasilishe kwamba, kwa kweli katika huu muda wa wiki mbili kelele zimekuwa ni nyingi sana kwa wanafunzi ambao wamekosa mikopo na kwa wanafunzi ambao wamepata kiwango cha chini kabisa cha mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu nilikuwa najiuliza maswali mepesi tu kwamba, Serikali imefanya vizuri sana kwenye kujenga sekondari, tena nyingi karibu kila kata na pengine kata zingine zina sekondari mpaka tatu. Pia Serikali imefanya vizuri sana kwenye vyuo, kwa maana ya ujenzi na kila kitu, lakini ongezeko la wanafunzi ambao wanasoma limekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa haya yote, nimeona kuna *gap* ambalo Serikali haijafanya vizuri. Serikali haijafanya vizuri kwenye eneo hili kwamba huku kote wametoka vizuri. Tumekuja vizuri, lakini shida kubwa imekuja kutoka *volume* ya wanafunzi ambao wanaingia vyuo vikuu ni kubwa sana, ni lazima tuongeze Bajeti. Kwa hiyo la kwanza, naishauri Serikali ije na mkakati hapa Bungeni wa kuhakikisha *ina-cover* wale wanafunzi wote wanaofaulu vizuri, wasibaki nyumbani.

Mheshimiwa Spika, hapa tunatengeneza bomu. Huwa najiuliza hata vigezo eti wanasema kwamba huyu alisoma shule ya *private*, labda alikuwa analipiwa milioni mbili, milioni mbili na kadhaa. Sasa nikawa najiuliza wazazi hatuelewi kama kuna wengine wanafilisika, hatuelewi kama kuna wazazi wengine wanastaafu, kama tunaelewa kwamba wapo wazazi ambao uwezo wao unapungua ni kwa nini tunawawekea masharti magumu kiasi hiki? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababau mimi leo inawezekana nina uwezo, kesho kutwa nisiwe na uwezo wa kifedha, kwa hiyo mtoto wangu abaki nyumbani? Kwa mfano, ongezeko tu la takwimu za jana, Tabora tumekwenda kwenye milioni 3.3, kitu ambacho lazima tubadilishe, lazima tu *allocate* hizi *resource* vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri hapa kwenye jambo lingine kubwa tu. Bodi ya Mikopo ni lazima watoke kwenye boksi walilojifungia, lazima wawe na uwezo wa kukaribisha *private sectors* kwenye uwekezaji wa mikopo kama mabenki. Ni kwa nini tusiwape mabenki angalau *ideas* na vigezo ili wawe na uwezo wa kutusaidia? Ni kwa nini tujifungie kwamba ni Serikali tu, wakati tunaelewa kabisa nchi zinazoendelea zinakwenda zaidi ya hiki ambacho tunachokifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba wote humu tumepewa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Ndiyo maana kuna mwingine

alijaribu kuitoa, tulipopewa ile Ilani ya Chama Cha Mapinduzi hatuwezi kukubali wananchi wetu, wanafunzi ambao wapo kwenye majimbo yetu waendeleo kuteseka kwa kukosa mikopo, sasa mwisho wa yote tutaulizwa haya, Ilani ilitekelezwa hapa utasemaje? Nilijenga tu madarasa halafu nikaacha watoto maelfu wamekaa nyumbani. Wamekaa huku bila kuwasaidia haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naiomba Serikali itoke kwenye boksi ije na kuhakikisha wanafunzi wote ambao wamefanya vizuri wanakwenda. Vilevile kigezo kingine ni zile taaluma ambazo wanakwenda, yaani mtu ambaye anakwenda Udaktari unampa asilimia ishirini, sio hali ya kawaida jamani tuelewe kabisa kuna mabadiliko ya tabia ya nchi, leo mkulima analima, kesho inawezekana asipate mazao. Sasa kama asipopata mtoto wake ameshayumba ulimpa asimilia ishirini. Tunajenga mazingira gani kwa hawa watoto?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwanza nirejee kusema tu, kama Serikali mkakati tunauhitaji na mkakati huo ujadiliwe kwa kina, lakini kama tulivyofanya kwenye sekta nyingine. Tumefanya vizuri tulipoyumba kidogo kwenye mafuta kukawa na mambo mazuri yakaja, tukafanya na maeneo mengine ambayo wameshauri Waheshimiwa Wabunge wengine. Hivyo, nashauri hili kwetu ni dharura kwa sababu simu tunazopokea hapa nina *message* ya bwana mmoja anaitwa bwana Bada katoka kutuma *message* hapa, Mheshimiwa Mbunge unatusaidiaje na kadhalika. Sasa ni maelfu ya watu.

Mheshimiwa Spika, kelele zinakuwa nyingi. Ukikuta Jimbo lina watu karibu laki tano, wazazi na sisi kule ni mafundi wa kuzaa, haya niambieni hizo kelele zinakuwaje? Haiwezekani hivi, ni lazima tuwasaidie watu na ndiyo kutekeleza kwenyewe Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo suala la ilani tuliyopewa kuinada lazima itekelezwe ili huko baadaye pia mambo yaweze kukaa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba ni vizuri hawa watu wa Bodi ya Mikopo wakubali mabadiliko, kuna malalamiko bado yanakuja tu, yaani malalamiko wasijione Miungu watu, wanatakiwa kuwa na *changes*. Utumishi wa sasa hivi ni utumishi wa *service delivery*, kauli nzuri na mambo mengine, unapigiwa simu na mtu amekwama badala umfafanulie vizuri unamwambia kamalize huko huko tumeshawapa maelekezo mpaka vijijini, Mtendaji wa Kijiji anajua taratibu za mikopo kwa undani? Wewe kama umepata fursa ya kutumikia watu watumikie. Kwa hiyo nataka wajirekebishe kwenye masuala yao ya maadili, huko nako wanalalamikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimwa Timotheo Mnzava ajiandae.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra kuhusiana na watoto wetu ambao wanakosa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kama muda wa saa moja tu uliopita nilikuwa naongea na Mheshimiwa Venant wa Jimbo la Igalula. Juzi jumapili nilikuwa natoka Tabora nimepita pale nikasimama, kuna mgahawa fulani nikasimama. Nikakutana na suala kama hili hili ambalo tunajadili hapa, kuna mtoto amefaulu vizuri pale anakwenda Mzumbe. Sasa nilikuwa namsimulia na michango iliyopita pale nami ni mmoja wa waliochanga pamoja ya kwamba nilikuwa *on transit*. Ni mtoto wa kike ambaye na yeye amekosa mkopo na hajui kama atapata mkopo na amefaulu viuzuri sana.

Mheshimiwa Spika, huwa najiuliza kuna ile wanasema unauziwa mbuzi kwenye gunia. Hii Bodi ya Mikopo imekuwa ikitoa takwimu nyingi sana za namna wanavyokopesha wanafunzi mbalimbali. Vilevile tukienda kwenye uhalisia hasa vijijini wanafunzi wengi waliofaulu vizuri wanakosa mikopo hiyo. Sasa sijui huu utoaji wao wanaangalia vigezo gani? Sawa wanasema ufaulu na vitu kama hivyo, lakini hawa wanaofaulu wengi wanakosa mikopo.

Mheshimiwa Spika, hii inakatisha tamaa sana. Tume-*promote* sana watu kusoma, kuna shule mpaka kwenye kata sasa zimekuwa *promoted* watu wanasoma kwenye kata. Watoto wakike na hasa vijijini, vijiji kama vya kule kwetu kanda ya ziwa ambako watoto wengi wa kike walikuwa wanaolewa kabla ya umri wao, kwa sababu walikuwa hawaendi shule. Sasa tumewa-*promote* wasome na kweli wanasoma na wanafaulu kweli, lakini hawapati mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni nini maana yake? Tunaanza kuwajengea tena ile tabia ya kuanza kurudi kulekule ambako sasa wazee watakuwa wanasema sasa hiyo shule yenyewe ina faida gani kwa sababu hata sasa mwanangu ukifaulu uwezi kwenda kokote? Kwa hiyo tunaanza tena kuwakatisha tamaa sisi wenyewe kwa kukosa utaratibu mzuri wa kuwapa mikopo. Hizi takwimu za juzi ambazo tayari sensa inaonyesha akinamama wako wengi zaidi, akinababa tuko wachache. Kwa maana nyingine muda sio mrefu nadhani akinababa watakuwa bidhaa adimu sana, kwa mujibu wa takwimu za sensa.

Mheshimiwa Spika, sasa watoto wa kike hawa ndio watakuwa wengi, ambao tunatakiwa tuwalinde vizuri kwa sababu huko mbele kwa *data* hizi, wapo watoto wa kike ambao watakosa hata kuolewa, lakini sasa wakose hata kazi au wakose elimu? Bora sasa hata wakipata elimu, elimu hiyo

itawasaidia hata kama atakosa mwenza wake huko mbele, lakini ana kazi yake nzuri, huyu mtoto wa kike atakuwa yupo *protected*. Kwa hali hii tunayokwenda nayo sasa hivi si nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia kuna malalamiko na hasa vijijini kwamba wamekuwa wakipewa upendeleo zaidi watu ambao wapo mijini, watoto ambao wapo mijini na ambao pengine ndugu zao wana uwezo ndiyo wamekuwa wakipata mikopo, malalamiko haya yapo. Sasa Bodi ya Mikopo wanapotoa taarifa zao, basi ikiwezekana watupe na za vijijini kwamba vijijini ni watoto wangapi ambao walikuwa wana-*qualify* mikopo, wameweza kupewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivyo kwa sababu malalamiko haya ya kwamba mijini na wale ambao wana uwezo watoto wao ndio wanapewa mikopo, itatusaidia sana kama Bodi ya Mikopo itakuja na *data* za wale wa vijijini, watoto wa mtu masikini kabisa ambao wameweza kupata hiyo mikopo ili tuendeleo kuwa-*promote* watoto wetu waendeleo kujua kwamba wakisoma watapata mikopo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra, kwamba Bodi ya Mikopo iangalie kwamba kweli hicho kinachosemwa ndicho kinachofanyika? Malalamiko ni mengi na yanakatisha tamaa kwamba watoto wengi bado hawafaidiki na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hiyo, ahsante sana (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi. Niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra, kwa namna alivyoiwasilisha hapa Bungeni na kwa namna hili tatizo linavyotukabili sisi wote katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo langu kwenye Jimbo la Vwawa, nimepigiwa simu na watu wa zaidi ya 36 wakilalamika kwamba wamekosa mikopo na wengine walihirisha mwaka jana wakawa na matumaini kwamba mwaka huu watapata, lakini hawajapata na hali ilivyo tatizo ni kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba hili tunalolijadili pengine tunaweza tusipate ufumbuzi kwa leo na tunaweza tusilijadili kadri inavyowezekana, lakini naliona kwamba lazima tuje na majawabu ya muda mfupi na tuje na ya muda mrefu. Sasa kwa muda mfupi nitapendeleo nini kwamba ambacho tunafikiria kwa sasa hivi. Kwa sababu nchi yeyote bila kuwa na maarifa, bila watu wake kuwa na maarifa ya kutosha. Watu bila

kuwa na ujuzi huwezi kujenga uchumi imara na huwezi kuleta maendeleo ndani ya nchi ile.

Mheshimiwa Spika, ndio maana Serikali ya Awamu ya Sita, imeamua kuweka uwekezaji mkubwa kwenye hili eneo. Ukiangalia namna tulivyowekeza kwenye shule za msingi, shule za sekondari, ukiangalia madarasa yanayoendelea kujengwa, vyuo vinavyoendelea kupanuliwa, kwa uwekezaji huu ni kwamba tunataka tuijenge jamii iliyoelimika, yenye ujuzi ambao ni mahiri, itakayoweza kuleta maendeleo ya nchi yetu na ndio tutaweza kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika uwekezaji huu wa shule za msingi na sekondari ni lazima uwiane na namna tunavyowapeleka kwenye vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya kati. Sasa hivi hapa pana changamoto, nafikiri lazima Serikali ituambie tunafanyaje ili tuweze kujinasua hapa. Bodi hii ya Mikopo imekuwepo kwa zaidi ya miaka 17. Ni wazi na mafanikio yapo, lakini zipo changamoto ambazo lazima tuziangalie kwa undani. Tuangalie suala la kibajeti, bajeti iliyo ukiangalia na idadi ya udahili inatosheleza? Lipo suala la muundo wa Bodi namna inavyotekeleza majukumu yake, kama taasisi, je, katika hali tuliyonayo, mazingira ya leo, huu muundo wa bodi unatosheleza? Katika hali tuliyonayo vigezo vinavyotumika katika kuwapatia watoto mikopo au kutowapatia, hivyo vigezo vinatosheleza? Namna tulivyojipanga kugharamia hii mikopo tumejipangaje? Kwa hiyo nafikiri yapo mengi ambayo ni ya msingi ili tuweze kujinasua.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupendekeza kwamba katika hali ya udharura iliyopo Serikali ituambie ina Bajeti ya shilingi ngapi ambazo imepata sasa hivi? Pia Bunge hili kwa sababu ndilo linalopitisha Bajeti, tuangalie kama inawezekana zikatafutwa fedha mahali pengine popote kama tulivyofanya wakati tulipokuwa na *crisis* ya kwenye kilimo, kama tulivyofanya katika maeneo mengine ili tuwekeze kwenye hili eneo angalau tuvuke kwa kipindi hiki, hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la muda mrefu, Wizara ifanye mapitio ya kitaasisi, ya kimuundo na kuangalia je, muundo tulionao huu unakidhi mahitaji ya leo ya sayansi na teknolojia? Naamini kwa kufanya hivyo, najua jitihada zimechukuliwa na Serikali, nimemsikia Waziri ameunda tume, amefanya nini, lakini ya msingi ya dharrla lazima kwanza tuje na Bajeti ya kutatua hili tatizo ndiyo tujipange sasa kwa siku zinazokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile la pili, tufanye mapitio ya sheria iliyopo, je, hii sheria inatosheleza? La tatu, tufanye mabadiliko ya mfumo wa utoaji wa mikopo na la nne tuangalie sasa mipango ya kupata fedha, siyo tu kwa upande wa Serikali bali tushirikishe na wadau wengine kuweza kuongeza fedha katika hili eneo na ikiwezekana badala ya kuitwa Bodi ya Mikopo iwe

ni Mfuko wa Elimu na ikiwa Mfuko wa Elimu, isiwe elimu ya juu tu hata elimu ya kati.

Mheshimiwa Spika, najua kuna tatizo la muda, basi nasema naunga mkono hoja na naamini Serikali itakuja na tamko kwa suala hili la dharura. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, bahati mbaya tu ni kwamba kwenye hoja hii Serikali itakuwa inachangia tu, ila nadhani mawazo yako wameyachukua kwa maana ya kuyafanyia kazi huko baadaye, kwa sababu hoja iliyopo mbele ni ya Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo tusije tukawa tunasubiri majibu kutoka upande wa Waziri.

Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Condester Sichalwe ajiandae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja muhimu sana kwa Taifa letu, lakini pia kwa maisha na mustakabali wa watoto wetu na vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kukiri na kutambua mchango na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali, kuendelea kuongeza Bajeti ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka fedha 2017/2018, mikopo ilikuwa ni billioni 427.5. Mwaka wa fedha uliopita na mwaka wa fedha tuliyonao mikopo ni billioni 570, ni hatua kubwa sana. Pamoja na hayo bado tuna changamoto na changamoto ni hii ambayo imeletwa na hoja na Mheshimiwa Ezra.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana bajeti iliyopita ya 2021 tulikuwa na billioni 570 na kwa takwimu za Bodi wenyewe wanufaika walikuwa ni laki moja elfu sabini na saba na mia nane tisini na mbili. Mwaka huu wa fedha tulionao bajeti ni ileile bilion 570 na matarajio ni wanufaika haohao laki moja sabini na saba mia nane tisini na tatu, anaongezeka mnufaika mmoja.

Mheshimiwa Spika, changamoto tuliyonayo wenzetu Serikalini hasa Bodi na Wizara ya Elimu walipaswa wawe wameiyona. Kilichotokea hapa ni nini? Mwaka jana wanufaika tuliyokuwa nao wanufaika wapya walikuwa ni elfu sabini mia sita na tisa. Wanufaika waliokuwa wakiendelea ni laki moja na elfu saba na miambili na themanini na tatu. Mwaka huu kwa Bajeti hii hii kwa taarifa za Bodi itawalazimu kuwapa wanufaika wanaoendelea laki moja na thelathini na tano mia nane tisini na tatu. Maana yake ni kwamba kwa idadi hile wanufaika wapya wanaoanza mwaka wa kwanza wanashuka kutoka elfu sabini mpaka wanufaika elfu arobaini na mbili. Kuna tofauti ya

wanafunzi wanufaika zaidi ya elfu thelathini ambao tunatarajia hawataweza kupata mikopo kwa Bajeti tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana elfu thelathini ni wengi na ni nguvu kazi kubwa sana kwa nchi yetu. Kama Taifa hatupaswi kukubali hata kidogo vijana hao wakashindwa kunufaika na mikopo hii na kushindwa kupata elimu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kwamba tuna vyanzo viwili tu vya fedha kwa ajili ya vijana wa vyuo vikuu. Kwanza ni pesa inayotoka kwenye Bajeti, pia pili ni marejesho yanayofanyika kutoka na wanufaika huko nyuma. Nishauri, ushauri wa muda mfupi kabisa, Serikali na Mheshimiwa Ezra, nimshauri kwenye maazimio, ni lazima Serikali ituletee mpango wa dharura ya namna ya kuwasaidia hawa vijana zaidi ya elfu thelathini ambao tunaamini kama tukifanya takwimu vizuri sio thelathini wataongezeka kwa sababu udahili unaongezeka na watu wanaongezeka. Serikali ilete mpango wa dharura, ni namna gani vijana hawa ambao tayari vyuo vimefunguliwa, wanakwenda kupata fedha za mikopo ya kuwasaidia kuweza kufanya masomo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili tulikuwa tunataka tushauri, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Hasunga, la kwanza ni lazima Serikali na sisi kama nchi, Wizara na Bodi tufanye tathmini upya ya utaratibu wa utoaji wa mikopo, utendaji kazi wa Bodi ya Mikopo, vigezo na masharti yote katika kuzingatia suala la utoaji wa mikopo. Lazima tufanye tathmini ya kitaifa ya muda mrefu kwamba mfumo huu tulionao unaweza kutufikisha au unakwenda kutukwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ufanyike uchunguzi, itengenezwe tume au kupitia Kamati ya Bunge, ufanyike uchunguzi wa vigezo vinavyotumika kutoa mikopo kwa watoto wetu, kwa sababu malalamiko ni mengi, vigezo vipo lakini kwa uhalisia kwenye macho ya faida ya kibinadamu hatuoni kama vinafanya kazi vizuri. Ufanyike uchunguzi wa kina wa vigezo vilivyotumika kwa miaka mitano mpaka miaka kumi, vigezo vilivyotumika, idadi na aina ya wanufaika walionufaika na mikopo ya elimu ya juu ili tujiridhishe kama Taifa kama tuko kwenye sehemu salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia sehemu nyingine tukafanye uchunguzi wa utaratibu wa urejeshaji wa mikopo hii na kiasi cha kinachorejeshwa, kinachoripotiwa na matumizi yanayotumika kwa ajili ya kutengeneza msingi mzuri kwa huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ezra, jambo hili ni la dharura, lazima twende na mpango wa dharura kama Bunge na kama nchi tuwasaidie vijana wetu. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe na Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami nimesimama kuunga hoja ya Mheshimiwa Eng. Ezra. Kama Taifa ni lazima tuwekeze kwenye elimu, *in a serious way we need to invest in human capital.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama Taifa na sisi ni lazima tuzalishe wataalam wa kuweza kuwauza nje, kama vile tunaona mataifa mengine madaktari wanatoka huko India, sijui China na kwingineko, ma-engineer, kama Taifa lazima tutengeneze wataalam na sisi ambao tunaweza tukawauza nje na ndiyo tunaweza kufikia huo uchumi wa kati ambao tunaufukuzia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli nashangaa sana. Nashangaa kwa nini, tunapata hii *crisis*, kila mwaka unakuta watoto wanaopata hii mikopo ni wachache wengine wanaachwa na Serikali inakuja inaona kabisa, hai-assume inakuwa imesha-project kwamba, kwa bajeti hii ambayo tunaomba pamoja na makusanyo ambayo tutakuwa tumechukua, kama ilivyosema mwaka jana imekusanya asilimia 78 tunao uhakika kulingana na *trend* ya ufaulu wa hawa wanafunzi, kwa sababu lazima mnaangalia *trend*, mwaka jana 2020 *form six* walimaliza hawa, katika hawa waliomaliza walio-qualify kwa mikopo, *let say* walikuwa ni 60%. 2021 *you have that trend*, kwa kufuatana na hiyo *trend* mnakuwa mnajua kabisa 2022 tutaweza kupata wahusika wambao wanaweza wakaomba *in the likeliness* kama asimia hizi na bajeti ambayo tumeomba ni hii.

Mheshimiwa Spika, sasa nikataka nijue Serikali inafanya tafiti ya kina kujua uhitaji halisi wa watoto hawa wa Kitanzania ambao unakuta wengi wao wamesomeshwa kwa shida sana. Kuna wengine wanafanya kuchangishiwa wakati wanaenda shule, unamchangishia akiwa sekondari, *high school*, unachangishiwa na wanakijiji na wengine, wakifika huko wanashindwa kupata mikopo wanabaki mtaani. Mama hawezi ku-afford hata 200,000/= *leave alone* hizo 5,000,000/= alizosema Mheshimiwa Ezra hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikataka nijue Mheshimiwa mwenye hoja, Mheshimiwa Ezra, katika maazimio yake mojawapo, nimesema kuanzia mwanzo, tuwekeze katika elimu tuweze kuwa na vyanzo mbadala. Tuwe na chanzo mbadala kabisa na hiki chanzo tuki-ring fence kama tatizo ni hela hazitoki, kiwe *ring fenced* kama inavyokuwa kwenye REA, tunajua kabisa hii ni kwa ajili ya elimu ya juu, mikopo. Iwekwe kama tunajua itapatikana sehemu gani tutakuwa tunapata kiasi fulani kama ilivyo kwenye REA, ili sasa watoto wetu wote wanaofaulu wanakuwa na sifa waweze Kwenda Chuo Kikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili huko nyuma, mpaka Mheshimiwa Tendega hapa ananiambia na yeye alinufaika, wazazi wetu walivyokuwa wanafika CHUO Kikuu walikuwa wanasomeshwa bure. Kama tunaona hapa tunaacha Watanzania wengi wa kimaskini nje na itakuwa ni motisha, wanaopata daraja la kwanza Serikali si tunawekeza kwenye elimu na ndio maana imewekwa kwenye kasma ya maendeleo, wanaopata daraja la kwanza tuwasomeshe bure, siyo mkopo, hao wengine sasa ndiyo tuwape huo mkopo. Hii itatoa motisha sana *I am telling you*, watafaulu kama nyuma waliweza wazazi wetu wamesoma bure, *why not now?* Tunaweza kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama tunaweza kuwekeza tukatoa fedha tukajenga barabara, tukajenga maji, tuone *human capital* na yenyewe ni *asset*. Ni kitu muhimu sana cha kuweza kuwekeza kwenye Taifa, kama tunavyosema tunawezekeza kwenye barabara, kwenye maji, *human capital* ni kitu muhimu sana kwenye Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa wale wanaopata *division one* wasomeshwe na Serikali, wanaopata *division one* unaweza ukasema hata *division one* ya kufikia *point* fulani ambayo itachagiza sana. *Let say* kama mnataka muweke kwenye sayansi, wanaopata *division one at this point* wanasomeshwa bure, itachagiza sana bila kubagua amesoma *private*, amesoma *public*, sijui amesomeshwa nan anani kwa sababu amefikisha hizo sifa basi aweze kupata huo mkopo, na hao wengine ambao wanafuata sasa ndiyo labda waweze kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, simu ni nyingi, malalamiko ni mengi, Watanzania masikini kabisa watoto wao wamefaulu vizuri na wako nyumbani hawawezi Kwenda shule. Ni kitu ambacho ni cha muhimu sana na cha uharaka kuweza kufanyiwa kazi. Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichelwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuunga hoja iliyopo mezani. Wakati naanza kuchangia mchango wangu naomba nirejee maneno ya Baba wa Taifa, Taifa la Afrika ya Kusini, ambaye ameshawahi kusema hapo, *“Education is a most powerful weapon which, you can use to change the world.”* Akimaanisha kwamba, elimu ndio silaha peke yake ambayo unaweza ukaitumia kuibadilisha dunia. Kwa muktadha wake huu ni nini?

Mheshimiwa Spika, sisi pia Watanzania pamoja na vizazi vyetu na hawa watoto ambao tunatarajia kuwasomesha, tunatarajia ya kwamba

elimu ndio silaha mojawapo ambayo wao wanaweza wakaitumia kuibadilisha jamii yetu, lakini pia kuwa washindani kwenye soko la dunia huko tuliko. Tukiangalia hapa kwenye takwimu za sensa ambazo tumepewa jana pale na Mheshimiwa Rais, Milioni 61 ya Watanzania na hiyo Laki Saba, ukiangalia kwa uhalisia utagundua idadi kubwa ya Watanzania ni Watanzania ambao wana kipato cha kawaida kabisa. Maana yake asilimia kubwa ni wakulima, asilimia kubwa wanafanya shughuli ndogondogo kwa ajili ya kuendesha maisha yao ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto wao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa ikiwa Watanzania hawa ni wa kawaida kabisa ambapo mtoto huyu hapati mkopo kabisa wa Chuo Kikuu, anapata mkopo chini ya kiwango au anaenda inafika hatua ameshadahiliwa kuanza masomo mpaka sasa hivi vyuo vimefunguliwa ni wiki ya pili, watoto bado hawajapata mikopo. Unajiuliza mzazi huyu ambae alikuwa akimsomesha mtoto wake kwa kuungaunga kwenye shule hizi za Kata kwa maisha magumu, sasa hivi ni wiki ya pili, mtoto labda amechaguliwa Dar-es-Salaam anatoka Mwanza Vijijini, mtoto amechaguliwa kwenda kusoma vyuo vilivyoko Mwanza ametoka huko Momba Vijijini, amefika na nini? Atalipia malazi nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wamemtaka atoe hela ya udahili ili aanze masomo. Mtoto huyu ambae Serikali imefuta ada kutoka O-Level mpaka sasa hivi A-Level, mzazi anapata wapi hela ya kumsaidia mtoto huyu kumdahili? Ada ni zaidi ya Milioni Mbili, mzazi ni mkulima wa kawaida ambaye analima magunia mawili au anachoma mahindi barabarani, anafanya usafi Mama ni *house girl*, Baba anaranda, anapata wapi ameachwa kwenye mkopo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninao ushauri katika jambo hili. Kwanza tunaomba Bodi ya Mikopo (HESLB) ivunjwe na ipitiwe tena. Ipo haja ya HESLB inapaswa kuchunguzwa kwanza, yapo malalamishi mengi sana ambayo wanufaika wa mikopo huko nyuma bado wanayalalamikia.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili Tukufu naomba niseme wazi ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mimi ni mnufaika ambaye nilikopeshwa mkopo na kupitia Bunge hili mwezi wa Kumi uliopita nimealiza mkopo wangu. Kwa hiyo, tafsiri yake kile changu ambacho mimi Serikali iliniwezesha, mtoto wa mkulima wa kawaida kutoka Momba, nikasoma na niko hapa na inawezekana isingekuwa mkopo ningekuwa nimeshaolewa saa hizi nina wajukuu hata Wanne kwa hiyo, tafsiri yake inawezekana hata watoto wengine sasa hivi wakikosa mkopo wataingia kwenye mazingira magumu, wataendelea kuteseka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, HESLB ivunjwe, ichunguzwe, ipitiwe upya tena, lakini yale marejesho ambayo watu wengine ambao wanarejesha wanaonekana

wanabambikiziwa yapitiwe tena pia, tuweze kuangalia Je, yale marejesho yanayorejeshwa hayawezi kuwasaidia watoto wapya ambao wanaingia? Je, hiki kiwango ambacho tulikipitisha hapa Bungeni hakiwasaidii watoto wapya ambao wanatakiwa kunufaika na mkopo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine ni kuwa, wako watoto wengi ambao wanafika chuo mwaka wa pili na wa tatu, wanashindwa kufanya mitihani yao kwa kukosa ada. Ninaomba Wizara ifungue dirisha, Wabunge tukiwaletea watoto hawa na sisi wakati mwingine ni binadamu, tunasaidia misiba, tunasaidia wagonjwa, inafika wakati tunashindwa. Mtoto yuko mwaka wa tatu, ameshindwa kufanya mtihani, ameomba mkopo zaidi ya mara tatu ameshindwa, mwaka wa tatu mtoto anaacha masomo?

Mheshimiwa Spika, tu-assume labda wewe mwaka wa tatu ungeachishwa masomo sasa hivi tungekuwa hatuna Spika hapo ulipokaa. Mwaka wa tatu ungeachishwa masomo tungekuwa hatuna Waziri Mkuu hapa ndani. Tunawaomba Bodi ya Mikopo mfungue dirisha, mtoto anapokuwa mwaka wa tatu ameshindwa kufanya mtihani wake kwa ajili ya kukosa ada laki nne, laki tano, tunaomba jamani watoto hawa muwape nafasi waweze kumaliza mitihani yao, waweze kufanya mitihani waende wakahangaika huko barabarani. Tuje hapa tujadili mambo mengine kwamba ajira ni changamoto, lakini kama tunasema *education is the best weapon in the world, let us give them the weapon*, acha tuwape silaha wakapambane huko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunawaomba sana watoto wasiache kufanya mitihani eti kwa sababu amekosa Laki Tano, amekosa Laki Sita. Hata sisi ni Wabunge wakati mwingine tunashindwa, siwezi mtoto afanye...

SPIKA: Ahsante sana dakika zako zimeisha Mheshimiwa.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja iliyoko mezani.

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massey, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntala, halafu tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais ametusaidia sana katika kutuletea fedha za elimu, hasa katika Majimbo yetu, kwenye shule za Msingi, shule za Sekondari na sasa ndiyo hili tatizo linajitokeza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuunga mkono mara moja hoja hii ya Mheshimiwa Ezra. Kwa sisi ambao tunaabudu katika Biblia, maneno ya Mungu yanasema hivi kwenye Mithali 4 Mstari wa 13, "Mkamateni sana elimu

msimuache aende zake, mshike maana yeye ni uzima.” Kama haitoshi Biblia inasema tena kwenye Kitabu cha Hosea, “Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa”. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimenukuu tena kwenye neno...

SPIKA: Sasa ngoja nikusaidie kidogo, ni watu wangu wanaangamizwa, sio wanaangamia, watu wangu wanaangamizwa.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, sawasawa. Kwa kukosa maarifa na maarifa yanaletwa na elimu. Kwenye misahafu, amenisaidia hapa Mheshimiwa Nahodha, Mtume anasema hivi, tafuteni elimu mpaka China. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nimejaribu kuangalia na kwenye Biblia yangu hapa nimefungua neno elimu limeandikwa mara 300 kwa umuhimu wake, neno tu elimu. Nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa, Mheshimiwa Rais wetu cha “Maisha Yangu Malengo yangu au Maisha Yangu Dhamira Yangu” amendika, yeye mwenyewe nanukuu: “Mimi leo ni Rais nisingefika hapa bila elimu” Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nia yangu ni kuonesha jinsi ambavyo elimu imepewa kipaumbele kwenye Biblia na Misahafu pia kwa viongozi wetu wa nchi. Tumeona sisi hapa leo hii, mimi kule Jimboni wanafunzi wengi wa vyuo wamerudi sasa kwa sababu kwa kweli hawana mikopo na hawawezi kuendelea bila mikopo. Ukiangalia bajeti ya mwaka jana, amesema Mbunge mmoja hapa na nimesoma ni zaidi ya Bilioni 427, tena mwaka huu Bilioni 570. Ni lazima sasa Serikali ije na *projection* tunapokwenda kwenye miaka ya bajeti tuhakikishe kwamba tatizo hili halijirudii tena, kwa sababu hili ni bomu na bomu hili linakuja pale ambapo sasa tunaendelea kukatishana tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika familia zetu maskini watu wengi kwa kweli kwa sasa wameshauza mashamba, wameuza ardhi, wamefanya mambo mengi kufikisha watoto katika *level* hii ya *University*. Sasa inapofika mtoto anakosa fedha ya mkopo ili kuendelea na masomo yake, hasa akiwa mwaka wa pili au mwaka wa tatu na kurudi nyumbani, hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, ukiangalia sasa hivi katika zile sifa za kupata mkopo, awe yatima, awe fukara, asiwe na wazazi, haya yote Serikali haina uwezo wa kujua moja kwa moja na kama inao basi maana yake ni kwamba, hali yetu imeshakuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba hii Bodi ya Mikopo ivunjwe mara moja kwa sababu inaonekana sasa haina namna ya kutusaidia, lakini pili utaratibu huu wa kuona namna gani ya kupata mkopo

kutoka mtoto wa fukara au masikini utaratibu huu uangaliwe upya kwa sababu, inaonesha kabisa hali ni mbaya kule kwenye maeneo yetu na wananchi wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, pia tuone tutafute hela ya dharura ili watoto hawa waweze kwenda shule, tusipofanya hivyo tutakuwa tumezalisha watoto ambao baadae hawawezi kuwa viongozi. Kwa mfano, ametoa mfano mtu mmoja hapa, Rais wetu wa Kwanza, Baba wa Taifa, ameenda shule na wakati ule bahati nzuri shule ilikuwa bure na ametoka kwenye familia tunayoijua. Rais wa Pili, Rais wa Tatu, Rais wa Nne na Rais wa Tano, bila ya elimu asingeweza kuwa Rais na huyu wa Sita kaenda sana, unajua leo hii bila elimu kwa nafasi hii ya Urais watoto wetu wale fukara hawawezi kuwa viongozi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Wabunge leo hii tusimame, tuungane kwa jambo hili, Serikali ije na fedha ya dharura kuwasaidia watoto hawa ambao wako nyumbani wanaotakiwa kwenda vyuo sasa. (Makofi)

SPIKA: Haya ahsante sana, muda wako umekwisha.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga hoja hii mkono. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mheshimiwa Prof. Nkenda ajiandae.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami nipongeze hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ezra. Ni kweli kwamba, Serikali kuna sera ya wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo wapate mikopo. Kwanza hiyo ni sera kabisa kwenye elimu, wanastahili kupata mikopo wale wote wanaotimiza vigezo.

Mheshimiwa Spika, niliongea katika Bunge lililopita, nikasema kwamba kama tunashindwa kuwapa wote asilimia 100, basi afadhali wote wapate *flat rate*. Hivi unampa mtoto mkopo wa asilimia 30 wakati mnajua hawa watoto wanatakiwa kufanya *research*, wanatakiwa kulipa hiyo *tuition*, wanatakiwa kula vizuri; asilimia 30 inatosha nini? Nilishauri basi ikiwezekana watoto wote wapate *flat rate* ili idadi kubwa ya wanafunzi waweze kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, na hii ya kuwabagua watoto wengine wasipate mkopo eti kwa sababu wamesoma *private* si haki na si sawa. Kwa sababu mtoto anaposoma sekondari mkataba ni kati ya mzazi na shule, kwa hiyo pale mzazi anahitajika alipe ada, ule ni mkataba wa shule na mzazi. Lakini mtoto anapoingia chuo kikuu ni mkataba kati ya yule mwanafunzi wa chuo

kikuu na chuo au na Serikali. Kwa hiyo hatuna haja ya kuweka ubaguzi, eti amesoma *private* asipate mkopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na watoto wengi walioniletea mimi maombi, eti wananiletea mimi maombi kama mwakilishi, wengi wametoka *private*, hasa huko KCMC aliposema Mheshimiwa Ezra. Wanaomba mikopo; SAUT wanaomba mikopo, Teofilo Kisanji wanakosa mikopo, na mara nyingi wakati wako karibu na mitihani.

Mheshimiwa Spika, hili jambo nimefurahi sana leo limeingia hapa. Umenisaidia sana Mheshimiwa Ezra; *I salute you*. Kwa hiyo tuangalie namna gani sasa tutajipanga, na vigezo vile ambavyo havileti haki viondolewe. Tutafute fedha ili sasa hivi watoto wote hao wapate stahiki zao ili waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, leo tunalalamika kwamba watoto wakimaliza vyuo vikuu hawafanyi kazi nzuri kwenye *field*. Ni kwa sababu sasa hivi watoto hawana hela za kufanya *research*, kwa hiyo hakuna ubunifu. Hawa watoto wana-copy tu vitu. Tunapata watoto wamemaliza vyuo vikuu lakini hawana ubunifu, ni kwa sababu ya hapa.

Mheshimiwa Spika, tuwekeze fedha kama walivyofanya Thailand, wamewekeza fedha kwenye elimu. Thailand ilikuwa ni nchi ya kawaida, maskini, leo Thailand inatupiga, Singapore inatupiga. Wamewekeza fedha kwenye elimu kuanzia *kindergarten*. Kwa hiyo tubadilike tuwekeze fedha kwenye elimu ili iwakomboe watoto wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mheshimiwa Ezra, mtoa hoja, ajiandae kuhitimisha hoja yake.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na Mheshimiwa Ezra Chiwelesa kwa hii hoja aliyoitoa.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Kamati yetu tumeshauri katika bajeti ya mwaka huu na katika bajeti iliyopita. Tumeyaona na tumeyasikia malalamiko ya vijana wanaoomba mikopo kwa ajili ya kujiunga na elimu ya chuo kikuu. Ni kweli kabisa, sisi tumewaita watu wa Bodi ya Mikopo, tumekaa nao, tumeongea nao, tumeangalia vigezo wanavyovitumia katika kutoa mikopo. Inachanganya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wanasema wanatoa mikopo kwa watoto waliofaulu vizuri, sawa, tunakubaliana nayo. Lakini wanatoa mikopo kwa

watoto ambao wazazi wamefariki, yaani Watoto yatima. Kuna watu wengine wamepata mikopo wazazi wapo, kuna watoto wengine ni yatima hawapati mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kibaya asilimia 62 ya mikopo iliyotoka wamekwenda kuwakopesha vijana wanaosoma masomo ya *arts*. Ukiwapa watoto wanaosoma masomo ya *arts* wanapofaulu wengi wamekwenda mtaani kutafuta kazi hawana ajira. Kwa hiyo unakuta watoto asilimia 62 hawana ajira, maana yake ni nini, hawarudishi mikopo. Asilimia iliyobaki ni kama 20, wamewapa watoto wanaosoma masomo ya sayansi, asilimia tano ni wale ambao hawakuomba mkopo.

Mheshimiwa Spika, tumeshauri hivi, na mimi nilizungumza humu kwa niaba ya Kamati, kwamba watueleze ni shilingi ngapi inahitajika kwa mwaka kuwapa mikopo wanafunzi wote Tanzania wanaostahili kuingia chuo kikuu. Wakatuambia fedha wanayopata ni bilioni 570, lakini wakipata bilioni 800 watatoa mikopo kwa wanafunzi wote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukaomba Serikali itafute hiyo bilioni 800, mtu yeyote anayehitaji kuingia chuo kikuu ana shida ya kifedha, *no matter* ni mtoto yatima au ana wazazi, kwa sababu kuna wazazi wengine hawana uwezo, wapewe mikopo watu wote waingie chuo kikuu wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu iende kutolewa, kwamba mzazi mwenye uwezo kumkopesha mtoto wako kuingia kuchukua mikopo, kumbuka kwamba akiingia kazini atakuwa na jukumu la kulipa mkopo ule. Kama hiyo elimu ikitolewa mzazi kwenda kuchukua mkopo iwe ni *last resort*, kwamba umekwama ndipo mtoto wako umuingize akachukue mkopo kwa sababu ule mkopo siyo wa mzazi, mkopo ni wa mtoto ambaye akishaingia kazini atastahili aulipe.

Mheshimiwa Spika, na la mwisho tukasema kwamba Bodi ya Mikopo kwa sababu ilianzishwa kwa ajili ya kusaidia wanafunzi kwenda kusoma ibadilishwe iwe *commercial*, wawe na utaratibu na mfumo mzuri wa kufuatilia ulipaji wa mikopo. Kwa sababu unafika sehemu wanakwama kukusanya madeni kwa hiyo wawe na utaratibu mzuri, ianzishwe kama ni benki ambayo itasaidiwa na Serikali kupewa ruzuku ili iweze kutoa mikopo kwa wanafunzi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naungana na Mheshimiwa Ezra. Hali ni mbaya, inabidi Serikali iliangalie hili na mrudi kwenye maoni ya Kamati muweze kuhakikisha tunatafuta hiyo fedha. Kama ni Bunge kupitisha tutafute hiyo fedha ili wanafunzi wote Tanzania wapewe mikopo waende wakasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, halafu mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kujadili hoja muhimu ya Mheshimiwa Engineer Ezra Chiwelesa ambayo kimsingi ina mambo makuu matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, mikopo inayotolewa inatoshia? Watu wanalalamika kwamba mikopo haitoshi, kuna watu wanashindwa kupata mkopo. La pili, mikopo hii, hata kama haitoshi, inatolewa kwa haki? Kwamba watu ambao kwa vigezo vilivyowekwa walitakiwa wapewe mikopo, wanapewa hiyo mikopo? Wako watu ambao hawakidhi hivyo vigezo wanapewa na ambao wanakidhi wanakosa mikopo? La tatu; Serikali ina mpango na mkakati gani?

Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kujadili hoja hii kwa kutoa maelezo kadhaa. La kwanza, tuanze na ugawaji wa mikopo kwa haki. Na Mheshimiwa Eng. Ezra ameeleza na ametoa mfano wa mtu ambaye ukimuangalia kabisa na wazazi wake inaonekana kwa vigezo hivi angetakiwa kupata mkopo lakini hakupata.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo imeweka vigezo na viko wazi, viko kwenye tovuti vya nani anaweza akapata mkopo kwa hali ya kiifamilia, aina ya masomo unayosoma na kuna *clusters* za masomo; la kwanza, la pili, la tatu. Viko wazi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajadili bajeti ya elimu hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge kadhaa walitaka Serikali ipitie kuhakiki kwamba tunapogawa hii mikopo vile vigezo ambavyo tumewaambia waombaji wa mikopo kweli tunavizingatia. Na kulikuwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa wanasema tunafahamu watu wengine ni yatima na vigezo vinasema kama wewe ni yatima utapata mkopo labda asilimia mia moja usome. Je, linafanyika hilo?

Mheshimiwa Spika, kwenye hilo nimeunda kamati ya watu makini kwelikweli, wataalam wa mifumo wanaoweza wakaingia kwenye kompyuta, huwadanganyi chochote, kutoka *Mzumbe University, University of Dar es Salaam* na kutoka Zanzibar kukagua, moja tu, vigezo hivyo *whether* ni vizuri au vibaya, vipo; tunavifuata?

Mheshimiwa Spika, mimi nilichogundua baada ya kuunda hii kamati, *resistance* ambayo ilikuwepo ya kuzuia isifanye kazi imenishawishi kwamba huenda kuna madudu makubwa sana katika bodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na mbinu mbalimbali zinatumika kuvujisha *information*, kutoa barua kwenye mitandao, kumtumia Kigogo, kuzunguka kuchafua, kuweka ukabila na vitu kama hivyo. Na hiyo kwa hakika inaonesha kwamba huu ukaguzi ni muhimu, unafanyika, utakamilika, na utafanyika kwa muda mfupi sana kwa sababu wanaingia kwenye mfumo, watacheki tutajua nini kinaendelea. Hicho Waheshimiwa Wabunge, tutawaletea taarifa. La pili; mkopo unatoshia? Kwa sababu hata kama vigezo hivyo kweli vikifuatwa, unatoshia? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie historia ya mikopo; tulianza, na nadhani Mheshimiwa Mnzava ametoa takwimu vizuri sana. Tulianza wakati fulani mwaka wa kwanza tunadahili wanafunzi 34,000. Kwa kila tunapongeza bajeti ya mikopo tunaongeza uwezo wa kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Na nitaeleza baadaye changamoto ya sasa hivi imetokana na nini na hatua gani tunazichukua.

Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa ambacho kimefanywa na Serikali, na kwa kweli hii ni *credit* kwa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa sababu alivyoingia madarakani mnakumbuka, kwa sababu bajeti inapitishwa humuhumu Bungeni, alikuta mikopo ya elimu ya juu ikiwa ni bilioni 464 na akafanya maamuzi matatu. kwanza iongezwe kutoka 464 kwenda 570, na ni nyongeza kubwa sana kwa mkupuo. Pili, akaondoa zile tozo, kuna moja ilikuwa asilimia 10 na nyingine asilimia sita, kuna *retention* na nyingine kama hujawahi kurudisha unakuwa *punished*. Kwa hiyo hivyo vyote vilikuwa vinasababisha mzigo kwa wanafunzi kurudisha mkopo kuwa mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa maamuzi hayo tumerahisisha mzigo kwa waliochukua mikopo ili waweze kurudisha, lakini vilevile udahili uliongezeka, nafikiri wanafunzi 70 kwa mwaka wa kwanza, kwa mara ya kwanza katika historia tangu tuanze Bodi ya Mikopo. Huo ni umamuzi uliofanyika baada ya Mheshimiwa Rais kuingia madarakani, ile bajeti ya kwanza ilisomwa hapa na mtangulizi wangu, Mheshimiwa Prof. Ndalichako, ndivyo tulivyokwenda huko.

Mheshimiwa Spika, sasa kabla sijaeleza chimbuko la changamoto hii tuliyonayo sasa hivi nieleze na hatua nyingine ambazo zinachukuliwa. Ukiacha mkopo kwamba bajeti sasa hivi imeongezwa kutoka bilioni 464 iliyopitishwa na Bunge kwenda bilioni 570, ilipitishwa na Bunge bajeti iliyopita na mwaka huu ilipitishwa kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, hatua za ziada ambazo zimechukuliwa, kabla sijaenda kwenye changamoto, ni pamoja na kwa mara ya kwanza Serikali kuanza kutoa *scholarship*, yaani kusomesha wanafunzi bila mkopo, unasomeshwa moja kwa moja. Na hii ilipitishwa na Bunge lako Tukufu, na Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tulivyoleta *proposal* hiyo kuanzisha kuhimiza watoto wanaotaka kusoma *science* na wanaofaulu vizuri sana, wao wapewe *scholarship*, wasomeshwe kama tulivyosoma sisi wengine moja kwa moja mpaka wamalize. Na wadau wengi wakasema hii iitwe *Samia Scholarship*.

Mheshimiwa Spika, tulipewa mapendekezo mengi sana, sisi tumeamua tu sasa inaitwa *Samia Scholarship*. Kuna wanafunzi 640, kwa kufaulu, na ufaulu huo ni wa wazi, hakuna upendeleo. Unaonekana kuanzia wa kwanza mpaka wa 640. Kama umefaulu vizuri kwenye *science* kama tulivyosema hapa Bungeni na ukaamua kwenda kusoma *science*, ama *engineering* au tiba, utasomeshwa na Serikali moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Serikali ime-engage *private sector* kuhakikisha kwamba tunaongeza fursa za mikopo. Kwa mfano *NMB*, na tulisema wakati tunasema bajeti hapa, tukawapongeza. Tumeongea nao, wametenga bilioni 200 kwa ajili ya mikopo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo inakuwa na masharti yake tofauti kidogo na Bodi ya Mikopo. Kwa sababu anayeweza kupata huo mkopo ni mtu ambaye ana miamala inayopita kwenye *NMB*. Kwa hiyo hilo tumelifanya, bilioni 200 ina *interest rate* ya asilimia tisa, lakini ni mzazi ambaye anapokea mshahara kwenye *NMB* kumsomesha mwanao au wewe mwenyewe unataka kwenda kusoma unaweza ukaitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na tuna-engage *private sector* kwa ajili ya kutoa mikopo. *Vodacom* kwa mfano, sasa hivi wanatoa *scholarships*, siyo mikopo, wanatoa *scholarships* moja kwa moja na tunaendelea ku-engage wadau mbalimbali. Na sisi tunapambana kuhakikisha kwamba tunarudisha fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo sasa hivi; baada ya mchakato wa bajeti, maana yake bajeti hiyo ni moja ya Serikali. Humu ndani vuta nikuvute, *budget ceiling* ikoje, inaongezwa au haiongezwi, mkimaliza tunakuja humu. Bajeti ya mikopo ilikuwa ni bilioni 550, ilikuwa ni ileile ambayo iliongezwa *with a big jump* kutoka 464 kwenda 570. Sasa kwa ku-maintain *constant budget* ile maana yake ni kwamba wale wanafunzi ambao udahili uliongezeka wakaingia mwaka wa kwanza, wanakwenda mwaka wa pili wanastahili kupata mikopo. Bila kuongeza hizo bilioni 570 zikaongezeka zaidi, udahili wa mwaka wa kwanza hauwezi kuwa sawa na wale ambao tulikuwa na wanafunzi 70 kwa hiyo *momentum* ile itakuwa *maintained* tu endapo bajeti ingekuwa zaidi ya bilioni 570.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tayari tuna-engage na Hazina na tumezungumza sana na Waziri wa Fedha kuangalia kwamba udahili huu ambao kwa mwaka wa kwanza ume-drop lakini mwaka wa pili

umeongezeka sana kwa sababu wale wa mwaka wa kwanza wameendelea na mwaka wa pili, idadi ya wanafunzi wanaopata mkopo mwaka wa pili sasa hivi ni kubwa kuliko ambavyo imewahi kutokea. Sasa kwa sababu wamechukua zile fedha wanaoingia mwaka wa kwanza idadi imepungua. Tuna-engage na Wizara ya Fedha, tuna mazungumzo naona yanakwenda vizuri kuangalia namna ya ku-rescue hii *situation*, kwamba *at least* ile *status quo* ya vigezo vilivyotumika wakati ule tuhakikishe kwamba tunaweza tuka-retain wale wanafunzi wakaendelea kupata mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mapendekezo hapa ni ya muda mfupi kama hili nililosema. Lakini kuna mapendekezo ya muda mrefu. Moja wapo ni kupitia upya Bodi ya Mikopo, lingine ni ku-engage zaidi *private sector* na la mwisho ni kuona tunaangaliaje mambo ya kibajeti; haya yote ni ya kwetu. Kwa sababu hata bajeti hii ya 570 tulileta hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge mkaturidhia, tukashukuru, tukasonga mbele. *Crisis* tumeiona wote, tunazungumza tunaamini baadaye tutajua cha kufanya kwenye *short term* na *long term* lazima tutakuja na mkakati kama ambavyo imependekezwa hapa kuhakikisha kwamba tunajaribu kuipunguza hii changamoto kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa muda wako. (Makofi)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Waziri nakushukuru. Nilisita kukukatisha, nilitaka umalizie mtiririko wako. Nisaidie jambo moja tu; katika hizi *Samia Scholarship* ambazo umesema ni watoto ambao wanakuwa na ufaulu mzuri kwenye masomo ya sayansi, kwa hiyo wanaokwenda kusoma udaktari ama tiba ni miongoni mwao. Huyu aliyesomwa hapa amekosaje hiyo *Samia Scholarship*? Hebu tusaidie au ile 1.7 haijafikia vile vigezo vya kupata hiyo *Samia Scholarship*?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza udaktari uko kwenye *cluster* ya kwanza ya watu wanapewa upendeleo kwenye mikopo. Lakini ili uweze kupata *scholarship* tunaangalia waliofaulu vizuri kuanzia wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano, bajeti yetu imeisha tulivyofikia 640. Wako wenye *first class* lakini wako chini ya 640. Na ninapenda kusema waliopewa *scholarship* ni nje kabisa ya hawa wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, lakini nitapenda kupata hizo *details* kwa sababu ndiyo maana tumeamua kui-audit Bodi ya Mikopo. Na inashangaza kupata *resistance* kwenye taasisi ya Serikali kama hii, kwamba usiguse mkopo, unahangaika, umeajiri watu wako, ndugu zako, na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hao wanaosoma udaktari kama alivyosema Mheshimiwa Eng. Ezra pale, kwa alivyofaulu nitapenda kwenda

1 NOVEMBA, 2022

kuangalia. Ni sehemu ya ukaguzi ambao tutauhakiki kuhakikisha kwamba kweli watu wanapata mkopo kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kawaida napaswa nimpe sasa mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake.

Kwa maelezo ya Waziri hapa ukiacha mengine yote aliyoyasema, hoja ya Bodi ya Mikopo kwamba inaweza ikamgomea kufanya kazi Waziri, hilo ni jambo zito. Na kwa sababu limesemwa humu Bungeni nitalitolea maelekezo muda mfupi baada ya kuhitimisha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, uhitimishe hoja yako.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kukubali hoja hii iwasilishwe hapa.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Wamechangia jumla ya wachangiaji 16, nadhani sitaweza kuwataja kwa majina kwa sababu ya muda, lakini niwashukuru sana kwa sababu mmeleza kwa kina, Watanzania wamesikia kwa sababu Bunge hili ni la Watanzania na hii ndiyo sehemu yao wanapoweza kusikiliza maoni yenu kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata wale ambao wamekosa mikopo wamesikia, kwa hiyo sina haja ya kuyarudia yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeongea kwa sababu ni dhahiri yameeleweka, kila mmoja ameyasikia. Ila sasa kwa sababu ya ku-save muda mimi ninaomba niende kwenye maazimio, kwa sababu tumesikia mengi hapa. Nina maazimio matatu ambayo nataka kuyawasilisha kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, kwa sababu tayari vyuo vimeshafunguliwa na watoto hawa wako majumbani wanahangaika, hawakupenda wawe nyumbani leo, ni kwa sababu wamekosa mikopo, tunaomba Serikali itoe tamko hapa la kuruhusu watoto hawa warudi vyuoni wakaungane na wenzao kipindi inatafutwa *solution* ili wasichelewe masomo kwa makosa ambayo siyo ya kwao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tupitische kama azimio ili wanafunzi hao, wale ambao wana vigezo na vinajulikana, lakini hawapo vyuoni kwa sababu pesa haijapatikana, kwa hiyo, Serikali itoe tamko na kama Bunge tuazimie ili sasa watoto hawa warudi shuleni, wakaungane na wenzao wakati *solution* inatafutwa.

Mheshimiwa Spika, azimio la pili,...

SPIKA: Kabla hujaenda kwenye azimio la pili; kwenye hilo la kwanza, ili Bunge lijue linahojiwa nini, kama umeliandika hebu ulisome maana umeenda na maelezo mengine ya ziada, kwa hiyo, hatutajua tunaazimia kwenye kitu gani? Kama unayo sentensi ya kuisema moja, mbili, tatu ili Bunge linapohojiwa, basi lijue linahojiwa nini? Kama unalo, lisome; kama huna, basi itabidi uandike.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, Azimio la kwanza; Kwa kuwa vyyo vimefunguliwa na baadhi ya watoto wameripoti vyyoni;

Na kwa kuwa wanafunzi hao wanavyo vigezo lakini wamekosa mikopo;

Hivyo Basi, waruhusiwe kuripoti vyyoni huku Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo wakitafuta fedha za haraka ili kukidhi uhitaji wa watoto hao. *(Makofi)*

SPIKA: Endelea na la pili.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, Azimio la pili; Kwa kuwa inaonekana shida kubwa hapa ni fedha;

Hivyo basi, Serikali ilete *budget review* hapa ili tuweze kujadili na hatimaye watoto hao ambao wamekosa fedha tuweze kupitisha kama Bunge ili fedha hiyo ipatikane kwa ajili ya kufanya nyongeza ya bajeti. *(Makofi)*

Sasa sijui ina....

SPIKA: Endelea tu, mimi nakusikiliza.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, Azimio la tatu; Kwa kuwa kutokana na michango ya Wabunge na hali iliyoko huko nje, malalamiko mengi yanailenga Bodi;

Na kwa kuwa tumeshindwa kupata majibu kwa muda mrefu;

Hivyo Basi, iundwe Tume Maalum ya Kibunge, ambacho ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi, ikapitie maoni ya Wabunge wote ambayo wameyataja hapa, pia iende Bodi ikachunguze nini kinaendelea huko kwa sababu inaonekana Serikali imeshindwa kuichunguza Bodi na hatimaye irudishe majibu ndani ya Bunge ili tuweze kufanya maamuzi kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ni hayo matatu.

SPIKA: Sawa. Azimio la kwanza na la tatu nimeyapata vizuri, hebu rejea la pili.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, la pili; Kwa kuwa inaonekana shida kubwa ni bajeti (fedha) ndiyo imefanya watoto wengi wasipate mikopo;

Hivyo Basi, Serikali ilete *budget review* ili kama Bunge tupitie na kutoa mapendekezo hatimaye tuweze ku-approve nyongeza ya bajeti kwa ajili ya *Loan Board* ili waweze kukopesha watoto wengi hao waliobaki huko bila fedha. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hilo ni la tatu. Ulisema yapo matatu?

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, ni matatu tu.

SPIKA: Haya hitimisha.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali maazimio haya kwa ajili ya kuyapitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Sasa kabla sijawahoji, azimio la kwanza la Mheshimiwa Ezra linahusu watoto wetu kuendelea ama kupokelewa vyuoni wakati Serikali inajipanga kutafuta pesa kwa ajili yao kwa sababu masomo yameshaanza. Azimio la pili linahusu mapitio ya bajeti; na azimio la tatu linahusu kuunda Tume kwa ajili ya kwenda kuichunguza Bodi ya Mikopo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mapitio ya bajeti, kwa mujibu wa utaratibu wetu ni mpaka nusu mwaka iwe imepita. Kwa hiyo, hili azimio la pili lililopendekezwa sitaweza kuwahoji Wabunge kwa sababu mapitio ni ya baadaye, hatutaweza kuyapitia kwenye Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, azimio la tatu linalohusu kuunda Tume kwa ajili ya kwenda kuchunguza; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Kamati inaendelea na kazi na Kamati zitaleta taarifa mwakani kwenye Bunge letu la Januari/Februari. Kwa hiyo, nadhani tuipe nafasi Kamati utakapofika wakati huo tutaona kama kuna

sababu ya kuunda hiyo tume au hapana kwa upande wa Bunge ili kwenda kufanya huo uchunguzi.

Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji kwenye hili la kwanza halafu nitoe maelekezo mahususi kuhusu hili la Tume ambalo halina uhusiano na maazimio. Sasa azimio nitakalokuwa nalihoji Bunge ni kuhusu wanafunzi kupokelewa vyuoni wakati Serikali ikijipanga. Natazama kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wakati akitoa maelezo yake hapa, amesema kwamba wapo kwenye mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango na yale mazungumzo yao yanaonekana yanaelekea sehemu nzuri, kama nimeelewa vizuri. Mheshimiwa Waziri, ndivyo?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nitoe *extra information* kwamba udahili ni kitu kimoja na mikopo ni kitu kingine. Kwa hiyo, wanafunzi wakidahiliwa, wengine hawana mikopo wanaenda na mwenye mkopo anaenda. Kwa hiyo, ni vizuri tuliangalie hilo tu.

Mheshimiwa Spika, hilo uliloniuliza ni kweli tume-engage *intensively* na Wizara ya Fedha na wote tunaona *gravity of situation*. Nashukuru. (Makofi)

SPIKA: Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, ili hoja yetu iende vizuri, kwa sababu tukishapitisha azimio hapa, Serikali itapaswa kulitekeleza. Ni lazima tuliweke kwa namna ambayo linatekelezeka.

Wako wanafunzi ambao wamedahiliwa vyuoni lakini hawana vigezo vya kupata mkopo hata kama pesa zingekuwepo. Sasa tunataka azimio letu lishughulike na wale wenye vigezo vya kupata mikopo ambao hawajapata mkopo. Kwa hiyo, lazima tuwe tumeelewana vizuri tusije tukapeleka ujumbe ambao kidogo utakuwa mtihani kuutekeleza. (Makofi)

Wanafunzi ambao wamedahiliwa wenye vigezo vya kupata mikopo ambao hawajapata mkopo ndiyo azimio hili la Bunge litakuwa linawahusu. (Makofi)

Kwa hiyo, kwa namna ile ile alivyoisoma Mheshimiwa Eng. Ezra, lakini kwa marekebicho haya ambayo yanahusu kundi hili maalum la wanafunzi, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kwa sababu nami sijapata fursa ya kuliandika, lakini nafikiri litakuwa linafanana kwamba wanafunzi wote wenye vigezo vya kupata mikopo ambao hawajapata mikopo mpaka sasa, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwawezesha wanafunzi hawa kupokelewa vyuoni ili waendelea na masomo yao wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya wanafunzi hao. (Makofi)

1 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Mhe. Eng. Ezra J. Chiwelesa la kuruhusu wanafunzi wote wenye vigezo vya kupata mikopo ambao hawajapata mpaka sasa, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwawezesha kupokelewa wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya wanafunzi hao, lilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa hoja hii ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Engineer Ezra Chiwelesa. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri mko hapa, tunashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pia yupo hapa, kama upande wa Serikali, Bunge limeazimia hivyo. Kwa hiyo, ninyi mkatafute namna ya kufanya mawasiliano na vyo binafsi na vya Serikali ambapo wale wanafunzi wanaostahili kupata mikopo na ambao hawajapata na pengine wasingeweza kupokelewa, kwa kuwa wenzao wameshaanza masomo na haya mazungumzo yanayoendelea, tunaamini yatazaa matunda mazuri, hawa wanafunzi watakuwa wameachwa nyuma sana. Kwa hiyo, kwa azimio hili la Bunge mwangalie namna mtakavyoweka hayo mawasiliano ili hao wanafunzi nao wapokelewe vyuoni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya yaliyosemwa hapa kuhusu Bodi ya Mikopo ukiacha ambayo Waheshimiwa Wabunge mmechangia na ambayo kwa kweli mimi ningerejesha kwenye Kamati ya Bunge kwamba walitazame jambo hilo, na kwamba wangeweza kuja kutoa mawazo baadaye wakati wakitoa taarifa, lakini sasa kwa kumsikia Mheshimiwa Waziri, inaonekana kana kwamba kuna mtu mahali au kuna watu mahali wanakataa kufuata maelekezo yanayotolewa ambayo ni ya msingi. Kwa sababu huenda hata hizi changamoto kama alivyosema Waziri na Wabunge wengine mmeonesha hapa kwamba pesa ambazo Bunge lilipitisha hazitoshelezi. Pamoja na kwamba taarifa aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Waziri wakati huo na ameitoa tena leo, kwamba kuna mikopo inayotoka Benki ya NMB, lakini inaonekana yapo masharti ambayo wapo wengine hawataweza kuyatimiza, kwa sababu mikopo hiyo kama nimeelewa vizuri ni kwamba inataka huyo mlipaji awe anatumia Benki ya NMB. Kwa hiyo, kama hatumii na ni mwanafunzi na kama ni yatima, sijajua ni mazingira gani atakuwa anatumia halafu aweze kulipa ndani ya muda gani. Sijasoma vizuri masharti, kwa hiyo, hali inaweza kuwa siyo nzuri.

Kwa hiyo, inawezekana changamoto ni nyingine lakini kwa hili la kuonesha pengine kiburi Fulani, ndilo linalonipa changamoto. Sasa kwa kuwa Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iko hapa, hii bodi ambayo tunazungumza mambo yake hapa, nafahamu kipindi hiki kwa sababu kuna changamoto za hawa ambao hawajapata mikopo, Mheshimiwa Waziri naamini hawakusikilizi kwa mengine, lakini kwenye haya watakusikiliza. Wao

1 NOVEMBA, 2022

wataitwa kwenye Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Kwa kuwa leo ni Jumanne na nafahamu watakuwa kwenye kipindi cha kuwasikiliza hao wanafunzi, Siku ya Ijumaa saa 7.00 mchana wawe kwenye hiyo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Halafu tutatoa fursa, Kamati ikishasikiliza, tujue ni kiburi au kitu kingine tofauti, kwa ngazi hii; lakini kwa maana ya kuichunguza; yale ya vigezo, kama inatoa mikopo sawa sawa, hizo siyo hoja ambazo wanaitiwa mbele ya kamati. Sasa hivi tunataka kuelewa kama Bunge, kwa nini hiyo Bodi ya Mikopo haisikilizi maelekezo?

Yale mambo mengine ya hoja za vigezo tutaifanya baadae kamati itakapotuletea taarifa yake kwenye Bunge la Januari/Februari. Hilo tutalifanya kwa wakati huo kama tutakuwa na sababu ya kuunda Tume, lakini sasa hivi nataka tu kuelewa kama hicho ni kiburi au ni jambo lingine. Kamati itatuambia vizuri na wiki ijayao Waheshimiwa Wabunge mtapewa taarifa kuhusu jambo hili, kamati ikiwa imeshawasikiliza hawa wa bodi.

Kwa hiyo, hayo ndiyo maelekezo mahususi kuhusu Bodi ya Mikopo, na hoja ya Mheshimiwa Eng. Ezra tumeshaimaliza na Bunge limeshaazimia wanafunzi ambao wanaostahili kupata mikopo ambao hawajapata mikopo, basi kwenye vyo vya Serikali na vyo binafsi, Serikali ifanye mawasiliano huko ili fedha wanazozitafuta zitapelekwa huko, lakini kwa sasa na wao waendeleo na masomo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba yetu baada ya kumaliza jambo lililokuwa mbele yetu.

Sasa nimwite Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (The Tanzania Investment Bill, 2022)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara ili aje awasilishe hoja yake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, UWEKEZAJI NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (*The Tanzania Investment Bill, 2022*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu toka niteuliwe kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuniamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mmekuwa mkinipa kwa nafasi mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akinipa nimsaidie. Ninawaomba sana mwendeleo kunipa ushirikiano huo ili nimsaidie vyema Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu vyema na kwa umahiri mkubwa. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamo wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanazofanya katika kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita kwa weledi na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba, kutunga sheria, kusimamia Serikali na kwa kutetetea na kutumikia wananchi kwa umahiri majimboni kwenu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa uteuzi wako kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia Kanda ya Afrika la Umoja wa Mabunge Duniani (*Chairperson of The African Geo-Political Group of Inter-Parliamentary Union (IPU)*).

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza pia Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watumishi wote wa Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi zao ikiwemo

kushiriki katika mchakato wa kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini, kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioalikwa na kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia ushauri wa kamati na imeleta jedwali la marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu, ambao pamoja na mambo mengine ni kumwongeza Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Nje kuwa Mjumbe wa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji Rasilimali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2020, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (*The Tanzania Investment Bill, 2022*) kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (*The Tanzania Investment Bill 2022*) unaopendekezwa ni kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2022 na kufutwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 1997. Lengo la Muswada huu ni kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini na kuboresha utekelezaji na utendaji katika kushughulikia masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ya Muswada huu inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Muswada, utaratibu wa kuainisha tarehe za kuanza kutumika kwa sheria inayopendekezwa Kutungwa, maelezo kuhusu matumizi ya sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya misamiati iliyotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya muswada yenye vifungu vya 4-17 inaweka mfumo wa kitaasisi wa usimamizi na uratibu wa uwekezaji nchini. Sehemu hii inaweka masharti yanayohusu kuendelea kuwepo kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambacho miongoni mwa masuala mengine, kitakuwa ndicho kituo kikuu cha Serikali cha uratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji nchini na kuishauri Serikali kuhusu Sera ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii pia inaweka masharti ya kuendelea kuwepo kwa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji itakayokuwa na jukumu la kutoa mwongozo na mwelekeo wa nchi katika masuala ya uwekezaji. Katika Sheria inayopendekezwa, Kamati hiyo itandelea kuwa ndio mamlaka itakayoidhinisha utolewaji wa vivutio mbalimbali kwa miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na kituo.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu hii inapendekeza pia kuweka masharti yatakayokiwezesha kituo kuanzisha mfumo unganishi wa kielektroniki. Mfumo huu unatusudia kuunganisha Mamlaka muhimu za Serikali zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uwekezaji. Hatua hiyo itatoa fursa kwa wawekezaji kupata huduma kwa urahisi. Masharti mengine katika sehemu hii ni pamoja na uanzishwaji wa Bodi, muundo na majukumu yake, vyanzo vya fedha vya kituo na utaratibu wa utunzaji na ukaguzi wa hesabu zake.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya muswada yenye vifungu kuanzia 18 hadi 24, inaweka masharti mbalimbali kuhusu uwekezaji. Katika sehemu hii masharti yanawekwa kwa ajili ya kuzitaka Taasisi za Serikali kushirikiana na Kituo katika kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji kupitia kituo huduma za mahali pamoja. Vilevile sehemu hii inaweka utaratibu wa maombi ya cheti cha vivutio, muda wa uhai wa cheti hicho cha vivutio anachoweza kupata mwekezaji. Muswada huu unapendekeza cheti cha vivutio kuwa na uhai wa kipindi cha miaka mitano kwa vivutio vya kifedha na kuendelea kuwa hai kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi kwa vivutio visivyo vya kifedha.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii pia inaainisha sifa za uwekezaji utakaostahili kupata vivutio. Miongoni mwa sifa hizo ni:-

- (i) Kiwango cha mtaji wa uwekezaji;
- (ii) Uwezo wa kuzalisha ajira za ndani; na
- (iii) Uwezo wa kuzalisha mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, aidha sehemu hii pia inabainisha kuwa vivutio vinavyosimamiwa chini ya sheria nyingine yoyote vitatolewa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya muswada yenye vifungu kuanzia 25 hadi 31, inaainisha haki na wajibu wa Serikali na wawekezaji. Muswada unapendekeza kuipa Serikali haki ya kusimamia shughuli za uwekezaji ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya sera na sheria ya nchi. Wajibu unaopendekezwa kwa mwekezaji katika sheria hii ni pamoja na

kutii sheria za nchi pamoja na kuendesha shughuli zake kwa namna inayolinda walaji, mazingira, usawa wa kijinsia na kutoa taarifa kwa mamlaka mbalimbali za Serikali pindi zinapohitajika. Sehemu hii inapendekeza kutoa haki kwa mwekezaji katika kipindi cha kutekeleza mradi. Haki hizo zinajumuisha:-

- (i) Kutobadilisha vivutio kwa namna itakayoathiri uwekezaji;
- (ii) Kuhamasisha faida, mapato na gawio kupitia benki yoyote pasipo kuweka masharti;
- (iii) Kutotaifisha kwa miradi ya uwekezaji bila fidia stahiki kwa mujibu wa sheria; na
- (iv) Kupata mikopo katika benki na taasisi za kifedha zilizosajiliwa ndani ya nchi kwa ajili ya kufadhili miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada yenye vifungu kuanzia 32 hadi 37, inahusu masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayohusiana na masuala ya uwekezaji, adhabu zake, pamoja na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria inayopendekezwa. Sehemu hii pia inajumuisha masharti kuhusu rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi uliotolewa na utaratibu wa ushughulikiaji wa migogoro baina ya wawekezaji na kituo au Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu hii pia inapendekeza kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 pamoja na kuweka masharti ya mpito kwa ajili ya masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na sheria inayopendekezwa kufutwa. Miongoni mwa masharti hayo ni kuendelea kutambuliwa kwa vivutio vilivyotolewa na mikataba iliyoingiwa na wawekezaji nchini ya sheria inayopendekezwa kufutwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (*The Tanzania Investment Bill, 2022*) na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu za sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

1 NOVEMBA, 2022

MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI TANZANIA WA MWAKA 2022 KAMA
ULIVYOWASILISHWA BUNGENI

ISSN 0856 – 01001X

No. 9

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

31st August, 2022

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 36 Vol. 103 dated 31st August, 2022
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

MUSWADA WA SHERIA YA UWEKEZAJI TANZANIA WA MWAKA 2022

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
KITUO CHA UWEKEZAJI NA MAJUKUMU YAKE

4. Kuendelea kuwepo kwa Kituo.
5. Malengo ya Kituo.
6. Majukumu ya Kituo.
7. Fursa za uwekezaji.
8. Mfumo unganishi wa kielektroniki.
9. Bodi.
10. Mwenendo wa uendeshaji wa Bodi.
11. Kamati za Bodi.
12. Mkurugenzi Mtendaji.
13. Sekretarieti.
14. Ukomo wa uwajibikaji kwa wajumbe na wafanyakazi.
15. Fedha za Kituo.
16. Mwaka wa fedha wa Kituo.
17. Hesabu, ukaguzi na taarifa.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YANAYOHUSU UWEKEZAJI

1 NOVEMBA, 2022

18. Kituo cha Huduma Mahala Pamoja.
19. Maombi ya cheti na usajili.
20. Uhai na kufutwa kwa cheti cha vivutio.
21. Uratibu wa uanzishaji wa biashara.
22. Manufaa.
23. Manufaa kwa uwekezaji wa kimkakati au uwekezaji maalum wa kimkakati.
24. Manufaa na vivutio vinavyosimamiwa na sheria nyingine.

SEHEMU YA NNE
HAKI NA WAJIBU WA SERIKALI NA WAWKEZAJI

25. Haki ya kudhibiti uwekezaji.
26. Wajibu wa mwekezaji.
27. Dhamana dhidi ya kurekebisha au kubadilishwa kwa manufaa.
28. Dhamana ya uwekezaji, uhamishaji wa mitaji, faida na gawio.
29. Kinga dhidi ya utafishaji au utwaaji.
30. Ukomo wa idadi ya wafanyakazi wa kigeni.
31. Upatikanaji wa mikopo kwa wawekezaji wa kigeni kutoka vyanzo vya ndani.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

32. Rufaa.
33. Utatuzi wa migogoro.
34. Makosa na adhabu.
35. Kanuni.
36. Kufutwa kwa Sheria Na. 26 ya 1997.
37. Masharti ya mpito.

TAARIFA

Muswada huo unakusudiwa kuwasilishwa Bungeni hivyo umechapishwa kwa ajili ya taarifa kwa umma ukiwa na madhumuni na sababu zake.

Dodoma,
30 Agosti, 2022

HUSSEIN A. KATTANGA,
Katibu Mkuu Kiongozi

MUSWADA
WA

Sheria ya kuweka masharti ya uwekezaji Tanzania, kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji, kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na uwezeshaji wa uwekezaji nchini, kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania, 1997 na masuala yanayohusiana na hayo.

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la Sheria
na kuanza
kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022 na itanza kutumika tarehe ambayo Waziri atateua kupitia tangazo katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2.-(1) Kwa kuzingatia kifungu hiki, Sheria hii itatumika kwa taasisi yoyote ya kibiashara iliyokidhi matakwa yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (2) isipokuwa-

Sura ya 123

(a) taasisi ya kibiashara iliyoidhinishwa kufanya shughuli za utafiti au uchimbaji wa madini chini ya Sheria ya Madini au inayoomba idhini ya kufanya shughuli nyingine zozote kama hizo;

Sura ya 392

(b) taasisi ya kibiashara iliyoidhinishwa kufanya shughuli za utafiti au uzalishaji mafuta au kujenga au kuendesha bomba la mafuta chini ya Sheria ya Petroli au inayoomba idhini ya kufanya shughuli nyingine zozote kama hizo; na

(c) taasisi ya kibiashara ambayo inajishughulisha na utengenezaji, utafutaji wa masoko au usambazaji wa kemikali hatarishi, silaha au aina yoyote ya milipuko.

(2) Biashara iliyoainishwa kwa madhumuni ya kifungu hiki ambayo inaweza kupata manufaa na kinga inayotolewa chini ya Sheria hii ni ile ambayo-

(a) ikiwa yote inamilikiwa na mwekezaji wa kigeni au ikiwa ni ubia, kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji si chini ya shilingi za Tanzania sawa na dola laki tano za Marekani (US\$ 500,000); au

(b) ikiwa inamilikiwa na Mtanzania, kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji si chini ya shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu hamsini (US\$ 50,000).

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)(a) na (b), masharti ya kifungu cha 28 yanayohusiana na dhamana ya uhamishaji wa mtaji, faida na gawio na kifungu cha 29 kinachohusiana na dhamana dhidi ya utafishaji yatatumika kwa taasisi yoyote ya kibiashara ambayo ina haki ya madini iliyotolewa chini ya Sheria ya Madini au leseni iliyotolewa chini ya Sheria ya Petroli kana kwamba mmiliki kwa madhumuni ya masharti hayo amepewa cheti cha vivutio na kinga.

Sura ya 123
Sura ya 392

(4) Hakuna chochote katika kifungu cha 29 kinachohusiana na utafishaji kitasomwa au kutafsiriwa

Sura ya 392
Sura ya 123

kuwa kinapunguza au kuongeza haki ya Waziri au Kamishna chini ya au kwa mujibu wa Sheria ya Petroli au Sheria ya Madini kufuta leseni iliyotolewa chini ya sheria hizo.

(5) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Kituo kitawasaidia wawekezaji wote, bila kujali kuwa Sheria hii inawahusu au la, kupata vibali, idhini, usajili, ridhaa, leseni na suala lolote linalohitajika kisheria kwa mtu kuanzisha na kuendesha shughuli za uwekezaji.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Kituo iliyoteuliwa chini ya kifungu cha 9;

“cheti” maana yake ni cheti cha vivutio kilichotolewa chini ya kifungu cha 19(1);

“Kituo” maana yake ni Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

“manufaa” inajumuisha nyenzo na vivutio vinavyotolewa na au kwa mujibu wa Sheria hii;

“mtaji” maana yake ni mchango wa fedha taslimu, mitambo, mashine, vifaa, majengo, vipuri, na mali nyinginezo za biashara tofauti na hadhi ambazo hazitumiki katika shughuli za kawaida za biashara na zinazoweza kudumu kwa zaidi ya miezi kumi na mbili;

“mtaji wa kigeni” maana yake ni fedha zinazoweza kubadilishwa, mtambo, mashine, vifaa, vipuri, malighafi na mali nyinginezo za biashara tofauti na hadhi zinazoingia Tanzania bila malipo ya awali ya fedha za kigeni na zinazokusudiwa kuzalisha bidhaa na huduma zinazohusiana na biashara ambayo Sheria hii inatumika;

“mwekezaji wa kigeni” ikiwa ni mtu binafsi maana yake ni mtu ambaye si raia wa Tanzania, na ikiwa ni kampuni, maana yake ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za nchi yoyote tofauti na Tanzania, kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Tanzania ambapo zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zinamilikiwa na mtu ambaye si raia wa Tanzania, na ikiwa ni ubia, maana yake ni ubia ambapo maslahi makubwa yanamilikiwa na mtu ambaye si raia wa Tanzania;

“mwekezaji wa ndani” maana yake ni mtu binafsi ambaye ni raia wa Tanzania, kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Tanzania ambapo hisa nyingi zinamilikiwa na mtu ambaye ni raia wa Tanzania, au ubia ambao maslahi makubwa yanamilikiwa na mtu ambaye ni raia wa Tanzania;

- “nyenzo” zinajumuisha leseni, idhini na vibali vinavyohitajika kwa ajili ya kuanzisha biashara ambazo mwekezaji atapaswa kupata kwa madhumuni ya Sheria hii;
- “taasisi ya kibiashara” maana yake ni kiwanda, mradi, shughuli au biashara ambayo Sheria hii inatumika au upanuzi, urekebishaji, ukarabati au uboreshaji wa kiufundi wa kiwanda, mradi, shughuli au biashara au sehemu yoyote ya biashara, ili mradi taasisi hiyo ya biashara inaendeshwa kwa madhumuni ya kupata faida na kwa misingi ya kibiashara;
- “uwekezaji” maana yake ni uanzishaji au umiliki wa mali mpya za biashara na inajumuisha upanuzi, urekebishaji au ukarabati wa biashara iliyopo;
- “vivutio” maana yake ni nafuu za kikodi, viwango vya kodi vya masharti nafuu au manufaa mengine yoyote anayoweza kupata mwekezaji chini ya sheria yoyote inayotumika kwa wakati huo; na
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji.

SEHEMU YA PILI

KITUO CHA UWEKEZAJI NA MAJUKUMU YAKE

Kuendelea
kuwepo kwa
Kituo

4.-(1) Kutaendelea kuwepo na chombo kitakachojulikana kama Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

(2) Kituo kitakuwa Wakala wa Serikali na kitakuwa chini ya usimamizi wa jumla wa Waziri.

(3) Kituo kitakuwa taasisi nafsi chenye urithishano undelevu na lakiri na kwa jina lake kitakuwa na uwezo wa-

(a) kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika, kuuza mali na kuingia mkataba au shughuli nyingine yoyote;

(b) kushtaki na kushitakiwa; na

(c) kufanya mambo mengine yoyote ambayo taasisi nafsi inaweza kufanya kwa mujibu wa sheria, kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Malengo ya
Kituo

5.-(1) Kituo kitakuwa sehemu ya huduma mahala pamoja kwa wawekezaji na kitakuwa ndicho chombo kikuu cha Serikali cha kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji Tanzania na kuishauri Serikali kuhusu sera ya uwekezaji na masuala yanayohusiana na hayo.

(2) Kwa madhumuni ya kuhamasisha, kuwezesha na kutekeleza kwa ufanisi miradi ya uwekezaji Tanzania, kutakuwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji itakayokuwa

na wajumbe wafuatao:

- (a) Waziri Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;
- (b) Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji, ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
- (c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (d) Waziri mwenye dhamana ya fedha;
- (e) Waziri mwenye dhamana ya ardhi;
- (f) Waziri mwenye dhamana ya katiba na sheria;
- (g) Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa;
- (h) Waziri mwenye dhamana ya sera na uratibu;
- (i) Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;
- (j) Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;
- (k) Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, ambaye pia atakuwa Katibu wa Kamati; na
- (l) mtu mwingine yeyote atakayealikwa na Waziri kadri itakavyohitajika baada ya kushauriana na Mwenyekiti.

(3) Kamati ya Taifa ya Uwekezaji, miongoni mwa mambo mengine-

- (a) itahakikisha kuwa mazingira mazuri kwa uwekezaji katika sekta binafsi na miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yanaendelezwa na kudumishwa;
- (b) itaongoza sera ya uwekezaji na kutoa mwelekeo wa pamoja kuhusu Mpango wa Taifa wa Uwekezaji;
- (c) itaidhinisha vivutio kwa wawekezaji wa kimkakati na wawekezaji maalum wa kimkakati; na
- (d) itasimamia miradi mikubwa yenye matokeo makubwa kitaifa kulingana na ukubwa, mtaji, manufaa ya kiteknolojia na ajira.

(4) Kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji, kutakuwa na Kamati ya Wataalam itakayoundwa na wajumbe kutoka katika taasisi za Serikali zinazohusika na uwekezaji kama itakavyoainishwa kwenye Kanuni.

(5) Waziri, baada ya kushauriwa na Bodi, atatengeneza kanuni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji na Kamati ya Wataalam.

Majukumu ya Kituo

- 6.-(1) Kwa madhumuni ya kifungu cha 5, Kituo-
- (a) kitakuwa taasisi kuu itayotekeleza na kuratibu uimarishaji wa taswira na rajamu ya nchi katika uwekezaji na uhamasishaji wa uwekezaji nchini;

- (b) kitaanzisha na kusaidia hatua zitakazoboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa wawekezaji wa ndani na nje;
- (c) kitakusanya, kupanga, kuchambua na kusambaza taarifa kuhusu fursa za uwekezaji na vyanzo vya mitaji ya uwekezaji, na pale kitakapombwa kitatoa ushauri kwa wawekezaji kuhusu upatikanaji na uchaguzi wa wabia wanaofaa katika miradi ya ubia;
- (d) kitahamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma kwa umma kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi;
- (e) kwa kushauriana na taasisi na wakala za Serikali, kitaainisha maeneo ya uwekezaji, mashamba au ardhi pamoja na huduma zinazohusiana na maeneo, mashamba au ardhi yoyote kwa madhumuni ya wawekezaji na uwekezaji kwa ujumla;
- (f) kitasaidia wawekezaji wote, ikiwa ni pamoja na wale ambao hawafungwi na masharti ya Sheria hii, kupata vibali, leseni, ridhaa, idhini, ruhusa, usajili na masuala mengine yanayohitajika kisheria kwa mtu kuanzisha na kuendesha shughuli za uwekezaji na kuwezesha vyeti vinavyotolewa na Kituo kutumika kikamilifu;
- (g) kitatunza taarifa kuhusu wawekezaji wote na uwekezaji kwa ujumla;
- (h) kitatoa, kuendeleza, kujenga, kubadilisha, kubadilisha ili kuendana na mahitaji, kudumisha na kusimamia maeneo ya uwekezaji, mashamba au ardhi pamoja na nyenzo zinazohusiana na maeneo, mashamba, ardhi hizo na kwa kuzingatia sheria husika, uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje;
- (i) kitaanzisha na kutunza kanzidata ya uwekezaji wa Watanzania nje ya nchi;
- (j) kitatoa na kusambaza taarifa zinazoendana na wakati kuhusu manufaa au vivutio vilivyopo kwa ajili ya wawekezaji;
- (k) kitashughulikia malalamiko yanayohusiana na uwekezaji;
- (l) kitafanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya uwekezaji iliyo chini ya mamlaka yake;
- (m) kitatekeleza na kusaidia shughuli za uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani ambazo ni muhimu katika kuhimiza na kuwezesha ongezeko la uwekezaji wa ndani, ikiwa ni

pamoja na programu za maendeleo ya ujasiriamali; na

(n) kitatekeleza majukumu mengine yoyote kwa ajili ya kufikiwa kwa malengo ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa jukumu lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1)(g), Kituo kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazosimamia uwekezaji, kitaanzisha mfumo utakaowezesha upatikanaji wa taarifa muhimu za wawekezaji nchini.

(3) Waziri kwa kushirikiana na mawaziri wenye dhamana ya mamlaka nyingine zinazosimamia uwekezaji, atatengeneza kanuni zitakazoainisha namna ya upatikanaji wa taarifa za wawekezaji na wajibu wa kila mamlaka.

Fursa za uwekezaji

7. Kituo kitabainisha fursa za uwekezaji zilizopo nchini na namna ya kuzifikia kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika.

Mfumo unganishi wa kielektroniki

8.-(1) Kituo kitaanzisha mfumo unganishi wa kielektroniki kwa ajili ya uwezesaji na uhamasishaji wa uwekezaji.

(2) Mfumo unganishi utakaoanzishwa kwa mujibu wa kifungu hiki utaunganisha mamlaka zote muhimu zinazohusika na utoaji wa leseni, vibali, idhini na ridhaa anazohitaji mwekezaji.

Bodi

9.-(1) Inaanzishwa Bodi ya Kituo ambayo itawajibika na utekelezaji wa majukumu ya Kituo.

(2) Bodi itakuwa na wajumbe tisa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) wajumbe wawili kutoka sekta binafsi;

(c) wajumbe wanne watakaoteuliwa kutoka-

(i) Wizara yenye dhamana ya fedha;

(ii) Wizara yenye dhamana ya ardhi;

(iii) Wizara yenye dhamana ya mamlaka za serikali za mitaa; na

(iv) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(d) wajumbe wengine wawili wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika masuala ya uwekezaji na usimamizi katika sekta ya umma au binafsi.

(3) Wajumbe waliotajwa katika kifungu kidogo cha (2)(b) hadi (d) watateuliwa na Waziri.

(4) Muda wa wajumbe wa Bodi kushika nafasi utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti - miaka minne;

(b) wajumbe waliorejewa katika kifungu kidogo cha

(2)(c) – miaka mitatu; na

(c) wajumbe waliorejewa katika kifungu kidogo

1 NOVEMBA, 2022

cha (2)(b) na (d) - miaka miwili.

(5) Kila mjumbe anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mmoja zaidi na baada ya muhula huo kuisha, hatastahili kuteuliwa tena.

(6) Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote mwenye utaalam au ujuzi katika suala lolote ambalo Bodi inajadili katika kikao chake, isipokuwa kwamba mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(7) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa Katibu wa Bodi.

(8) Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu kwa kuitaaruifu kimaandishi mamlaka yake ya uteuzi.

(9) Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kwa mujibu wa taratibu na miongozo iliyowekwa.

(10) Kwa kawaida Bodi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana katika kikao cha dharura pale itakapobidi.

Mwenendo
wa uendeshaji
wa Bodi
Kamati za
Bodi

10. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itajiwekea utaratibu wa kuitisha na kuendesha vikao vyake.

11.-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu ya Kituo, Bodi inaweza kuteua Kamati za Bodi zinazojumuisha wajumbe wa Bodi na inaweza kuwapangia majukumu yoyote ambayo Bodi inaweza kuamua.

(2) Kamati ya Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote mwenye utaalam au ujuzi katika suala lolote ambalo Kamati inajadili katika kikao chake, isipokuwa kwamba mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Mkurugenzi
Mtendaji

12.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo ambaye atateuliwa na Rais kwa mapendekezo ya Waziri kuhudumu-

(a) kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano ambacho hakitaongezwa; na

(b) kwa vigezo na masharti yaliyoainishwa katika hati ya uteuzi wake au kama Bodi inavyoweza kuamua.

(2) Kwa kuzingatia maelekezo ya jumla ambayo Bodi inaweza kutoa, Mkurugenzi Mtendaji atawajibika kwa usimamizi wa kila siku wa Kituo na utekelezaji wa maamuzi ya Bodi.

Maafisa na
wafanyakazi
wengine wa
Kituo

13.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya sheria zinazosimamia utumishi wa umma, Bodi itaajiri maafisa na wafanyakazi wengine wa Kituo kwa idadi na ngazi mbalimbali kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya Kituo na kwa vigezo na masharti kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Kituo kitaanzisha ofisi za kanda zenye idadi na mgawanyo wa maafisa na wafanyakazi kama Bodi

inavyoweza kuamua.

(3) Bodi inaweza kukasimu baadhi ya mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa ajili ya uteuzi wa wafanyakazi katika ngazi yoyote inavyoweza kuamua.

Ukomo wa uwajibikaji kwa wajumbe wa Bodi na wafanyakazi

14. Mjumbe, afisa au mfanyakazi mwingine wa Kituo hatawajibika kwa nafasi yake binafsi katika mashauri ya madai, kuhusiana na chochote alichotenda au kutotenda kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Fedha za Kituo

15.-(1) Fedha kwa ajili ya kukiwezesha Kituo kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii zitajumuisha-

- (a) fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo;
- (b) ada na tozo zinazotozwa kwa utoaji huduma kwa wawekezaji na wahusika wengine kuhusiana na majukumu ya Kituo chini ya Sheria hii; na
- (c) fedha nyingine zozote zitakazopokelewa na Kituo kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii.

(2) Ndani ya miezi mitatu kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, Kituo kitaandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio ya mapato na matumizi ya Kituo kwa mwaka unaofuata na kinaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya idhini makadirio yoyote ya ziada ya mwaka husika.

(3) Kwa kuzingatia maelekezo mengine yoyote ya Bodi, hakuna matumizi yatakayofanywa kwa fedha za Kituo isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bodi chini ya makadirio ya mwaka wa fedha ambapo matumizi hayo yatafanyika au katika makadirio ya ziada.

(4) Kwa idhini ya Bodi, Kituo kinaweza kuwekeza fedha zozote zisizohitajika kwa matumizi ya haraka kadri kitakavyoona inafaa.

Mwaka wa fedha wa Kituo Hesabu, ukaguzi na taarifa

16. Mwaka wa fedha wa Kituo utakuwa kipindi cha mwaka mmoja utakaoishia tarehe 30 Juni.

17.-(1) Hesabu za Kituo zitaandaliwa kwa mujibu wa viwango vya hesabu vilivyoidhinishwa na zitakaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.

- (2) Mara baada ya hesabu za Kituo kukaguliwa na

kwa vyovyote vile si zaidi ya miezi minne baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, Bodi itawasilisha kwa Waziri nakala ya taarifa ya hesabu zilizokaguliwa pamoja na nakala ya taarifa iliyotolewa na mkaguzi kuhusu hesabu za Kituo.

(3) Ndani ya miezi mitano baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, Kituo kitaandaa na kuwasilisha kwa Waziri taarifa inayohusu shughuli na uendeshaji wa Kituo katika mwaka husika pamoja na-

- (a) nakala ya hesabu za Kituo zilizokaguliwa;
- (b) nakala ya taarifa ya mkaguzi kuhusu hesabu; na
- (c) taarifa nyingine yoyote ambayo Waziri anaweza kuelekeza.

(4) Ndani ya muda usiozidi miezi mitatu baada ya kupokea hesabu na taarifa ya Kituo, Waziri ataziwasilisha Bungeni.

SEHEMU YA TATU

MASHARTI YANAYOHUSU UWEKEZAJI

Kituo cha
Huduma
Mahala
Pamoja

18.-(1) Kwa madhumuni ya kukifanya Kituo kuwa Kituo cha Huduma Mahala Pamoja, idara za Serikali, wakala za Serikali na taasisi nyingine za umma zitashirikiana kikamilifu na Kituo katika utekelezaji wa majukumu chini ya Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, baada ya kushauriwa na Bodi kimaandishi, kumuomba Waziri husika kuweka katika ofisi za Kituo maafisa wowote watakoainishwa na maombi hayo yatatekelezwa.

(3) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), endapo leseni au idhini zinahitajika na mwekezaji, Kituo kitawasiliana kwa maandishi na mamlaka husika ili kuhakikisha leseni na idhini zinazohitajika zinapatikana.

(4) Mamlaka husika itakayopokea maombi chini ya kifungu kidogo cha (3) itatoa leseni au idhini inayohitajika au mrejesho kimaandishi wa ushughulikiaji wa maombi husika ndani ya siku kumi na nne za kazi baada ya kupokea maombi hayo.

(5) Endapo Kituo hakitapata mrejesho wa ushughulikiaji wa maombi kutoka kwa mamlaka husika ndani ya muda ulioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (4), leseni au idhini husika itachukuliwa kuwa imetolewa.

(6) Endapo maombi ya kibali au idhini yatakataliwa na mamlaka husika, mwekezaji anaweza kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya leseni au idhini husika kwa mujibu wa sheria inayosimamia utoaji wa leseni au idhini hiyo.

Maombi ya
cheti na

19.-(1) Maombi yote ya vyeti vya vivutio na kinga

usajili

chini ya Sheria hii yatawasilishwa kwenye Kituo na Kituo kitatoa vyeti kwa utaratibu utakaoainishwa kwenye Kanuni.

(2) Endapo maombi ni ya uwekezaji mpya, yatakuwa na-

- (a) jina na anwani ya taasisi ya kibiashara inayopendekezwa, hadhi yake kisheria, taarifa za benki, majina na anwani za kila mkurugenzi au mbia na jina, anwani, utaifa na umiliki wa hisa kwa kila mwanahisa;
- (b) sifa, uzoefu na maelezo mengine muhimu ya wasimamizi wa mradi;
- (c) aina ya shughuli ya kibiashara inayopendekezwa na eneo linalopendekezwa ambapo shughuli hiyo itafanyika;
- (d) mchanganuo wa mtaji unaopendekezwa au kiasi cha uwekezaji na makadirio ya ukuaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo;
- (e) taarifa ya namna uwekezaji utakavyofadhiliwa;
- (f) uthibitisho wa mtaji wa kutosha unaopatikana kwa uwekezaji; na
- (g) ahadi kwamba mradi utatekelezwa kama ilivyooneshwa katika makadirio ya mradi.

(3) Endapo maombi ni kwa ajili ya kukarabati au kupanua biashara iliyopo au vyote kwa pamoja, yatakuwa na-

- (a) jina la biashara iliyopo na Katiba yake;
- (b) sifa za wasimamizi wa mradi;
- (c) taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa miaka mitatu iliyopita;
- (d) aina ya ukarabati au upanuzi;
- (e) mchanganuo wa mtaji na makadirio ya ukuaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo;
- (f) ufadhili wa mradi wa ukarabati au upanuzi, pamoja na uthibitisho wa upatikanaji wa fedha; na
- (g) ahadi kwamba upanuzi au ukarabati utatekelezwa kama ilivyooneshwa kwenye makadirio.

(4) Kituo kitatunza rejesta ya taasisi za kibiashara zote zilizothibitishwa itakayokuwa na taarifa kadri Bodi itakavyoamua.

(5) Cheti cha vivutio hakitahamishwa au kurekebishwa bila idhini ya Kituo.

(6) Endapo kwa sababu yoyote ile mmiliki wa cheti ataacha kufanya uwekezaji ulioainishwa kwenye cheti, atakitaarifu Kituo kwa maandishi na atastahili kupata haki zote na atakuwa na wajibu chini ya Sheria hii hadi tarehe ambayo aliacha kufanya uwekezaji na kwa tarehe hiyo cheti chake kitachukuliwa kuwa kimeisha muda wake.

(7) Mmiliki wa cheti atakitaarifu Kituo kwa maandishi pale ambapo-

- (a) mtu mwingine tofauti na mmiliki wa cheti amerithi uwekezaji;
- (b) jina au taarifa za biashara zimebadilika; au
- (c) uwekezaji umeongezeka au kuna mabadiliko makubwa katika uwekezaji.

(8) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5), mtu tofauti na mmiliki wa cheti ambaye ameathiriwa na au ana maslahi katika mabadiliko chini ya kifungu kidogo cha (7), anaweza kukitaarifu Kituo ikiwa mmiliki wa cheti atashindwa kukitaarifu Kituo ndani ya muda muafaka.

Uhai na
kufutwa kwa
cheti cha
vivutio

20.-(1) Cheti cha vivutio kilichotolewa chini ya Sheria hii-

- (a) kuhusiana na vivutio vya kifedha, kitakuwa hai kwa muda usiozidi miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa; na
- (b) kuhusiana na vivutio visivyo vya kifedha, kitakuwa hai kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1)(a), uhai wa cheti cha vivutio unaweza kuongezwa kwa kipindi kingine kadri itakavyoamuliwa na Kituo baada ya kuwasilisha maombi na sababu za msingi.

(3) Cheti cha vivutio kitafutwa endapo Kituo kitaridhika kwamba-

- (a) cheti kilipatikana kwa njia ya udanganyifu au kwa kutoa taarifa za uongo;
- (b) mmiliki wa cheti amekiuka masharti ya utoaji wa vivutio;
- (c) cheti kimehamishwa kwa mtu au uwekezaji mwingine bila idhini ya Kituo;
- (d) mmiliki wa cheti hajaanza kutekeleza mradi ndani ya miaka miwili ya kwanza tangu kutolewa kwa cheti bila sababu za msingi; au
- (e) mmiliki wa cheti hajawasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji na maendeleo ya mradi wa uwekezaji kwa miaka miwili mfululizo.

(4) Utaratibu wa kufuta cheti cha vivutio na masuala mengine kuhusu ukomo wa cheti cha vivutio kwa kuzingatia aina na umuhimu wa mradi wa uwekezaji utakuwa kama itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Uratibu wa
uanzishwaji
wa taasisi za
kibiashara
Sura ya 212

21. Kituo kitaratibu uanzishaji wa taasisi za kibiashara zinazosimamiwa na Sheria hii ikiwa ni pamoja na-

- (a) usajili wa taasisi za kibiashara chini ya Sheria ya Makampuni au sheria nyingine yoyote inayohusika na uanzishaji wa biashara; na

- (b) kuwezesha wawekezaji kupata leseni, vibali, nyenzo au huduma muhimu.

Manufaa

22.-(1) Taasisi ya kibiashara iliyopewa cheti chini ya Sheria hii itakuwa na haki ya kupata manufaa yanayoendana na biashara hiyo chini ya masharti ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ushuru wa Forodha, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani au sheria nyingine yoyote inayotumika kwa wakati huo.

(2) Manufaa chini ya kifungu kidogo cha (1) hayatahusisha-

- (a) gari lisilotumika moja kwa moja kwenye mradi lililoainishwa chini ya Namba za Utambuzi 8702.10.19, 8702.90.19 na Sura Na 8703 katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa ili mradi zuiio lililowekwa halitahusisha mwekezaji ambaye cheti chake cha vivutio kilitolewa kabla ya au tarehe 30 Juni, 2006;
- (b) trela iliyoagizwa kutoka nje ya nchi iliyoainishwa chini ya Namba za Utambuzi 8716.31.90 na 8716.40.90 katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa;
- (c) gari lililotengenezwa zaidi ya miaka nane kabla ya kuingizwa nchini;
- (d) gari lisilotumika moja kwa moja kwenye mradi lenye injini yenye uwezo unaozidi 3000;
- (e) vifaa vya ofisi, shajara, samani, sukari, vinywaji baridi, pombe kali, vigae, magari yasiyotumika moja kwa moja kwenye mradi, vyombo vya chakula, viyoyozi, majokofu, matandiko, saruji, nondo, mabati, PVC na mabomba ya HDPE yenye Namba za Utambuzi 3917.23.00 na 3917.21.00 katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa mtawalia, matrela na vifaa vya kielektroniki vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi;
- (f) mawasiliano ya simu, isipokuwa bidhaa za mtaji kwa ajili ya usimikaji wa minara ya mawasiliano ya simu.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), msamaha wa ushuru wa forodha utakaotolewa kwa bidhaa za mtaji usio asili utatolewa kwa asilimia 75 ambapo mwekezaji atalipa asilimia 25 ya ushuru unaopaswa kulipwa.

Manufaa kwa uwekezaji wa kimkakati au uwekezaji maalum wa kimkakati

23.-(1) Uwekezaji maalum wa kimkakati na uwekezaji wa kimkakati utatambuliwa na kupata vivutio vya ziada kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(2) Bila kujali kifungu cha 2(2), taasisi ya

kibiashara itachukuliwa kuwa uwekezaji wa kimkakati ikiwa-

- (a) kwa biashara-
 - (i) inayomilikiwa na mzawa, kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji si chini ya shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani milioni ishirini (US\$ 20,000,000); na
 - (ii) inayomilikiwa yote na mwekezaji wa kigeni au kwa ubia, kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji si chini ya shilingi za Kitanzania sawa na dola za Marekani milioni hamsini (US\$ 50,000,000); na
 - (b) inazalisha angalau ajira za ndani elfu moja zenye idadi ya kutosha ya nafasi za juu kwenye miradi isiyohitaji teknolojia ya hali ya juu na ya kisasa;
 - (c) ina uwezo wa kuongeza mauzo ya nje angalau kwa asilimia hamsini ya bidhaa zinazozalishwa au kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje;
 - (d) ina uwezo wa kuchochea uzalishaji kwa kuanzisha kongani za kiuchumi katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi;
 - (e) inaongeza ujuzi wa kiufundi kwa kuhaulisha teknolojia mpya kwa watanzania; au
 - (f) ina uwezo wa kuzalisha bidhaa au kutoa huduma muhimu kwa maendeleo katika sekta za kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia vipaumbele kwa wakati huo.
- (3) Serikali inaweza kubainisha miradi na kuipa hadhi ya uwekezaji maalum wa kimkakati.
- (4) Hadhi ya uwekezaji maalum wa kimkakati inaweza kutolewa kwa mradi unaokidhi vigezo vifuatavyo-
- (a) kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji usiopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani milioni mia tatu (US\$ 300,000,000); na
 - (b) miamala ya fedha za mtaji wa uwekezaji inafanywa kupitia taasisi za ndani za kifedha na bima zilizosajiliwa;
 - (c) angalau ajira za ndani elfu moja na mia tano za moja kwa moja zenye idadi ya kutosha ya nafasi za juu zinazalishwa kwenye miradi isiyohitaji teknolojia ya hali ya juu na ya kisasa; au
 - (d) uwezo wa kuzalisha kwa kiasi kikubwa mapato ya fedha za kigeni, kuzalisha bidhaa muhimu zitakazopunguza kiwango cha uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi au usambazaji wa

nyenzo muhimu zinazohitajika kwa maendeleo katika sekta ya kijamii, kiuchumi au kifedha.

(5) Baada ya mradi kupewa hadhi ya uwekezaji wa kimkakati au uwekezaji maalum wa kimkakati, Waziri atapendekeza kwa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji vivutio maalum vya ziada.

(6) Bila kujali mamlaka ya Waziri chini ya kifungu kidogo cha (5), vivutio vitakavyopendekezwa havitahusisha vivutio katika vifaa vya ofisi, shajara, samani, sukari, vinywaji baridi, pombe kali, vigae, magari yasiyotumika moja kwa moja kwenye mradi, vyombo, viyoyozi, jokofu, matandiko, saruji, nondo, mabati, PVC na mabomba ya HDPE yenye Namba ya Utambuzi 3917.23.00 na Namba ya Utambuzi 3917.21.00 katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa mtawalia, matrela yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi yenye Namba ya Utambuzi 8716.31.90 na vifaa vya kielektroniki vyenye Namba ya Utambuzi 8716.40.90 katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa.

(7) Endapo Kamati ya Taifa ya Uwekezaji itaidhinisha vivutio maalum vya ziada, vivutio hivyo vitatolewa kwa mujibu wa sheria husika.

(8) Kamati ya Taifa ya Uwekezaji inaweza kupitia kila mradi uliopewa vivutio maalum vya ziada kuhusiana na uzingatiaji wa masharti ya vivutio vilivyotolewa na kuishauri Serikali kuhusu kuendelea kutoa au kusitisha vivutio hivyo.

Manufaa na vivutio vinavyosimamiwa na sheria nyingine

24. Endapo mtu anastahili manufaa au vivutio vya kifedha au visivyo vya kifedha chini ya Sheria hii na manufaa au vivutio hivyo vinasimamiwa na sheria nyingine, manufaa au vivutio hivyo vitatolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria husika.

SEHEMU YA NNE

HAKI NA WAJIBU WA SERIKALI NA WAWEKEZAJI

Haki ya kusimamia uwekezaji

25. Serikali itakuwa na haki ya kuchukua hatua zote za kusimamia uwekezaji ili kuhakikisha kuwa shughuli za uwekezaji nchini zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi na malengo ya Sheria hii na madhumuni ya kisera ya kijamii na kiuchumi.

Wajibu wa mwekezaji

26. Mwekezaji anayetambulika na Sheria hii atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kutii sheria za nchi;

(b) kuwasilisha kwa wakati taarifa zinazohitajika na taasisi zinazohudumia wawekezaji ili kuziwezesha kutekeleza majukumu kwa ufanisi;

- (c) kuendesha shughuli za uwekezaji kwa namna inayolinda walaji, mazingira, usawa wa kijinsia na kuendeleza ujuzi kwa wafanyakazi;
- (d) kuwasilisha kwa Kituo taarifa za mwaka za utekelezaji na maendeleo ya mradi wa uwekezaji;
- (e) kutumia malighafi na rasilimali nyingine zinazopatikana au kuzalishwa nchini; na
- (f) kuruhusu maafisa wa Kituo kufanya ufuatiliaji wa vivutio vilivyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

Dhamana dhidi ya kurekebisha au kubadilishwa kwa manufaa

27. Kwa madhumuni ya kuweka mazingira ya uwekezaji yanayotabirika, taasisi ya kibiashara ambayo imepewa vivutio chini ya Sheria hii itakuwa na haki ya kunufaika na vivutio husika vilivyotolewa, na katika kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa, vivutio hivyo havitarekebisha au kubadilishwa kwa namna itakayomuathiri mwekezaji.

Dhamana ya uwekezaji, uhamishaji wa mitaji, faida na gawio

28. Kwa kuzingatia kifungu hiki, taasisi ya kibiashara inayosimamiwa na Sheria hii inahakikishiwa kuwa, kwa kupitia benki yoyote iliyoidhinishwa na kwa aina ya fedha inayoweza kubadilishwa kwa uhuru, itaweza kuhamisha bila masharti-

- (a) faida halisi au gawio linalotokana na uwekezaji;
- (b) malipo yanayohusiana na urejeshaji wa mkopo pale ambapo mkopo umepatikana kutoka nje ya nchi;
- (c) mapato, baada ya makato ya kodi na malipo mengine, endapo taasisi ya kibiashara itauzwa au kufilisika au faida yoyote inayotokana na uwekezaji; na
- (d) malipo ya stahiki na marupurupu mengine kwa wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa nchini Tanzania katika taasisi ya kibiashara.

Kinga dhidi ya utafishaji au utwaaji

29.-(1) Kwa kuzingatia vifungu vidogo vya (2) na (3)-

- (a) taasisi ya kibiashara haitataifishwa au kutwaliwa na Serikali; na
- (b) mtu anayemiliki mtaji wote au sehemu ya mtaji wa taasisi ya kibiashara hatalazimishwa na sheria kusalimisha maslahi yake ya mtaji kwa mtu mwingine.

(2) Serikali haitatwaa taasisi ya kibiashara au sehemu ya taasisi ya kibiashara inayosimamiwa na Sheria hii isipokuwa kama utwaaji huo ni kwa mujibu wa sheria inayoweka masharti ya-

- (a) malipo ya fidia ya haki na kwa wakati; na
- (b) haki ya kwenda mahakamani au kwenye vyombo vya usuluhishi kwa ajili ya uamuzi wa maslahi au haki ya mwekezaji na kiasi cha fidia anachostahili kupata.

(3) Fidia yoyote inayolipwa chini ya kifungu hiki italipwa kwa wakati na idhini ya kurejeshwa kwa fidia hiyo katika aina ya fedha inayoweza kubadilishwa itatolewa pale inapohitajika.

Ukomo wa idadi ya wafanyakazi wa kigeni

30. Kila taasisi ya kibiashara iliyopewa cheti cha vivutio chini ya Sheria hii itaruhusiwa kuwa na wafanyakazi wa kigeni kwa kuzingatia ukomo wa idadi ulioainishwa katika sheria inayosimamia masuala ya ajira kwa wageni:

Isipokuwa kwamba, kwa madhumuni ya masharti ya kifungu cha 18, Kituo kitaratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki inayotolewa chini ya kifungu hiki.

Upatikanaji wa mikopo kwa wawekezaji wa kigeni kutoka vyanzo vya ndani

31.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 2, mwekezaji wa kigeni anaweza, kuhusiana na biashara anayoendesha, kupata mikopo kutoka benki na taasisi za fedha za ndani hadi kufikia ukomo uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushauriana na Kituo kwa kuzingatia kiasi cha mtaji wa kigeni uliowekezwa katika taasisi ya kibiashara.

(2) Mwekezaji wa kigeni anayepata mkopo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atahakikisha kwamba mapato ya mkopo huo yanatumika kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli zilizoainishwa katika maombi yake ya mkopo.

(3) Benki inayotoa mkopo inaweza, kwa madhumuni ya kifungu hiki, kuteua afisa au wakala wake ili kuthibitisha matumizi sahihi ya mkopo uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1).

SEHEMU YA TANO

MASHARTI YA JUMLA

Rufaa na mapitio

32.-(1) Mtu ambaye hataridhika na uamuzi uliotolewa na Kituo chini ya Sheria hii anaweza kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Mwekezaji ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji kuhusu uidhinishaji wa vivutio anaweza kuwasilisha maombi kwa Kamati hiyo ili iweze kupitia tena uamuzi wake.

(3) Utaratibu wa kukata rufaa au kuwasilisha maombi ya mapitio utainishwa kwenye kanuni.

Utatuji wa migogoro

33.-(1) Endapo mgogoro utatokea kati ya mwekezaji na Kituo au Serikali kuhusu taasisi ya

kibiashara, juhudi zote zitafanywa ili kutatua mgogoro huo kwa njia ya majadiliano ili kufikia suluhu.

(2) Mgogoro kati ya mwekezaji na Kituo au Serikali kuhusu taasisi ya kibiashara ambao utashindwa kusuluhishwa kwa majadiliano unaweza kuwasilishwa katika vyombo vya usuluhishi kwa kuzingatia mojawapo ya njia zifuatazo kama zitakavyokubaliwa na pande zote-

- (a) kwa mujibu wa sheria za usuluhishi za Tanzania;
- (b) kwa mujibu wa kanuni za utaratibu wa usuluhishi wa Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji; au
- (c) ndani ya makubaliano yoyote baina ya nchi mbili au zaidi kuhusu kinga ya uwekezaji yaliyofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya nchi anayotokea mwekezaji.

Makosa na
adhabu

34.-(1) Mtu ambaye wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ya kikazi katika usimamizi wa Sheria hii anamiliki au anasimamia nyaraka au taarifa yoyote iliyopatikana chini ya Sheria hii na ambaye atawasilisha nyaraka au taarifa hiyo au sehemu ya nyaraka au taarifa hiyo kwa mtu mwingine yeyote ambaye hajaidhinishwa kwa sheria yoyote au na Bodi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote.

(2) Mwajiriwa wa Kituo ambaye ana wajibu wa kutekeleza chini ya Sheria hii na ameshindwa kutekeleza wajibu huo au ameteketeleza wajibu huo kwa uzembe atachukuliwa hatua za kinidhamu ambazo Bodi au mamlaka husika ya nidhamu inaweza kuamua.

(3) Mtu ambaye-

- (a) kwa kujua au kwa uzembe anatoa taarifa za uongo au za kupotosha;
- (b) anakataa au anapuuza kutoa taarifa ambayo Kituo kinaweza kuhitaji kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii; au
- (c) anakataa bila sababu halali kumruhusu afisa aliyeidhinishwa kuingia kwenye eneo lake la biashara au vinginevyo anazuia ukaguzi wowote unaofanywa na afisa aliyeidhinishwa katika kutekeleza majukumu yake ya ufuatiliaji, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

(4) Endapo kosa limetendwa na taasisi mkurugenzi, mbia, afisa mkuu wa usimamizi au afisa anayehusika katika taasisi hiyo atachukuliwa pia kuwa

ametenda kosa hilo.

Kanuni

35. Waziri, baada ya kushauriwa na Bodi, anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya kutekeleza masharti ya Sheria hii.

Kufutwa kwa
Sheria
Sura ya 38

36. Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 inafutwa.

Masharti ya
mpito

37.-(1) Bila kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu cha 36, cheti cha vivutio kilichotolewa au makubaliano yaliyoingiwa chini ya Sheria iliyofutwa yataendelea kuwa halali kwa kuzingatia vigezo na masharti ya kutolewa au kuingiwa kwake kana kwamba cheti hicho cha vivutio kimetolewa au makubaliano hayo yameingiwa chini ya Sheria hii, na yatakuwa halali hadi mwisho wa muda ambao mmiliki au mnufaika wake alikuwa na haki ya kunufaika na manufaa, vivutio au kinga yoyote; na baada ya kumalizika kwa muda ulioainishwa masharti ya Sheria hii yataanza kutumika.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mtu mwenye cheti cha vivutio kwa mujibu wa vigezo na masharti ya Sheria iliyofutwa, hatadai manufaa, kinga au vivutio vyovyote chini ya Sheria hii hadi baada ya kumalizika kwa muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1).

(3) Suala lolote linaloendelea mbele ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilichoanzishwa chini ya Sheria iliyofutwa litahesabiwa kuwa linaendelea mbele ya Kituo.

(4) Makubaliano yoyote yanayoendelea kwa mujibu wa kifungu hiki yatatoa manufaa ambayo yalikuwa yakitolewa awali chini ya makubaliano hayo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

1 NOVEMBA, 2022

(5) Endapo taasisi ya kibiashara iliyokuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii imezingatia ipasavyo masharti ya Sheria iliyofutwa, kuhusiana na matakwa yoyote ya kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji ulioainishwa katika Sheria iliyofutwa, taasisi hiyo ya kibiashara hiyo itachukuliwa kuwa halali bila kujali masharti yoyote ya Sheria hii yanayoeleza vinginevyo.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka, 2022 kwa lengo kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji Tanzania na kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini. Aidha, Muswada unaopendekezwa unakusudia kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tano. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi, yanayojumuisha jina la Sheria, utaratibu wa kuainisha tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa, maelezo kuhusu matumizi ya Sheria inayopendekezwa kutungwa na tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka mfumo wa kitaasisi wa uratibu na uwezeshaji wa uwekezaji nchini. Sehemu hii inaweka masharti yanayohusu kuendelea kuwepo kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, ambacho miongoni mwa masuala mengine kitakuwa ndicho chombo kikuu cha Serikali cha kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji nchini na kuishauri Serikali kuhusu sera ya uwekezaji. Sehemu hii pia inaweka masharti ya kuendelea kuwepo kwa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji itakayokuwa na jukumu la kutoa mwongozo na mwelekeo wa nchi katika masuala ya uwekezaji. Katika Sheria inayopendekezwa, Kamati hii itaendelea kuwa ndiyo mamlaka itakayoidhinisha utolewaji wa vivutio mbalimbali kwa miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na Kituo. Aidha, Sehemu hii inapendekeza pia kuweka masharti yatakayokiwezesha Kituo kuanzisha mfumo unganishi wa kielektroniki. Mfumo huu unalenga kuunganisha mamlaka muhimu za Serikali zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uwekezaji. Hatua hii itatoa fursa kwa wawekezaji kupata huduma kwa urahisi. Masharti mengine katika Sehemu hii ni pamoja na uanzishwaji wa Bodi, muundo na majukumu yake, vyanzo vya fedha vya Kituo na utaratibu wa utunzaji na ukaguzi wa hesabu zake.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uwekezaji. Katika Sehemu hii, masharti yanawekwa kwa ajili ya kuzitaka taasisi za Serikali kushirikiana na Kituo katika kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji kupitia Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja. Vilevile, Sehemu hii inaweka utaratibu wa maombi ya cheti cha vivutio, muda wa uhai wa cheti

hicho na vivutio anavyoweza kupata mwekezaji. Muswada huu unapendekeza cheti cha vivutio kuwa na uhai wa kipindi cha miaka mitano kwa vivutio vya kifedha, na kuendelea kuwa hai kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi kwa vivutio visivyo vya kifedha. Sehemu hii inaainisha pia sifa za uwekezaji utakaostahili kupata vivutio. Miongoni mwa sifa hizo ni kiwango cha mtaji wa uwekezaji, uwezo wa kuzalisha ajira za ndani na uwezo wa kuzalisha mapato ya fedha za kigeni. Aidha, Sehemu hii pia inabainisha kuwa vivutio vinavyosimamiwa chini ya sheria nyingine yoyote vitatolewa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika sheria hizo.

Sehemu ya Nne ya Muswada inaainisha haki na wajibu wa Serikali na wawekezaji. Muswada unapendekeza kuipa Serikali haki ya kusimamia shughuli za uwekezaji ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya sera na sheria za nchi. Wajibu unaopendekezwa kwa mwekezaji katika sehemu hii ni pamoja na kutii sheria za nchi, kuendesha shughuli zao kwa namna inayolinda walaji, mazingira na usawa wa kijinsia na kutoa taarifa kwa mamlaka mbalimbali za Serikali pale zitakapohitajika. Sehemu hii inapendekeza kutoa haki kwa mwekezaji katika kipindi cha kutekeleza mradi. Haki hizo zinajumuisha kutobadilishiwa vivutio kwa namna itakayoathiri uwekezaji, kuhamisha faida, mapato na gawio kupitia benki yoyote pasipo kuwekewa masharti, kutotaifishwa kwa miradi ya uwekezaji bila fidia stahiki kwa mujibu wa sheria na kupata mikopo katika benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa ndani ya nchi kwa ajili ya kufadhili miradi ya uwekezaji.

Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayohusiana na masuala ya uwekezaji na adhabu zake pamoja na mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria inayopendekezwa. Sehemu hii inajumuisha pia masharti kuhusu rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wowote uliotolewa na utaratibu wa ushughulikiaji wa migogoro baina ya wawekezaji na Kituo au Serikali. Aidha, Sehemu hii pia inapendekeza kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 pamoja na kuweka masharti ya mpito kwa ajili ya masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na Sheria inayopendekezwa kufutwa. Miongoni mwa masharti hayo ni kuendelea kutambuliwa kwa vivutio vilivyotolewa na mikataba iliyoingiwa na wawekezaji chini ya Sheria inayopendekezwa kufutwa.

Dodoma,
29 Agosti, 2022

ASHATU K. KIJAJI,
Waziri wa Uwekezaji,
Viwanda na Biashara

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

1 NOVEMBA, 2022

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira aje asome maoni ya Kamati.

MHE. DAVID M. KIHENZILE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mazingira kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, iliupokea Muswada huu Mwezi Septemba, 2022 baada ya kusomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 23 Septemba, 2022 ili iufanyie kazi na tarehe 18 Oktoba, 2022, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu malengo na madhumuni ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, dhana ya Sheria ya Uwekezaji siyo dhana ngeni katika mizania ya Sheria na Uwekezaji hapa Tanzania na nchi nyingine. Nchi nyingi za Afrika kama vile Kenya, Rwanda na Afrika Kusini tayari wana hii Sheria. Kwa Nchi ya Kenya Sheria hii ilitungwa Mwaka 2004 na inaitwa *Investment Promotion Act (No.6)* ya Mwaka 2004 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2021. Kwa Nchi ya Rwanda, Sheria ilitungwa mwaka 2021 na inaitwa *Investment, Promotion and Facilitation Act, (No.6)* ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Malengo na Madhumuni ya Muswada; Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania (Na.9) ya mwaka 2022. Sheria inayopendekezwa ina madhumuni ya kuweka masharti ya mazingira bora kwa wawekezaji Tanzania, kuweka Mfumo wa Kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini na kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, utafiti unaonesha kuwa nchi nyingi duniani na zile zinazotuzunguka, zimefanya mapitio ya Sheria za Uwekezaji ili kuweka mazingira bora na shindani kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuzingatia mabadiliko ya haraka katika mifumo ya kiuchumi duniani. Mapitio hayo yamewezesha kuboresha utoaji wa huduma na uratibu kwa wawekezaji. Vile

vile mapitio hayo yameimarisha utendaji wa Taasisi zinazohusika na uwekezaji katika nchi hizo katika kutoa huduma mahala pamoja kwa ufanisi (*True One Stop Centre*) na kuzingatia ushiriki katika uchumi wa Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Tano kama zinavyoonekana kuanzia ukurasa wa 3-4 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa jumla wa Muswada; kwa kuzingatia Kanuni ya 24(2)(a), (b), (c) na (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia vifungu vyote 37 vya Muswada na kujiridhisha na malengo na madhumuni ya sheria inayotungwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 18 Oktoba, 2022 ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu malengo na madhumuni ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, tarehe 19 Oktoba, 2022, Kamati ilikutana na kupokea maoni ya Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Mitandao ya Kijamii ili kusikiliza na kupokea maoni yao kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kitaalam wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya Wadau, Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Maoni ya wadau kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi wa Muswada na hatimaye kutoa maoni kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 21 Oktoba, 2022, Kamati ilikutana na mtoa hoja, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kushauriana naye kuhusu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi uliofanyika. Yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Serikali ilikubali kuchukua mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wadau waliochangia katika Muswada huu wamekubaliana na malengo na madhumuni ya Muswada na kuipongeza Serikali kwa hatua hii ya kutunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia Kifungu kwa Kifungu na baada ya kupokea na kuchambua Madhumuni na Malengo ya Muswada huu Kamati iliona

kwamba kwa maslahi ya Sekta ya Uwekezaji Tanzania, kuna haja ya kuvifanyia maboresho Vifungu 37 vya Muswada huu kwa kutazama mazingira tuliyonayo hapa Tanzania na kwa kutazama pia sheria za namna hii zilivyo katika nchi nyingine (*International Comparative Perspective*).

Mheshimiwa Spika, vifungu vilivyohitaji kuboreshwa zaidi ni kama vilivyooneshwa kwenye ukurasa wa saba wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, pande zote mbili zilikubaliana kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha vifungu vyote vilivyokuwa na utata ili viwe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati katika Muswada huu yamezingatia uchambuzi wa Kitaalamu wa Muswada huu uliofanywa na Kamati kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, Maoni na ushauri wa Kamati; kama nilivyoeleza awali Kamati ilifanya Uchambuzi wa Muswada kifungu kwa kifungu, hatua hiyo iliwezesha kutolewa kwa Maoni na Ushauri kwa Serikali kuhusu maboresho ya vifungu vya Muswada kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Jumla; Kamati ina maoni na mapendekezo ya jumla yafuatayo:-

- (a) Hadhi ya Kituo cha Uwekezaji ilivyo kwa sasa haiwezeshi Mfumo madhubuti wa Kitaasisi kwa ajili ya uratibu na uwezesaji wa uwekezaji nchini. Kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza Kituo cha Uwekezaji kipewe mamlaka kamili. Narudia, Kamati inapendekeza Kituo cha Uwekezaji kipewe mamlaka kamili badala ya kuendelea kuwa Wakala wa Serikali, lengo likiwa ni kukipa nguvu ya utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofi*)
- (b) Kamati inapendekeza kuwa baada ya Sheria hii kutungwa na Bunge lako itafsiriwe katika lugha ya Kiingereza ndani ya siku 30. Sababu ni uhalisia wa uwekezaji ambao kutokana na vivutio katika Muswada huu Wawekezaji wengi wanatarajiwa kutoka mataifa mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu vifungu vya Muswada, katika kifungu cha 1 kuhusu Jina, Kamati inashauri Jina la Sheria lisomeke "Sheria ya Kuvutia na Kulinda Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2022". Aidha, maoni na ushauri mwingine wa Kamati ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa tisa wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika kifungu cha 5(2) , Kamati inashauri kwamba aongezwe Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Sababu ni kwamba Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiye mwenye dhamana ya kusimamia Sera ya Mambo ya Nje ambayo yamejikita katika diplomasia ya uchumi. Pia huyu ndiye msimamizi wa Mabalazi walioko nje ya nchi wanaohamasisha na kuvutia wawekezaji walioko nje kuja kuwekeza nchini.

Mheshimimwa Spika, katika kifungu cha 9 kuhusu Wajumbe wa Bodi ya Kituo; Kamati inashauri kwamba Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji uzingatie uwiano wa kijinsia. Lengo ni kuona kuwa uwakilishi wa wanaume na wanawake katika Wajumbe wa Bodi. Hii itasaidia pia kujenga uwezo wa wanawake katika nafasi za uongozi na usimamizi bora wa utekelezaji wa sheria hii kwa jicho la kutazama makundi yote katika jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 9(4)(b) na (c) kuhusu muda wa Wajumbe wa Bodi kushika nafasi zao, Kamati inapendekeza kwamba muda wa Wajumbe kushika nafasi zao iwe miaka mitatu kwa makundi yote isipokuwa Mwenyekiti wa Bodi ibaki miaka minne. Sababu ni kuondoa tofauti kati ya Wajumbe kutoka Serikalini na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 18(4) kuhusu muda wa utoaji wa Leseni, Kamati inapendekeza muda wa utoaji wa leseni au idhini uwe siku saba za kazi kama ilivyobainishwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Sura ya Pili Ibara ya 22(l) Ukurasa wa 19 wa Ilani. Lengo ni kuwavutia wawekezaji wengi na kuondoa urasimu.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 20(1)(a) na (b) kuhusu uhai na kufutwa kwa cheti cha vivutio; Kamati inashauri Muswada utoe tafsiri ya maana ya vivutio vya kifedha na visivyo vya kifedha ili vijulikane kwa urahisi na wawekezaji wa ndani na wa kigeni, wasomi na wasio wasomi.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 26 kuhusu wajibu wa mwekezaji, Kamati inashauri kiongezwe kifungu (g) mara baada ya kifungu (f) kitakachosomeka;

(g) “kutunza taarifa za ukaguzi wa hesabu na fedha za kila mwaka na kuwasilisha taarifa hizo Kituoni” na

(h) “kutekeleza Mradi kwa mujibu wa Mpango Kazi uliokubaliwa wakati wa maombi ya vivutio vya Uwekezaji’.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 33(1) kuhusu Utatuzi wa migogoro, ndani ya siku 60 katikati ya neno majadiliano na ili. Sababu ni kuweka ukomo wa muda wa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 34 (1) Kamati inashauri isomeke faini isiyopungua milioni tano na isiyozidi milioni kumi au kifungu kisichopungua miezi sita au kisichoziidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 34(2), Kamati inashauri kuongeza maneno ya mwajiriwa au mwajiriwa wa Wizara, Idara au Taasisi ya Umma'' katikati ya neno "Kituo" na neno "ambaye."

Mheshimiwa Spika, napenda kuliaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imekubali mapendekezo mengi ya Kamati na kuyaweka katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa katika Bunge hili. Serikali pia imetoa maelezo ya ziada na ufafanuzi katika maeneo ya Muswada ambayo Kamati ilihitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba uchambuzi wa Kitaalam uliofanywa katika Muswada huu, utasaidia kupatikana kwa Sheria bora ya kusimamia Sekta ya Uwekezaji nchini na kufungua ukurasa mpya kwa wawekezaji nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa fursa ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashantu Kijaji, pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Kigahe Exaud Silaoneka kwa ushirikiano wao wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao: -

- (i) Baraza la Kilimo Tanzania (ACT);
- (ii) Chama cha Mwakili wa Tanganyika (TLS);
- (iii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- (iv) Shirikisho la Wafanyabiashara na Wawekezaji Tanzania (Tanzania Trade and Investment Coalition - TATIC);
- (v) IResolve;

- (vi) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation*); na
- (vii) Umoja wa Makampuni ya Simu Tanzania (*TAMNOA*).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa maoni na ushauri wa msingi wa kuuboresha Muswada huu. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelewa Mwihambi, *ndc*, kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Angelina Langisi Sanga na Ndugu Nyamwanja Chipanda Chilemeji, Wanasheria wa Bunge Ndugu Praisegod Zakaria Lukio, Ndugu Evelyne Shibandiko na Ndugu Nesta Kawamala na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA
UWEKEZAJI TANZANIA WA MWAKA 2022 – KAMA ILIVYOWSILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI:

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022.

1.2 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, iliupokea Muswada huu Mwezi Septemba, 2022 baada ya kusomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 23 Septemba, 2022 ili iufanyie kazi, na tarehe 18 Oktoba, 2022, Waziri wa Uwekezaji,

Viwanda na Biashara alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Madhumuni ya Muswada huu.

1.3 Mheshimiwa Spika, dhana ya Sheria ya Uwekezaji siyo dhana ngeni katika mizania ya Sheria na Uwekezaji hapa Tanzania na nchi nyingine. Nchi nyingi za Afrika kama vile Kenya, Rwanda na Afrika Kusini tayari wana hii Sheria. Kwa nchi ya Kenya Sheria hii ilitungwa Mwaka 2004 na inaitwa **Investment Promotion Act Na.6 ya Mwaka 2004** ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2021. Kwa nchi ya Rwanda Sheria ilitungwa mwaka 2021 na inaitwa **Investment, Promotion and Facilitation Act Na. 6 ya mwaka 2021**.

Kwa nchi ya Afrika Kusini Sheria ilitungwa Mwaka 2015 na inaitwa **Protection of Investment Act, Na. 22 ya Mwaka 2015**. Uingereza Sheria hii ilitungwa tarehe 4 Januari, 2022 na inaitwa **National Security and Investment Act ya mwaka 2022**.

1.4 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa Maoni yao kuhusu Muswada huu.

Aidha, Wadau walifika mbele ya Kamati tarehe 19 Oktoba, 2022 na kutoa maoni yao ambayo yamekuwa na mchango mkubwa katika Uchambuzi wa Muswada huu.

2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na. 9 ya mwaka 2022. Sheria inayopendekezwa ina Madhumuni ya kuweka masharti ya Mazingira bora kwa Wawekezaji Tanzania, kuweka Mfumo wa Kitaasisi kwa ajili ya Uratibu na Usimamizi wa Uwekezaji nchini na kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, utafiti unaonesha kuwa nchi nyingi duniani na zile zinazotuzunguka zimefanya mapitio ya Sheria za Uwekezaji ili kuweka mazingira bora na shindani kwa Wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuzingatia mabadiliko ya haraka katika Mifumo ya Kiuchumi duniani. Mapitio hayo yamewezesha kuboresha utoaji wa huduma na uratibu kwa Wawekezaji. Vile vile mapitio hayo yameimarisha utendaji wa Taasisi zinazohusika na Uwekezaji katika nchi hizo katika kutoa Huduma Mahala Pamoja kwa Ufanisi (True One Stop Centre) na kuzingatia ushiriki katika uchumi wa Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2020, Sura ya Pili **Ibara ya 22 Ukurasa wa 18-19 (a) - (L)** Serikali iliwaahidi Wananchi kuboresha mazingira ya Uwekezaji. Kwa kutaja mambo machache Chama kiliahidi: -

(a) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza Uwekezaji na kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje kwa kushirikisha Sekta Binafsi;

(b) Kuimarisha upatikanaji wa Ardhi ya Uwekezaji kwa kuhimiza Mamlaka za Serikali kujenga maeneo ya Uwekezaji, kulipa fidia na kuweka miundombinu ya Msingi ili kufanikisha Uwekezaji; na

(c) Kupitia upya taratibu za utoaji vibali vya ujenzi ili kuhakikisha kwamba vibali hivyo vinatolewa ndani ya siku saba za kazi.

Aidha, kutokana na hamasa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutangaza na kufungua mipaka ya uwekezaji nchini, nidhahiri kwamba Muswada huu unalenga kuweka Mfumo Madhubuti na Endelevu ambao utaondoa vikwazo na dosari zilizokuwa kikwazo kwa Wawekezaji nchini na hivyo kuwavutia Wawekezaji wengi kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tano zifuatazo: -

2.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inajumuisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na Jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi na tafsiri ya misamati na maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada unaopendekezwa.

2.2 Sehemu ya Pili ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka Mfumo wa Kitasisi wa Uratibu na Uwezeshaji wa Wawekezaji nchini, kuendelea kuwepo kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kuendelea kuwepo kwa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji, inaweka masharti yatakayokiwezesha Kituo kuanzisha Mfumo Unganishi wa Kielektroniki, Uanzishaji wa Bodi, Muundo na Majukumu yake, Vyanzo vya fedha vya Kituo na Utaratibu wa utunzaji na ukaguzi wa hesabu;

2.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali ya Uwekezaji. Ikiwemo kuzitaka Tasisi za Serikali kushirikiana na Kituo katika kutoa huduma kwa Wawekezaji kupitia Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja. Aidha, sehemu hii inaweka utaratibu wa maombi ya cheti cha Vivutio, muda wa uhai wa cheti hicho na vivutio anavyoweza kupata Mwekezaji. Vile vile sehemu hii inabainisha kuwa vivutio vinavyosimamiwa na Sheria nyingine yoyote vitatolewa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika Sheria hizo;

2.4 Sehemu ya Nne ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu Haki na Wajibu wa Serikali na Wawekezaji. Serikali inapewa haki ya kusimamia shughuli za Uwekezaji ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa kwa kuzingatia Misingi ya Sera na Sheria za nchi. Kwa upande wa Wawekezaji wanatakiwa kutii Sheria za nchi, kuendesha shughuli zao kwa namna inayolinda walaji, mazingira na Usawa wa Kijinsia na kutoa taarifa kwa Mamlaka mbalimbali za Serikali pale zitakapohitajika;

2.5 Sehemu ya Tano ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayohusiana na masuala ya Uwekezaji na adhabu zake pamoja na Mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria inayopendekezwa. Shemu hii pia inafuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 pamoja na kuweka masharti ya mpito kwa ajili ya masuala mbalimbali yaliyokuwa yanasimamiwa na Sheria inayopendekezwa kufutwa. Miongoni mwa masharti hayo ni kuendelea kutambuliwa kwa vivutio vilivyotolewa na Mikataba iliyoingwiwa na Wawekezaji chini ya Sheria inayopendekezwa kufutwa.

3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

3.1 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 24 (2) (a), (b), na (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia Vifungu vyote **37** vya Muswada na kujiridhisha na Malengo na Madhumuni ya Sheria inayotungwa katika Muswada huu.

3.2 Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 18/10/2022 ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu Malengo na Madhumuni ya Sheria hii.

3.3 Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, tarehe 19 Oktoba, 2022, Kamati ilikutana na kupokea maoni ya Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Mitandao ya Kijamii ili kusikiliza na kupokea maoni yao kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kitaalamu wa Muswada huu.

3.4 Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya Wadau Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya Wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Maoni ya Wadau kwa kiasi kikubwa

yameisaidia Kamati katika kufanya Uchambuzi wa Muswada na hatimaye kutoa maoni kwa Serikali.

3.5 Mheshimiwa Spika, Tarehe 21/10/2022 Kamati ilikutana na mtoa hoja, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kushauriana naye kuhusu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi uliofanyika. Yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Serikali ilikubali kuchukua Mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

3.6 Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wadau waliochangia katika Muswada huu wamekubaliana na Malengo na Madhumuni ya Muswada na kuipongeza Serikali kwa hatua hii ya kutunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania.

3.7 Mheshimiwa Spika, Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia Kifungu kwa Kifungu na baada ya kupokea na kuchambua Madhumuni na Malengo ya Muswada huu Kamati iliona kwamba kwa maslahi ya Sekta ya Uwekezaji Tanzania kuna haja ya kuvifanyia maboresho Vifungu 37 vya Muswada huu kwa kutazama mazingira tuliyonayo hapa Tanzania na kwa kutazama pia Sheria za namna hii zilivyo katika nchi nyingine (International Comparative Perspective).

3.8 Mheshimiwa Spika, baadhi ya Vifungu vilikuwa na makosa ya Sarufi, maana na mpangilio, tayari vimeingizwa katika jedwali la marekebisho la Serikali. Kwa mfano, katika Ibara ya 2 (5) ya Muswada sentensi "**Bila kujali Kifungu cha (1) Kituo kitawasaidia** Wawekezaji wote, Kamati imeshauri isomeke "**Kituo Kitawahudumia**". Serikali imeyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyajumuisha katika jedwali la marekebisho.

3.9 Mheshimiwa Spika, Vifungu ambavyo vilihitaji kuboreshwa zaidi ni kama ifuatavyo: - Kifungu cha 1 kuhusu Jina la Sheria, Kifungu cha Pili kuhusu Matumizi, Kifungu cha 3 kuhusu tafsiri ya neno mtaji, Kifungu cha 4, kuhusu kuendelea kuwepo kwa Kituo cha Uwekezaji, Kifungu cha 5 kuhusu malengo ya Kituo, Kifungu cha 6 Kuhusu majukumu ya Kituo, Kifungu cha 9 kuhusu uanzishwaji wa Bodi, Kifungu cha 13 kuhusu Maafisa na Wafanyakazi wengine wa Kituo, Kifungu cha 14 kuhusu Ukomo wa Uwajibikaji kwa Wajumbe wa Bodi na Wafanyakazi, Kifungu cha 18 kuhusu Kituo cha Huduma Mahala Pamoja, Kifungu cha 19 kuhusu Maombi ya Cheti na Usajili, Kifungu cha 20 kuhusu Uhai na kufutwa kwa cheti cha vivutio, Kifungu cha 21 kuhusu Uratibu wa uanzishwaji wa Taasisi za kibiashara, Kifungu cha 22 kuhusu Manufaa, Kifungu cha 23 kuhusu manufaa kwa Uwekezaji wa Kimkakati au Uwekezaji Maalum wa Kimkakati, Kifungu cha 26 kuhusu Wajibu wa Mwekezaji, Kifungu cha 27 kuhusu Dhamana dhidi ya kurekebishwa au kubadilishwa kwa manufaa, Kifungu cha 33 kuhusu Utatuzi

wa migogoro, Kifungu cha 34 kuhusu makosa na adhabu.

Aidha, Kamati inapendekeza **kiongezwe Kifungu kimpya cha 38 kuhusu namna Sheria itakavyo wasaidia, kuwawezesha na kuwalinda Wawekezaji Wazawa.**

3.10 Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, pande zote mbili zilikubaliana kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha Vifungu vyote vilivyokuwa na utata ili viwe bora zaidi.

3.11 Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati katika Muswada huu yamezingatia Uchambuzi wa Kitaalamu wa Muswada huu uliofanywa na Kamati kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kwenye Kamati.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali Kamati ilifanya Uchambuzi wa Muswada Kifungu kwa Kifungu hatua hiyo iliwezesha kutolewa kwa Maoni na Ushauri kwa Serikali kuhusu maboresho ya Vifungu vya Muswada kama ifuatavyo: -

4.1 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni na mapendekezo ya jumla yafuatayo:
-

4.1 Hadhi ya Kituo cha Uwekezaji ilivyo kwa sasa haiwezeshi Mfumo madhubuti wa Kitaasisi kwa ajili ya Uratibu na Uwezeshaji wa Uwekezaji nchini, kwa sababu hiyo, Kamati inapendekeza Kituo cha uwekezaji kipewe **Mamlaka kamili** badala ya kuendelea kuwa **Wakala wa Serikali**, lengo ni kukipa nguvu ya utekelezaji wa majukumu yake;

4.2 Kamati inapendekeza kuwa baada ya Sheria hii kutungwa na Bunge 'itafsiriwe katika **Lugha ya Kiingereza ndani ya siku 30**. Sababu ni uhalisia wa Uwekezaji ambao kutokana na vivutio katika Muswada huu Wawekezaji wengi wanatarajiwa kutoka mataifa mbalimbali.

4.3 Kamati inapendekeza Serikali iongeze **Kifungu cha 38** katika Muswada kitakachoeleza **namna ya kuwasaidia, kuwawezesha, na kuwalinda, Wawekezaji Wazawa.**

4.2 Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Vifungu vya Muswada

4.2.1 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 1 kuhusu Jina, Kamati inashauri Jina la Sheria lisomeke “**Sheria ya kuvutia na kulinda Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022**”.

4.2.2 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 3 cha Tafasiri, Kamati inashauri kuongezeke Maneno “**Ardhi**” na “**Hakimiliki**” (*Intellectual Property Right*) kwenye tafsiri ya neno “**Mtaji**”.

4.2.3 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 4 Kamati inashauri maelezo ya pembeni yasomeke “**Uwepo wa Kituo na Malengo**”.

4.2.4 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha **5 (1)** Kamati inashauri Kifungu hiki sasa **kisomeke 4 (4)**. Lengo ni kuweka mpangilio mzuri wa Vifungu vya Muswada.

4.2.5 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 5** Kamati inashauri maelezo ya pembeni yasomeke “**Kamati ya Taifa ya Uwekezaji**”.

4.2.6 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 5 (2) Kamati inashauri Kifungu hiki sasa **kisomeke 5(1)**, Kifungu cha **5(4) kisomeke 5(2)**, Kifungu cha **5(3)** kibaki kilivyo na Kifungu cha **5(5) kisomeke 5(4)** Lengo ni kuweka mpangilio mzuri wa Vifungu vya Muswada.

4.2.7 Mheshimiwa Spika, kuhusu Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji katika Kifungu cha 5 (2), Kamati inashauri kwamba aongezwe “**Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**”. Sababu ni kwamba Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiye mwenye dhamana ya kusimamia Sera ya Mambo ya Nje ambayo imejikita kwenye Diplomasia ya Uchumi. Huyu pia ndiye msimamizi wa Mabalazi walioko nje ya nchi wanaohamasisha na kuwavutia Wawekezaji wa Nje kuja kuwekeza nchini.

4.2.8 Mheshimiwa Spika, kuhusu neno kitawasidia katika Kifungu cha 6 (1) (f), Kamati inashauri lisomeke “**kitawahudumia**” Lengo ni kuleta maana nzuri ya jukumu la Kituo.

4.2.9 Mheshimimwa Spika, katika Kifungu cha 9 (2) kuhusu Wajumbe wa Bodi ya Kituo, Kamati inashauri kwamba **Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji uzingatie uwiano wa Kijinsia**. Lengo ni kuona kuwa uwakilishi wa Wanaume na Wanawake katika Wajumbe wa Bodi. Hii itasaidia pia kujenga uwezo wa Wanawake katika nafasi za Uongozi na Usimamizi bora wa utekelezaji wa Sheria hii kwa jicho la kutazama makundi yote katika Jamii.

4.2.10 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 9 (4) (b) (c) kuhusu muda wa Wajumbe wa Bodi kushika nafasi zao, Kamati inapendekeza kwamba muda

wa Wajumbe kushika nafasi zao iwe **miaka mitatu** kwa Makundi yote isipokuwa Mwenyekiti wa Bodi ibaki miaka Minne. Sababu ni kuondoa tofauti kati ya Wajumbe kutoka Serikalini na wa Sekta Binafsi.

4.2.11 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kufuta kwa maelezo ya Utangulizi Aya ya 13 kwa kufuta maneno “**Sekretarieti**” badala yake yatumike maneno “**Maafisa na Wafanyakazi wengine wa Kituo**” ili kuendana na maelezo ya Kifungu cha 13 cha Muswada huu.

4.2.12 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kufuta kwa maelezo ya Utangulizi **Aya ya 14** kwa kufuta maneno “**Ukomo wa uwajibikaji**” na badala yake yatumike maneno “**Kinga dhidi ya madai kwa Wajumbe wa Bodi na Wafanyakazi**” ambapo pia yatumika kwenye maelezo ya pembeni ya Kifungu cha 14 cha Muswada.

4.2.13 Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 18(4) kuhusu muda wa utoaji wa Leseni, Kamati inapendekeza muda wa Utoaji wa Leseni au Idhini uwe **siku 7 za kazi** kama ilivyobainishwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 Sura ya Pili Ibara ya 22 (L) Ukurasa wa 19 wa Ilani. Sababu ni kuwavutia Wawekezaji na kuondoa urasimu.

4.2.14 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 20 (1) (a)** na (b) kuhusu uhai na kufutwa kwa cheti cha vivutio, Kamati inashauri Muswada utoe tafsiri ya maana ya **vivutio vya kifedha na visivyo vya kifedha ili vijulikane** kwa urahisi na Wawekezaji wa ndani na wa kigeni, Wasomi na wasio wasomi.

4.2.15 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 22 (2) (d) na (e)** kuhusu manufaa, Kamati ilitoa maoni kuwa Muswada ufafanue utofauti wa magari hayo na endapo gari la mwekezaji mwenye cheti cha vivutio lisilotumika moja kwa moja kwenye mradi na lenye injini isiyozidi uwezo wa cc. 3000 lina sifa ya kupata vivutio. Baada ya kushauriana na Serikali, Serikali ilikubali kwamba kinachoelezwa kwenye **Aya ya (d)** tayari kimejumuishwa katika **Aya ya (e)**, hivyo ilikubali **kuondoa Aya (d)** ili kuondoa mkanganyiko kama inavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisha ya Serikali.

4.2.16 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 26** kuhusu Wajibu wa Mwekezaji, Kamati inashauri kiongezwe **Kifungu (g)** mara baada ya Kifungu (f) kitakachosomeka **(g) “kutunza taarifa za ukaguzi wa hesabu na fedha za kila mwaka na kuwasilisha taarifa hizo Kituoni”** na **(h) “kutekeleza Mradi kwa mujibu wa Mpango Kazi uliokubaliwa wakati wa maombi ya vivutio vya Uwekezaji”**.

4.2.17 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 33 (1)** kuhusu Utatuzi wa migogoro, Kamati inashauri kuongeza maneno “**ndani ya siku 60**” katikati ya neno majadiliano na ili. Sababu ni kuweka ukomo wa muda wa majadiliano.

4.2.18 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 34 (1)** Kamati inashauri isomeke faini **isiyopungua Milioni Tano** na **isiyozidi Milioni Kumi** au **kifungo kisichopungua miezi sita** au **kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja**.

4.2.19 Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 34 (2)**, Kamati inashauri kuongeza maneno **“au mwajiriwa wa Wizara, Idara au Taasisi ya Umma”** katikati ya neno Kituo na neno ambaye.

4.2.20 Mheshimiwa Spika, napenda kuliaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekubali mapendekezo mengi ya Kamati na kuyaweka katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa katika Bunge hili. Serikali pia imetoa maelezo ya ziada na ufafanuzi katika maeneo ya Muswada ambayo Kamati ilihitaji ufafanuzi.

4.21 Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba uchambuzi wa Kitaalamu uliofanywa katika Muswada huu utasaidia kupatikana kwa Sheria bora ya kusimamia Sekta ya Uwekezaji nchini na kufungua ukurasa mpya kwa Wawekezaji nchini Tanzania.

5.0 HITIMISHO

5.1 Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa fursa ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

5.2 Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashantu Kijaji (Mb), pamoja na Naibu Waziri Mhe. Kigahe Exaud Silaoneka (Mb) kwa ushirikiano wao wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

5.3 Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao: -

- Baraza la Kilimo Tanzania (ACT);
- Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS);
- Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS);
- Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- Shirikisho la Wafanyabiashara na Wawekezaji Tanzania (Tanzania Trade and Investment Coalition - TATIC),
- IResolve
- Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation), na;
- Umoja wa Makampuni ya Simu Tanzania (TAMNOA).

5.4 Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa maoni na ushauri wa msingi wa kuuboresha Muswada huu.

Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Eric James Shigongo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Mb – Mjumbe
7. Mhe. Usonge Hamad Juma, Mb – Mjumbe
8. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb – Mjumbe
9. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb – Mjumbe
10. Mhe. Lucy John Sabu, Mb – Mjumbe
11. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb – Mjumbe
12. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb – Mjumbe
13. Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb – Mjumbe
14. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb – Mjumbe
15. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Maryam Omar Said, Mb, - Mjumbe
18. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb – Mjumbe
20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb – Mjumbe
22. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb – Mjumbe
23. Mhe. Dkt. James Kimea Alfred, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Salim Hassan Turkey Toufiq, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb
26. Mhe. Hamis, Mohamed Mwinjuma mb, - Mjumbe

5.5 Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwihambi, ndc, kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, ndc, Mkurugenzi Masaidizi Ndg. Michael Chikokoto, ndc, Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Angelina Langisi Sanga, na Ndg. Nyamwanja C. Chilemeji, Wanasheria wa Bunge Ndg. Praisegod Zakaria Lukio, Ndg. Evelyne Shibandiko, na Ndg. Nesta Kawamala na Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

1 NOVEMBA, 2022

5.6 Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

David M. Kihenzile (Mb),
MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA.

Oktoba, 2022.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa maoni hayo ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa ili tutoe fursa kwa hoja nyingine iwasilishwe ili jioni tutakapokutana tuhitimisha hoja zote. Sasa nimwite katibu.

NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI.

Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022
(The Personal Data Protection Bill, 2022)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Mosses Nnauye, aje awasilishe muswada wake.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:
Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Bill, 2022*).

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu kwako pamoja na Bunge lako tukufu, Serikali yote chini ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri wote na Viongozi wote kwa ujumla katika nyanja mbalimbali, kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote hiki cha utumishi wangu kama Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kufikisha kwako salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu wa

Jimbo la Amani Mkoa wa Mjini Magharibi Mheshimiwa Mussa Hassan Musa kilichotokea Zanzibar Tarehe 13 Oktoba, 2022. Ninaomba utufikishie salamu hizi kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa na watu wote waliofikwa na msiba huo. Mungu aendelee kuilaza roho ya marehemu mahala pema peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu vema na kwa umahiri mkubwa. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuzindua matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, zoezi ambalo limekuwa na mafanikio makubwa sana. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayofanya katika kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita kwa weledi na umahiri mkubwa

Mheshimiwa Spika, vilevile nichuke nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyevidi wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Pia napenda kukupongeza kwa uteuzi wako kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia Kanda ya Afrika la Umoja wa Mabunge Duniani (*Chairperson of the African Geopolitical Group of Inter-Parliamentary Union (IPU)*). Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Ninawaahidi ushirikiano wangu na wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninawapongeza sana kwa ushiriki wenu kwenye kufanikisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Wizara.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru na kuwapongeza Watumishi wenzangu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wakiongozwa na Naibu Waziri Injinia Andrea Mathew Kundo, Watumishi wa Wizara hii chini ya Katibu Mkuu, Dkt. Jim Yonazi pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mohamed Khamis Abdulla kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Wizara, ikiwemo kutoa ushirikiano mkubwa katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu za dhati kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioalikwa na Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ipasavyo ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Bill, 2022*) kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Bill, 2022*) uliowasilishwa Bungeni kwa mara ya kwanza mnamo Tarehe 23 Septemba, 2022 unapendekeza kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Act, 2022*). Lengo la kutunga Sheria hii ni kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu tisa. Sehemu ya Kwanza yenye Vifungu cha 1 hadi 5 inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi, tafsiri, malengo ya sheria na misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Miongoni mwa malengo ya sheria hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa uchakataji wa taarifa binafsi unaongozwa na misingi ya sheria na kuweka utaratibu wa ushirikishwaji wa wahusika wa taarifa katika matumizi ya taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada yenye Vifungu vya 6 mpaka 13 inahusu masharti ya uanzishwaji na muundo wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na uteuzi wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu wa Tume. Kifungu cha 7 cha Muswada kinaainisha majukumu ya Tume ambapo miongoni mwa majukumu ni kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada yenye vifungu vya 14 hadi 21 inahusu masharti ya usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi. Aidha, ili kuiwezesha Tume kuwatambua watu wote wanaohusika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, usajili utatofautiana kati ya Taasisi

za Umma na Taasisi binafsi kwani kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria inayopendekezwa Taasisi zote za Serikali zinazohusika na ukusanyaji wa taarifa binafsi zitazingatiwa kuwa zimesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne yenye Vifungu kuanzia 22 mpaka 30 inaaanisha masharti kuhusu utaratibu wa ukusanyaji, utumiaji na uhifadhi wa taarifa binafsi. Aidha, Sehemu hii inaaanisha mazingira ambapo taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa. Masharti ya Sehemu hii pia yanazuia uchakataji wa taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mhusika wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano yenye Vifungu 31 na 32 vya Muswada inahusu masharti ya usafirishaji wa taarifa binafsi nje ya mipaka ya nchi yetu ambapo dhana ya utoshelevu itatumika kama kigezo kwa nchi ambazo zinaweza kupokea taarifa binafsi kutoka nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita yenye Vifungu 33 hadi 38 inaaanisha haki za mhusika wa taarifa binafsi ikijumuisha haki ya kupata taarifa zake, kusahihisha taarifa hizo na kuzuia uchakataji wa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ina Vifungu vya 39 mpaka 50 inahusu masharti ya kushughulikia malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria. Inapendekezwa Tume ipewe mamlaka ya kupokea malalamiko, kuyachunguza, kuyatolea maamuzi na kutoa adhabu ya faini za kiutawala.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane yenye Vifungu vya 51 mpaka 57 inaweka masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya mapato ya Tume na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu za Tume.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa na ya mwisho yenye Vifungu vya 58 hadi 65 ya Muswada inahusu masharti mengineyo ambayo ni pamoja na masharti kuhusu mazingira yanayopendekezwa kuondolewa katika mawanda ya Sheria. Lengo la masharti yanayopendekezwa ni kuifanya Serikali kutokuwa kikwazo katika utekelezaji wa shughuli muhimu za kijamii. Masharti mengine ni mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni chini ya Sheria inayopendekezwa, makosa na adhabu ikiwa ni pamoja na yale yanayotendwa na makampuni na matakwa kwa wakusanyaji wa taarifa kuandaa kanuni za maadili za Ulinzi wa Taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza Sheria tarajiwa kuwa na Jedwali moja ambalo limeandaliwa chini ya Kifungu cha 8(6) cha Muswada. Jedwali linaanisha masuala mbalimbali kuhusu Bodi ya Tume ikiwemo muda wa Wajumbe kushika nafasi, ukomo wa wajumbe, shughuli za Bodi kutobatilishwa kwa sababu ya kasoro, vikao vya Bodi, mgongano wa

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.34. Vol. 103 dated 31st August, 2022
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

maslahi,
mwaliko wa
mtaalamu,
akidi,
muhtasari wa
vikao, uamuzi
wa Bodi, na
malipo ya
Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa mwaka 2022 na kuupitisha katika hatua za Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimae kuwa Sheria ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

**MUSWADA WA SHERIA WA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WA MWAKA 2022
KAMA ULIVYOWASILISHWA BUNGENI**

MUSWADA WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WA MWAKA 2022

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu Jina

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI**

1. Jina na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Malengo ya Sheria.
5. Misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi.

**SEHEMU YA PILI
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

6. Uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.
7. Majukumu ya Tume.
8. Uanzishwaji wa Bodi.
9. Majukumu ya Bodi.
10. Kamati za Bodi.
11. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.
12. Muda wa kuhudumu wa Mkurugenzi Mkuu.
13. Watumishi wa Tume.

**SEHEMU YA TATU
USAJILI WA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI**

14. Usajili wa wakusanyaji na wachakataji.
15. Rejesta ya wakusanyaji na wachakataji.
16. Kipindi cha usajili.
17. Ukaguzi wa taarifa zilizosajiliwa.
18. Kufutwa kwa usajili.
19. Makosa yanayohusiana na usajili.
20. Rufaa kuhusiana na usajili.
21. Usajili wa taasisi za umma.

**SEHEMU YA NNE
UKUSANYAJI, UTUMIAJI, UFICHUAJI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI**

22. Ukusanyaji wa taarifa binafsi.
23. Chanzo na utoaji wa tarifa binafsi.
24. Taarifa binafsi kutumika kwa usahihi.
25. Taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.
26. Mipaka ya ufichuaji wa taarifa binafsi.
27. Usalama wa taarifa binafsi.
28. Uhifadhi na utoaji wa taarifa binafsi.
29. Usahihishaji wa taarifa binafsi.
30. Katazo la uchakataji wa taarifa binafsi nyeti.

**SEHEMU YA TANO
USAFIRISHAJI WA TAARIFA BINAFSI NJE YA NCHI**

31. Kusafirisha taarifa binafsi kwenda nchi yenye ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi.
32. Kusafirisha kwenda nchi isiyo na ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi.

**SEHEMU YA SITA
HAKI ZA WAHUSIKA WA TAARIFA**

33. Haki ya kupata taarifa binafsi.
34. Haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kumuathiri mhusika wa taarifa.
35. Haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya utangazaji wa biashara.
36. Haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa kiotomatiki.
37. Haki ya fidia.
38. Kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa binafsi.

**SEHEMU SABA
UCHUNGUZI WA MALALAMIKO**

39. Malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi.
40. Notisi ya uchunguzi.
41. Usiri wa uchunguzi.
42. Mamlaka ya Tume wakati wa uchunguzi.
43. Kuizua Tume.
44. Kutumia msaada wa mtu au ma`mlaka nyingine.
45. Notisi ya utekelezaji.
46. Notisi ya adhabu.

1 NOVEMBA, 2022

47. Faini za kiutawala.
48. Marejeo ya uamuzi.
49. Haki ya rufaa.
50. Malipo ya fidia.

SEHEMU YA NANE MASHARTI YA FEDHA

51. Vyanzo vya fedha za Tume.
52. Usimamizi wa fedha.
53. Makadirio ya mapato na matumizi na udhibiti wa fedha.
54. Matumizi ya fedha.
55. Makadirio ya nyongeza.
56. Akaunti na ukaguzi.
57. Taarifa za kila mwaka na mikataba ya utekelezaji.

SEHEMU YA TISA MASHARTI MENGINEYO

58. Mazingira yanayoondolewa katika mawanda ya Sheria hii.
59. Amri ya uhifadhi.
60. Makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria.
61. Makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria.
62. Makosa yanayotendwa na kampuni au shirika.
63. Adhabu ya jumla.
64. Kanuni.
65. Kanuni za maadili ya ulinzi wa taarifa binafsi.

JEDWALI

1 NOVEMBA, 2022

TAARIFA

Muswada huu unakusudiwa kuwasilishwa Bungeni hivyo umechapishwa kwa ajili ya taarifa kwa umma ukiwa pamoja na madhumuni na sababu zake.

Dodoma,
30 Agosti, 2022

HUSSEIN A. KATTANGA
Katibu Mkuu Kiongozi

Muswada
wa

Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa lengo la kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi, na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza
kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 na itanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar isipokuwa kwa Tanzania Zanzibar haitatumika kwa mambo yasiyo ya muungano.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
“afisa ulinzi wa taarifa binafsi” maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mkusanyaji na kupewa jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Sheria hii;
“kanuni za maadili” maana yake ni kanuni zinazobainisha maadili na miiko ya wachakataji na wokusanyaji wa taarifa binafsi zinazoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 65;
“mahakama” maana yake ni mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza suala husika;
“mchakataji” maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo inachakata taarifa binafsi kwa ajili na kwa niaba ya mkusanyaji chini ya maelekezo ya mkusanyaji, isipokuwa kwa watu ambao, chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya mkusanyaji, wanaruhusiwa kuchakata taarifa binafsi, na itajumuisha mwakilishi wake;
“mhusika wa taarifa” maana yake ni mhusika wa taarifa binafsi zinazochakatwa kwa mujibu wa Sheria hii;
“Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa

Tume aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11;

“mkusanyaji” maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo peke yake au kwa pamoja na taasisi nyingine huamua madhumuni na njia za uchakataji wa taarifa binafsi; na pale ambapo madhumuni na njia za uchakataji zimebainishwa katika sheria, “mkusanyaji” ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma iliyoteuliwa kwa mujibu wa sheria na itajumuisha mwakilishi wake;

“mpokeaji” maana yake ni mtu, taasisi nafsi, taasisi ya umma au mtu mwingine yeyote ambaye anapokea taarifa binafsi kutoka kwa mkusanyaji;

“mtaalamu wa afya” maana yake ni mtu anayetoa huduma za afya na kutambuliwa hivyo kwa mujibu wa sheria;

“mtoto” ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mtoto;

“mtu mwingine” maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma tofauti na-

- (a) mhusika wa taarifa;
- (b) mkusanyaji au mchakataji; na
- (c) mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kuchakata taarifa binafsi;

“nyaraka” maana yake ni njia yoyote ambayo taarifa imerekodiwa, iwe imechapishwa au ipo kwenye mkanda au filamu au kwa njia ya kielektroniki au vinginevyo na inajumuisha ramani, mchoro, picha, filamu, filamu ndogo, mkanda wa video, rekodi ya sauti au rekodi inayosomeka kwa mashine au rekodi yenye uwezo wa kuzalishwa kutoka kwa rekodi inayosomeka kwa mashine kwa njia ya vifaa au programu, au mchanganyiko wa zote mbili, vinavyotumiwa na mkusanyaji kwa madhumuni ya kutunza kumbukumbu;

“rejesta” maana yake ni rejesta iliyoanzishwa na Tume kwa mujibu wa kifungu cha 15;

“taarifa binafsi” maana yake ni taarifa kuhusu mtu anayetambulika ambazo zimetunzwa kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na-

- (a) taarifa binafsi zinazohusu rangi, asili ya kitaifa au kikabila, dini, umri au hali ya ndoa ya mtu binafsi;
- (b) taarifa binafsi zinazohusu elimu, historia ya matibabu, jinai, ajira au miamala ya kifedha ya mtu binafsi;
- (c) namba yoyote ya utambulisho, alama au namna nyingine maalum inayomtambulisha mtu binafsi;
- (d) anwani, alama za vidole au kundi la damu la mtu binafsi;
- (e) jina la mtu binafsi linaloonekana katika taarifa binafsi za mtu mwingine anayehusiana naye au pale ambapo ufichuzi wa jina hilo utadhihirisha taarifa binafsi za mtu;
- (f) taarifa iliyotumwa kwa mkusanyaji wa taarifa binafsi na mtu, ambayo ni wazi kuwa taarifa hiyo ni binafsi au ya siri, na majibu kwa taarifa hiyo yanaweza kufichua maudhui ya taarifa ya awali, na mtazamo au maoni ya mtu mwingine yeyote kuhusu mhusika wa taarifa;

“taarifa binafsi nyeti” inajumuisha-

- (a) taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto, taarifa

- inayohusu makosa, hukumu za jinai au hatua za kiusalama, taarifa za kibayometriki;
- (b) ikiwa imechakatwa, ni taarifa binafsi inayoonyesha asili ya rangi au kabila, itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, ushirika, uanachama wa vyama vya wafanyakazi, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na
 - (c) taarifa binafsi yoyote ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi inachukuliwa kuwa ina athari kubwa kwa haki na maslahi ya mhusika wa taarifa;
- “taarifa za vinasaba” maana yake ni taarifa binafsi yoyote inayotokana na uchambuzi wa tindikali ya vinasaba;
- “Tume” maana yake ni Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6;
- “uchakataji” maana yake ni uchambuzi wa taarifa binafsi, kwa njia za kiotomatiki au vinginevyo, kama vile kukusanya, kurekodi au kushikilia taarifa binafsi au kufanya uchambuzi kwenye taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na-
- (a) kuzipanga upya, kuzichukua na kuzitumia kama zilivyo au kuzibadilisha;
 - (b) kuzirejesha au kuzitumia; au
 - (c) kuziwianisha, kuzichanganya, kuzuia matumizi yake, kuzifuta au kuziharibu;
- “usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi” maana yake ni usafirishaji wowote wa taarifa binafsi wa kimataifa, unaovuka mipaka kwa njia za kielektroniki; na
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mawasiliano.

Malengo ya Sheria

4. Malengo ya Sheria hii ni-
- (a) kudhibiti uchakataji wa taarifa binafsi;
 - (b) kuhakikisha kwamba uchakataji wa taarifa binafsi za mhusika wa taarifa unaongozwa na misingi iliyowekwa katika Sheria hii;
 - (c) kulinda faragha za watu binafsi;
 - (d) kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa kulinda taarifa binafsi; na
 - (e) kuwapa wahusika wa taarifa haki na nafuu katika kulinda taarifa binafsi kutokana na uchakataji usiofuata masharti ya Sheria hii.

Misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi

5. Mkusanyaji au mchakataji atahakikisha kwamba taarifa binafsi-
- (a) zinachakatwa kihalali, kwa haki na kwa uwazi;
 - (b) zinakusanywa kwa madhumuni mahususi, yaliyobainishwa na halali, na taarifa hizo hazitaendelea kuchakatwa kwa namna tofauti na madhumuni yaliyoainishwa;
 - (c) zinatoshelwa na ni muhimu kwa madhumuni ya uchakataji kama ilivyokusudiwa;
 - (d) ni sahihi na pale inapobidi, zinaboreshwa kwa kuchukua hatua zote muhimu kuhakikisha taarifa binafsi zisizo sahihi zinafutwa au kurekebishwa bila kuchelewa;

1 NOVEMBA, 2022

- (e) zinahifadhiwa katika namna inayoruhusu utambuzi wa mhusika wa taarifa kwa muda usiozidi ule unaohitajika kwa madhumuni ya uchakataji wa taarifa binafsi husika;
- (f) zinachakatwa kwa kuzingatia haki za mhusika wa taarifa;
- (g) zinachakatwa kwa namna ambayo itahakikisha usalama wa taarifa binafsi, ikijumuisha ulinzi dhidi ya uchakataji usioruhusiwa au ulio kinyume cha sheria na dhidi ya hasara, uharibifu au madhara yoyote, kwa kutumia hatua sahihi za kiufundi au za kiutawala; na
- (h) hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume cha masharti ya Sheria hii.

SEHEMU YA PILI TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Uanzishwaji wa
Tume ya Ulinzi
wa Taarifa
Binafsi

6.-(1) Inaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

(2) Tume itakuwa taasisi nafsi yenye mamlaka ya urithishaji wa kudumu na lakiri yake, na kwa jina lake itakuwa na uwezo wa-

- (a) kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika, kutoa mali na kuingia mikataba au makubaliano mengine yoyote;
- (b) kushtaki au kushtakiwa; na
- (c) kutekeleza jukumu lolote lingine ambalo taasisi nafsi yoyote kisheria inaweza kutekeleza kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Majukumu ya
Tume

7. Majukumu ya Tume yatakuwa-

- (a) kufuatilia utekelezaji wa Sheria hii kwa wakusanyaji;
- (b) kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa Sheria hii;
- (c) kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;
- (d) kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;
- (e) kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;
- (f) kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;
- (g) kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii; na
- (h) kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Uanzishwaji wa Bodi

8.-(1) Inaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo itakuwa ni chombo cha usimamizi wa Tume na ambacho kitakuwa na wajumbe saba kama ifuatavyo:

- (a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti; na
- (b) wajumbe wengine watano.

(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watateuliwa na Rais kwa kuzingatia utaratibu kwamba iwapo Mwenyekiti anatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atatoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Wajumbe wengine watano chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) watateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa watu wenye sifa na uzoefu katika eneo la TEHAMA, sheria, uhandisi, fedha au utawala.

(4) Ili kudumisha uadilifu wa Tume na kwa madhumuni ya kuepusha mgongano wa maslahi, mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume iwapo kutokana na aina ya madaraka aliyonayo anaweza kuwa na ushawishi kwa Tume.

(5) Mkurugenzi Mkuu wa Tume atakuwa katibu wa Bodi.

(6) Masuala mengine kuhusu Bodi na uendeshaji wa shughuli zake yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Majukumu ya Bodi

9.-(1) Bodi itasimamia utendaji wa Tume ili kuhakikisha kuwa utendaji huo unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia Tume.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Bodi itakuwa na wajibu wa-

- (a) kutoa miongozo ya kimkakati na kuunda sera za uendeshaji na usimamizi wa Tume;
- (b) kusimamia shughuli na utendaji kazi wa menejimenti ya Tume;
- (c) kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, ikijumuisha kuidhinishwa kwa mpango kazi wa mwaka, bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza;
- (d) kuidhinisha mipango ya uwekezaji ya Tume;
- (e) kuidhinisha ripoti za utendaji kazi wa Tume;
- (f) kuidhinisha kanuni za maadili kwa watumishi wa Tume;
- (g) kuidhinisha na kusimamia taratibu za usimamizi wa fedha na kanuni za utumishi wa Tume;
- (h) kuidhinisha uondoshaji wa mali za Tume; na
- (i) kutekeleza wajibu mwingine wowote kwa kadri Tume itakavyoona inafaa kwa ajili ya kutimiza malengo yake kwa mujibu wa Sheria hii.

Kamati za Bodi

10. Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kuunda na kuteua kutoka miongoni mwa wajumbe wake, kamati zozote kadri itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu

11.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais.

1 NOVEMBA, 2022

(2) Mtu atateuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana sifa zifuatazo:

- (a) amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika na ana angalau shahada ya kwanza katika nyanja za TEHAMA, uhandisi, sheria, uchumi, fedha au utawala;
- (b) ana uzoefu wa utumishi usiopungua miaka kumi katika angalau moja ya nyanja zilizotajwa katika aya (a); na
- (c) ana ujuzi au utaalamu katika nyanja ya ulinzi wa taarifa.

Muda wa
kuhudumu wa
Mkurugenzi
Mkuu

12. Mkurugenzi Mkuu atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na baada ya kipindi hicho kumalizika, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Watumishi wa
Tume

13.-(1) Tume, kwa kuzingatia sheria za utumishi wa umma, itaajiri watumishi kwa idadi itakayohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume.

(2) Tume inaweza kuteua washauri na wataalam katika taaluma mbalimbali kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayowekwa na Tume.

SEHEMU YA TATU USAJILI WA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI

Usajili wa
wakusanyaji na
wachakataji

14.-(1) Mtu hatakusanya au kuchakata taarifa binafsi bila kusajiliwa kama mkusanyaji au mchakataji chini ya Sheria hii.

(2) Mtu anayekusudia kukusanya au kuchakata taarifa atawasilisha maombi ya usajili kwa Tume.

(3) Tume inaweza, katika muda utakaoainishwa katika kanuni, kukubali au kukataa maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2).

(4) Tume itatoa cheti cha usajili kwa mkusanyaji au mchakataji aliyekidhi matakwa ya usajili na kusajiliwa chini ya kifungu hiki.

(5) Endapo Tume itakataa maombi ya usajili itapaswa kumtaarifu mwombaji kwa maandishi juu ya uamuzi wake na sababu ya uamuzi huo.

Rejesta ya
wakusanyaji na
wachakataji

15.-(1) Tume itaanzisha na kutunza rejesta ya wakusanyaji na wachakataji waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Rejesta ya wakusanyaji na wachakataji itajumuisha taarifa kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Mkusanyaji au mchakataji anaweza, wakati wowote, kuomba kwa Tume kuhuisha au kubadili taarifa yoyote iliyoingizwa katika rejesta.

Kipindi cha
usajili

16.-(1) Kipindi cha usajili kitakuwa ni miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa kwa cheti cha usajili.

1 NOVEMBA, 2022

(2) Maombi ya kuhuisha usajili yatawasilishwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya kuisha kwa kipindi cha usajili kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Ukaguzi wa taarifa zilizosajiliwa

17. Kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni na baada ya kulipwa kwa ada iliyoainishwa, Tume inaweza kuruhusu mtu yeyote kupekua na kupakua taarifa yoyote iliyoingizwa katika rejesta.

Kufutwa kwa usajili

18. Tume inaweza kufuta usajili uliofanyika chini ya Sheria hii kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Makosa yanayohusiana na usajili

19. Mtu atakayekiuka masharti ya Sehemu hii au kutoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati wa usajili au uhuishaji anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika kifungu cha 63.

Rufaa kuhusiana na usajili

20. Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Tume chini ya Sehemu hii anaweza kuwasilisha rufaa kwa njia ya maandishi kwa Waziri.

Usajili wa taasisi za umma

21. Mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, taasisi za umma zinazoshughulika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi zitachukuliwa kuwa zimesajiliwa chini ya Sheria hii na zitapaswa kuzingatia masharti ya Sheria.

SEHEMU YA NNE UKUSANYAJI, UTUMIAJI, UFICHUAJI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI

Ukusanyaji wa taarifa binafsi

- 22.-(1) Sehemu hii itatumika kwa-
- (a) uchakataji wowote wa taarifa binafsi uliofanywa kwa taarifa yote au sehemu ya taarifa hiyo kwa njia ya kielektroniki au isiyo ya kielektroniki;
 - (b) uchakataji wa taarifa binafsi unaofanywa katika utekelezaji wa majukumu ya mkusanyaji anayeishi katika Jamhuri ya Muungano au katika sehemu ambayo sheria za Jamhuri ya Muungano zinatumika kwa mujibu wa sheria za kimataifa;
 - (c) uchakataji wa taarifa binafsi unaofanywa na mkusanyaji au mchakataji anayeishi nje ya Jamhuri ya Muungano, ikiwa uchakataji huo umefanyika nchini na sio kwa madhumuni ya kupitisha nchini taarifa binafsi kwenda nchi nyingine.
- (2) Mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi iwapo-
- (a) taarifa binafsi inakusanywa kwa madhumuni halali yanayohusiana na kazi ya mkusanyaji; na
 - (d) ukusanyaji wa taarifa binafsi ni muhimu au unatokana, au kuhusiana moja kwa moja, na madhumuni halali.
- (3) Mkusanyaji hatakusanya taarifa binafsi kwa njia zisizo halali.

Chanzo na
utoaji wa taarifa
binafsi

23.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi moja kwa moja kutoka kwa mhusika wa taarifa.

(2) Kabla ya kukusanya taarifa binafsi, mkusanyaji atahakikisha kuwa mhusika-

- (a) anatambua madhumuni ya ukusanyaji wa taarifa binafsi;
- (b) anafahamu kuwa ukusanyaji wa taarifa binafsi ni kwa madhumuni yaliyoidhinishwa; na
- (c) anawafahamu wapokeaji wa taarifa binafsi waliokusudiwa.

(3) Mkusanyaji hatalazimika kuzingatia kifungu kidogo cha (1) iwapo-

- (a) taarifa binafsi husika zimekwisha wekwa wazi;
- (b) mhusika wa taarifa binafsi ameidhinisha taarifa zake kukusanywa kutoka kwa mtu mwingine;
- (c) utekelezaji wake umeshindikana katika mazingira husika;
- (d) kutokutekelezwa kwake ni kwa mujibu wa sheria; na
- (e) utekelezaji wake unaweza kuathiri madhumuni ya ukusanyaji.

Taarifa binafsi
kutumika kwa
usahihhi

24. Kwa kuzingatia madhumuni ambayo taarifa binafsi zinapendekezwa kutumika, mkusanyaji ambaye ana taarifa binafsi hatatumia taarifa hizo kwa mazingira yaliyopo bila kuchukua hatua zinazohakikisha kuwa taarifa hizo zimekamilika, ziko sahihi, zinaendana na maudhui na hazipotoshi.

Taarifa binafsi
kutumika kwa
madhumuni
yaliyokusudiwa

25.-(1) Taarifa binafsi zilizokusanywa kwa mujibu wa Sheria hii zitatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

(2) Endapo mkusanyaji ana taarifa binafsi ambazo amekusanya kwa madhumuni maalum, anaweza kutumia taarifa hizo kwa madhumuni mengine iwapo-

- (a) mhusika ameidhinisha matumizi ya taarifa binafsi kwa dhumuni hilo;
- (b) matumizi ya taarifa binafsi kwa dhumuni hilo yameidhinishwa au kuhitajika kisheria;
- (c) dhumuni ambalo taarifa binafsi imetumika linahusiana moja kwa moja na dhumuni la ukusanyaji wa taarifa hiyo;
- (d) taarifa binafsi inatumika-
 - (i) kwa namna ambayo mhusika hatambuliki; au
 - (ii) kwa madhumuni ya takwimu au utafiti na haitachapishwa kwa namna ambayo inaweza kumtambulisha mhusika;
- (e) mkusanyaji anaamini kwa sababu za msingi kuwa matumizi ya taarifa binafsi kwa hayo madhumuni mengine ni muhimu ili kuzuia au kupunguza madhara kwa uhai au afya ya mtu husika au mtu mwingine, au kwa afya au usalama wa jamii; au
- (f) matumizi ya taarifa binafsi kwa hayo madhumuni

mengine ni muhimu katika uzingatiwaji wa sheria.

Mipaka ya
ufichuaji wa
taarifa binafsi

26. Endapo mkusanyaji ana taarifa binafsi, hatafichua taarifa hizo kwa mtu tofauti na mhusika wa taarifa, isipokuwa kwa mazingira yaliyoainishwa katika kifungu cha 25.

Usalama wa
taarifa binafsi

27.-(1) Mkusanyaji na wawakilishi wake watahakikisha kuwa taarifa binafsi zinalindwa, kwa kuchukua hatua za kiusalama zinazohitajika kwa usalama wa taarifa hizo dhidi ya upotevu wa kizembe, uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa binafsi bila idhini.

(2) Hatua za kiusalama zitakazochukuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) zinapaswa kuhakikisha kiwango cha usalama kinachohitajika kwa kuzingatia-

(a) mabadiliko ya kiteknolojia na gharama za kutekeleza hatua hizo; na

(b) aina ya taarifa binafsi inayopaswa kulindwa na madhara yanayoweza kutokea kwa mhusika wa taarifa.

(3) Mkusanyaji au mchakataji atapaswa kuteua afisa ulinzi wa taarifa binafsi atakayehakikisha hatua za kiudhibiti na za kiusalama zinachukuliwa ili kulinda taarifa binafsi zinazokusanywa au kuchakatwa.

(4) Utekelezaji wa shughuli za mchakataji utasimamiwa kwa mkataba utakaoainisha uhusiano kati ya mchakataji na mkusanyaji kwa namna ambayo mchakataji atatekeleza shughuli zake kwa maelekezo ya mkusanyaji, na kwamba pamoja na hayo, mchakataji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha anazingatia viwango vya usalama sawa na vinavyoelekezwa na Sheria hii.

(5) Mkusanyaji atakuwa na wajibu wa kuitaarifu Tume, haraka iwezekanavyo, kuhusu uvunjifu wa usalama unaoathiri taarifa binafsi zinazochakatwa kwa niaba ya mkusanyaji.

Uhifadhi na
utoaji wa taarifa
binafsi

28.-(1) Endapo mkusanyaji atatumia taarifa binafsi kwa madhumuni maalum kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25, atatakiwa kuhifadhi taarifa hizo kwa kipindi ambacho kitaainishwa katika kanuni ili kuhakikisha kuwa mhusika wa taarifa anapata fursa ya kuzipata taarifa hizo pale atakapozihitaji.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza, kwa kanuni, kuanisha taratibu za uhifadhi na uteketezaji wa taarifa binafsi alizonazo mkusanyaji kwa kuzingatia madhumuni ya uhifadhi.

Usahihishaji wa
taarifa binafsi

29.-(1) Endapo katika nyaraka au jalada ambalo upatikanaji wake umeruhusiwa chini ya Sheria hii kuna taarifa binafsi ambazo mhusika wa taarifa hizo anadai kuwa-

(a) hazijakamilika, sio sahihi au zinapotosha; au

(b) haziendani na dhumuni la uhifadhi wa taarifa husika,

mkusanyaji, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, na baada ya kupokea maombi ya mhusika wa taarifa na kujiridhisha nayo, anaweza kurekebisha taarifa hizo.

(2) Mkusanyaji, wakati wa kufanya marekebisho

kwenye taarifa binafsi chini ya kifungu hiki, atahakikisha kuwa hafuti kumbukumbu ya maandishi ya nyaraka kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho.

(3) Endapo mkusanyaji hataridhika na sababu za maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza kukataa kufanya marekebisho yoyote kwenye taarifa binafsi na kumtaarifu mwombaji sababu za kukataa maombi.

Katazo la
uchakataji wa
taarifa binafsi
nyeti

30.-(1) Mtu hatachakata taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi ya mhusika wa taarifa.

(2) Idhini chini ya kifungu kidogo cha (1) inaweza kuondolewa na mhusika wa taarifa wakati wowote na bila maelezo au gharama yoyote.

(3) Waziri, kupitia kanuni, anaweza kuamua mazingira ambayo katazo la uchakataji wa taarifa binafsi lililoelezwa chini ya kifungu hiki halitaweza kuondeva hata kwa ridhaa ya mhusika wa taarifa.

(4) Endapo mhusika wa taarifa ambaye ridhaa yake inaombwa kwa madhumuni ya Sheria hii ni mtoto, mtu asiyekuwa na akili timamu au mtu mwingine yeyote asiye na uwezo wa kutoa ridhaa, ridhaa ya mtu huyo itapatikana kutoka kwa mzazi, mlezi, mrithi, wakili wake au mtu mwingine yeyote anayetambulika kisheria kwa niaba yake anayepaswa kutoa ridhaa.

(5) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika iwapo-

- (a) uchakataji ni muhimu kwa uzingatiaji wa sheria nyingine;
- (b) uchakataji ni muhimu kulinda maslahi muhimu ya mhusika wa taarifa au ya mtu mwingine, iwapo mhusika wa taarifa hawezi kutoa ridhaa yake au hajawakilishwa na mwakilishi wake kisheria;
- (c) uchakataji ni muhimu kwa ajili ya kufungua, uendeshaji au utetezi wa madai ya kisheria;
- (d) uchakataji unahusiana na taarifa binafsi zilizowekwa wazi kwa umma na mhusika wa taarifa;
- (e) uchakataji ni muhimu kwa madhumuni ya tafiti ya kisayansi na Tume, kwa miongozo maalum, imeainisha mazingira ambayo uchakataji huo unaweza kufanyika; au
- (f) uchakataji ni muhimu kwa madhumuni ya kitabibu kwa maslahi ya mhusika wa taarifa, na taarifa binafsi nyeti zinazohusika, zinachakatwa chini ya usimamizi wa mtaalamu wa afya kwa mujibu wa sheria inayosimamia huduma hizo.

SEHEMU YA TANO

USAFIRISHAJI WA TAARIFA BINAFSI NJE YA NCHI

Kusafirisha
taarifa binafsi
kwenda nchi
yenye ulinzi wa
kutosha wa
taarifa binafsi

31.-(1) Tume inaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kuzuia usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi.

(2) Taarifa binafsi itasafirishwa kwenda nchi yenye mfumo wa kisheria unaotoa ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi

pale ambapo-

- (a) mpokeaji atabainisha kuwa taarifa binafsi ni muhimu kwa utekelezaji wa jukumu lenye maslahi ya umma au kwa mujibu wa shughuli halali za mkusanyaji wa taarifa binafsi; au
- (b) mpokeaji atabainisha umuhimu wa kusafirisha taarifa na hakuna sababu ya kudhani kwamba maslahi halali ya mhusika wa taarifa yanaweza kuathiriwa na usafirishaji au uchakataji katika nchi inayopokea.
- (3) Mkusanyaji atapaswa, bila kujali kifungu kidogo cha (2), kufanya tathmini ya muda mfupi ya umuhimu wa usafirishaji wa taarifa binafsi.
- (4) Mpokeaji atahakikisha kuwa umuhimu wa usafirishaji wa taarifa binafsi unaweza kuthibitishwa baadaye.
- (5) Mkusanyaji atahakikisha kwamba mpokeaji anachakata taarifa binafsi kwa madhumuni ambayo yalipelekea kusafirishwa kwa taarifa husika pekee.

Kusafirisha
kwenda nchi
isiyo na ulinzi
wa kutosha wa
taarifa binafsi

32.-(1) Taarifa binafsi zitasafirishwa kwenda nchi nyingine tofauti na zile zilizotajwa katika kifungu cha 31, ikiwa ulinzi wa kutosha umehakikishwa katika nchi ya mpokeaji na taarifa inasafirishwa kwa dhumuni la kuruhusu uchakataji ulioruhusiwa kufanyika na mkusanyaji.

(2) Utoshelevu wa kiwango cha ulinzi unaotolewa na nchi nyingine utatathminiwa kwa kuzingatia-

- (a) mazingira yote yanayozunguka usafirishaji wa taarifa binafsi husika;
- (b) aina ya taarifa binafsi;
- (c) madhumuni na muda wa uchakataji unaopendekezwa;
- (d) nchi ya mpokeaji;
- (e) sheria husika zinazotumika katika nchi nyingine; na
- (f) kanuni za kitaaluma na hatua za kiusalama ambazo zinazingatiwa katika nchi ya mpokeaji.

(3) Waziri baada ya kushauriana na Tume na kwa kupitia kanuni, ataainisha aina ya uchakataji na mazingira ambayo usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi hautaruhusiwa.

(4) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda kwa mpokeaji nje ya nchi au katika nchi ambayo haina uhakika wa ulinzi wa kutosha unaweza kufanyika pale ambapo-

- (a) mhusika wa taarifa ametoa idhini kwa usafirishaji unaopendekezwa;
- (b) usafirishaji ni muhimu kwa utekelezaji wa mkataba kati ya mhusika wa taarifa na mkusanyaji au utekelezaji wa hatua za awali za mkataba zilizochukuliwa kwa kujibu ombi la mhusika wa taarifa;
- (c) usafirishaji ni muhimu kwa ajili ya kuingia au kutekeleza mkataba ulioingiwa au utakaoingiwa kati ya mkusanyaji na mtu mwingine kwa maslahi ya mhusika wa taarifa;

- (d) usafirishaji ni muhimu au unahitajika kisheria kwa maslahi ya umma, au kwa ajili ya ufunguaji, uendeshaji au utetezi wa madai ya kisheria;
- (e) usafirishaji ni muhimu kwa ajili ya kulinda maslahi halali ya mhusika wa taarifa; na
- (f) usafirishaji unafanywa kwa mujibu wa sheria, unalenga kutoa taarifa kwa umma na unatoa fursa ya mashauriano kwa umma kwa ujumla au kwa mtu yeyote mwenye maslahi halali kuwasilisha maoni yake kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika sheria.

(5) Bila kuathiri masharti ya Sheria hii, Tume inaweza kuidhinisha usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nchi ya mpokeaji au nchi nyingine yoyote ambayo haijaweka ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi katika sheria zake, ikiwa mkusanyaji ataihakikishia Tume kwamba kuna ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi, uhuru na haki za msingi za mhusika wa taarifa, na utekelezaji wa haki za mhusika wa taarifa, na kwamba ulinzi huo unaweza kutekelezwa kupitia hatua zinazojitosheleza za kisheria, kiusalama na masharti husika ya mkataba.

SEHEMU YA SITA HAKI ZA WAHUSIKA WA TAARIFA

Haki ya kupata
taarifa binafsi

33.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mhusika wa taarifa ana haki ya-

- (a) kufahamishwa na mkusanyaji yeyote endapo taarifa binafsi zinachakatwa na mkusanyaji huyo au mkusanyaji mwingine kwa niaba ya mkusanyaji huyo;
- (b) kupewa na mkusanyaji maelezo ya-
 - (i) taarifa binafsi zinazomhusu;
 - (ii) madhumuni ya uchakataji; na
 - (iii) wapokeaji au makundi ya wapokeaji waliopewa au wanaoweza kupewa taarifa hizo;
- (c) pale ambapo uchakataji wa taarifa binafsi kwa njia ya kiotomatiki kwa madhumuni ya kutathmini masuala yanayomhusu, umetumika au unaweza kutumika kama msingi pekee wa maamuzi yenye athari kubwa kwake, kufahamishwa na mkusanyaji kuhusu sababu zilizotumika kufikia uamuzi huo.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), mkusanyaji hatalazimika kutoa taarifa kwa mhusika wa taarifa endapo taarifa hizo-

- (a) siyo sahihi;
- (b) zinahusika katika uchunguzi kwa mujibu wa sheria; au
- (c) zimezuiliwa kwa amri ya mahakama.

Haki ya kuzuia
uchakataji
unaoweza
kumuathiri
mhusika wa
taarifa

34.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), mhusika wa taarifa ana haki ya kumtaka mkusanyaji kupitia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, kusitisha au kutoanza uchakataji wa taarifa binafsi yoyote inayomhusu ikiwa

uchakataji huo unaweza kusababisha madhara makubwa kwake au kwa mtu mwingine.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika katika mazingira yaliyoondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii.

Haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya utangazaji wa biashara

35.-(1) Mhusika wa taarifa, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, anaweza kumtaka mkusanyaji kuacha kuchakata taarifa zake binafsi kwa madhumuni ya matangazo ya biashara.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mhusika wa taarifa anaweza kuingia mkataba na mkusanyaji kwa madhumuni ya kutumia au kuchakata taarifa zake binafsi kwa ajili ya kunufaika kifedha.

(3) Katika kifungu hiki “matangazo ya biashara” yanajumuisha wasilisho, kwa namna yoyote, ya tangazo la kibiashara linaloelekezwa kwa mtu fulani.

Haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa kiotomatiki

36.-(1) Mhusika wa taarifa anaweza, kupitia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, kumtaka mkusanyaji kuhakikisha kwamba uamuzi wowote unaofanywa na mkusanyaji au kwa niaba ya mkusanyaji ambao una athari kubwa kwa mhusika wa taarifa, hautegemei uchakataji kwa njia ya kiotomatiki pekee.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), pale ambapo uamuzi wenye athari kubwa kwa mhusika wa taarifa unategemea uchakataji wa kiotomatiki pekee-

(a) mkusanyaji atalazimika mapema iwezekanavyo kumtaarifu mhusika wa taarifa kwamba uamuzi ulichukuliwa kwa kutegemea uchakataji wa kiotomatiki; na

(b) mhusika wa taarifa anaweza kumtaka mkusanyaji kushughulikia upya uamuzi.

(3) Kifungu hiki hakitatumika ikiwa uamuzi uliofanywa-

(a) ni muhimu kwa ajili ya kuingia au kutekeleza mikataba kati ya mhusika wa taarifa na mkusanyaji;

(b) umeruhusiwa na sheria yoyote;

(c) ni kutokana na ridhaa iliyotolewa na mhusika wa taarifa.

Haki ya fidia

37.-(1) Mhusika wa taarifa atakayepata madhara kwa sababu za ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji kutokana na madhara hayo.

(2) Mhusika wa taarifa ambaye haki zake zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sheria hii atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji ikiwa-

(a) mlalamikaji ndiye mhusika wa taarifa aliyethiriwa;

(b) haki za mhusika wa taarifa zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji huo; na

(c) athari hizo zinahusiana na uchakataji wa taarifa binafsi kinyume na masharti ya Sheria hii.

(3) Endapo Tume itajiridhisha na maombi ya mhusika

wa taarifa-

- (a) kwamba amepata madhara kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi yoyote, katika mazingira yanayompatia haki ya kulipwa fidia chini ya kifungu hiki; na
- (b) kwamba kuna hatari kubwa ya ukiukwaji zaidi kuhusiana na taarifa binafsi husika katika mazingira hayo,

Tume inaweza kuamuru kurekebishwa, kuzuiwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.

(4) Tume, pale ambapo imetoa amri chini ya kifungu kidogo cha (3) na endapo itaona kuwa ni busara, inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kuwajulisha wahusika wengine ambao wamepatiwa taarifa binafsi kuhusu marekebisho, zuio, ufutaji au uharibifu wa taarifa hizo.

(5) Katika kuamua endapo ni sahihi kuhitaji taarifa chini ya kifungu kidogo cha (4), Tume itazingatia idadi ya watu ambao wataapaswa kuarifiwa.

Kurekebisha,
kuzuia, kufuta
na kuharibu
taarifa binafsi

38.-(1) Pale ambapo Tume itaridhika kwa maombi ya mhusika wa taarifa kuwa taarifa binafsi zinazomhusu mhusika huyo siyo sahihi, Tume inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kurekebisha, kuzuia, kufuta au kuharibu taarifa hizo.

(2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika hata kama taarifa binafsi ni kumbukumbu sahihi zilizopokelewa na mkusanyaji au mchakataji kutoka kwa mhusika wa taarifa au mtu mwingine.

(3) Pale ambapo taarifa binafsi siyo sahihi, Tume inaweza kumuelekeza mkusanyaji au mchakataji kurekebisha taarifa hizo kwa kadri itakavyoona inafaa.

(4) Pale ambapo taarifa binafsi zinazolalamikiwa zimerekebishwa, zimezuiwa, zimehuishwa, zimefutwa au zimeharibiwa chini ya kifungu hiki, mkusanyaji au mchakataji atatakiwa kuwataarifu wahusika wengine ambao walipatiwa taarifa binafsi husika kuhusu kurekebishwa, kuzuiwa, kuhuishwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.

SEHEMU YA SABA UCHUNGUZI WA MALALAMIKO

Malalamiko
dhidi ya
ukiukwaji wa
msingi ya
ulinzi wa taarifa
binafsi

39.-(1) Mtu yeyote anayehisi kuwa haki zake zimekiukwa katika mchakato wa-

(a) ukusanyaji, uhifadhi au uteketezaji wa taarifa binafsi na mkusanyaji; au

(b) matumizi au ufichuaji wa taarifa binafsi zinazohifadhiwa na mkusanyaji, anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume.

(2) Pale ambapo Tume imejiridhisha kuwa kuna sababu za msingi za kuchunguza suala chini ya Sheria hii, Tume inaweza kuanzisha uchunguzi wa malalamiko kuhusiana na suala hilo.

(3) Malalamiko yatakayowasilishwa katika kifungu hiki yatachunguzwa na kumalizika ndani ya siku tisini tangu tarehe

ya kupokelewa.

(4) Tume inaweza, kwa kuzingatia mazingira ya malalamiko, kuongeza muda ulioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa kipindi kisichozidi siku tisini.

Notisi ya
uchunguzi

40. Kabla ya kuanza uchunguzi wa malalamiko chini ya Sheria hii, Tume, katika namna itakayoainishwa katika kanuni, inapaswa kumpa notisi ya uchunguzi mkusanyaji anayehusika na malalamiko na nia ya kufanya uchunguzi katika suala hilo.

Usiri wa
uchunguzi

41.-(1) Uchunguzi wa malalamiko chini ya Sheria hii utafanyika kwa siri.

(2) Mkurugenzi Mkuu au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba yake ya kupokea taarifa binafsi zinazohusu uchunguzi wowote chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, atapaswa kukidhi matakwa yoyote ya kiusalama kwa kuchukua kiapo cha usiri kinachopaswa kuchukuliwa na watu ambao wanatekeleza majukumu kama hayo.

Mamlaka ya
Tume wakati
wa uchunguzi

42.-(1) Wakati wa kuchunguza malalamiko, Tume itakuwa na mamlaka ya-

- (a) kuita na kumtaka mtu kuhudhuria mbele ya Tume;
- (b) kupokea na kukubali ushahidi na taarifa nyingine, kwa kiapo au kwa hati ya kiapo au vinginevyo;
- (c) kuingia katika jengo lolote linalomilikiwa na mkusanyaji yeyote kwa ajili ya kujiridhisha endapo jengo hilo linakidhi mahitaji ya usalama;
- (d) kumhoji mtu yeyote au kuondoka na kifaa chochote chenye taarifa binafsi katika jengo lolote alimoingia kwa mujibu wa aya (c); na
- (e) kuchunguza au kupata nakala za, au dondoo kutoka kwenye vitabu, nyaraka au kumbukumbu nyingine zilizopatikana katika jengo alimoingia kwa mujibu wa aya (c) zenye suala lolote linalohusika na uchunguzi.

(2) Wakati wa uchunguzi wa malalamiko chini ya kifungu hiki, mlalamikaji na mkusanyaji anayelalamikiwa anaweza kupewa nafasi ya kufanya mawasilisho kwa Tume.

(3) Bila kujali sheria nyingine yoyote, Tume inaweza kuchunguza taarifa binafsi iliyorekodiwa katika namna yoyote inayohifadhiwa na mkusanyaji, na katika kufanya hivyo, Tume haitazuiliwa kupata taarifa yoyote.

(4) Nyaraka au andiko lolote litakalotolewa chini ya kifungu hiki na mkusanyaji au mtu mwingine yeyote litarejeshwa na Tume ndani ya siku kumi za kazi baada ya maombi kuwasilishwa kwa Tume na mkusanyaji au mtu huyo, lakini hakuna chochote katika kifungu kidogo hiki kitakachoizua Tume kuhitaji nyaraka au andiko hilo kuwasilishwa tena kwa mujibu wa kifungu hiki.

Kuizuia Tume

43. Mtu ambaye, kuhusiana na utekelezaji wa mamlaka iliyotolewa chini ya Sheria hii-

- (a) ataizua au kuikwamisha Tume katika utekelezaji wa mamlaka yake;

1 NOVEMBA, 2022

- (b) atashindwa kutoa msaada au taarifa zilizoombwa na Tume;
- (c) atakataa kuiruhusu Tume, inapotekeleza majukumu yake, kuingia katika majengo yoyote au kuondoka na nyaraka au kifaa chochote chenye taarifa binafsi; au
- (d) ataipa Tume taarifa yoyote ambayo ni ya uongo au ya kupotosha,

anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kutumia
msaada wa mtu
au mamlaka
nyingine

44.-(1) Kwa madhumuni ya kukusanya taarifa au kwa uchunguzi wowote chini ya Sheria hii, Tume inaweza kushirikiana au kumtumia mtu au mamlaka nyingine yoyote kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya kuisaidia Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Mtu au mamlaka nyingine itakayoshirikishwa au kutumiwa na Tume kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), itakuwa na mamlaka sawa na mamlaka iliyo nayo Tume katika kutekeleza mamlaka ya uchunguzi kwa mujibu wa Sheria hii.

Notisi ya
utekelezaji

45.-(1) Pale ambapo Tume imeridhika kuwa mtu ameshindwa kuzingatia kifungu chochote cha Sheria hii, Tume inaweza kutoa notisi ya utekelezaji kwa mtu huyo ikimtaka kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu ndani ya kipindi kitakachoainishwa katika notisi.

(2) Notisi ya utekelezaji itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1)-

- (a) itaainisha kifungu cha Sheria hii ambacho kimekiukwa;
- (b) itaainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana au kuondoa tatizo husika;
- (c) itabainisha kipindi ambacho hatua husika zitapaswa kutekelezwa ambacho hakitapungua siku ishirini na moja; na
- (d) itaeleza haki ya kukata rufaa.

Notisi ya
adhabu

46.-(1) Pale ambapo Tume itajiridhisha kuwa mtu ameshindwa au anashindwa kuzingatia notisi ya utekelezaji iliyotolewa chini ya kifungu cha 45, Tume inaweza kutoa notisi ya adhabu inayomtaka mtu kulipa kwa Tume faini ya kiasi kitakachoainishwa kwenye notisi.

(2) Katika kuamua iwapo inaweza kutoa notisi ya adhabu kwa mtu na kuamua kiasi cha adhabu, Tume itapaswa, kadiri itakavyoona muhimu, kuzingatia-

- (a) aina na uzito wa ukiukwaji, na muda ambao ukiukwaji huo umekuwa ukiendelea;
- (b) endapo ukiukwaji umefanywa kwa nia oву au uzembe;
- (c) hatua yoyote iliyochukuliwa na mkusanyaji au mchakataji ili kupunguza madhara waliyoyapata wahusika wa taarifa zikiwemo hatua za kiufundi na za kiutawala;

1 NOVEMBA, 2022

- (d) ukiukwaji aliowahi kufanya mkusanyaji au mchakataji awali;
- (e) kiwango cha ushirikiano alichoonesha kwa Tume kwa lengo la kurekebisha ukiukwaji na kupunguza athari hasi za ukiukwaji zinazoweza kujitokeza;
- (f) aina ya taarifa binafsi zilizoathiriwa na ukiukwaji;
- (g) namna ambayo Tume ilifahamu kuhusu ukiukwaji, ikijumuisha endapo mkusanyaji au mchakataji aliifahamisha Tume;
- (h) kiwango ambacho mkusanyaji au mchakataji alizingatia notisi za utekelezaji na notisi za adhabu zilizowahi kutolewa awali;
- (i) uzingatiaji wa kanuni za maadili au vigezo na masharti ya usajili;
- (j) endapo adhabu itakuwa na ufanisi; na
- (k) kigezo kingine chochote kinachoweza kutumika kuongeza au kupunguza adhabu, ikiwa ni pamoja na faida za kifedha alizozipata au hasara alizosababisha, moja kwa moja au vinginevyo, kutokana na ukiukwaji huo.

Faini za
kiutawala

47. Kiwango cha juu cha adhabu kinachoweza kutolewa na Tume katika notisi ya adhabu kuhusiana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii, ni shilingi milioni mia moja.

Marejeo ya
uamuzi

48.-(1) Tume baada ya kuombwa au kwa utashi wake yenyewe inaweza kufanya marejeo ya uamuzi na maelekezo yake iliyoyotoa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii.

(2) Baada ya kufanya marejeo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) Tume inaweza kutengua, kubadilisha au kusitisha uamuzi au maelekezo yake iliyoyotoa awali.

Haki ya rufaa

49. Mtu ambaye hataridhika na hatua yoyote ya kiutawala itakayochukuliwa na Tume, ikiwa ni pamoja na maelekezo yaliyotolewa katika notisi ya utekelezaji au adhabu iliyotolewa katika notisi ya adhabu, anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu.

Malipo ya fidia

50.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 37, Tume inaweza pamoja na adhabu nyingine zilizotolewa chini ya Sheria hii, kumuamuru mkusanyaji au mchakataji aliyesababisha madhara kwa mhusika wa taarifa kutokana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii kulipa fidia kwa mhusika wa taarifa.

- (2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1)-
 - (a) mkusanyaji anayehusika katika uchakataji wa taarifa binafsi atawajibika kwa madhara yatakayotokana na uchakataji huo; na
 - (b) mchakataji anayehusika na uchakataji wa taarifa binafsi atawajibika kwa madhara yatakayotokana na uchakataji huo ikiwa-
 - (i) hajatekeleza wajibu ulioelekezwa mahsusi kwa wachakataji chini ya Sheria hii; au
 - (ii) ametenda kinyume na maelekezo halali ya

1 NOVEMBA, 2022

mkusanyaji.

(3) Mkusanyaji au mchakataji hatawajibika kwa namna iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (2) ikiwa mkusanyaji au mchakataji huyo atathibitisha kuwa hakuhusika kwa namna yoyote katika tukio lililosababisha madhara.

(4) Katika sehemu hii, "madhara" yanajumuisha upotevu wa fedha na madhara yasiyohusisha upotevu wa fedha.

SEHEMU YA NANE MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya
fedha za Tume

51. Fedha za Tume zitajumuisha-
- (a) kiasi cha fedha ambacho kinaweza kutengwa na Bunge;
 - (b) fedha zitakazopatikana kutokana na huduma, ushauri au malipo mengine;
 - (c) fedha zitakazotokana na michango, zawadi au ruzuku;
 - (d) mikopo; na
 - (e) mapato mengine yatakayotokana na utendaji wa shughuli za Tume chini ya Sheria hii.

Usimamizi wa
fedha

52. Fedha za Tume zitasimamiwa na Bodi kwa mujibu wa sheria za fedha na zitatumika kugharamia matumizi yanayohusiana na utekelezaji wa majukumu ya Tume chini ya Sheria hii

Makadirio ya
mapato na
matumizi na
udhibiti wa
fedha

53.-(1) Mkurugenzi Mkuu atapaswa, katika kipindi kisichopungua miezi mitatu kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha katika Bodi ili kuidhinisha, bajeti inayojumuisha makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume itawasilisha nakala ya bajeti kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Waziri anaweza kuitaka Tume kufanya marekebisho katika bajeti ikiwa kwa maoni yake bajeti haiwakilishi makadirio sahihi na ya kuridhisha ya mapato na matumizi.

Matumizi ya
fedha

54. Matumizi hayatafanyika kutoka kwenye fedha za Tume isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bodi chini ya kifungu cha 53(1) kuhusiana na mwaka wa fedha ambao matumizi yaliidhinishwa.

Makadirio ya
nyongeza

55.-(1) Bodi inaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha husika, kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio yoyote ya nyongeza ya makadirio ya mwaka husika.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi Mkuu anaweza, pale ambapo dharura imetokea katika utekelezaji wa majukumu ya Tume, kufanya matumizi ambayo hayajaidhinishwa na Bodi ambapo Mkurugenzi Mkuu atalazimika, ndani ya miezi mitatu inayofuata, kuomba idhini ya Bodi kwa matumizi hayo.

Akaunti na ukaguzi

56.-(1) Tume itaweka vitabu vya hesabu na kutunza kumbukumbu sahihi za shughuli zake kwa mujibu wa viwango vya uhasibu.

(2) Tume itapaswa, ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, kuandaa ripoti ya utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka huo wa fedha, na nakala moja ya ripoti hiyo pamoja na nakala ya hesabu zilizokaguliwa zitawasilishwa kwa Waziri.

Sura ya 286

(3) Hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwingine aliyesajiliwa kama mkaguzi chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu aliyeteuliwa kwa dhumuni hilo.

Taarifa za kila mwaka na mikataba ya utekelezaji

57.-(1) Ndani ya muda wa miezi miwili baada ya kupokea hesabu zilizokaguliwa na taarifa ya mkaguzi wa hesabu, Mkurugenzi Mkuu atapaswa kuwasilisha kwa Waziri taarifa ya mwaka husika ikijumuisha-

- (a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya mkaguzi kwenye akaunti hizo;
- (b) taarifa ya utekelezaji wa malengo muhimu na taarifa nyingine yoyote inayohusiana na utekelezaji wa malengo hayo;
- (c) taarifa ya uendeshaji wa Tume katika mwaka wa fedha husika; na
- (d) taarifa nyingine kama ambavyo Waziri anaweza kuhitaji.

(2) Waziri atawasilisha Bungeni nakala ya taarifa ya mwaka ya Tume ndani ya miezi miwili au katika mkutano wa Bunge unaofuata.

SEHEMU YA TISA MASHARTI MENGINEYO

Mazingira yanayoondolewa katika mawanda ya Sheria hii

58.-(1) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachomuondolea mkusanyaji au mchakati wajibu wa kuzingatia misingi ya sheria katika ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi na uchukuaji wa hatua muhimu katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa taarifa binafsi alizonazo.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), uchakataji wa taarifa binafsi unaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii ikiwa uchakataji huo-

- (a) unafanywa na mhusika wa taarifa katika shughuli zake binafsi;
- (b) unafanywa kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote au amri ya mahakama;
- (c) unafanyika kwa madhumuni ya ulinzi na usalama wa Taifa na maslahi ya umma;
- (d) unafanyika kwa madhumuni ya kuzuia au kubaini uhalifu;
- (e) unafanyika kwa lengo la kubaini au kuzuia ukwepaji wa kodi;
- (f) unafanyika katika ukaguzi wa ubadhirifu wa fedha za umma; au

(g) ni kwa madhumuni ya upekuzi kwa ajili ya uteuzi katika nafasi ya utumishi wa umma.

(3) Waziri anaweza kuanisha mazingira mengine ambayo yanaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii na masharti mengine kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki.

Amri ya uhifadhi

59.-(1) Tume inaweza kuomba amri ya mahakama kwa ajili ya uhifadhi wa haraka wa taarifa binafsi yoyote, ikijumuisha taarifa binafsi zinazopita katika mfumo, endapo kuna sababu za msingi kuwa taarifa hizo zina hatari ya kupotea au kubadilishwa.

(2) Endapo mahakama itajiridhisha, chini ya kifungu kidogo cha (1), kuwa amri inaweza kutolewa chini ya kifungu kidogo hiki, itatoa amri ya uhifadhi inayoainisha kipindi kisichozidi siku tisini ambapo amri hiyo itatekelezwa.

(3) Mahakama inaweza, kwa maombi ya Tume, kuongeza muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa muda ambao mahakama itaona inafaa.

Makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria

60.-(1) Mkusanyaji ambaye, bila sababu za msingi, atafichua taarifa binafsi kwa njia yoyote ambayo haiendani na madhumuni ambayo taarifa hiyo imekusanywa anatenda kosa.

(2) Mchakataji ambae, bila sababu ya msingi, atafichua taarifa binafsi iliyochakatwa na mchakataji bila idhini ya awali ya mkusanyaji anatenda kosa.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (4), mtu ambaye-

(a) atapata taarifa binafsi, au atapata taarifa yoyote inayojumuisha taarifa binafsi, bila idhini ya mkusanyaji au mchakataji ambaye anahifadhi taarifa hiyo; au

(b) atafichua taarifa binafsi kwa mtu mwingine, anatenda kosa.

(4) Mtu atakayeza taarifa binafsi ambayo imepatikana kwa ukiukwaji wa kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (4), tangazo linaloonesha kwamba taarifa binafsi inauzwa au inaweza kuuzwa itachukuliwa kuwa ni ofa ya kuuza taarifa binafsi.

(6) Mtu atakayebainika kutenda kosa chini ya kifungu hiki atakapotiwa hatiani atawajibika-

(a) ikiwa ni mtu binafsi, kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungu kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja; na

(b) ikiwa ni kampuni au shirika, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi bilioni tano.

Makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi kinyume

61. Mtu ambaye ataharibu, atafuta, atapotosha, ataficha au kubadilisha taarifa binafsi kinyume cha sheria anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungu

1 NOVEMBA, 2022

cha sheria

kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Makosa yanayotendwa na kampuni au shirika

62. Pale ambapo kosa chini ya Sheria hii limetendwa na kampuni au shirika, kampuni au shirika hilo na kila afisa wa shirika ambaye kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au kuruhusu ukiukaji atawajibika kwa kosa hilo.

Adhabu ya jumla

63.-(1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria hii, anatenda kosa na pale ambapo hakuna adhabu mahususi iliyoainishwa, atakapotywa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(2) Baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, mahakama inaweza kuamuru kukamatwa kwa vifaa vyake vyenye taarifa binafsi vilivyohusika katika kutenda kosa.

Kanuni

64.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1), kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zinaweza kuainisha-

- (a) mazingira ambayo yataondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii;
- (b) taratibu za usajili chini ya Sheria hii;
- (c) majukumu ya afisa ulinzi wa taarifa kuhusiana na ulinzi wa taarifa binafsi;
- (d) majukumu ya mwakilishi wa mkusanyaji wakati wa kufanya kazi za ukusanyaji na uchakataji kwa niaba ya mkusanyaji;
- (e) taratibu za utekelezaji wa haki chini ya Sheria hii;
- (f) taratibu za uwasilishaji wa malalamiko chini ya Sheria hii;
- (g) masharti ya uchakataji wa taarifa binafsi nyeti;
- (h) viwango sahihi vinavyohusiana na usalama wa taarifa vinavyopaswa kuzingatiwa na wakusanyaji;
- (i) ada mbalimbali kuhusiana na shughuli za utekelezaji wa masharti ya Sheria hii;
- (j) taratibu za uhifadhi na utekelezaji wa taarifa binafsi zinazohifadhiwa na wakusanyaji;
- (k) aina ya uchakataji na mazingira ambayo usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi hautaruhusiwa;
- (l) jambo lolote ambalo ni muhimu au linafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kanuni za maadili ya ulinzi wa taarifa binafsi

65.-(1) Kila mkusanyaji atapaswa kutengeneza kanuni za maadili au sera kwa ajili ya ulinzi wa taarifa binafsi zitakazobainisha maadili na miiko inayopaswa kuzingatiwa wakati wa ukusanyaji au uchakataji wa taarifa binafsi.

(2) Kanuni au sera chini ya kifungu kidogo cha (1) zitawasilishwa kwa Tume kwa ajili ya mapitio na kuidhinishwa.

1 NOVEMBA, 2022

(3) Wakati wa mapitio wa kanuni au sera za maadili, Tume itajiridhisha, pamoja na mambo mengine, endapo rasimu za kanuni au sera za maadili zilizowasilishwa zimezingatia masharti ya Sheria hii na ya sekta husika na pale itakapooona inafaa, inaweza kutafuta maoni ya wahusika wa taarifa au wawakilishi wao na kushauriana na mkusanyaji husika kwa madhumuni ya kufanya marekebisho muhimu kabla ya kuziidhinisha.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8(6))

TARATIBU ZA BODI

Muda wa wajumbe
kushika nafasi

1.-(1) Muda wa wajumbe wa Bodi kushika nafasi utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti - miaka minne; na

(b) wajumbe wengine - miaka mitatu.

(2) Kila mjumbe anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mmoja zaidi na baada ya muhula huo kuisha, hatastahili kuteuliwa tena.

(3) Mjumbe yeyote anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa notisi ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na atakoma kuwa mjumbe kuanzia tarehe iliyoainishwa katika notisi au ikiwa hakuna tarehe iliyoainishwa, kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa notisi na mamlaka ya uteuzi.

Ukomo wa wajumbe

2. Mjumbe wa Bodi anaweza wakati wowote kukoma kuwa mjumbe kutokana na sababu zifuatazo:

(a) kupoteza uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili;

(b) tabia mbaya au utovu wa nidhamu kwa namna ambayo italetwa au kuwa na uwezekano wa kuleta sifa mbaya kwa Bodi;

(c) kutohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila kutoa taarifa; au

(d) kujiuzulu.

Kutokuhudhuria
vikao vya Bodi

3.-(1) Endapo mjumbe yeyote hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila taarifa, Bodi inaweza kuishauri mamlaka ya uteuzi kuhusu suala hilo na mamlaka ya uteuzi inaweza kutengua uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwingine badala yake.

(2) Iwapo mjumbe yeyote kwa sababu ya ugonjwa, udhaifu au kutokuwepo katika Jamhuri ya Muungano hawezi kuhudhuria kikao chochote cha Bodi, Waziri anaweza kuteua mjumbe wa muda badala yake na mjumbe huyo wa muda atakoma kushika wadhifa huo baada ya mjumbe husika kurejea katika nafasi yake.

Shughuli za Bodi
kutobalishwa kwa
sababu ya kasoro

4. Shughuli za Bodi hazitakuwa batili kwa sababu ya kutokamilika idadi ya wajumbe wakati wa kikao husika au kwa kasoro yoyote katika uteuzi wa mjumbe yeyote au kwa kigezo kuwa mjumbe yeyote wakati wa uteuzi hakuwa na sifa au hakustahili kuteuliwa.

1 NOVEMBA, 2022

Vikao vya Bodi

5.-(1) Bodi itakutana kila robo mwaka kwa nyakati na mahali itakapoona inafaa kwa ajili ya shughuli zake.

(2) Mwenyekiti au pale ambapo hayupo, Makamu Mwenyekiti, anaweza kuitisha kikao maalum au kikao cha dharura cha Bodi.

(3) Kikao cha kawaida cha Bodi kitaitishwa na Mwenyekiti na taarifa inayobainisha mahali, tarehe na muda wa kikao itatolewa kwa wajumbe si chini ya siku kumi kabla ya tarehe ya kikao na endapo Mwenyekiti hawezi kuitisha kikao kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine yoyote au hayupo katika Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao hicho.

(4) Bodi inaweza kuendelea na shughuli zake bila kujali kuwa nafasi yoyote ya ujumbe iko wazi.

Mgongano wa maslahi

6.-(1) Pale ambapo mjumbe wa Bodi wakati wowote ana mgongano wa maslahi kuhusiana na-

(a) suala lolote lililo mbele ya Bodi kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa;

(b) jambo lolote ambalo Bodi inaweza kutarajia kuwa linaweza kufika mbele yake kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa,

mjumbe atafichua mara moja mgongano wa maslahi kwa wajumbe wengine wa Bodi na kuacha kushiriki katika, au kuendelea kuwa sehemu ya, kujadili au kuamua jambo hilo.

(2) Iwapo Bodi itafahamu kwamba mjumbe ana mgongano wa maslahi kuhusiana na jambo lolote lililo mbele ya Bodi, itamuelekeza mjumbe huyo kutoshiriki au kutoendelea kushiriki katika kujadili au kuamua suala hilo.

(3) Mjumbe wa Bodi atachukuliwa kuwa amekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) ikiwa-

(a) atashindwa bila sababu za msingi kuweka wazi maslahi yake kama anavyotakiwa; au

(b) kwa kujua atatoa tamko la uongo au la kupotosha ambalo lina athari katika uamuzi,

mtu huyo atakuwa anatenda kosa na atapaswa kujiuzulu katika wadhifa wake.

Mwaliko wa mtaalamu

7. Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika mijadala ya Bodi na kutoa utaalum kama Bodi itakavyohitaji, lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi

8. Akidi katika kikao chochote cha Bodi itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi.

Muhtasari wa vikao

9. Muhtasari wa kila kikao cha Bodi utahifadhiwa na kuthibitishwa na Bodi katika kikao kitakachofuata.

Uamuzi wa Bodi

10. Uamuzi wa Bodi katika suala lolote utakuwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliopo na pale ambapo kura hizo zitalingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu.

Bodi kuendesha taratibu zake

11. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na mamlaka ya kusimamia taratibu zake kuhusiana na vikao na ufanyaji wa shughuli zake.

Malipo ya wajumbe

12. Wajumbe wa Bodi watalipwa ada na posho kama itakavyoamuliwa na mamlaka husika.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 kwa lengo la kuweka masharti ya misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; kukuza ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi pamoja na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka masharti ya utangulizi ambayo ni jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi yake na ufafanuzi wa maneno na misamiati iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, Sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Sehemu hii pia inaweka masharti kuhusu malengo ya Sheria inayopendekezwa na misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi. Miongoni mwa malengo hayo ni kuhakikisha kuwa uchakataji wa taarifa binafsi unaongozwa na misingi ya sheria na kuweka utaratibu wa ushirikishwaji wa wahusika wa taarifa katika matumizi ya taarifa zao.

Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu masharti ya uanzishwaji na muundo wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, uteuzi wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu. Sehemu hii inaainisha pia majukumu ya Tume ambapo miongoni mwa majukumu ya msingi ya Tume ni kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kwa lengo la kuwatambua, kupokea na kuchunguza malalamiko kutoka kwa wahusika wa taarifa na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na matumizi sahihi ya taarifa binafsi. Lengo la Sehemu hii ni kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi utakaosimamia udhibiti wa matumizi yasiyo sahihi ya taarifa binafsi.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inahusu masharti ya usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi. Sehemu hii pia inaainisha masharti ya vyeti vya usajili, ukaguzi wa taarifa zilizosajiliwa na kipindi cha usajili kwa lengo la kuhakikisha usimamizi thabiti wa watu wanaojihusisha na uchakataji wa taarifa binafsi. Aidha, ili kuiwezesha Tume kuwatambua watu wote wanaohusika na ukusanyaji na uchakati wa taarifa binafsi, Tume inapendekezwa kupewa mamlaka ya kuanzisha na kutunza rejesta itakayokuwa na taarifa zote za msingi kuhusiana na watu hao.

Sehemu ya Nne ya Muswada inaainisha masharti kuhusu utaratibu wa ukusanyaji, utumiaji na uhifadhi wa taarifa binafsi. Aidha, Sehemu hii inaainisha mazingira ambapo taarifa binafsi zinaweza kufichuliwa. Kwa mujibu wa Sehemu hii, mkusanyaji anaweza kutumia au kufichua taarifa binafsi endapo mhusika wa taarifa ameidhinisha matumizi au taarifa zake kufichuliwa kwa mtu mwingine. Vilevile, mkusanyaji anaweza kufichua taarifa binafsi endapo anatakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. Sehemu hii pia inaweka masharti mahsusi kuhusu usalama wa taarifa binafsi ambapo kila mkusanyaji anapaswa kuweka mfumo madhubuti wa kuhifadhi taarifa binafsi utakaozingatia mabadiliko ya teknolojia na aina ya taarifa zinazohifadhiwa. Masharti ya Sehemu hii pia yanazuia uchakataji wa taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mhusika wa taarifa. Taarifa binafsi nyeti zinazorejewa katika Sehemu hii ni pamoja na taarifa zinazohusu watoto, taarifa za kibayometriki, taarifa za itikadi za kisiasa na taarifa za kiafya.

Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu masharti ya usafirishaji wa taarifa binafsi nje ya nchi ambapo dhana ya utoshelevu itatumika kama kigezo kwa nchi ambazo zinaweza kupokea taarifa binafsi kutoka nchini. Dhana ya utoshelevu kwa mujibu wa masharti yanayopendekezwa inataka usafirishaji wa taarifa binafsi uhusishe nchi zenye mifumo ya sheria ya kutosha ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Sehemu ya Sita ya Muswada inaainisha haki za mhusika wa taarifa binafsi ikijumuisha haki ya kupata taarifa zake, kusahihisha taarifa hizo, haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kumuathiri mhusika wa taarifa na haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kwa madhumuni ya kutumika kibiashara kinyume na matakwa ya mhusika.

Sehemu ya Saba ya Muswada inahusu masharti ya kushughulikia malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa wajibu uliowekwa kisheria. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, inapendekezwa kuwa Tume ipewe mamlaka ya kupokea malalamiko, kuyachunguza na kuyatolea uamuzi kwa kuzingatia misingi iliyoainishwa kwenye Sheria. Katika Sehemu hii, Tume inapendekezwa kupewa pia mamlaka ya kutoa adhabu za faini za kiutawala pale itakapojiridhisha kwa kutegemea kiwango cha ukiukwaji uliofanyika. Aidha, sambamba na masharti ya adhabu, Sehemu hii pia inaweka masharti yanayoweza muathirika wa vitendo vinavyotokana na ukiukwaji wa Sheria hii kulipwa fidia kwa madhara atakayopata. Sehemu hii inatoa pia fursa ya rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Tume. Lengo la masharti ya Sehemu hii ni kuwa na mfumo mahsusi wa ushughulikiaji wa malalamiko yanayohusu taarifa binafsi.

Sehemu ya Nane ya Muswada inaweka masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya mapato ya Tume na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu za Tume. Moja ya vyanzo vya mapato vinavyopendekezwa katika Sehemu hii ni kiasi cha fedha ambacho kitatengwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inahusu masharti mengineyo ambayo imeonekana ni muhimu pia kujumuishwa katika Sheria inayopendekezwa. Miongoni mwa masuala muhimu katika Sehemu hii ni masharti kuhusu mazingira ambayo yanapendekezwa kuondolewa katika mawanda ya Sheria. Mazingira hayo ni pamoja na uchakataji wa taarifa binafsi kwa madhumuni ya ulinzi na usalama wa Taifa, kuzuia au kubaini uhalifu na ukwepaji wa kodi, ukaguzi wa ubadhirifu wa fedha za umma na ufanyaji wa upekuzi kwa ajili ya uteuzi katika nafasi ya utumishi wa umma. Lengo la masharti yanayopendekezwa ni kuifanya Sheria kutokuwa kikwazo katika utekelezaji wa shughuli muhimu za Serikali na kijamii. Masharti mengine katika Sehemu hii ni mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni chini ya Sheria inayopendekezwa, makosa na adhabu ikiwa ni pamoja na yale yanayotendwa na makampuni na matakwa ya wakusanyaji wa taarifa kuandaa kanuni za maadili za ulinzi wa taarifa binafsi.

Dodoma,
29 Agosti, 2022

NAPE MOSES NNAUYE
Waziri wa Habari, Mawasiliano
na Teknolojia ya Habari

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso aje awasilishe maoni ya Kamati

MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022. Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge, siku ya Alhamis, Tarehe 23 Septemba, 2022. Hatua hiyo ilifuatiwa na uamuzi wako wa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ukiongozwa na masharti ya Kanuni ya 97 (1) na Kanuni 136 (14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Bunge niliyoirejea awali, inaitaka Kamati inayohusika ipange kuujadili Muswada mapema iwezekanavyo. Kwa kutambua masharti hayo, mapema wakati wa Vikao vya Kamati za Bunge vya Tarehe 17 – 28 Oktoba, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilianza kuufanyia kazi Muswada huu. Uchambuzi wa Muswada huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa fasili ya 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya Kamati kuchambua Muswada huu ni kuhakiki mapendekezo katika Muswada huu ili kubaini kama kuna maslahi yoyote kwa Bunge na kutunga Sheria inayopendekezwa. Kamati ilibaini kwamba kuna maslahi mahsusi katika Muswada huu yenye manufaa yanayoweza kupatikana kwa kuweka masharti ya msingi kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa jumla wakati wa uchambuzi wa Muswada huu ulilenga kuliwezesha Bunge kuzingatia ahadi za Serikali kwa wananchi na misingi ya uendeshaji wa sekta ndogo ya teknolojia ya habari nchini. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linatarajiwa kutengeneza misingi ya kisheria ya kulinda haki za wananchi. Katika Sheria hii haki hizo zitalindwa wakati wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi utakaofanywa na vyombo vya Serikali au binafsi kwa namna inayozingatia maslahi ya Umma na uhai endelevu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu pamoja na matokeo ya Uchambuzi. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kuamua, taarifa hii inajumuisha maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kama inavyoonekana katika Taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu zilizotumika. Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, imeweka sharti kwa Taarifa ya Kamati kuonesha njia au mbinu zilizotumika kufanya kazi inayoripotiwa. Aidha, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuhakiki uthabiti wa matokeo ya

uchambuzi wa Muswada huu, naomba kubainisha njia au mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu kama ifuatavyo: -

- (i) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Njia hii iliwezesha Kamati kupata mantiki ya mambo na masharti mbalimbali yanayopendekezwa;
- (ii) Kufanya mapitio ya maudhui ya Muswada kuanzia jina refu la Muswada hadi sababu na madhumuni. Lengo la kufanya hivyo ni kubaini masharti ya kisheria yanayopendekezwa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Njia hiyo ni muhimu kupata tathmini ya jumla kuhusu kufaa au kutokufaa kwa mapendekezo katika Muswada huu;
- (iii) Kuoanisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria iliyojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za umma chini ya sekta ndogo ya teknolojia ya habari;
- (iv) Kujadili dhana kuu ya ulinzi wa Taarifa binafsi ambayo ni kiini cha Sheria hii inayokusudiwa kutungwa na Bunge. Njia hii imesaidia kujenga mtazamo mpana kwa ajili ya kuhakiki maudhui ya Muswada kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi; na
- (v) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kama inavyoelekezwa na masharti ya Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Njia hii ililenga kuliwezesha Bunge kuendelea kuzingatia mtazamo wa umma katika utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, njia hizo kwa ujumla wake zimeiwezesha Kamati kuchambua Muswada huu kwa ukamilifu. Ni imani ya Kamati kuwa matumizi ya njia hizo yanaipa taarifa hii uwezo wa kulisaidia Bunge kukidhi matarajio ya wananchi wakati wa kuamua kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa Muswada. Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki mpangilio, masharti, maudhui na dhamira kwa ujumla. Uhakiki ulifanyika kwa mapitio ya jumla ya maudhui na baadae uchambuzi wa Ibara kwa Ibara. Lengo kuu katika hatua hiyo lilikuwa ni kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria yanayopendekezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilijikita kwenye uchunguzi wa matini ya Muswada ili kujiridhisha na:-

- (i) Iwapo kuna mahitaji ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;
- (ii) Iwapo masharti yanayopendekezwa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi yanaendana na ahadi na mwelekeo wa jumla wa Nchi, Kanda na Dunia;

- (iii) Iwapo mpangilio, masharti na maudhui vinakidhi mahitaji ya kuwa na sheria inayopendekezwa; na
- (iv) Iwapo Bunge likiupitisha Muswada huu litakuwa limezingatia misingi ya utungaji wa sheria inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yanaweza kubainika vizuri kwa muundo wa matokeo ya uchambuzi unaoelezwa katika taarifa hii. Kimtiririko, taarifa hii inabainisha upembuzi wa maudhui ya lbara za Muswada wa Sheria ili kujiridhisha endapo yanakidhi mahitaji. Kamati inaamini kuwa mtiririko huu utaliwezesha Bunge kufanya uamuzi unaotatua tatizo kuhusu haki za taarifa binafsi kisheria au kuziba ombwe kuhusu taarifa binafsi ipasavyo kwa kuzingatia misingi ya utungaji wa Sheria bora.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya uchambuzi wa Muswada huu ni kubaini uthabiti wa masharti na maudhui yanayopendekezwa ili kulishauri Bunge inavyostahili. Kwa ujumla utaratibu wa Kibunge wa kushughulikia hoja hadi kufikia uamuzi, unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki na upembuzi wa kina wa hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu ili kuliwezesha Bunge kupata undani wa jambo linalolengwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza mtoa hoja mapema leo hii, Muswada huu ni pendekezo la Sheria inayokusudia kuweka masharti kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi wakati wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa hizo, unaofanywa na vyombo vya serikali na binafsi. Kwa madhumuni hayo, jambo kuu la kulichunguza kwa undani ni ulinzi wa taarifa binafsi (*data protection*). Kwa tafsiri ya jumla, ulinzi wa taarifa binafsi ni udhibiti wa kisheria wa taarifa binafsi katika upatikanaji, uchakataji na matumizi ya taarifa hizo zinazokusanywa na kuchakatwa na vyombo vya Serikali au binafsi.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa taarifa binafsi unawahakikishia wananchi usalama wa taarifa zao ili kulinda heshima na kuhifadhi utu wao. Aidha, kukosekana kwa ulinzi wa taarifa binafsi kunaweza kuwa na madhara kwa usalama wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi (*personal data*) katika vyombo vya Serikali na binafsi unahitaji kuwekewa misingi na masharti ili kudhibiti matumizi ya taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo, Kamati ilihitaji kubaini pengo la kisheria kuhusu udhibiti wa taarifa binafsi zinazokusanywa na kuchakatwa na vyombo vya Serikali au binafsi. Ubainishaji wa pengo hilo ulifanyika kwa kupata mtazamo wa jumla kuhusu udhibiti huo pamoja na mwelekeo unaotolewa na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa nchi yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa jumla kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi (*personal data protection*) umejengwa kwa Kamati kupitia machapisho mbalimbali yanayohusu udhibiti wa taarifa zilizokusanywa ulivyo duniani, Afrika na kikanda. Utaratibu huu unaweza kutoa uzoefu juu ya udhibiti wa kisheria wa taarifa binafsi katika upatikanaji wa matumizi taarifa hizo ambazo hukusanya na kuchakatwa na vyombo vya Serikali au binafsi.

Mheshimiwa Spika, kupitia machapisho mbalimbali Kamati ilibaini kuwa dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi inahitaji kuwekewa masharti ya kisheria ili kulinda usalama wa utu wa watu katika kila nchi. Mahitaji hayo yamebainika katika mapitio ya misingi ya ulinzi na faragha za taarifa binafsi iliyowekwa na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (*UNESCO*). Miongoni mwa misingi hiyo ni masharti ya kutumia taarifa binafsi kwa kuzungatia ustirifu, usikilifu.

Mheshimiwa Spika, kutoka na misingi ya ulinzi (*protection*) wa faragha (*privacy*) iliyobainishwa na *UNESCO*, Kamati imeridhia kwamba upo umuhimu wa kuweka masharti ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi chini katika vyombo vya Serikali na binafsi na namna inavyozingatia ustirifu wa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kikanda, Kamati ilitafuta uzoefu ndani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) na kwenye nchi za Afrika Mashariki. Lengo ni kujifunza namna nchi nyingine zilivyodhibiti taarifa binafsi zilizokusanywa na kuchakatwa katika vyombo vya Serikali na binafsi. Uzoefu huo ni sehemu muhimu ya kuliwezesha Bunge kuamua kuupitisha au kutokuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa *SADC*, Jumuiya hiyo iliweka Sera iliyotoa mwongozo kuhusu usawa wa sheria zinazohusu ulindwaji wa taarifa na teknolojia ya habari. Sera hiyo pamoja na mambo mengine inasisitiza nchi wanachama kuwa na mifumo itakayosaidia kupambana na ukiukwaji wa haki ya ulinzi wa taarifa binafsi katika ukusanyaji, uchakataji, usambazaji, uhifadhi na utumiaji wa taarifa hizo. Kwa msisitizo huo, Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi wanachama wa *SADC*, inahitaji Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hivyo, Muswada huu umeletwa katika muktadha unaoendana na hali halisi.

Mheshimiwa spika, Kwa kuongeza uelewa, Kamati imepitia Mwongozo wa Sheria kuhusu Muswada ya Kimtandao wa Mwaka 2008 wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwongozo huu unabainisha maeneo muhimu kwa nchi wanachama kuzingatia katika utungaji wa Sheria za Kimtandao ikiwemo kulinda taarifa binafsi za watumiaji wa mitandao. Kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi, mwongozo huo unasisitiza wajibu wa vyombo vinavyokusanya na kuchakata taarifa binafsi kuzingatia haki za mhusika wa taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msisitizo huo, Kamati ilibaini kwamba, Tanzania nayo inahitaji kuwa na Sheria inayotaja wajibu wa vyombo vinavyohusika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuzingatia haki ya mhusika wa taarifa hizo. Mahitaji hayo pamoja na mengineyo ni miongoni mwa mambo yanayopaswa kulisukuma Bunge kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Jambo muhimu kwa Bunge lako Tukufu ni kuhakiki masharti ya sheria inayopendekezwa kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi na kujiridhisha kama yanaweza kupitishwa kama yalivyo au kurekebisha kwa kadiri inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mtazamo wa jumla duniani, Afrika na Kikanda, Kamati inatafuta uzoefu wa nchi zingine kama vile Kenya na Uganda kwa Afrika Mashariki na Zambia, Madagascar na Botswana kwa nchi za SADC. Katika nchi hizo zimetungwa Sheria zinazohusu udhibiti wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa nchini Kenya kuna Sheria ya Ulinzi wa Data (*Data Protection Act*) ya Mwaka 2019. Sheria hiyo imeanzisha Ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data inayoongozwa na Kamishna wa Data. Kwa wenzetu wa Uganda, Bunge lilitunga Sheria ya Ulinzi wa Data na Faragha ya Mwaka 2019 (*Data Protection and Privacy Act, 2019*). Sheria hiyo imeanzisha Ofisi ya Ulinzi wa Data Binafsi chini ya Mamlaka ya Taifa ya Teknolojia ya Habari (*National Information Technology Authority – NITA*). Kwa upande wa Zambia, Bunge lilitunga Sheria ya Ulinzi wa Data ya Mwaka 2021...

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nusu saa naambiwa hapa zimebaki dakika nne. Kwa hiyo naomba ujielekeze kwenye maoni na ushauri ili muda usije ukaisha halafu taarifa yako utaseme iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama ulikuwa hujasema hapo mwanzo, kama ulishasema basi malizia maoni, muda umebaki mfupi.

MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri; kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

- (a) Serikali iweke wazi vyanzo vya fedha vitakavyotumika kuendesha shughuli za Tume katika kusimamia mambo ya ulinzi wa Taarifa Binafsi.
- (b) Kwa kuzingatia kwamba, kanuni ni nyenzo muhimu inayofafanua utekelezaji wa masharti ya sheria inayohusika, Serikali isimamie vyema utungaji wa Kanuni za Sheria hii ili zisipishane na dhamira ya Bunge na zisikose uhalisia.

- (c) Haki ya wahusika wa Taarifa (*data subjects*) walioachana na taarifa zilizokusanywa kuendelea kuhusishwa na taarifa hizo tofauti na utashi wao izingatiwe katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Aidha, Stahili ya Marehemu kuhusu ulinzi wa taarifa zake iwekewe utaratibu wa kuizingatia.
- (d) Ili kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria inayotungwa na Bunge, vigezo au sababu zinazoweza kutumiwa kufuta usajili wa Mkusanyaji au Mchakataji wa Taarifa Binafsi viwekwe wazi.
- (e) Kwa madhumuni ya kuzingatia misingi ya utawala bora wakati wa utekelezaji wa Sheria hii, ni vizuri kuzingatia suala la jinsia katika uteuzi wa wajumbe wa bodi.

Mheshimiwa Spika, maoni haya, yanatokana na matokeo ya Uchambuzi uliofanyika. Aidha, yamezingatia muafaka uliofikiwa kati ya Waziri na Kamati baada ya uchambuzi na mashauriano. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi, makubaliano ya Kamati na Waziri na maoni haya niliyoyatoa, vitawezesha majadiliano yatakayosaidia Sheria bora inayopitishwa leo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nashukuru kwa uamuzi wako wa kuleta Muswada wa Sheria wa ulinzi wa taarifa binafsi kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Uzoefu wa wajumbe katika Sekta ya Habari na Mawasiliano umekuwa mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi. Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya wadau umesaidia kupata mawazo yenye tija katika uzingatiaji wa maslahi ya umma wakati wa kujadili Muswada huu. Kwa hatua hii niwashukuru tena wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Wadau hao ni; Tume ya haki za binadamu, Muungano wa mabenki Tanzania, Jamii Forum, Muungano wa Kampuni za simu Tanzania – TAMULOA, *Multi Choice*, *Tanganyika Law Society*, *Vodacom*, *Legal human Centre* na *GSMA*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha ukamilifu wa taarifa hii. Ninaamini kwa taarifa hii, Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua na kuzingatia maslahi ya umma, taifa na uhai endelevu wa nchi yetu. Aidha, niwashukuru wajumbe wote ambao walishiriki.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Moses Nawiye na Wataalamu mbali mbali kutoka Serikalini kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi Muswada. Maelezo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati. Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelewa Mwihambi, na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu

Athuman Hussein kwa kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru Ndugu Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi na Makatibu wa Kamati Ndugu Janeth Malangu na Ndugu Victory Mrema, pamoja na Ndugu Grace Samweli, Msaidizi wa Shughuli za uratibu, kwa kufanikisha kazi za Kamati kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU
MUSWADA WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WA MWAKA 2022 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa binafsi ya Mwaka 2022 (The Personal Data Protection Bill 2022). Muswada huu ulisomwa mara ya kwanza Bungeni wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge, siku ya Alhamisi, tarehe 23 Septemba, 2022. Hatua hiyo ilifuatiwa na uamuzi wako wa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ukiongozwa na masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** na **Kanuni 136 (14)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Bunge niliyoirejea awali, inaitaka Kamati inayohusika ipange kuujadili Muswada mapema iwezekanavyo. Kwa kutambua masharti hayo, mapema wakati wa vikao vya Kamati za Bunge vya tarehe 17 – 28 Octoba, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilianza kuufanyia kazi Muswada huu. Uchambuzi wa Muswada huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **fasili ya 7(1) (b)** cha **Nyongeza ya Nane** ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya Kamati kuchambua Muswada huu ni kuhakiki mapendekezo katika Muswada huu ili kubaini kama kuna maslahi yoyote kwa Bunge ya kutunga Sheria inayopendekezwa. Kamati ilibaini kwamba kuna Maslahi mahususi katika Muswada huu

yenye manufaa yanayoweza kupatikana kwa kuweka masharti ya msingi kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

1.2 Mwelekeo wa Jumla wakati wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa Jumla wakati wa Uchambuzi wa Muswada huu ulilenga kuliwezesha Bunge kuzingatia ahadi za Serikali kwa wananchi na misingi ya uendeshaji wa Sekta ndogo ya teknolojia ya habari nchini. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linatarajiwa kutengeneza misingi ya kisheria ya kulinda haki za wananchi. Katika sheria hii haki hizo zitalindwa wakati wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi utakaofanywa na vyombo vya serikali au binafsi kwa namna inayozingatia maslahi ya Umma na uhai endelevu wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kwa msingi huo, taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu pamoja na matokeo ya Uchambuzi. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kuamua, Taarifa hii inajumuisha Maoni na Ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kama inavyoonekana katika Taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

1.3 Njia au Mbinu zilizotumika

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, imeweka sharti kwa Taarifa ya Kamati kuonesha Njia au Mbinu zilizotumika kufanya kazi inayoripotiwa. Aidha, ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kuhakiki uthabiti wa matokeo ya uchambuzi wa Muswada huu, naomba kubainisha njia au mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu kama ifuatavyo: -

- (a) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Njia hii iliwezesha Kamati kupata mantiki ya mambo na masharti mbalimbali yanayopendekezwa;
- (b) Kufanya mapitio ya Maudhui ya Muswada kuanzia jina refu la Muswada hadi Sababu na Madhumuni. Lengo la kufanya hivyo ni kubaini masharti ya kisheria yanayopendekezwa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Njia hiyo ni muhimu kupata tathmini ya jumla kuhusu kufaa au kutokufaa kwa mapendekezo katika Muswada huu;
- (c) Kuoanisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria inayojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za Umma chini ya sekta ndogo ya teknolojia ya Habari;

- (d) Kujadili dhana kuu ya ulinzi wa Taarifa binafsi ambayo ni kiini cha Sheria hii inayokusudiwa kutungwa na Bunge. Njia hii imesaidia kujenga mtazamo mpana kwa ajili ya kuhakiki maudhui ya Muswada kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi; na
- (e) Kupokea na kusikiliza Maoni ya Wadau kama inavyoelekezwa na masharti ya Kanuni ya 97(2) na 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Njia hii ililenga kuliwezesha Bunge kuendelea kuzingatia mtazamo wa umma katika utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Njia hizo kwa ujumla wake zimeiwezesha Kamati kuchambua Muswada huu kwa ukamilifu. Ni imani ya Kamati kuwa matumizi ya njia hizo yanaipa Taarifa hii uwezo wa kulisaidia Bunge kukidhi matarajio ya wananchi wakati wa kuamua kuhusu Muswada huu.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki mpangilio, masharti, maudhui na dhamira kwa ujumla. Uhakiki ulifanyika kwa mapitio ya jumla ya maudhui na baadaye uchambuzi wa Ibara kwa Ibara. Lengo kuu katika hatua hiyo lilikuwa ni kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria yanayopendekezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilijikita kwenye uchunguzi wa matini (text) ya Muswada ili kujiridhisha:

- (a) Iwapo kuna mahitaji ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;
- (b) Iwapo masharti yanayopendekezwa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi yanaendana na ahadi na mwelekeo wa jumla wa nchi, kanda na dunia;
- (c) Iwapo mpangilio, masharti na maudhui vinakidhi mahitaji ya kuwa na sheria inayopendekezwa; na
- (d) Iwapo Bunge likiupitisha Muswada huu litakuwa limezingatia misingi ya utungaji wa sheria inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo yanaweza kubainika vizuri kwa muundo wa matokeo ya uchambuzi unaoelezwa katika Taarifa hii. Kimitiririko, Taarifa hii inabainisha Upembuzi wa Maudhui ya Ibara za Muswada wa Sheria ili kujiridhisha endapo yanakidhi mahitaji. Kamati inaamini kuwa mtiririko huu utaliwezesha Bunge kufanya uamuzi unaotatua tatizo kuhusu haki za taarifa binafsi kisheria au kuziba

ombwe kuhusu taarifa binafsi ipasavyo kwa kuzingatia misingi ya utungaji wa sheria bora.

2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Uchambuzi wa Muswada huu ni kubaini uthabiti wa masharti na maudhui yanayopendekezwa ili kulishauri Bunge inavyostahili. Kwa ujumla utaratibu wa kibunge wa kushughulikia hoja hadi kufikia uamuzi, unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki na upembuzi wa kina wa hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu ili kuliwezesha Bunge kupata undani wa jambo linalolengwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kama alivyoeleza mtoa hoja mapema leo hii, Muswada huu ni pendekezo la Sheria inayokusudia kuweka masharti kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi wakati wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa hizo, unaofanywa na vyombo vya serikali na binafsi. Kwa madhumuni hayo, jambo kuu la kulichunguza kwa undani ni ulinzi wa taarifa binafsi (Data Protection). Kwa tafsiri ya jumla, ulinzi wa taarifa binafsi (Data protection) ni **udhibiti wa kisheria wa taarifa binafsi (personal data) katika upatikanaji, uchakataji na matumizi ya taarifa hizo zinazokusanywa na kuchakatwa na vyombo vya serikali au binafsi.**

Mheshimiwa spika, Ulinzi wa taarifa binafsi unawahakikishia wananchi usalama wa taarifa zao ili kulinda heshima na kuhifadhi utu wao. Aidha, kukosekana kwa ulinzi wa taarifa binafsi kunaweza kuwa na madhara kwa usalama wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi (personal Data) katika vyombo vya serikali na binafsi unahitaji kuwekewa misingi na masharti ili kudhibiti matumizi ya taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu huo, Kamati ilihitaji kubaini pengo la kisheria kuhusu udhibiti wa taarifa binafsi zinazokusanywa na kuchakatwa na vyombo vya serikali au binafsi. Ubainishaji wa pengo hilo ulifanyika kwa kupata mtazamo wa jumla kuhusu udhibiti huo pamoja na mwelekeo unaotolewa na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa nchi yetu kama ifuatavyo:-

2.2.1 Mtazamo wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Mtazamo wa jumla kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi (Personal Data Protection) umejengwa kwa kamati kupitia machapisho mbalimbali yanayohusu udhibiti wa taarifa zinazokusanywa ulivyo duniani, Afrika na kikanda. Utaratibu huo unaweza kutoa uzoefu juu ya **“Udhibiti wa kisheria wa taarifa**

binafsi (personal data) katika upatikanaji na matumizi ya taarifa hizo ambazo hukusanywa na kuchakatwa na vyombo vya serikali au binafsi."

Mheshimiwa Spika, Kupitia machapisho mbalimbali, Kamati ilibaini kuwa dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi inahitaji kuwekewa masharti ya kisheria ili kulinda usalama na utu wa watu katika kila nchi. Mahitaji hayo yamebainika katika mapitio ya misingi (principles) ya ulinzi na faragha za taarifa binafsi iliyowekwa na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO). Miongoni mwa misingi hiyo ni masharti ya kutumia taarifa binafsi kwa kuzingatia usitirifu (Confidentiality).

Mheshimiwa Spika, Kutokana na misingi ya ulinzi (Protection) na faragha (Privacy) iliyobainishwa na UNESCO, Kamati imeridhika kwamba, upo umuhimu wa kuweka masharti ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi nchini katika vyombo vya serikali na binafsi kwa namna inayozingatia usitirifu wa taarifa hizo (Data confidentiality).

Mheshimiwa spika, Kwa upande wa Kikanda, Kamati ilitafuta uzoefu ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kwenye nchi za Afrika Mashariki. Lengo ni kujifunza namna nchi nyingine zinavyodhibiti taarifa binafsi zilizokusanywa na kuchakatwa katika vyombo vya serikali na binafsi. Uzoefu huo ni sehemu muhimu ya kuliwezesha Bunge kuamua kuupitisha au kutokuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa SADC, Jumuiya hiyo iliweka Sera inayotoa mwongozo kuhusu usawa wa Sheria zinazohusu ulindwaji wa taarifa na teknolojia ya habari. Sera hiyo pamoja na mambo mengine inasisitiza nchi wanachama kuwa na mifumo itakayosaidia kupambana na ukiukwaji wa haki ya ulinzi wa taarifa binafsi katika ukusanyaji, uchakataji, usambazaji, uhifadhi na utumiaji wa taarifa hizo. Kwa msisitizo huo, Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi wanachama wa SADC, inahitaji Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Personal Data Protection Act). Hivyo, Muswada huu umeletwa katika muktadha unaoendana na hali halisi.

Mheshimiwa spika, Kwa kuongeza uelewa, Kamati imepitia mwongozo wa sheria kuhusu masuala ya kimtandao wa mwaka 2008 wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Mwongozo huu unabainisha maeneo muhimu kwa nchi wanachama kuzingatia katika utungaji wa sheria za kimtandao ikiwemo kulinda taarifa binafsi za watumiaji wa mitandao. Kuhusu ulinzi wa taarifa

binafsi, mwongozo huo unasisitiza wajibu kwa vyombo vinavyokusanya na kuchakata taarifa binafsi kuzingatia haki za mhusika wa taarifa (Data Subject).

Mheshimiwa Spika, kutokana na msisitizo huo, Kamati ilibaini kwamba, Tanzania nayo inahitaji kuwa na Sheria inayotaja wajibu wa vyombo vinavyohusika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuzingatia haki ya mhusika wa taarifa hizo (Data Subject). Mahitaji hayo pamoja na mengine ni miongoni mwa mambo yanayopaswa kulisukuma Bunge kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Jambo muhimu kwa Bunge lako Tukufu ni kuhakiki masharti ya sheria inayopendekezwa kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi na kujiridhisha kama yanaweza kupitishwa kama yalivyo au kurekebishwa kwa kadiri inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mtazamo wa jumla duniani, Afrika na kikanda, Kamati ilitafuta uzoefu wa nchi zingine kama vile Kenya na Uganda kwa Afrika Mashariki na Zambia, Madagaska na Botswana kwa nchi za SADC. Katika nchi hizo zimetungwa Sheria zinazohusu udhibiti wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi (personal Data).¹

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa nchini Kenya kuna Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya Mwaka 2019. Sheria hiyo imeanzisha Ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data inayoongozwa na Kamishna wa Data. Kwa wenzetu wa Uganda, Bunge lilitunga Sheria ya Ulinzi wa Data na Faragha ya mwaka 2019 (Data Protection and Privacy Act, 2019). Sheria hiyo imeanzisha Ofisi ya Ulinzi wa Data Binafsi chini ya Mamlaka ya Taifa ya Teknolojia ya Habari (National Information Technology Authority – NITA). Kwa upande wa Zambia, Bunge lilitunga Sheria ya Ulinzi wa Data ya Mwaka 2021 (Data Protection Act, 2021). Sheria hiyo ya Zambia, imeanzisha Ofisi ya Kamishna wa Data na kuweka utaratibu wa kuwa na Wakaguzi wa Data. Katika nchi ya Botswana ilitunga sheria ya ulindaji wa Data mwaka 2018 (Data Protection Act, 2018) na inasimamiwa na Tume ya Ulinzi wa Data. Pia katika nchi ya Madagasca ilipitisha sheria ya Ulinzi wa Data na Faragha (Data Protection and Privacy Act, 2014) sheria hiyo imeanzisha Tume ya ulinzi wa Data na Faragha.

¹Neno Data ni neno la Kiswahili kama linavyoonekana katika uk. Wa 164, Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la 2, mwaka 2016, na English – Swahili Dictionary, Toleo la Tatu, TUKI, 2006, Kamusi Teule ya Kiswahili, Toleo la Pili, 2019, uk. 121, Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 2TATAKI uk. 59, Toleo la Pili (2004). Kamusi ya Kiswahili sanifu TUKI, 2019, uk. 92, Kamusi ya Karne ya 21, Toleo Nne, 2019 uk. ... na Kamusi Sanifu ya Kompyuta, uk. 49, Kiputiputi, Toleo la kwanza 2011 na Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia. TUKI UNESCO&SIDA, 1990. Uk. 34

Mheshimiwa Spika, jambo la kujifunza linalotokana na uzoefu huo ni kwamba, kati ya mwaka 2019 na 2021 kwenye Kanda ya Afrika Mashariki na upande wa SADC, suala la masharti ya Sheria kuhusu Data binafsi limepewa msukumo maalumu. Katika mifano rejea, nchi ya karibuni kuwa na Sheria yenye madhumuni kama ya Muswada huu ni Zambia, mwaka 2021. Kwetu Tanzania Mwaka huu 2022 na hasa leo, Bunge linajadili Muswada wa Sheria unaoweka masharti kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Personal Data). Naomba kulikumbusha Bunge hili kuwa, masharti ya aina hiyo si mapya ndani ya SADC, Afrika Mashariki na Duniani kwa ujumla kama nilivyoeleza.

2.2.2 **Mapitio ya Miongozo ya Ndani ya Nchi**

Mheshimiwa Spika, Miongozo ya ndani kuhusu uendeshaji wa nchi inahitaji kuzingatwa na kuwa rejea muhimu kwa Bunge kufanya uamuzi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilizingatia Miongozo Mkuu ambao ni Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ilani hiyo ni ahadi iliyotolewa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu. Lengo lilikuwa ni kupima kama matarajio ya Wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Miongozo mwingine uliorejewa na Kamati ni Sera ya Taifa ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kwamba, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoongoza Serikali, kiliwaahidi wananchi kuwa Serikali itasimamia kikamilifu faragha na usiri wa taarifa zao. Ahadi hiyo ilitolewa kupitia Aya ya **61(b)** kwenye ukurasa wa 97 wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Aya hiyo inaeleza kuwa Chama cha Mapinduzi kitaisimamia serikali:

"Kuongeza Faragha na usiri wa Taarifa za wananchi katika Mawasiliano kwa kukamilisha kutunga sheria ya kuimarisha ulinzi wa Taarifa na Takwimu".²

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni sehemu ya hatua za kuzingatia ahadi waliyopewa wananchi kuhusu ulinzi wa taarifa (Data) na Takwimu. Kwa mantiki hiyo, Maoni yanayoboresha masharti ya Sheria inayopendekezwa yanahitajika wakati wa mjadala wa Bunge unaouongoza leo hii. Naliomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu kwa mtazamo unaojitokeza katika Taarifa ninayoiwasilisha sasa.

² Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (2020: 97), **Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.**

Mheshimiwa Spika, zaidi ya Ilani niliyoitaja, mwongozo mwingine uliotumika kujenga mtazamo wa Kamati ni Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2016 inayohusu maelekezo juu ya mazingira ya TEHAMA na Udhhibiti wake. Lengo lilikuwa ni kuona kama mwelekeo wa kisera unaendana na mapendekezo ya masharti katika Muswada huu. Kamati ilibaini kuwa **Aya ya 3.6** ya sera hiyo inatambua suala la kisera la faragha ya taarifa. Utambuzi huo unaendana na mahitaji ya ulinzi wa taarifa binafsi ambao unawekewa masharti ya kisheria kwa mapendekeo katika Muswada huu.

2.3 Uchambuzi wa Ibara za Muswada

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Ibara kwa Ibara ulifanyika kwa kusoma na kutafakari kila sentensi na kila neno katika Muswada. Utaratibu huo unazingatia umuhimu wa Kamati kuhakiki Matini (text) ya Muswada na kuona kama inakidhi matarajio ya sheria inayopendekezwa. Lengo ni kutoa ushauri kwa nia ya kuboresha masharti ya sheria yanayopendekezwa kwa kadri itakavyohitajika. Kusudio ni kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu ushauri wake kwa Bunge. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa, Kamati ililazimika kusoma na kutafakari neno kwa neno ili kupendekeza marekebisho yaliyohitajika.

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- (a) Ibara arobaini na tisa (49) kati ya Ibara 65 zinajitosheleza na zinafaa kupitishwa kama zilivyo;
- (b) Ibara kumi na sita (16) zinastahili kurekebishwa ili Sheria inayopendekezwa itungwe kwa kuzingatia mambo ya msingi na maslahi ya wananchi wanaowakilishwa katika Bunge hili; na
- (c) Vipengele viwili (2) vya Jedwali linalohusu Taratibu za Bodi ambalo linaanzishwa chini ya Ibara ya 8(6) vinahitaji kurekebishwa ili viendane na maudhui ya Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo hayo, mtoa hoja, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, aliafikiana na Kamati kuhusu baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa. Kwa muafaka huo Waziri aliandaa Jedwali la marekebisho lililofikishwa mbele ya Kamati na baadae kuahidi kulileta Bungeni. Kwa mantiki hiyo, maoni haya yamezingatia makubaliano kati ya Kamati na Mtoa Hoja. Nichukue

fursa hii kwa niaba ya Kamati, kuipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni ya msingi yenye maslahi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI

3.1 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

- (a) Serikali iweke wazi vyanzo vya fedha vitakavyotumika kuendesha shughuli za Tume katika kusimamia mambo ya ulinzi wa Taarifa Binafsi;
- (b) Kwa kuzingatia kwamba, kanuni ni nyenzo muhimu inayofafanua utekelezaji wa masharti ya sheria inayohusika, Serikali isimamie vyema utungaji wa Kanuni za Sheria hii ili zisipishane na dhamira ya Bunge na zisikose uhalisia;
- (c) Haki ya wahusika wa Taarifa (data subjects) walioachana na taarifa zilizokusanywa kuendelea kuhusishwa na taarifa hizo tofauti na utashi wao izingatiwe katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Aidha, Stahili ya Marehemu kuhusu ulinzi wa taarifa zake iwekewe utaratibu wa kuizingatia;
- (d) Ili kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria inayotungwa na Bunge, vigezo au sababu zinazoweza kutumiwa kufuta usajili wa Mkusanyaji au Mchakataji wa Taarifa Binafsi viwekwe wazi; na
- (e) Kwa madhumuni ya kuzingatia misingi ya utawala bora wakati wa utekelezaji wa Sheria hii, ni vizuri kuzingatia suala la jinsia katika uteuzi wa wajumbe wa bodi.

3.2 Majumuisho

Mheshimiwa Spika, Maoni haya, yanatokana na matokeo ya Uchambuzi uliofanyika. Aidha, yamezingatia muafaka uliofikiwa kati ya Waziri na Kamati baada ya uchambuzi na mashauriano. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi, makubaliano ya Kamati na Waziri na maoni haya niliyoyatoa, vitawezesha majadiliano yatakayosaidia Sheria bora inayopitishwa leo.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Uzoefu wa Wajumbe katika Sekta ya Habari na Mawasiliano umekuwa na mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi, Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau umesaidia kupata mawazo yenye tija katika uzingatiji wa maslahi ya Umma wakati wa kujadili Muswada huu. Kwa hatua hii niwashukuru tena Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Wadau hao ni: -

- a) Tume ya haki za binadamu;
- b) Muungano wa mabanki Tanzania;
- c) Jamii Forum;
- d) Muungano wa Kampuni za simu Tanzania - TAMULOA;
- e) Multi Choice;
- f) Tanganyika Law Society;
- g) Vodacom;
- h) Legal human Centre; na
- i) GSMA.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha ukamilifu wa taarifa hii. Ninaamini kwa taarifa hii, Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi ya Umma, Taifa na uhai endelevu wa Tanzania. Aidha, kwa kutambua mchango wa Wajumbe, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb - "
5. Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb - "
6. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb - "
7. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb - "
8. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb - "
9. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb - "
10. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb - "
11. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb - "
12. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb - "
13. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb - "
14. Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb - "
15. Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb - "
16. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb - "

1 NOVEMBA, 2022

17. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb - "
18. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly, Mb - "
19. Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb - "
20. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb - "
21. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb - "
22. Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb - "
23. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb - "
24. Mhe. Angelina Malembeka, Mb - "

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari mhe. Nape Moses Nnauye, na Wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada. Maelezo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelewa Mwihambi, *ndc* na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* kwa kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi na Makatibu wa Kamati Ndg. Janeth Malangu na Ndg. Victory Mrema, pamoja na Ndg. Grace Samweli, Msaidizi wa Shughuli za uratibu, kwa kufanikisha kazi za Kamati kama ilivyostahili.

4.2 **Wasilisho**

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Moshi Selemani Kakoso, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA MIUNDOMBINU**

1 Novemba, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mawasilisho hayo. Waheshimiwa Wabunge tulipaswa kuanza na uchangiaji lakini muda wetu umekwenda, kwa hivyo uchangiaji tutaanza mchana tutakaporejea.

Kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, niwataje Wabunge ambao tutaanza nao kwenye mchango. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Geoffrey

1 NOVEMBA, 2022

Idelphonce Mwambe na Mheshimiwa Stella Fiayo. Wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

(Saa 7.30 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022
(The Tanzania Investment Bill, 2022) na Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa
Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (The Personal Data Protection Bill, 2022)**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa mwaka 2022 uliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kupongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao umekuja kwa wakati muafaka, umekuwa ukingojewa na Watanzania, wawekezaji wa ndani na wa nje kwa muda mrefu. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni mwendelezo tu wa yale ambayo Mheshimiwa Rais alituambia alipokuja kutuhutubia hapa tarehe 22 mwezi Aprili, mwaka 2021, aliposema kwamba nchi yetu imekuwa ikilalamikiwa kwa kutokuwa na mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, ikiwemo kutokuwa na sera zinazotabirika na utaratibu wa kodi usio na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameanza kutekeleza. Tumeshuhudia katika miaka mmoja na nusu au miwili, ambayo amekuwa

madarakani, hali ya uwekezaji imeongezeka ambayo inaashiria wazi kabisa kwamba utekelezaji wa yale aliyotuambia ndani ya Bunge hili unakwenda vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda kusema, sumu ya uwekezaji *whether* uwe ni wa ndani au ni wa nje, uko katika maeneo mawili ambayo ni sheria ya kutotabirika na urasimu. Niseme kwamba suala la kutotabirika kwa kiasi kikubwa tunaendelea kuishukuru Serikali na tunatambua, ndiyo maana tuna *blueprint*, utekelezaji wake umeanza. Tulikuwa tunaiangalia muda mfupi uliopita, wameweza kuondoa tozo nyingi sana, wameweza kurekebisha baadhi ya tozo; katika tozo karibu 300, tayari wameshashughulika na zimebakia tozo 114 ambazo wanaendelea kuzishughulikia. Kwa hiyo, inasaidia kwenye kutabirika kwa mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, urasimu bado ni tatizo kwa wawekezaji. Kwa kweli tulikuwa tumetegemea na Mwenyekiti wangu wa Kamati ameweza kuyasema hapa, tulikuwa tumelichakata hili jambo vizuri tukiamini kwamba labda mawazo yetu katika kamati yanaweza kusaidia kupunguza urasimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti wetu na kwa kuangalia majirani na tuelewe uwekezaji ni ushindani; unapoongelea uwekezaji, maana yake unaongelea ushindani, uwe wa ndani au wa nje.

Mheshimiwa Spika, tuliloliona ni kwamba hata ukipewa cheti cha uwekezaji kwa maana ya *incentives* za TIC, bado unatakiwa uanze kuhangaika na kushughulika na taasisi na idara za Serikali, ushughullike na wakala za Serikali ambazo ndiyo zinatoa vibali. TIC wao wanakupa kibali kikubwa kimoja, lakini sheria inawataka, ukisoma kwenye *section 18 subsection 1* mpaka 5, unakuta mwendelezo mzima wa nini kinatakiwa kitokee? Sasa tuwashukuru Wizara wamechukua mawazo ya kamati kwa kiasi fulani walipokubali kuweka *limit* ya kutoa hiyo *certificate*. Ilikuwa ndani ya siku 14, sasa itatolewa ndani siku saba. Kwa hiyo, ni maendeleo mazuri, yanaashiria kwamba tunakwenda vizuri na tunakwenda mwendo wa Rais wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado kuna mitego mingi ndani ya sheria hiyo. Maana unatoa ombi la kupewa *incentives*. Ukishapewa ombi lako na TIC, unahitaji kupata vibali vingine. Ndani ya vibali hivyo, inatakiwa upewe majibu ya vibali vile ambavyo unavihitaji katika idara na taasisi nyingine za Serikali ambako ndiyo imekuwa ni tatizo. Sheria inasema kwamba wanatakiwa ndani ya siku saba wawe wamekupa majibu na kwamba usipopata majibu, aidha upate leseni au upate idhini ya kile unachokitaka, au (na ndiyo hapo lilipo tatizo) upewe mrejesho.

Mheshimiwa Spika, hili neno “mrejesho”, wakati mwekezaji ameomba vibali, ndiyo kansa ya uwekezaji, kwa sababu mrejesho haujawa *defined*, mrejesho hauelezewi. Maana yake ni kwamba utajibiwa kwa barua kwamba jambo lako linashughulikiwa na maana yake ni kwamba ukishajibiwa linashughulikiwa, siku saba ni kama hazina maana tena, kwa sababu haziwezi ku-*run* tena, kwa sababu umeshajibiwa kwamba jambo lako linashughulikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana sisi kwa busara, tuliona ni vema *TIC*, unapopata nafasi ya kutunga sheria, hii sheria imetungwa zaidi ya miaka 25 iliyopita na inatungwa upya, tuliona ni wakati muafaka kwa Serikali kuja na kitu tofauti kitakachoweza kukidhi haja ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Hilo lingetokea kwa kuifanya *TIC* kuwa mamlaka kamili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado *TIC* inaitwa kituo. Maana “kituo”, kuna Kituo cha Polisi, kuna Kituo cha Basi; sasa wawekezaji wa ndani na nje, kwa kweli tulidhani kwamba kuweka mamlaka ingesaidia nchi. Ingesaidia kuifanya *TIC* iwe na mamlaka, iweze kufanya maamuzi na kwenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hilo, niongelee vile vile ushiriki wa sekta binafsi. Tunashukuru na kwamba Serikali imeendelea, Wizara imeendelea kuiamini sekta binafsi katika vyombo vya maamuzi. Kwa hiyo, Bodi ya *TIC*, ina *private sector*, lakini chombo kikubwa cha maamuzi ni kile ambacho kinatoa vile vile vivutio vya ziada. Chombo hicho kina Wajumbe 11 jumlisha mmoja. Hawa 11 ni Wajumbe wote kutoka Serikalini. Unaanza na Mawaziri saba, Waziri Mkuu akiwa ndiyo Mwenyekiti. Halafu unakuta *BOT Governor*, then unamkuta kiongozi wa *TIC* kwa maana ya *Secretary General* kwa maana ya Katibu wa *TIC*. Pia kuna mtu mmoja ambaye huyo anaweza akawa *invited* muda wowote. Sasa tungependa angalau kuwe na mtu mmoja wa *private sector*.

Mheshimiwa Spika, najua tunatunga sheria, tulitakiwa tulete mabadiliko. Niseme hatuwezi kuleta mabadiliko sasa lakini busara ya Serikali itumike. Tunakwenda kwenye kipindi ambacho tunafanya kazi na *private sector*. Hapa Waziri wa ujenzi alituambia, miradi mingi mikubwa ya barabara na ujenzi wa ma-*airport* sasa itakwenda kwa mtindo wa *PPP*, maana yake ni *Private Public Partnership*. Sasa tufike mahali tuanze kuamini kwamba tunahitaji *private sector* kwenye vyombo vingine vikubwa vya maamuzi kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, wengine wanadhani maslahi ya Taifa maana yake lazima uwe Serikalini ndiyo utambue maslahi ya Taifa. Unaweza kuwa kwenye *private sector* ukayafahamu vizuri na ukaisaidia nchi vizuri zaidi. Ni kwa nia njema kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, vivutio vya uwekezaji vya ziada vinatolewa katika mazingira ambayo inatakiwa mwekezaji aombe. Tufike mahali tujue tunashindana. Kwa hiyo, vingekuwa vinaeleweka angalau kwa kiasi fulani ili mtu asiende Rwanda au Kenya ambako wana mamlaka tayari na wanafanya maamuzi kwa haraka sana tunavyosikia na kupitia taarifa mbalimbali tulizonazo ili sasa vivutio hivyo viweze kuwavuta watu katika maeneo mbalimbali hasa yale ya mbali kama vile maeneo ya mikoani ambako kuna viwanda vile vya zamani vya *processing*, vya *agriculture* na vya *skin* na *hides* vingeweza vikajengwa kwa wingi na vikawa *modernized*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naona muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofi!*)

SPIKA: ahsante sana. Mheshimiwa Zahoro Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, ajiandae.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi. Naomba kuelekea kwenye Muswada wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, lakini nataka kujikita kwenye maeneo matatu. K

Mheshimiwa Spika, kwanza malengo ya kudhibiti, kwa sababu inawezekana hapa wengi tusielewe, lakini kwa nini umeletwa Muswada huu; ndiyo ambapo nataka kwenda.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ukurasa wa nane, naomba ninukuu kwanza ila kwa *interest* ya muda nitasoma tu haraka haraka halafu nitajaribu kueleza. Yako malengo (a) mpaka (e), kwa maana haya ni malengo Matano:-

- (a) Kudhibiti uchakataji;
- (b) Kuhakikisha kwamba uchakataji wa tarifa binafsi za muhusika unaongozwa na misingi;
- (c) Kulinda faragha;
- (d) Kuweka utaratibu wa kisheria; na
- (e) Kuwapa wahusika wa taarifa haki na nafuu ya kulinda taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, nini maana yake? Maana yake hapa duniani tulipo, *whether* tunapenda au hatupendi, lazima tulinde faragha za taarifa za watu binafsi. Kwa sababu dunia hii ni ya mitandao na taarifa unaweza ukazitafuta kwa njia ya mitandao. Kwa hiyo, lengo au madhumuni ya hii ni kulinda. Tumejiwekea hapa malengo lakini kubwa zaidi ni kulinda faragha ya mtu mmoja mmoja lakini ikiwa inalindwa kwa mujibu wa sheria. Sasa utakapokiuka sheria hii maana yake nini? Maana yake kutakuwa na sheria ya kuweza kumdhibiti kila mtu ambaye anachakata au anakusanya taarifa nje ya utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, kwa sababu kuna malengo, tumejiwekea na misingi. Wenzetu hapa wameweka misingi nane. Kwa *interest* ya *time*, naomba ninukuu tu haraka haraka. Kwanza, zitakuwa zinachakatwa kihalali kwa maana ya mujibu wa sheria. Hapa tunajifanyia tu lakini sasa tunaweka sheria ili kuhakikisha kwamba taarifa zinachakatwa kwa mujibu wa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, zinakusanywa kwa madhumuni maalum. Ili taarifa zifanyiwe kazi, ili zichakatwe, zitafutwe maana yake zinatafutwa kwa sababu maalum, siyo kwamba unamtafuta mtu tu kwa sababu unamtafuta. Zinatafutwa ili zifanyiwe kazi maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine, zinatoshleza na ni muhimu kwa madhumuni ya uchakataji. Tunatafuta taarifa kamilifu, siyo kipande kipande. Lengo letu ni kwamba tunapohitaji taarifa, lazima ziwe na mwanzo na ziwe na mwisho na ziwe za kujitosheleza na sahihi. Tunatafuta taarifa sahihi, siyo za ku-cook. Hata hivyo zitahifadhiwa kwa namna inayoruhusu utambuzi wa mhusika, na zitachakatwa kwa kuzingatia haki. Hatuwezi kutafuta taarifa hizi halafu zikawa zinachezewa bila kujali kwamba kuna mwingine zinavyochakatwa taarifa zake ni kwa kumwonea.

Mheshimiwa Spika, mwisho zinachakatwa kwa namna ambayo itahakikisha usalama wa taarifa binafsi ikijumuisha ulinzi dhidi ya uchakataji usioruhusiwa au ulio kinyume cha sheria. Maana yake ni nini? Ni kwamba kila kitakachofanyika katika kutafuta taarifa hii, kitafanywa ndani ya misingi ya sheria wala haifanywi kwa ajili ya kumkomoa mtu, tunahitaji taarifa kwa kazi maalum, kwa shughuli maalum, lakini kitu kizuri zaidi, mtu mwenyewe atakuwa anapewa taarifa kwamba tunazitafuta hizi kwa ajili hii, lakini hata yeye mwenyewe atapewa fursa ya kuweza kuhakikisha kwamba anashiriki na kama anazo zitatumika na ataombwa zitumike akijua kwamba zinatumika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba twende kwenye ukurasa wa 13 pale, kuna chanzo cha utoaji wa taarifa. Naomba pia kwa *interest* ya muda, ninukuu hapa kwenye ukurasa wa 13 ambayo inazungumzia chanzo. Wanasema chanzo, imeandikwa hapa, kwa mujibu wa kifungu cha 23(1). Kwa kuzingatia kifungu hicho, kinasema hivi: "Kabla ya kukusanya taarifa binafsi, mkusanyaji atahakikisha kuwa muhusika; moja, anatambua madhumuni ya ukusanyaji; pili, anafahamu kuwa ukusanyaji wa taarifa binafsi na madhumuni yake; na tatu anawafahamu wapokeaji wa taarifa binafsi." (Makofi)

Mheshimiwa Spika, inawezekana tulio wengi hatuelewi na tulio wengi inawezekana tunaamini kwamba tunatafutana. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge, nasi tuwe sehemu ya kuwapa taaluma wengine kwamba dunia ya leo hatuna pa kujificha. Dunia ya leo taarifa ziko kiganjani,

lakini dunia ya leo ukitaka la kwako la dhahiri linajulikana, la siri litajulikana tu. Sasa ni bora tufanye utaratibu wa kisheria ili mwananchi yeyote ambaye taarifa zake zitatumika bila ya *consent* yake, maana yake huyu anayo nafasi ya kwenda Mahakamani. Leo tunafanya kwa sababu tu, lakini sheria hii itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, sisi kama Tanzania hatuishi kwenye kisiwa. Tunahitaji kupata taarifa kutoka kwa wenzetu pia kwenye Mataifa mengine kwa sababu sasa hivi taarifa zinasafiri mara moja. Ndani ya dakika moja au *second* moja unaweza kupata taarifa kutoka China au popote. Kwa hiyo, litakapokuwa limewekwa hili, nasi kama Bunge tukawa tumeridhia kupitisha sheria hii, maana yake tutalisaidia Taifa letu na tutajisaidia na sisi wenyewe kuhakikisha kwamba taarifa zetu hazichezewi.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, walielewe hili, lakini nao wawe sehemu ya kuisaidia Serikali kwa sababu kinyume chake sisi tutapambana na vikwazo vingi vya uchumi ambavyo wenzetu kama hatukupitisha hii wataona kama sisi hatufanyi kazi na wao. Kwa sababu ni ulimwengu wa kubadilishana taarifa, lakini taarifa za ukweli, taarifa ambazo siyo za kutengeneza ili kuhakikisha kwamba taarifa iliyoko Tanzania ndiyo hiyo hiyo iliyoko kwenye eneo lingine ili tusiweze kufanya makosa kwenye utambuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, waikubali sheria hii, waipitisha ili tuweze kufanya kazi na dunia, ili tuweze kukusanya taarifa, tuzichakate, tuzi-*share* lakini ndani ya sheria na wenzetu waweze ku-*share* na sisi ili nasi tukitaka za kwao iwe ni rahisi sana kuweza kuzipata ili tusaidie maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi!)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe na Mheshimiwa Stella Fiyao, ajiandae.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kuchangia kwenye Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Serikali kwa kuja na sheria hii ambapo kimsingi tumeisubiri kwa muda mrefu na ilikuwa ni hamu ya Watanzania kupata Sheria hii ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa ajili ya kulinda mambo mbalimbali ambayo yapo kwenye taarifa zao ambazo wamezitoa.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana tulivyoweza kukutana na wadau, walionesha wazi wanaishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kuileta sheria hii. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge tunapaswa kuleta shukurani hizo kwa Serikali na Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa dhamira yake, lakini tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kutuletea sheria hii na ufafanuzi wa Muswada huu. Tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba namna ambavyo tumekuwa sisi kama nchi, tumeridhia maazimio mbalimbali ya Kimataifa. Miongoni mwa maazimio hayo yalikuwa ni pamoja na kulinda taarifa binafsi za watu. Sisi kama nchi ilikuwa bado hatuna sheria ambayo inaweza kuendana na maazimio hayo. Kwa hiyo, kuja sheria hii ni wakati muafaka kwamba wenzetu duniani sasa wataona namna ambavyo tunaungana nao katika suala hili la kulinda taarifa binafsi za watu.

Mheshimiwa Spika, hiyo kama haitoshi, ni kwamba leo hii tunafanya shughuli nyingi kupitia ICT. Mambo mengi yanafanyika kutoka kwenye kiganja kwa maana tunatumia kwenye utaratibu wa TEHAMA. Hatuna namna ambapo tutakwepa baadhi ya mambo ambayo yako duniani. Kwa hiyo kwenye eneo hili kama nchi tunaamini kabisa itaongeza imani kubwa kwa wawekezaji kuendelea kuwekeza kwenye sekta hii ya TEHAMA. Sekta ya TEHAMA inakuwa, leo hii vijana wengi wamewekeza kwenye TEHAMA, maana yake ni kwamba kuleta sheria hii inaongeza *confidence* ya wale wanaoshughulika kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwamba tuiptishe sheria hii ili ikaisaidie Serikali katika kuongeza wigo wa ajira kwa ajili ya wananchi wetu. Naamini kabisa kupitia sheria hii, itakuwa ni jibu ambalo limekuwa likitafutwa kwa muda mrefu katika kutatua changamoto zilizopo kwenye eneo hili la TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile wawekezaji wengi katika eneo hili walikuwa wanasita kuwekeza kama ambavyo nimesema. Leo hii wamekuwa wana mahitaji ya kuona namna ambavyo dhamira ya Serikali yetu katika eneo hili. Leo hii tukiweza kufanya hivyo na biashara kubwa duniani leo ni iko kwenye mtandao. Leo hii ukiangalia Shirika letu la Posta wamefanya kazi nzuri sana, wanasema duka lako mkononi mwako, maana yake ni kwamba leo hii kupitia haya tutawafanya watu wawe na imani zaidi na hata na taasisi zetu za Serikali kuacha zile za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu mimi binafsi naona sheria imekuja wakati muafaka, tuiptishe kama ambavyo imeelezwa vizuri kwa urefu madhumuni yake, nani ambaye anatakiwa kutoa taarifa, kwa wakati gani na sababu gani, itasaidia sana kuondoa changamoto ambazo tulikuwa nazo huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria nzuri hii ambayo Wabunge tunapitisha na bahati nzuri sana wewe mwenyewe umekuwa unatamani sheria hii ambayo tutaipitisha ikafanye kazi vilevile. Kumekuwa na changamoto ya kanuni na tunamwamini sana Mheshimiwa Waziri, niombe sana sheria ikitungwa nzuri iende hivyo hivyo na kanuni zake ziwe nzuri. Tumekuwa tukipitisha hapa baadhi ya sheria tukiruhusu ile *room* ya kwenda kutengeneza kanuni, kanuni inaenda inaharibu kabisa ile sheria. Mwisho wa siku sasa Wabunge tinaulizwa hivi mlipitishaje hii sheria? Kumbé kanuni imeenda kuharibu kabisa maudhui mazima ya sheria ambayo tumeipitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo msisitizo wangu ni hapo, tunapitisha sheria hii, lakini niombe kama alivyosema asubuhi Mheshimiwa Waziri nitaenda kutunga kanuni kwa mujibu wa kanuni ambayo nimeruhusiwa, lakini ni vizuri kanuni hiyo iendane na sheria hii ambayo tunaenda kupitisha leo kwa sababu kuna baadhi ya kifungu kimeeleza Waziri ataona vinginevyo katika utungaji wa kanuni. Hili eneo linaweza likawa ni mwiba mwingine kwa ajili ya kuharibu sheria ambayo tunaenda kuipitisha leo. Kwa hiyo, niombe sana tutakapokuwa tunakaa ni vizuri hata wewe Mheshimiwa Spika, ukajiridhisha na zile kanuni tu uzione ili angalau zile kanuni ziendane na sheria tuliyopitisha.

Mheshimiwa Spika, wewe bahati nzuri ni Mwanasheria umebobea, lakini leo unaletewa sheria ambayo kesho inaonekana *useless* haina maana yoyote. Nadhani kupitia Kamati yako ya Sheria Ndogo, kupitia Kamati yako ya Katiba na Sheria wazione hizo kanuni wazipitishé. Ambacho tulibaini, juzi wadau walivyokuja wameonyesha wana imani kubwa na Bunge lako, wana imani na Bunge hili, kwa hiyo kupitia kanuni isiondoe imani ambayo wadau na wananchi wa Tanzania wanayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja na naomba tuiptishé sheria hii ni nzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godfrey Idelphoncé Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge ajiandae.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuomba kufanya marekebisho kidogo ya jina langu la kwanza ni Geoffrey na siyo Godfrey.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niendeleé kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutusaidia tuweze kufika siku ya leo na tuweze kujadili Muswada huu kwa mustakabali wa nchi yetu. Kipekee nipende sana kumshukuru sana

Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kutaka kuimarisha mifumo ya ufanikishaji uwekezaji kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka hivi karibuni Mheshimiwa Rais amefanya juhudi kubwa, kwanza alianza na slogan yake ya kufungua nchi, akimaanisha kwamba anawaalika watu wote wa ndani na nje ya nchi tuweze kushirikiana kujenga uchumi wa nchi yetu. Zaidi ya hapo Mheshimiwa Rais alifanya jambo kubwa la uzinduzi wa filamu ya *Royal Tour* na lengo kubwa lilikuwa ni kuitangaza nchi yetu akilenga maeneo ya uwekezaji pia kuimarisha shughuli za kuvutia utalii kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye michango yangu kuhusiana na Muswada huu wa Sheria ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa, nchi yoyote duniani na sisi naamini kwamba ni pamoja na hao wengine, tunatakiwa tuguswe na masuala ya ajira kwa vijana. Kwa hiyo msingi wa kuwa na sheria au mabadiliko ya sheria kama haya au kuwa na sheria mpya kama hii pia ilenge kwenye kuhakikisha kwamba tunatengeneza fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine tunatakiwa tupanue wigo wa kodi, Taifa lolote kuwa imara ni lazima liwe na uwezo wa kukusanya kodi ili kuhudumia bajeti yake. Kwa hiyo kitendo cha kuwa na sheria iliyo bora ya kuvutia, ya kuhamasisha uwekezaji na biashara, tafsiri yake tunatengeneza watu wengi wa kulipa kodi, iwe ni watu wa kiasili (*natural persons*) au iwe ni makampuni (*legal persons*). Kwa hiyo naamini kabisa sheria hii au Muswada huu umelenga kwenye kuibua fursa mpya au vyanzo vipya vya mapato kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi tumesema wakati wote, kwamba tuna rasilimali nyingi kwenye nchi yetu, ni namna gani tunazitumia kwenye kubadilisha maisha ya wananchi wetu, naamini Muswada huu unalenga huko, lakini kijiografia tuko vizuri kama nchi ambayo tupo karibu na bandari kuu za kwenye eneo la Afrika Mashariki, pia tuna idadi kubwa ya watu. Mheshimiwa Rais jana ametutangazia kwamba tuna watu milioni 61, 741,120 kwenye nchi yetu, ni soko kubwa. Kwa hiyo ukijumlisha na soko la Afrika Mashariki na soko la SADC ni soko kubwa.

Mheshimiwa Spika, matarajio makubwa katika nchi yamewekwa kwenye sheria hii, kwa sababu unapokuwa na sheria mpya huwa mara nyingi inabeba matarajio ya watu. Watu wanajua kwamba kuna mambo mapya yanakuja kwa ajili ya kuimarisha mifumo iliyopo. Kingine tunakuwa na sheria mpya ili kuboresha ile sheria ya zamani, kuchukua mambo mapya ambayo tunafikiri ilikuwa ni changamoto katika utekelezaji wa ile sheria ya

awali. Hali kadhalika sheria mpya hubeba hisia na ule usasa wa mawazo ya namna ya kuweza kuenenda kwenye eneo lile ambalo tutalikusudia na kwa case hii kwetu sisi ni eneo hili la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pia tunatakiwa tulenge kuboresha mifumo ya kitaasisi, kisera lakini hata kitaratibu zetu za utendaji wa kazi. Kwa hiyo tunaamini kwamba kulikuwa na ulazima wa Muswada huu wa sheria kuja Bungeni ili tuweze kuutendea haki na kuwapa nafasi wananchi wetu kuwa na mfumo bora wa kitaasisi pia kisera, mambo mapya ambayo tunayaingiza pia utaratibu wetu au *working processes* za kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora zaidi na kuepuka urasimu na vitu vingine ambavyo vimezungumzwa na wenzangu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu pia Benki ya Dunia ilianzisha tangu mwaka 2008, walianzisha mpango wa upimaji taratibu za urahisi wa kufanya biashara kwenye nchi. Nchi ambazo zinapimwa ziko 190 kupitia moja ya *group of companies* za World Bank zinaitwa IFC (*International Finance Corporation*), tunapimwa ni namna gani taratibu zetu ni rahisi sana kwenye kufanikisha biashara. Kwenye hizi kuna viashiria 11 vimepangwa, kuanzia kwenye kuanzisha biashara mpaka kufunga biashara, hapo katikati kuna namna ya kupata mikopo, namna ya kuunganishiwa umeme, namna ya kulipa kodi, namna ya kupata vibali mbalimbali, kwa hiyo tunapimwa.

Mheshimiwa Spika, sasa Muswada huu naamini kwamba lengo lake kubwa pia ni kuhakikisha kwamba nchi yetu tunajipandisha kutoka nafasi ambazo tumezizowea 140,141, 190 tuje kwenye *top 100* ili angalau tuweze kuheshimika duniani na kuaminika kwamba ni nchi ambayo tunavutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya nina ushauri, ukiangalia Muswada huu nia yake ni njema sana na niipongeze sana Serikali kwa sababu Muswada huu kwanza umechelewa kuja Bungeni. Nashukuru sana dhamira ya Serikali kutaka kuhakikisha kwamba tunajengewa mazingira sahihi zaidi ya uwekezaji ambapo tutatengeneza nafasi nyingine ya kutatua changamoto zote ambazo wenzangu wamezizungumza katika michango yao ya awali, lakini pia tuaminike kwa sekta binafsi kama wafanyabiasha ambao wao ndio tunawatarajia wawe ndio wazalishaji wakubwa wa fursa za ajira kwa vijana wetu. Serikali kawaida inaajiri watu mpaka 700,000 tu katika watu milioni 28 au 29 ambao wana uwezo wa kufanya kazi na wa zaidi ya miaka 18. Sasa hao wengine watakoajiriwa na sekta binafsi, ni jukumu la Serikali na sisi kama Wabunge na Serikali kuona tunawasaidia kuweza kufungua hizo fursa ili vijana wetu wengi wapate ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa nina mchango ufuatao kwenye baadhi ya maeneo. La kwanza, mawanda sasa sijui itakuwa ni Kiswahili sahihi au *scope, coverage* ya Muswada huu wa Sheria bado unafinya Sheria ya Uwekezaji hii

ambao ndio inakuwa ni *framework law*, ni *mother law*, ni sheria kuu inaifinya isijihusishe na masuala yoyote ya uwekezaji kwenye madini, isijihusishe na wawekezaji kwenye *petrol* na *gas* wala kwenye kemikali hatarishi (*hazardous chemicals*) jambo ambalo nafikiri siyo sahihi kwa sasa. Naomba Serikali ifungue, sheria hii ndio sheria mama iweze kusimamia uwekezaji kwenye maeneo yote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, tumekuwa tukizungumza kuhusu kutotabirika kwetu kwa vivutio ambavyo tunavitoa. Leo yametoka haya, kesho kuna maelekezo mengine yametoka, unakosekana mwelekeo. Napendekeza vivutio vyote ambavyo tunavifahamu *standard*, nchi za wenzetu wamefanya lakini sheria yetu yenyewe ya EPZA imetoa, tuviingize kwenye sheria badala ya kusubiri kukaa pembeni na kupata hisani ya mtu mmoja au kamati. (Makofi)

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, vilevile nilikuwa natamani sana niungane na ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika moja malizia muda wako umeshaisha.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nilikuwa natamani niungane na wenzangu kwamba Kituo cha Uwekezaji sasa ifike wakati tukipe nguvu, kiwe ni *commission* kama wenzetu wanavyofanya kule Ethiopia, Egypt, Mauritius kule ni kituo chenye mamlaka, Uganda, Kenya ni *Investment Authorities* au *Commission*, kiwe na nguvu, kiwe na uwezo wa kuwa na *a proper one stop center providing services* kwa *investors* kuliko kuwa kama kilivyo sasa hivi kwamba ni kituo tu.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana basi naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Fiyao atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jembe ajiandae.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Pia niipongeze Wizara kwa kuleta Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu. Naamini Muswada huu utaenda kuwa mwarobaini wa changamoto ambayo wananchi wetu wamekuwa wakikutana nayo.

Ninavyosema changamoto hakuna asiyejua kwamba kukosekana kwa hii sheria kumepelekea wananchi kukumbana na changamoto nyingi sana ikiwa ni pamoja na kuingiliwa katika mambo yao binafsi. Sisi sote ni mashahidi wa miaka miwili, mitatu iliyopita kuna watu waliingiliwa mpaka kwenye akaunti zao, wakasachiwa na wakakutwa wana kiasi cha shilingi ngapi na wakafilisiwa, wote ni mashahidi.

Mheshimiwa Spika, naamini Muswada huu unakwenda kuwa mwarobaini kwa Taifa letu na pia unakwenda kusaidia kuongeza wawekezaji wa nje na ndani kwenye Taifa letu kwa sababu tunajua tumechelewa kuna maeneo tumekosa wawekezaji ni kwa sababu ya kukosa tu hii sheria. Sasa naamini Bunge hili likipitisha hii sheria, tutakwenda kupata wawekezaji wa nje na ndani wa kutosha kwa sababu wawekezaji wengi wanashindwa kuwekeza kwenye Taifa ambalo halina hii Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, lakini sasa naamini tunakwenda kupata wawekezaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba niwe na mambo machache ya kushauri. Kwenye Muswada huu ni muhimu kukaongezwa neno faragha ili kuleta uzito wa hii sheria. Tukiongeza neno faragha, tunajua neno faragha limebeba tafsiri kubwa ili tulete uzito mkubwa wa hii sheria, tuliongeze hili neno kwenye hiki kichwa cha hii sheria na hii itaweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa kwenye huu Muswada ikiwa kwenye kifungu cha 47 faini za kiutawala. Kwenye faini za kiutawala imezungumziwa kwamba faini ya mwisho itakuwa ni shilingi milioni 100, lakini hawajatoa ufafanuzi kwamba hiyo milioni 100 italenga makosa yapi. Jambo hili linaenda kuleta mwanya wa watu kuonewa hata kama leo hii watatuambia kwamba mambo haya yatakwenda kuonekana kwenye kanuni, amesema ndugu yangu Mtaturu pale. Mambo ya kanuni Wabunge tunakuwa hatuhusiki, tunatunga sheria salama na rafiki kwa wananchi, lakini hawa wananchi wetu wanakwenda kuumizwa na kanuni ambazo zinakuwa zimetungwa na Wabunge tunakuwa hatujazipitia. Kwa hiyo hapo tunakwenda kutengeneza tatizo.

Mheshimiwa Spika, ili twende sawa na sheria hizi zikawe salama ni zikawe rafiki kwa wananchi wetu, ni vyema kwenye utungaji wa kanuni wakaangalia maslahi mapana ya mwananchi ili mwananchi asiende kuumizwa huko. Naamini tukifanya hivyo hili linaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nisiwe na maneno mengi sana ya kusema kwenye hili jambo, lakini niombe tu niwashawishi Wabunge wenzangu kwenye Bunge hili kwamba tuiptishe sheria hii ili tuweze kwenda kunufaika kama Taifa na iweze kuwasaidia wananchi wetu wa chini na wa kawaida ambao wameendelea kuonewa kwa kukosekana sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Ulinzi Binafsi. Kipekee kabisa niipongeze Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan ambayo kwa hakika imeonesha uwezo mpana wa kufanya maoteo ya kesho kwa Taifa letu. Uwepo wa Muswada huu wa Sheria ya Taarifa Binafsi hakika ni matokeo ya kuwa na Serikali yenye maono mapana na kuiangalia kesho kwa upana wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia Muswada huu wa Sheria ya Taarifa Binafsi hakika ni Muswada sahihi kwa wakati sahihi ambao unakidhi haja ya sasa ya matakwa ya maendeleo ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Taarifa Binafsi ukiangalia malengo yake na ukiangalia misingi yake kwa hakika imelenga kuleta maadili katika matumizi ya teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, wanasayansi wanasema kwamba; *the next world war will become between the human kind technology* na wengine wanadiriki kusema kwamba *the next pandemic* itakuwa ni ya *technology*. Kwa hiyo niipongeze Serikali kwa maono mapana ya kuhakikisha Taifa hili tunakwenda kujikinga ipasavyo kwa ukuaji wa teknolojia hii.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 5 ya Muswada huu wa Sheria imezungumza suala zima la usafirishaji wa taarifa binafsi. Kipengele hiki kimenifurahisha kwa sababu moja kuu ifuatavyo; kama Taifa tumeweza kuiangalia maana halisi na muktadha pana wa teknolojia ya habari. Suala zima la kusafirisha taarifa binafsi linaweza kufanywa na mtu mwenyewe binafsi kwa kuji-*subject* katika mitandao ya kijamii, kwa maana ya kwamba unapoingiza taarifa zako huna uhakika wa asilimia mia moja kwamba *facebook* hatoweza kuzitumia vinginevyo. Vilevile tunajua kwamba makampuni yaliyopo ndani yanatumia *software* ambazo *server* zake hazipo humu nchini kwetu. *Server* zipo mbali huko katika Mataifa yaliyoendelea zaidi ya kiteknolojia, kwa maana *data* zinakuwa zinahamishwa *whether* tunataka au hatutaki, Sheria hii imembana mkusanyaji kuhakikisha kwamba anatengeneza sera kamilifu zitakazolinda usalama wa taarifa binafsi. Akienda kununua *server* huko aliponunua taifa hili atuhakikishie kwamba *data* zitakazokuwa *served externally* au *internally* zinaendelea kulindwa kwa usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimefurahishwa mno na kipengele hiki lbara ya 5 pamoja na lbara ya 65 ambayo imemtaka mkusanyaji kutengeneza sera kwa ajili ya kulinda usalama wa taarifa binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Sheria hii ni muhimu sana kwa Taifa letu, kama ambavyo wenzangu wengine wametangulia kuzungumza, katika kuuendea uchumi wa kidigitali sheria hii ina umuhimu wa aina yake. Vilevile sheria imeweka vizuri mazingira ya utekelezaji kwa maana imeunda Tume na tume ikawekewa *executive board* itakayokuwa inadhibiti utekelezaji wa shughuli zake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niseme kwamba, katika lbara ya 51muktadha mpana wa ukusanyaji wa mapato umeelezwa kwa maana ya vyanzo vya mapato, lakini bado naiona Serikali ina kazi ya kufanya katika eneo hili, tunahitaji kupata *outline* ya uwazi kuona ni kiasi gani ile muktadha halisi wa uchumi wa kidigitali unafafanuliwa katika vyanzo vya mapato ili tusiweze kuendesha tume hile ambayo itakuwa ina ajiri kwa kuendelea kutoka kwenye vyanzo vingine vya mapato wakati huu muktadha wa uchumi wa kidigitali unaweza kujizalishia ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kabisa Wabunge wenzangu tuiptishe Sheria hii. Lakini Serikali ikakae chini ije na *outline* nzuri ya vyanzo vya mapato wa kuendesha ile Tume pamoja na Bodi ambayo itaanzishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria hii naona kabisa kuna haja baadae ya ku-*harmonize* Sheria nyingine ambazo zipo ili kuweza kukidhi haja na utekelezaji wenye ufanisi wa Sheria hii. Nasema hivi kwa sababu gani? Kwenye Sheria hii kuna haki ya kusahaulika kwa maana ya kwamba, kwa maana ya kwamba *data* zangu zimekuwa zinatumiwa kwenye kampuni Fulani, labda ninapofariki inatakiwa nipate haki ya kusahaulika ndani ya muda fulani, lakini ukiangalia *Money Laundering Act* inazungumzia miaka 10 ya haki ya kusahaulika. Ukiangalia *Tax Act* inazungumzia miaka Saba ya haki ya kusahaulika, ukiangalia Sheria ya *TCRA* inazungumzia miaka Mitano ya haki ya kusahaulika.

Mheshimiwa Spika, *Vodacom* unapokuwa na *lane* yao ndani ya miezi mitatu haujaitumia unasahaulika ndani ya miezi mitatu, kwa hiyo sheria hii *i-harmonize* na iweke usawa kwamba kama ninapotumia *lane* fulani ya *Vodacom*, ninasahaulika ndani ya miaka mitatu na mimi vilevile ninahaki ya kusahaulika haraka iwezekanavyo baada ya kuonekana nimefariki au vingine vyovyote vile. Tunasema sheria ni msumeno inakata huku na huku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niseme kwamba, kutokana Muswada huu wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, tunafahamu kwamba kunakuwa na *hackers*, kunakuwa na *crackers* na kuwakuwa na *a lot of* watumiaji

ambao kwa mujibu wa upeo wao mkubwa wa Sheria hii wanaweza kufanya lolote kwenye sheria hii. Mimi ninaungana kabisa na mwenzangu aliyetangulia kwamba sheria hii inapaswa kuitwa Sheria ya Ulinzi Binafsi na Faragha. Maana halisi ya kuanzishwa au kutafuta kulinda sheria binafsi ni baada ya kwamba teknolojia imetuacha wazi. *The technology threats* ndiyo ambayo inapelekea kuundwa kwa taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi neno la maana na la msingi ni faragha ili kuweza kulinda taarifa binafsi ili kumfichia mtu faragha zake. Ukweli ni kwamba hata Taifa letu linahitaji faragha, kiukweli kabisa tunahitaji faragha na ni muhimu sana kipengele hiki kuingia katika jina la Muswada huu, kwa maana ya kwamba....

SPIKA: Ahsanteni sana Mheshimiwa.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwatwe na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge ajiandae.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia machache kwenye Muswada huu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kama kuna kipindi ambacho Tanzania inaenda kujijengea heshima Kimataifa pamoja na mambo yote ambayo yamefanyika, basi kwa kupitisha sheria hii tunaenda kuingia kwenye hanga za juu sana na tutakuwa tumejitengenezea heshima kubwa Duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako linaenda kuingia kwenye vitabu vya kutunga sheria ambayo kila mtu alikuwa anaisubiri. Wananchi wengi na wadau wameipongeza sana Serikali. Wamekupongeza sana kwa kukubali kuleta Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kuelezea manufaa ya Sheria hii kwa sababau kila mmoja ameeleza na kila mmoja anajua, ninachotaka kuisistiza ni kwamba taarifa zetu binafsi ni biashara, huko Duniani na huko kwenye hanga taarifa zetu ni biashara, zitaenda kutumika kibiashara. Katika kutumika kibiashara ni lazima tuhakikishe taarifa zetu ni sahihi na zinalindwa, kulindwa kwake kunakuja na sheria hii. Ndiyo maana katika kulinda haya maslahi kuna kitu tumekisema kwa juu juu sana, ni kwenye jina la Sheria hii, tunaposema tu Ulinzi wa Taarifa Binafsi mimi nafikiri kuna kitu kinapungua.

Mheshimiwa Spika, hii sheria ikiongezewa faragha mbele, ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha italetwa uzito sana, kuna nchi tayari wameishafanya hivyo New Zealand wanasema *Data Protections and Privacy* na hapa jirani Uganda wanataja hivyo hivyo, Tanzania tunapata wapi kigugumizi kuweka hiyo *privacy*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache kwenye *privacy*. Tukiacha Sheria ikawa hivi, kuna mtu mwingine atakuja hadharani ataanza kukuuliza wewe unaitwa nani? Ulizaliwa lini? Jina la Baba yako ni lipi? Kwa sababu hatujaweka *privacy*, *privacy* ni jinsi pia ya kuchukua hizo *data*, mkakae pembeni kwa siri na huyo mchukua *data*, mchukua taarifa, sasa tusipolinda hiyo nafikiri tutakuwa bado hatujajenga msingi ambao utakuwa imara sana.

Mheshimiwa Spika, kule Wanyakyusa mtoto wa kike hawezi kutaja jina la Baba Mkwe. Sasa ukilifanya hili liwe peupe kuna mtu atahukumiwa kwa kutaja jina la Baba Mkwe wake, usije ukafikiri kwa mfano sisi ng'ombe kama mkwe hawezi kusema kusema ng'ombe atasema hata linaloelekeana atasema ngwafi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninaomba hebu hili neno la faragha liingizwe ili taarifa zetu tunapozitoa pia ziwe ni siri. Mtu unaumwa magonjwa makubwa ambayo hutaki watu wengine wajue, huwezi ukasema na mwingine anasikia ni lazima kuwe na utaratibu wa *privacy*, utaratibu wa faragha kama neno faragha siyo zuri kwa Kiswahili tutafute neno lingine kuweka uzito, naomba sana hili neno liongezwe.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna vitu pamoja na uzuri wa sheria hii, kuna mtu ambaye tumemsahau, wakati wote sisi ni marehemu watarajiwa ukifa taarifa zako zinabaki kwenye vyombo. Je, kuna sehemu gani ambapo huyo marehemu ataenda kulindwa na taarifa hizo? Ninaomba tuweke taarifa za marehemu ni jinsi gani zitakavyolindwa na ni nani atayezisimamia? Kuacha hivi hivi, mimi Baba yangu alifariki, wengine hapa Baba zao wamefariki *data* zao tuna uhakika gani kwamba zitalindwa na sheria hii? Ninaomba hilo kama siyo sasa basi kwenye Kanuni liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho Sheria yeyote inayotungwa ili iwe nzuri, inatakiwa ilete manufaa na isiwe mzigo kwa wananchi, isiwe mzigo. Tumetunga sheria hii vizuri sana, sheria hii inaenda kusimamiwa na Tume lakini Tume itasimamiwa na Bodi, hawa ni watu wengi sana na hawa watu wengi watahitaji rasilimali fedha, woga wangu na baridi ninayoipata nikwamba mbona vyanzo vya pesa bado hatujawiweka vizuri. Sheria yetu haijawa wazi, inasema tu Bunge litapitisha, Bunge litapitisha kwa Bajeti ipi? Kwa nini wasitengeneze na wao vyanzo vyao? Ninaomba tunapoelekea huko mbele tuangalie jinsi ya kupata vyanzo ambavyo vitaelezwa *EWURA*, walipokuwa wanatunga Sheria walisema watatoa wapi pesa. Sisi kwenye sheria hii

tumesema kiujumla mno, ningeomba tuweke vizuri kwenye Muswada huu, tujue ni jinsi gani tunaenda kupata pesa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote sidhani kama kuna Mtanzania ambaye anaipenda Tanzania hatatupongeza kwa kupitisha Sheria hii, na mimi ninasema tuungane wote Wabunge hapa, tuipitisha Sheria hii kwa manufaa na mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan ajiandae.

MHE. INNOCENT S BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenipa afya na nguvu kuwepo katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niipongeze Serikali Muswada huu ambao ni muhimu na kwa kweli niseme ulichelewa. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kuwa tayari kupokea maoni ya Kamati pia maoni ya wadau, hakukuwa na mvutano wowote ule na Serikali ilitoa ushirikiano mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu ni muhimu sana. Tumekuwa tukishuhudia mambo mengi ambayo yanafanyika kwenye mitandao, tunashuhudia vitu ambavyo ni vya ajabu, ninaamini kuletwa kwa Muswada huu unaenda kulinda maadili ya Watanzania. Leo hii ukifungua kwenye mitandao, unakutana na vituko vya ajabu na mitandao hii inafunguliwa na watoto wetu, wanajifunza vitu ambavyo kwa kweli vinaondoa maadili yetu lakini ninaamini kwa Muswada huu sasa tunaweza kudhibiti hata wale ambao wanaleta taarifa ambazo zinaweza zikaondoa maadili yetu katika Taifa letu. Kwa hiyo, Muswada huu ni mzuri sana ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono Muswada huu kwa sababu unaenda kulinda utu wetu na unaenda kulinda taarifa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niliseme ni kwamba Muswada huu ni mzuri sana lakini ni lazima tujue chanzo cha mapato cha kuweza kuendeleza Muswada huu, maana tunaweza tukawa tumetunga Muswada lakini hatuna chanzo chochote cha mapato. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri utueleze hapa utakapokuwa una-*wind* hapa utuambie ni chanzo kipi ambacho tutaweza kupata mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niliseme ni kwamba Muswada huu unaenda kuinua biashara ya kimtandao, kwa sababu hawa wanaofanya biashara kwenye mtandao watakuwa na uhakika wa taarifa zao kulindwa na huu Muswada. Jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni kwamba, tumekuwa tukipitisha Sheria nzuri, nyingi na kwa kweli ukisikia Wabunge wanapokuwa wakichangia hapa Sheria zinakuwa ni nzuri lakini kwenye utekelezaji, wakati wa kutunga Kanuni zinakuwa Sheria za ajabu, tunaonekana Wabunge tumetunga Sheria za ajabu, tumefanya vitu vya ajabu. Hata mambo yaliyojitokeza kwenye tozo, tukaonekana Wabunge hakuna kitu chochote tulichotunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninashauri Bunge hili kama ndiyo tunaletewa Miswada hii kuipitisha iwe Sheria sasa tuwe na nguvu ya kuleta Kanuni hizi ambazo Serikali inaenda kuzitunga ili tujue kile ambacho sisi tumekipika, kinapakuliwa vipi, siyo tunakuja hapa, tunajadili Muswada, tunauweka vizuri halafu mwisho wa siku tunakuja kuletewa Kanuni za ajabu. Kwa hiyo, ninaomba sana hili jambo lazima liangaliwe, Bunge lazima lisimame kuhakikisha Sheria tunazoitunga na Kanuni zake zinakwenda kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Ninakushuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhan na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil ajiandae.

MHE. HAJI MAKAME. MLENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Muswada wa Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kabla ya kuchangia Muswada huu wa Uwekezaji, yale maoni yote yanayotokana na Kamati ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara naunga mkono kwa sababu nami ni miongoni mwa wanakamati ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwenye Muswada huu kuhusu jina la Muswada. Jina la Muswada limeandikwa jina la uwekezaji. Muswada wa mwaka 2022, jina hili ndilo ambalo linatokana na Sheria ile ambayo tunaenda kuifuta ya mwaka 1997. Hatuna tatizo na jina la Muswada lakini ingependeza zaidi kwa sababu Sheria hii ni ya Uwekezaji na uwekezaji ni sehemu muhimu sana katika Taifa, Taifa linategemea sana wawekezaji na ndiyo maana Sheria hii tumeenda kuibadilisha na kuleta Sheria mpya ivutie wawekezaji waje kufanya uwekezaji ndani ya nchi ili nchi iweze kupata mapato na kupata ajira ya watu wetu lakini kuweka uwekezaji na kupata fedha nyingi katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kamati katika sehemu hii tulipendekeza Sheria hii iitwe kuwa ni Sheria ya Kuvitia na Kulinda Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022. Aidha, wakati tulipokuwa tunazungumza na kujadiliana na Serikali walikubaliana na sisi na walikuja na kipengele kimoja tu ambacho pengine hawakukubaliana nasi, nao tulikuwa hatukai pamoja, hatuwezi kujadili ili kuweza kuona tunafikia katika hatua moja. Kwa bahati mbaya sana *schedule of amendment* tumeipta hapa asubuhi leo wakati karibu Muswada unasomwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakubaliana na Kamati yangu kwamba Muswada huu uwe na jina la kuvutia na kulinda uwekezaji Tanzania. Jina hili ni sehemu ya uwekezaji, tumeangalia nchi mbalimbali wamebadilisha jina la sheria yao na wameweka majina ambayo yanaweza yakavutia uwekezaji, hii ni sehemu ya kuvutia, jina maana yake mwwekezaji anapofungua tu sheria anakutana mwanzo na hili jina. Hili jina ikiwa sehemu ya kivutio maana yake litamshawishi kuona kwamba yeye anakuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niende katika Sehemu ya Pili. Tuliona kwamba hiki kituo kubadilisha jina na kuitwa kituo, tuna majina mengi ya vituo ikiwemo jina la kituo cha Polisi na vituo vingine, kwa sababu hawa wanaenda kufanya kazi kubwa. Tumewapa mamlaka makubwa, tumewafanya watu hawa waweze kuwashawishi wawekezaji waje Tanzania waweze kuwekeza, maana yake tumewapa majukumu makubwa, kwa nini tunaogopa kuwapa mamlaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala ulikuwa mkubwa ndani ya Kamati yetu juu ya suala hili, Kamati yetu tunasema kwamba tunapenda na tunashauri Serikali kituo hiki kisiwe kituo na iwe Mamlaka kwa sababu hii itawapa nguvu ya kufanya kazi zile ambazo zimekusudiwa, kuita kituo maana yake bado tuna hofu ya kwamba hawa wanaweza kufanya kitu gani? Lakini tukiwapa Mamlaka maana yake tumewawezesha yale ambayo tunayatarajia wao waende wakayafanye. Kwa hivyo inatakiwa tuje na jina hili kwenye ushauri wetu nami naunga mkono ushauri huu wa kituo hiki kubadilisha jina na kuitwa Mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho ni kwamba tuliishauri Serikali kuongezwe Kifungu cha 38, hivi Vifungu vipo 37 lakini kiongezwe Kifungu cha 38 ambacho maalum kitawangalia wazawa. Kwa nini tunataka kuwaangalia wazawa? Kwa sababu wao ndio ambao wanatakiwa washike uchumi wa nchi hii. Wazawa tunapowaacha nyuma maana yake tunaweza tukakosa watu ambao wanaweza kuhimili uchumi wa nchi hii, tukikosa watu wanaoweza kuhimili uchumi wa nchi hii ni hatari, kwa hivyo tuwaangalie Watanzania namna nzuri ambayo wanaweza kuwa mabillionea kama marehemu alivyosema katika hotuba yake wakati amekuja Bungeni hapa. Kwa hiyo, nasi tumeona kwamba ipo haja Kifungu hiki kiwepo na wazawa wasaidiwe. Kwa nini tumesema hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine linatokea tatizo wazawa wanakosa nguvu ya uwekezaji hasa pale ambapo inatokea wanakuja wageni wanakopa pesa mabenki ya nje, wanapokopa mabenki ya nje riba inakuwa ndogo sana lakini mabenki yetu bado riba ipo juu wanashindwa kushindana. Kwa hiyo, Kifungu hiki ni vizuri kikaongezwa na kuangaliwa maalum kwa Watanzania na kuona kituo au mamlaka ya uwekezaji ina uwaangalia Watanzania namna njema ambavyo anaweza kuwakuza kuwekeza ili waweze kuboresha uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema awali kwamba naungana na maoni yote ambayo yametolewa na Kamati yangu, lakini leo nimekusudia kuboresha katika maeneo haya ambavyo nimeyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Kwa sababu hawa wanaenda kufanya kazi kubwa tumewapa mamlaka makubwa, tumewafanya watu hawa waweze kuwashawishi wawekezaji waje Tanzania waweze kuwekeza. Maana yake tumewapa majukumu makubwa, kwa nini tunaogopa kuwapa mamlaka?

Mheshimiwa Spika, mjadala ulikuwa mkubwa ndani ya Kamati yetu juu ya suala hili na Kamati yetu imegonga na kusema kwamba tunapenda na tunaishauri Serikali kituo hiki kisiwe kituo na iwe mamlaka kwa sababu hii itawapa nguvu ya kufanya kazi zile ambazo zimekusudiwa. Kutokuita kituo maana yake bado tuna hofu ya kwamba hawa wanaweza kufanya kitu gani, lakini tukiwapa mamlaka maana yake tumewawezesha yale ambavyo tumeyatarajia wao waende wakafanye. Kwa hiyo, tuje na jina hili, ni ushauri wetu na mimi naunga mkono ushauri huu wa kituo hiki kubadilisha jina na kuitwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niende katika mchango wangu wa mwisho kwamba tuliishauri Serikali kwamba kiongezwe kifungu cha 38. Hivi vifungu viko 37, lakini kiongezwe kifungu cha 38 maalum ambacho kitawaangalia wazawa. Kwa nini tunataka kuwaangalia wazawa? Ni kwa sababu wao ndio ambao wanatakiwa washike uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, wazawa tunapowaacha nyuma maana yake sisi tunaweza tukakosa watu ambao wanaweza kuhimili uchumi wa wa nchi hii. Tunapokosa watu ambao wanaweza kuhimili uchumi wa nchi hii, hii ni hatari kwa hivyo, tuwaangalie Watanzania namna nzuri ambavyo wanaweza kuwa mabilionea kama marehemu alivyosema katika hotuba yake wakati anakuja Bungeni hapa. Kwa hiyo na sisi tumeona kwamba ipo haja kuona kwamba kifungu hiki kiwepo na wazawa wasaidiwe, kwa nini tumesema hivyo?

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine linatokea tatizo wazawa wanakosa nguvu ya uwekezaji, hasa pale ambapo inatokea wanakuja wageni wanakopa pesa nje, yaani benki za nje. Wanapokopa benki za nje riba inakuwa ndogo sana, lakini benki zetu bado riba iko juu, wanashindwa kushindana. Kwa hiyo, kifungu hiki ni vizuri kikaongezwa na kuangaliwa maalum Watanzania na kuona Kituo au Mamlaka ya Uwekezaji inawaangalia Watanzania namna njema ambavyo wanaweza kuwakuza kuwekeza ili waweze kuboresha uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema awali kwamba naungana na maoni yote ambayo yametolewa na Kamati yangu, lakini leo nimekusudia kuboresha katika maeneo haya ambavyo nimeyazungumza. Ahsante sana naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla ajiandae.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu kwenye hoja zilizoletwa mezani leo.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu kuna miswada miwili, kuna Muswada wa Haki ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kuna Muswada wa Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu naomba niulekeze kwenye Muswada wa Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania wa mwaka 2022. Kwa mujibu wa *index* ya utafiti ya uwekezaji ya Afrika inayoitwa *Deloit Africa Investment Attractiveness Index* iliyofanya tafiti kwa kutumia vigezo viwili vya *market access* au *market size* pamoja na *business environment* imeiweka Tanzania kwenye *rank* ya nane kwa mazingira mazuri na bora kwenye kuwekeza, ikiwa ya tatu kwa *East Africa*, tukiongozwa na Kenya na Rwanda. Na kwa mujibu wa *data* ya *World Bank* ya mwaka 2020 Tanzania ni nchi ya 141 kati ya 190 kwenye mazingira mazuri ya kuruhusu uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 tulipitisha *blue print* na lengo la *blue print* lilikuwa ni kutafuta suluhisho la matatizo ya uwekezaji yaliyokuwa yanatukumba kama Taifa. Tulikuwa tunakwama wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukapitisha *blue print* ikiwa kama *regulatory reforms* ku-improve *business environment* ya Tanzania. Sasa kwa masikitiko makubwa sana nimesoma *blue print*, nikilinganisha na mabadiliko yanayolewa kwenye sheria yaani huu muswada, nikawa nakosa *connection* ya vipi muswada huu uta-*accommodate*, utauganisha matokeo ya *blue print* na hoja zilizoletwa na mapendekezo na tunavyoelekea mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo mwaka 2022 tunapitisha muswada huu ambao baadae utakuwa sheria, hatujui tutakaa kwa muda gani kuja kupitisha muswada mwingine mpya ambao tutatunga sheria mpya ya uwekezaji. Kwa hiyo, hii ndio nafasi yetu pekee ya kuishauri Serikali ili kuleta mazingira mazuri ya uwekezaji Tanzania. (Makofi)

Kwa hiyo, Waziri anapokuja kufanya majumuisho atujibu, aseme ni kwa vipi mapendekezo na hoja zilizoletwa kwenye *blue prints* na *effectiveness* zilizoonekana zitaleta tija kwenye muswada huu, mimi sijaona, nilivyosoma vyote sijapata kuona. Kwa hiyo, inawezekana yeye anayo majibu yaani kiasi gani *blue print* imekuwa *accommodated* ndani ya muswada ulioko mbele yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye kifungu cha pili cha muswada wa sheria, kinatoa masharti kwamba sheria hii itatumika kwa taasisi za kibiashara zilizokidhi matakwa yaliyoko kwenye kifungu cha 2(2).

Sasa nilivyokuwa nakisoma kifungu kidogo cha pili kikasema; kwa Mtanzania, kifungu kidogo cha (2)(b), Mtanzania ambaye atapewa *favor* zilizomo ndani ya muswada huu ambazo tunaziita *vivutio* na atapata tija na ulinzi unaoletwa kwenye muswada huu ni Mtanzania ambaye ataweka mtaji usiopungua dola za Kimarekani 50,000.

Mheshimiwa Spika, dola za kimarekani 50,000 ukizipiga kwa *Tanzania shilling* ya sasa ni zinakaribia milioni 115. Ni Watanzania wangapi wana shilingi milioni 115 za kuweka mitaji ya kuanzisha biashara mpya ambazo watakuja kuhitaji *incentives* na huruma zilizoko kwenye muswada huu?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wetu wengi hawawezi, hawana mitaji hiyo. Wanaanza wakiwa *underground*, mitaji midogo, wanaanza biashara *from the grassroot*, kwa hiyo, ni vigumu kupata unafuu uliotolewa na muswada wa sheria hii na kuna faida nyingi zinaletwa humu kwenye *vivutio*, kuna misamaha ya kodi, kuna vitu kwenye jinsi ya usajili, ridhaa, leseni urahisi wake wa kupatikana, zote hizo, lakini sasa leo unaenda kuweka kifungu ambacho unasema ili Mtanzania alindwe na matakwa ya sheria hii ni lazima awe kafikisha mtaji wa dola 50,000. Tunaenda wapi? Kwa nini tusiweke kwa Watanzania tupunguze kiwango cha mtaji ili kuwaruhusu Watanzania wengi wanaofanya biashara, hasa wadogo, wawe *accommodated* ndani ya muswada huu utakapokuwa sheria kuja kuwalinda na kuwapa unafuu.

Mheshimiwa Spika, moja katika *industry* inayokuwa kwa kasi sana ni mafundi washoni wa nguo (*tailoring*). Mimi nataka nikutajie baadhi tu ya *tailoring marts* zinazofanya vizuri sana sasa hivi; moja ni *Shine by Catherine* ya dada yangu Mheshimiwa Catherine Magige, nyingine ni *Carenitho Smart*, yuko dada anatushona yuko nje hapo tu, nyingine ni *Better Design* ya dada

yangu Mheshimiwa Sylvia Sigula, kuna nyingine *JM International Collection* ni kijana wa Kitanzania, kuna nyingine inaitwa Suti Bega. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka mitano mpaka 10 tutakuwa hatuvai tena suti zinazotoka Uturuki wala China, tutakuwa tunavaa suti zinazoshonwa na mafundi wetu Tanzania, kwa sababu imani ya kuwaamini mafundi wetu inakua siku hadi siku. Hii suti niliyovaa hapa imeshonwa na Mtanzania. (Makofi)

Sasa moja katika maeneo ambayo nahisi bado Muswada wa Sheria za Uwekezaji hauwatendei haki ni wafanyabiashara wanaokuwa, wanaojikwamua, hasa hawa miongoni mwao ni hawa ma-*tailoring* ambao ni Watanzania wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwekezaji anayetoka nje akija akianzisha kiwanda cha kutengeneza aidha misumari au mabati atapata unafuu wa kuingiza *raw materials* ya *wire rods* kama *raw materials*, lakini Mtanzania anayeshona anaingiza kitambaa kama bidhaa sio *raw material*. Kwa hiyo, akiingiza kama bidhaa yeye anakinunua kama bidhaa, anaenda kukikata akishone suti, anaanza kukamatwa anaponunua bidhaa, halafu akishashona suti hiyo ikiingia dukani anaanza kukamatwa tena.

Mheshimiwa Spika, sasa maoni yangu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30 kengele ya pili imeshagonga.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, sawa ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kwamba lazima tutengeneze mazingira wakati wetu ni huu. Tukikubali kupitisha muswada ambao bado hautoi nafuu nzuri kwa Watanzania wetu tutakuja kukaa tena zaidi ya miaka 15/20 kusubiri jambo hili litokee tena.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue jitihada na maoni yetu kuona wanafanyaje kushughulikia jambo hili ili kuifanya Tanzania iwe sehemu nzuri ya uwekezaji. Haya ndio maoni yangu. (Makofi)

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Tarimba Abbas ajiandae.

MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi nikiwa ni miongoni mwa wachangiaji wa sheria hii.

Kwanza niseme tu mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ambao tulijadili kwa kina huu Muswada wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Mimi nasema hatujachelewa, tumekuja muda mzuri na muda muafaka kwa ajili ya kujadili na kupitisha sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika sheria hii tulipata wadau wengi kwa mara ya kwanza, walifurika kwenye chumba chetu na kwa muda wote kulikuwa hakuna mizozo ya kisheria na kanuni na miongozo yao, walitukubalia na sisi tukawakubalia, lakini katika kujadili suala hili kuna neno lilijitokeza, kuongezwa neno faragha ili kutia nyama kwenye sheria hii na ndio maana wajumbe wengi ukiona waliosimama hapa kitu faragha imo, ingawa muswada ndani yake humo ndani kuna neno linaitwa faragha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nakubaliana na neno faragha na liangaliwe vizuri kwenye kamusi ya Kiswahili ya Oxford, lina maana yake. Kamusi ya Kiswahili ya Oxford neno faragha lina maana yake, sitaki kuendelea sana, lakini nasema kwamba sheria hii ikipitishwa itajenge utu wetu, heshima yetu na faragha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ndogo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ajiandae.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii. Nilitaka tu kumpa taarifa Mheshimiwa Ramadhan kwamba na mimi hii suti niliyovaa leo, hii *blazer*, imeshonwa na kijana wa Kitanzania anaitwa Mtani Nyamakababi, lakini pia nitakayovaa kesho imeshonwa na Sheria Ngowi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenda kwenye hoja ni kwamba tunatunga Sheria ya Uwekezaji katika zama ambapo mataifa mengi duniani yametunga sheria zinazofanana na hii ya kwetu, lakini pia tunatunga sheria hii tukizingatia kwamba sheria inayohusiana na uwekezaji kwa kiasi kikubwa ni sheria ambayo inapaswa kuweka mazingira ya kufanya biashara na mazingira ya kuvutia mitaji ndani ya nchi vizuri zaidi. Sasa kwa masikitiko makubwa sheria hii haiendi kutufikisha mahali pa tofauti sana na tulipo sasa, hayo ni masikitiko yangu.

Mheshimiwa Spika, na ninasema hivyo kama tutajilinganisha na nchi za hapa jirani tu, tukiacha zile za mbali, tukijilingaisha na Rwanda kwa mfano, walipotunga sheria yao ya uwekezaji waliunda chombo kinaitwa *RDB (Rwanda Development Board)*. *Rwanda Development Board* ni *One Stop Centre* kwa uhalisia wake, sio kwa maneno ni *One Stop Centre*; ukifika pale utasajili kampuni yako, utajisajili kwenye kodi, utajisajili kwenye taasisi kama *OSHA*, kwenye taasisi kama *NSSF*, taasisi zote za *compliance* utazikuta pale *RDB* na utaondoka na *documents* zote pale, utalipa *fees* zote pale, tozo zote pale, unaondoka pale na makaratasi yako unaenda kufungua ofisi unaanza biashara, lakini sheria yetu hii ambayo tunaenda kuitunga leo haijaweka mazingira hayo ya kuwa *One Stop Centre* kwa uhalisia wake, hilo ni jambo linalosikitisha.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya maendeleo kwenye dunia inataka pale ambapo wewe umechelewa kuingia kwenye jambo basi siku unayoingia uingie vizuri zaidi, uwe tofauti na wale ambao waliingia miaka mitano nyuma. Sasa sisi tunapoenda kutunga sheria ambayo wala haizifikii sheria za nchi nyingine ambazo zilitungwa miaka mitano, miaka kumi hapo nyuma ni jambo la kusikitisha kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *Silicon Valley* ya kule Marekani ni *technological hub*. Ni sehemu ambapo wanafanya *incubation* ya wagunduzi na wavumbuzi wa teknolojia za kisasa, lakini China alipoimarisha uchumi wake na akaanza kufanya utafiti (*research and development*), akaanzisha mji wake kuufananiaha na ule wa *Silicon Valley*. Alipokuja kujenga mji unaitwa Shenzhen, amejenga mji mzuri na wa kitofauti sana ambao unatoa *challenge* kubwa sana kwa *Silicon Valley* ya kule Marekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata sisi tunapoenda kutunga sheria yetu leo tulipaswa kutunga sheria ambayo itazishinda kwa vivutio sheria ambazo zimeshatangulia za majirani zetu tu hapa, hata tusijilinganishe na watu wa mbali sana, majirani zetu kama Mauritius wana sheria nzuri za uwekezaji, majirani zetu kama Kenya, majirani zetu kama Rwanda nimewataja, wana sheria nzuri sana za uwekezaji ambazo zinaweka mazingira rahisi sana ya kufanya biashara. Kwa sababu unapotunga sheria ya kuvutia uwekezaji vitu vikubwa viwili ni *key*, cha kwanza ni urahisi wa kufanya biashara kwenye hiyo nchi, lakini cha pili, kutabirika kwa mifumo na miundo ya kisheria yaani *legal framework* yote iwe inatabirika katika hiyo nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi sheria yetu kwa mfano pamoja na masharti mazuri yaliyowekwa kwenye *Blue Print for Regulatory Reforms* kwenye biashara na uwekezaji ningetarajia vile vivutio na yale masharti mazuri yaliyowekwa kwenye *blue print* yangeingizwa kwenye *general provisions* za hii sheria, lakini sheria hii haikufanya hivyo. Hilo ni jambo ambalo nimelishangaa kidogo nilipokuwa naipitia hiyo sheria kabla ya kuja kuchangia hapa kwamba tumeweka masharti mazuri sana kwenye *blue*

print, lakini hatujayaweka kwenye sheria, kwa nini? Sielewi! Ningetarajia kwa kweli nione masharti yale yamewekwa kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama tungetaka kupata mafanikio yanayotusababishia kutimiza hayo malengo makuu mawili niliyoyasema ya *easy of doing business* na *predictability* basi tungepaswa kuipa hadhi kubwa zaidi hii TIC, kwa sasa hivi ni Kituo cha Uwekezaji, lakini kama tungetaka kuipa nguvu zaidi hii TIC tungeweza kufanya mambo mawili, tungeipa mamlaka kamili kuifanya *authority* ama tungeipa mamlaka kamili kwa kuifanya kuwa *commission*. Na kufanya hivyo tungeweza kuwataka sasa, kwa mujibu wa sheria, TRA wakaleta afisa wao pale mwenye mamlaka kamili akawa anatumia sheria ya TRA kutokea pale TIC kwa hivyo, akawa anafanya mambo yote kutokea pale TIC.

Mheshimiwa Spika, BRELA wangeleta mtu wao pale, Afisa ambaye anakasimiwa mamlaka na yule Mkurugenzi Mkuu wa BRELA anakuja kukaa hapa TIC. Afisa mkubwa, siyo *junior* ambaye akishapokea maombi ya wawekezaji aondoke na mafaili ayapeleke tena BRELA na yule wa TRA ayapeleke tena TRA na yule wa NSSF ayapeleke tena NSSF. Tungetarajia hizi ofisi zote; OSHA na wengine wote ambao wanahusika na masharti ya *compliance* wawekwe pale TIC.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ingekuwa ni *commission* na pengine hao maafisa wanaohusika na *compliance* wangukuwa ni makamishna ambao wangukaa pale na wangukuwa na mamlaka kamili ambayo yanakasimiwa na zile sheria nyingine. Hapo tungesema tumefanya mabadiliko makubwa na hivyo tumejenga Shenzhen ambayo ni ya kisasa ukilinganisha na *Silicon Valley* ile ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, pia tungetaka kuongeza mamlaka, kwa hiyo mamlaka mpya ambayo naifikiria kichwani, basi hata uwekezaji kwenye madini, kwenye kemikali hatarishi, ungepaswa kusimamiwa na mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Vile vile vivutio vyote ambavyo vinatolewa nje ya mamlaka hii vingepaswa kutolewa kwenye mamlaka hii. Badala yake leo hii tuna ile Kamati inaitwa NISC, ambayo nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye Mwenyekiti wake, ingepaswa kujadili mambo mengine lakini siyo kujadili vivutio vya uwekezaji. Mambo yote ya vivutio tungeyaweka sehemu moja, kwamba kuna miradi inayokwenda kujadiliwa tena NISC ama kuna Waziri fulani anajadili miradi yake kwenye eneo lake au sekta yake, naye anatoa vivutio vyake, hapana. Vivutio vyote tungeevichukua tukavilundika kwenye hiyo mamlaka na ikafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ...

1 NOVEMBA, 2022

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana, shukrani. *(Makofi)*

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba, atafuatiwa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Waziri ajiandae.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa dhiti kabisa kwa kunipa nafasi hii, Mungu akubariki sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza katika hoja iliyoko mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022. Kabla sijaendelea na mchango wangu, naomba niunge mkono hoja hii na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waweze moja kwa moja kuupitisha huu Muswada na kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwanza katika mtazamo wa mwekezaji. Mimi *Alhamdulillah* nashukuru pia ni mmoja kati ya wawekezaji. Wawekezaji wana mitazamo yao, Serikali ina mitazamo yake. Sasa hebu tuangalie mtazamo wa mwekezaji. Mtazamo wa mwekezaji uko katika sura mbili sana, wamekubaliana ni sura mbili. Sura ya kwanza wanajiuliza: Je, hii fedha yangu ninapoipeleka itafanya kazi ya kuleta faida? Ndiyo kitu kikubwa. Pale wanaangalia kitu wanakiita *the power of compounding*; Kiswahili chake kidogo kinanipa mashaka. Upande mwingine wanaangalia *risk* na *returns* katika *investments*.

Mheshimiwa Spika, sasa hebu tuangalie *the power of compounding*. Hapa wanasema ni utaratibu wa uwekezaji ambao unakuhakikishia kupata faida na gawio ambalo pengine unaweza ukalitumia kuendeleza biashara yako ile ile ama kutengeneza *investment* nyingine. Hao ndio *investors*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, wao wanaangalia sababu tatu kuu, kwa nini kuwepo na *investment*? La kwanza, wanaangalia mapato ya Serikali kwa maana ya kodi, ile *investment* itengeneze utaratibu wa kuipatia Serikali mapato. Vilevile uwekezaji usaidie kuboresha hali ya kifedha kwa watu pale wanapofanya shughuli za kibiashara katika zile *investments* ambazo zimewekwa. Ya tatu, kuleta ajira na mambo mengine ambayo yanahusiana.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia katika jambo kama hilo, kuja na Muswada kama huu maana yake sasa tunajielekeza katika ule utaratibu ambao tunajiuliza kumbe ni muhimu sana kwa Serikali kuleta utaratibu mzuri wa uwekezaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri zaidi kuliangalia lile ambalo Waheshimiwa Wabunge wengine wamelizungumzia; *ease of doing business*. Tuipongeze Serikali kwa juhudi kubwa ambazo wameanza kuzifanya katika mwaka wa fedha huu tulionao wakati tukipitisha bajeti. Sheria karibu 14 na zaidi zimeangaliwa na kufanyiwa marekebisho. Nini faida yake? Hebu tuangalie faida ya yale madogo tu tuliyoyafanya katika masuala mazima ya *ease of doing business*.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungimzia hapa *position* yetu tuliyokuwanayo. Mwaka 2019 tulikuwa ni nchi ya 141 kutoka kwenye nafasi ya 144 mwaka 2018. Sasa wataalam wa *World Bank* wanasema mwaka 2022, huu tulionao, yawezekana tukapanda tukawa ni nchi ya 138 kwenye vile vigezo vyao. Mwaka 2024 *outlook* inaonesha tutapanda kufikia nchi ya 136, maana yake Tanzania tunapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, kama tunapiga hatua, lakini hatua zenyewe ni ndogo, siyo kubwa, naishauri Serikali kwamba kwa kuwa yawezekana kupiga hatua kwa kufanya marekebisho katika sheria zetu, na siyo tu sheria ya uwekezaji, tuangalie *supporting laws* nyingine, kwa sababu sheria ya uwekezaji ni sheria mama, lakini kuna sheria nyingine zinazotusaidia kwa mfano, sheria za kodi, sheria za upatikanaji wa *business licenses*, sheria za *repatriation* ya faida na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa kwa Serikali kuangalia katika nchi zikiwemo nchi ambazo ziko karibu, ameizungumzia sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla; maeneo ambayo yamefanya vizuri na siyo tu kutegemea kufanya mambo ya kubahatisha. *I am sorry* natumia neno “kubahatisha”, kwa maana pengine hii itafanya kazi ama haitafanya kazi, lakini cha msingi ni kutafuta yale maeneo ya kisheria ama ya kiuendeshaji ambayo tukiyaifanyia marekebisho, hakika yatatupa *quick wins*. Tuna kazi ya kufanya na lazima tuziangalie hizo taratibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuangalia yote hayo, kuna juhudi hapa zinafanywa na Mheshimiwa Rais. Nataka nilete mfano wa juhudi aliyoifanya alipokwenda *Dubai Expo* mwaka 2021. Kulikuwa na *MOUs* nyingi sana pale zimesainiwa, kuna mikataba mingi pale imesainiwa; nilitaka nijue baada ya kusainiwa yale mambo ambayo yanavutia *investment* kwa Tanzania, ni vipi sasa Serikali imejikita katika kuhakikisha kwamba mambo yale yanaendelezwa na kweli yanatuletea tija katika uwekezaji wa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, tunaboresha sheria, naam, lakini sheria peke yake bila ya sisi kubadilika na kuwa ni watu ambao tunaendana na dunia ya sasa inayokaribisha *investment* na *investors* wasionekane ni maadui; kulikuwa na wakati *investors* hapa walikuwa wanakimbiakimbia sana, tuwakaribishe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Tanzania huko nje, sisi ambao tunapata nafasi ya kuzungumza na wenzetu, tunaona wanaiangalia Tanzania kama moja ya nchi ambayo imefanya marekebisho makubwa sana katika sheria zake za kukaribisha *investment*. Hivyo, tuchukue mtazamo huo ambao ni mzuri kufanya Tanzania ineemeke na Mtanzania mmoja mmoja aneemeke kwenye njia kama hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, na kwa ushauri huo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigaha, atafuatiwa na Mheshimiwa mtoa hoja halafu nitaita *set* nyingine ya wachangiaji.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii hoja muhimu ya Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ambao ni muhimu sana. Kwanza nianze kwa kuunga mkono mapendekezo yaliyowasilishwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo: Umuhimu wa kutunga sheria hii mpya ya uwekezaji ulizingatia sana maoni ya wadau mbalimbali ambao ni wa ndani na nje ikijumuisha na taasisi za Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (*UNCTAD*) ambao pia kwa vipindi tofauti wamekuwa wakifanya tathmini ya utekelezaji wa sheria yetu.

Mheshimiwa Spika, pia sheria hii ni sehemu ya utekelezaji wa *blueprint*. Wachangiaji wamesema wengi, na mimi niseme ile *Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment in Tanzania*, moja ya changamoto zilizokuwepo ni pamoja na kuwa na sheria na sera mbalimbali ambazo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa sheria unachangia katika kuhakikisha tunaweka mazingira ambayo yanatabirika kwa wawekezaji wa ndani na wa nje katika nchi yetu. Katika Muswada huu tumeona kwa kuzingatia umuhimu wa Watanzania kupata au kuwekeza kwa kunufaika na

vivutio hivi, moja ya maeneo ambayo yameangaliwa ni hayo na kupunguza mtaji au fedha zinazohitajika kupata vivutio kutoka Dola za Kimarekani 100,000 mpaka 50,000. Hii ni moja ya maeneo ambayo yameangaliwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka sheria hii kama walivyosema wachangiaji wengi, ni ya muda mrefu; ya tangu mwaka 1997 na katika kipindi hiki kuna marekebisho mengi yamefanywa na sasa ikafikia wakati kwamba hatuwezi kuendelea tena kurekebisha, kwa hiyo, lazima tulete itungwe upya kama sheria ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli moja ya maeneo ambayo yameangaliwa katika Muswada huu ni kuona namna gani tunaweka sheria hii iwe inatabirika. Moja ya viashiria vilivyokuwa vinavunja moyo wawekezaji hasa kutoka nje, ni kutokutabirika kwa sheria zetu. Ila katika Muswada huu tumeona wameweka sharti la muda wa mradi, miaka mitano. Maana yake mwekezaji akiwekeza anakuwa na uhakika kwamba katika muda ule aliyopewa wa vivutio wa miaka mitano, maana yake hakutakuwa na mabadiliko katika uwekezaji wake. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo wadau wengi walikuwa wanachangia kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaipa nguvu zaidi TIC. Waheshimiwa wachangiaji wa Muswada huu wamesema tuweke kama mamlaka. Ni kweli, moja ya maeneo makubwa ambayo Muswada huu umeangalia pia ni kuipa jukumu la kuratibu na kuandaa jam za uwekezaji nchini (*National Investment Branding*) Kituo cha Uwekezaji. Kwa hiyo, maana yake imeongezea nguvu tofauti na hapo awali kabla ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sheria inataka tuwe na mfumo wa kielektroniki wa kuwezesha usajili wa miradi utakaounganishwa na mifumo ya taasisi nyingine muhimu zote zinazohudumia wawekezaji hapa nchini. Maana yake Muswada huu unaweza kutusaidia sasa kupunguza malalamiko ya wawekezaji kwenda kutafuta huduma kwenye taasisi tofauti tofauti. Maana yake tukiitekeleza itarahisisha angalau kupunguza ule usumbufu ambao wanapata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo yameongelewa na wachangiaji ni kuhusiana na suala la *One Stop Centre*. Ni kweli, katika changamoto mojawapo ambazo wawekezaji walikuwa wanakutananza ni pamoja na hili la kutokuwa na taasisi ambayo ina mfumo unaohudumia watu wengi kwa mahali pamoja (*One Stop Centre*).

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine ambazo tunadhani baada ya kukamilika kwa Muswada huu na mfumo huu wa kielektroniki, utapunguza ule usumbufu wa kwenda kwenye taasisi tofauti tofauti ambazo tunaamini

katika mfumo huu utawezesha kuwa na sehemu moja ya kupata huduma, au tunasema huduma ya mahali pamoja.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia ni kuona namna gani ya kupunguza usumbufu au tuangalie *mindset*. Mheshimiwa Tarimba amesema kwa wawekezaji, lakini mtazamo kwa ujumla wa Watanzania kwamba Muswada huu utusaidie sasa pia na sisi wengine kuelewa umuhimu wa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kupitia Muswada huu, sheria hii, pia tunapitia na sera ambazo zitatusaidia kuhakikisha Watanzania wengi wananufaika na sheria hii ya uwekezaji na mazingira haya rafiki ya kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, umeongelewa umuhimu wa kuangalia sekta nyingine ambazo hazisimamiwi na sheria hii. Tunaamini tutaendelea kufanyia kazi kwa maana ya kuhakikisha pia uboreshaji kwenye utendaji wetu wa kila siku katika utekelezaji kupitia Muswada huu na sera ambazo zinatumiya uwekezaji, tunaweza kuweka mazingira ambayo yatasaidia na sekta zote ambazo ni muhimu zisiwe changamoto kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono hoja ya Muswada huu ili uweze kupitishwa.

Mheshimwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, uhitimishe hoja yake.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Nitoe shukrani kwa Mheshimiwa David Kihenzile, Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Haji Mlenge, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Abbas Tarimba na Naibu Waziri Mheshimiwa Exaud Kigahe kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wameshiriki mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, suala la kutunga sheria ni jambo endelevu, ndiyo maana kila mwaka Serikali inakuja na Miswada mbalimbali kwa lengo la kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano. Serikali imezingatia maoni yaliyotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa Muswada huu kulikuwa na hitaji la kuzungumza kama Muswada huu umezingatia utekelezaji wa *blueprint*. Ukiangalia maudhui katika *blueprint* malengo ya Serikali ni kuondoa urasimu, lakini vile vile kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili kuweza kuvutia uwekezaji na biashara na kulinda biashara ambazo tayari tunazo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia maudhui ya Muswada huu yamelenga kulinda na kuvutia uwekezaji, kwa mantiki hiyo, Muswada huu ni sehemu ya kutekeleza *blueprint*. Kwa hiyo ningependa niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba *blueprint* ni *comprehensive* na Serikali inaendelea kufanya kila jitihada za kiseria, kisheria na kikanuni kuhakikisha tunaendelea kutekeleza *blueprint*. Kwa hiyo huu ni mwendelezo na Muswada huu unaenda kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna *concern* ya jina, kwamba jina likiwa linavutia (*jina by itself*) linaweza likawavutia wawekezaji. Hata hivyo, napenda kuwaondoa wasiwasi pia kwenye suala la jina. Ukiangalia kwenye *literature* wawekezaji kwenye nchi yoyote wanaangalia nini, sio jina *as such* kama jina la kituo, kwa mfano *Tanzania Investment Centre* bali wawekezaji kabla hawajaenda kuwekeza kwenye nchi yoyote wanaangalia masuala mbalimbali. Kwanza, uwepo wa amani katika hiyo nchi na Tanzania tunajivunia kuwa ni kisima cha amani. Hivyo, hiyo nayo ni *factor* ya kuvutia uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wawekezaji vile vile huwa wanaangalia uwepo wa rasilimali watu (*work force*) je, ni *competitive*, ukiangalia *unit labour cost* ya kutengeneza bidhaa fulani ukilinganisha na nchi nyingine, je, nchi yako ina-*compete* katika hilo. Kwa hiyo ndio maana tunaendelea kuwekeza katika elimu, katika Vyujo vya Ufundi Stadi ili kuwaandaa watu wetu kuwa *competitive* ili iwe ni sehemu ya kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, lingine, wawekezaji huwa wanaangalia *predictability* yaani sera zako zinatabirika kiasi gani, sheria na hata siasa. Nchi ambazo zina machafuko au amani haina uhakika yaani haitabiriki, nchi hiyo haiwezi kuvutia uwekezaji. Yote haya tunaona ni namna gani nchi yetu tuko *competitive*, kwa sababu haya yote ninayoyataja nchi yetu tuna kila sababu ya kujivunia na kuwa na *confidence* kwamba tunaweza kuvutia uwekezaji. Hata hivyo, inabidi tujikite kwenye suala ambalo hata kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge na hili jambo nadhani linahitaji muda wa kutosha kutoa elimu kwa jamii, suala la *mindset*. Hatuwezi kufanya na kutegemea kwamba tutatunga sheria ambayo itakuwa ni *silver bullet* ya kila kitu, kama ni urasimu ipo sehemu sheria inaweza ikapunguza, lakini ipo asilimia kubwa ya kupunguza urasimu kwa kubadilisha fikra za sisi wenyewe kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika pamoja na Wabunge wenzangu kwenye suala la *mindset changes*, sisi wote kama viongozi tuna jukumu la kuisaidia jamii yetu kuwa na *mindset* ambayo ni *facilitative* badala ya kuwa *frustrating* hata kwenye utumishi wa umma, vile vile kuvutia uwekezaji, kuvutia biashara, *mindset* ya kudhibiti (*regulatory*) ni *mindset* ambayo inatucheleweshwa. Kwa hiyo kwenye hili tuendeleo kushirikiana ili tuweze kuwa na fikra chanya ya sisi viongozi, utumishi wa umma na kuendelea kuelimisha ili kuwa na mikakati ya kuhakikisha tunakuwa na *mindset* sahihi ya kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji huwa pia wanaangalia *fiscal structure* au *fiscal regime* ya nchi ikoje kwenye upande wa kodi kwa maana ya *tax payments, regime* ikoje na hata *non-tax payment* upande wa halmashauri zetu, zile tozo na *non-tax charges* ambazo halmashauri zetu zinatoza. Wawekezaji huwa wanaangalia vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu masuala ambayo yamejitokeza, ningependa kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeleta Muswada huu unaolenga kuwa sheria bora zaidi kuliko ile ya mwaka 1997. Suala la jina, kwa mfano kuna Mheshimiwa Mbunge alisema kwamba, wawekezaji wanapenda nini. Napenda niwakumbushe kwamba Mwaka 1990 tulikuwa na Sheria inaitwa *The National Investment (Promotion and Protection Act, 1990)* unaona ni jina lefu, lakini malengo yalilenga kutibu kile ambacho pia tumekichangia hapa kwamba tuweke *protection* kwenye jina lakini pia tuweke *promotion*. Hata hivyo, mwaka 1997, tulifanya marekebisho ya sheria hii ambayo leo hii pia tumeiboresha na sheria hiyo imebadilishwa mara nyingi ili kuifanyia maboresho. Kwa hiyo ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kikubwa ni maudhui yaliyopo kwenye sheria na sio jina limebeba uvutiaji kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, vile vile Muswada huu utakuwa sheria bora kwa kuwa umebeba matarajio ya wananchi wetu. Muswada huu pia unalenga kuwa sheria itakayoboresha mifumo ya kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba kwa nini sheria hii haijainclude sekta za madini, gesi asili na *extractive industry* kwa ujumla wake. Ukiangalia nchi zote *rich countries* huwa zinakuwa na *tax regime* inayojitegemea kwenye usimamizi wa *extractive industries*. Sisi Tanzania sio kwamba tuko peke yetu *bench mark* nchi zote ambazo zina utajiri wa gesi ya asili huwa zina *a different tax regime* kwa ajili ya kusimamia sekta hizi, lakini sheria hii haizui Kituo kuwa *facilitative* hata kwenye uwekezaji ambao uko kwenye hizo sekta. Kwa hiyo hilo nalo ningependa kuwaondolea wasiwasi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, kwa nini sekta binafsi kusiwe na mjumbe? Ukiangalia muundo wa Serikali, muda wote huwa inashirikiana na *Tanzania Private Sectors Foundation* ipo *Tanzania National Business Council* na *Tanzania Chamber of Commerce Industry Association*. Kwa hiyo pamoja na maboresho ya sheria hii bado Serikali itakuwa inawajibika na kulazimika kushirikiana na taasisi hizi za sekta binafsi ili kuhakikisha tunashirikiana ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuwahakikishia wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwenye upande wa kanuni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa, dakika mbili malizia.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kanuni, sheria yenyewe inalenga kuwa *facilitative*. Nitashangaa sana kwamba sisi ambao tumeleta Sheria hii iwe *facilitative* kwenye uwekezaji na ufanyaji biashara wenyewe tukatengeneze kanuni ambazo zitatufunga. Kwa hiyo napenda kuwatoa wasiwasi kwamba Kanuni ambazo tutazitunga ni kwa ajili ya kusaidia na kuipa nguvu sheria hii iweze kufacilitate uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nimalizie na suala la mtaji (*threshold*) Serikali imezingatia kuwawezesha Watanzania wenzetu kuwa sehemu ya kunufaika na hivi vivutio na ndio maana masharti yametoka hitaji la dola laki moja kuwa dola elfu hamsini. Hii haimaanishi kwamba kila atakayetaka kufanya biashara anazuiwa kufanya biashara. Sheria hii imelenga wale ambao wamekuwa wakihitaji *incentives* za Kituo basi waweze kunufaika na ndio sababu Serikali imeona ni vyema kushusha kutoka dola laki moja kwenda dola elfu hamsini. Hata hivyo, zipo sheria mbalimbali ambazo zitaendelea kusaidia wafanyabiashara wadogo sana na wakubwa ili waendeleo kufanya biashara zao na kuweka mazingira ya kuwasaidia

wakue. Watakapofika kwenye uhitaji wa kwenda TIC basi sheria hii itakuwepo na ndio maana imezingatia suala la Watanzania ambao kipindi cha nyuma ya mwaka 1997 ilikuwa mpaka uwe na dola laki moja lakini sasa imeshusha kuwa dola elfu hamsini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa nimwite Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari aje ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022. Jumla ya Wabunge saba wamechangia Muswada huu na naomba kwa heshima kuwatambua, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Stella Fiyao, Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil.

Mheshimiwa Spika, natambua hoja nyingi zilizotolewa ni za ushauri ambazo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutazingatia kwenye utengenezaji wa kanuni, lakini kwenye utelelezaji wa sheria ambayo tunaipendekeza kupitishwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitambue kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya Kudumu ya Miundombinu. Katika taarifa yao kwetu ambayo tumeipitia tumezingatia ushauri wao na niwahakikishie Mwenyekiti na Kamati yako kwa niaba ya Bunge wamefanya kazi nzuri sana ambayo imerahisisha kazi yetu kuendelea huko mbele.

Mheshimiwa Spika, pengine niguse hoja tatu kwa kifupi sana ambazo ni muhimu kuzitolea ufafanuzi. Hoja ya kwanza, aliitoa *Engineer Ulenge*, hoja ya haki ya marehemu, mtu ambaye hayupo tena duniani. Nataka niwahakikishie ukiangalia kifungu cha 30(4) kimetaja sio tu haki ya marehemu, lakini pia haki ya mtoto, haki ya mtu asiye na akili timamu, au mtu mwingine yeyote asiye na uwezo wa kutoa ridhaa, kwa sababu katika kulinda haki hizi tumetaka itolewe ridhaa. Kwa hiyo, inapotokea mtu ni marehemu au ni mtoto au hana akili timamu au hana uwezo wa kutoa ridhaa, sheria imependekeza na imetaja mzazi, mlezi, mrithi au wakili wake

na kadhalika ambao wanaweza kufanya kwa niaba yake . Kwa hiyo jambo hili limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ya suala la vyanzo vya mapato ambalo tumelijadili kwenye Kamati lakini na Wabunge wameligusia hapa. Kwanza inathibitisha utayari wa Bunge kutaka sheria hii itekelezwe na ndio maana wamekuwa *concerned* na vyanzo vya mapato. Jambo hili nalipongeza sana na limetufaraji sana. Nilithibitishie Bunge lako katika ibara ya 51A-E, tumeorodhesha vyanzo vya mapato na mojawapo ni bajeti ya Serikali kupitia Wizara yetu ambayo itakuja hapa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo niwahakikishie kwamba tuna hakika tume na vyombo vyake vitakwenda sawasawa kwa sababu bajeti itapita hapa, lakini tumeorodhesha vyanzo vile.

Mheshimiwa Spika, tumeweka pia uwezekano wa kuongeza vyanzo kwenye kanuni kwa maana ya kwamba mazingira wakati mwingine huwa yanabadilika. Kwenye sekta yetu ya *TEHAMA* fursa huwa zinaweza kutokea katikati kwa hiyo badala ya kujifunga vyote kwenye sheria tumeweka *room* ya kuwa na vyanzo vingine kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, hapa pengine nigusie hoja ya utungaji wa kanuni. Kwanza nilithibitishie Bunge lako kwamba, Kanuni zitakazotungwa zitazingatia Sheria iliyotungwa kwa sababu haiwezekani kutunga kanuni ambayo haitaheshimu sheria ambayo Wabunge wameipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, la pili, kanuni hizi tutawahusisha wadau ili kuhakikisha zinazingatia yale matakwa na hali halisi ya Sheria ambayo mmeitunga hapa. Wadau hao ni wengi na wanaweza wakawa hata mpaka Wabunge wenyewe. Hata hivyo, tunajua kupitia Kamati ya Sheria Ndogo za Bunge, kuna uwezekano wa kanuni hizi kupitiwa pia. Kwa hiyo ni uhakika kanuni hizi zitakuwa salama. Niwahakikishie kwamba tutatunga kanuni nzuri, zitazingatia Sheria lakini pia tutahakikisha tunawashirikisha wadau na kuhakikisha tumezingatia mazingira yote na kanuni hizi zitakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, tumepokea pongezi nyingi kwa niaba ya Serikali na kwa kweli kwa niaba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, sheria hii imeanza kuchakatwa miaka kama tisa iliyopita na haikuwezekana, lakini kwa usimamizi mzuri wa Rais Samia na Serikali ya Awamu ya Sita, imewezekana na leo tumeandika rekodi nzuri ya kuingiza nchi yetu kwenye nchi zinazo heshimu na kuzingatia ulinzi wa taarifa binafsi. Kwa kweli, niwashukuru Wabunge kwa uamuzi huu wa busara sana na uzalendo mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ukiacha mambo mengine ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025, ibara ya 61B inayosema hivi:

1 NOVEMBA, 2022

“CCM itasimamia Serikali yake kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa kukamilisha kutunga Sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu”.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi tulichokifanya hapa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, nawashukuru kwa kuunga mkono. Vile vile tulichofanya hapa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 ambayo nayo inasisitiza ulinzi wa taarifa binafsi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa na nawashukuru sana, mwelekeo wa duniani leo, mataifa makubwa na uwekezaji mkubwa hawaendi kuwekeza kwenye nchi ambayo haina sheria au mfumo unaolinda taarifa binafsi. Ukienda Ulaya wamekubaliana, kwa hiyo tumeathirika na kuna baadhi ya wawekezaji walishindwa kuja kwa sababu ya kutokuwepo kwa sheria hii. Kuna baadhi ya mikataba na makubaliano tuliyoingia duniani. Mnakubaliana ila wakitaka kuja wanauliza mna sheria ya kulinda taarifa binafsi kama hawana wanakwenda. Tumezidiwa na baadhi ya majirani zetu kwa sababu wenyewe walitangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo leo Bunge lako limefanya uamuzi wa kizalendo wa kuifanya nchi yetu sasa iwavutie wawekezaji hao ambao kwenye nchi zao wana sheria hii. Bila shaka sheria hii itakaposainiwa, tutaona mafuriko ya wawekezaji wakija na hasa kwenye sekta ya TEHAMA ambayo itazalisha ajira nyingi sana. Nchi zinazotuzunguka za SADC na Afrika Mashariki, uwekezaji bila kuwa na sheria hii, unakuwa mgumu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumezingatia mawazo yao, ushauri wao na tutakwenda kuutekeleza kwenye kanuni na utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu kwa hoja zote mbili. Katibu.

NDG.LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 (*The Tanzania Investment Bill, 2022*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

1 NOVEMBA, 2022

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022
(The Tanzania Investment Bill, 2022)**

Jina Refu la Muswada

(Jina Refula Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 1

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 2

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 3

Kifungu cha 4

Kifungu cha 5

Kifungu cha 6

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 7

Kifungu cha 8

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 9

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 10

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

1 NOVEMBA, 2022

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 24

MWENYEKITI: Kuna Mbunge amegonga meza kuashiria ana jambo ama alikuwa anapongeza? Waheshimiwa Wabunge, wakati huu wa Kamati ya Bunge Zima, huwa yanaashiria kwamba una jambo unataka kusema.

Kifungu cha 25

Kifungu cha 26

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

Kifungu cha 29

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31

Kifungu cha 32

Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 35

1 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 36

Kifungu cha 37

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa

T A A R I F A

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 *(The Tanzania Investment Bill 2022)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na Marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022 *(The Tanzania Investment Bill, 2022)* kama ulivyorekebishwa kwenye Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Tanzania wa Mwaka 2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji kwa lengo la kuweka mazingira bora kwa Wawekezaji, kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi,

1 NOVEMBA, 2022

uvutiaji, uhamasishaji na usimamizi wa uwekezaji nchini. Kufuta Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 1997 pamoja na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa Mara ya Tatu)

*(Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania
wa Mwaka 2022) Ulipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada umekwishasomwa kwa mara ya Tatu na kwa maana hiyo kwa upande wa Bunge tumemaliza kazi yetu ya kutunga Sheria, kwa maana ya utungaji wa Sheria ya Uwekezaji wa Tanzania ya mwaka 2022 sasa Bunge limeshaupitisha Rasmi. Kwa utaratibu wetu tutaupeleka kwa Mheshimiwa Rais ili upate kibali chake na hivyo uanze kutumika.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Naibu Waziri wa Uwekezaji wa Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri waliyoifanya siku ya leo ya kuwasilisha hoja hii pia kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kupitia taarifa ya Kamati yetu ambayo imewasilishwa hapa ni dhahiri kwamba Serikali ilitoa ushirikiano wakati wa mjadala wa ngazi ya Kamati. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali kwa ushirikiano huu.

Waheshimiwa Wabunge, ninawapongeza pia Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kazi nzuri waliyoifanya kupitia Muswada huu na hivyo kuliwezesha Bunge kufika sehemu ambayo inaweza kutoa maamuzi. Mheshimiwa Waziri, yako mambo kadhaa ambayo Kamati imetoa mawazo kwenye taarifa yao na Serikali hamjayafanyia kazi kwenye haya marekebisho. Mojawapo ni jambo la kubadili hiki kituo na kuwa Mamlaka iliyokamili. Sasa, kwenye hiyo mamlaka mtaiita Kamisheni au Mamlaka kama zingine zinavyoitwa hilo ni suala linguine, lakini ni suala la msingi sana kwa sababu nimesikiliza hoja upande wa Serikali na nimesikiliza upande wa hoja ya Kamati na upande wa Wabunge namna walivyochangia humu ndani, sijapata picha kama Serikali haitaki kufanya hilo jambo. Kwamba Serikali inaona ina sababu kabisa za msingi na ni hizi hapa sijaziona kwa nini hamtaki isiwe Mamlaka. Kwa michango ya Wabunge iliyotoka humu ndani, tunaamini kwamba pamoja na mambo mengine, kwa sababu Kamati imeonesha mambo mengi ambayo inatamani myafanyie kazi ili hiki kinachoitwa Kituo kitakapopata Mamlaka, basi tuweze kuona mabadilikokatika hili eneo, kwa sababu Wawekezaji wanakimbizwa na sababu nyingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, humu nimesikia sababu mbili kwamba Sheria zetu ziwe ni Sheria ambazo zinadumu kwa kipindi fulani ili mtu awe anajua haibadiliki kesho, yaani mazingira wawe hayabadiliki kila wakati hilo ni

1 NOVEMBA, 2022

mojawapo. Mheshimiwa Waziri umejibu ukaweka na hoja nyingine hapo ambazo ni za Msingi kabisa lakini uhalisia wote tunaufahamu humu ndani, kwamba kituo hiki cha uwekezaji hakifanyi kazi inayopaswa kufanywa ndiyo maana uwekezaji nchini upo chini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu humu ndani Wabunge wamesema na Kamati wamesema ni muhimu kujiridhisha wenzetu wanapokimbilia wawekezaji wanavyo vivutio gani nasi tuviweke viwe wazi. Vitaweza kuwa hivyo, tukitoa fursa kwa hiki kituo chetu kuwa Mamlaka ili kiwe kinafanya maamuzi na siyo sasa katika ngazi hii huku kuna Bodi lakini wakati huo huo tunacho chombo kingine tena cha Kitaifa hapo juu, hiki chombo cha Kitaifa juu kimajaa wanasiasa humo ndani. Nilikuwa napitia orodha, sasa hao wanasiasa kidogo inakuwa ni mtihani wakati mwingine, kwa kupatikana tu siyo kwamba pengine mambo hawajui au hawawezi kufanya maamuzi, bali kuwakusanya kundi lote lile na leo mmemuongoza Waziri wa Mambo ya Nje ni kama mmetengeneza Baraza Dogo la Mawaziri, hiyo kidogo inaleta changamoto. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo tunaamini baada ya kupitisha Sheria hii na kwa sababu mnaendelea kuangalia ile *blueprint* na kuendelea kuleta marekebisho mbalimbali, tunaamini kwa sababu mnaendelea kuyafanyiakazi hayo, basi na haya ambayo Kamati yetu imesema na Wabunge wamependekeza humu ndani, mueendeleo kuyafanyia kazi kama sehemu ambayo tunataka nchi yetu ipige hatua kwenye hili eneo la uwekezaji. Hivyo, tunawatakiwa kila la kheri katika utekelezaji Mheshimiwa Rais atakaposaini Sheria hii na kuwa sasa Sheria kamili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba kwa sababu hatujamaliza bado. Katibu.

NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022
(The Personal Data Protection Bill, 2022)**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

Jina Refu la Muswada.

(Jina Refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 3

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 4

MWENYEKITI: Ukigonga unasimama ili nijue ni upande gani. Mheshimiwa Neema Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufafanuzi wa Serikali kwenye maeneo yafuatayo ambayo naamini kabisa yanalenga sehemu ya malengo ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi kwenye eneo la kwanza ni kwamba ulinzi wa taarifa binafsi unapaswa pia uguse zile taarifa zinazokusanywa na Serikali pamoja na taasisi zake ambazo haziko chini ya Wizara hii. Sasa jambo halijaweka wazi sana hivyo nahitaji ufafanuzi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Pili ni kuhusiana na hizi taarifa nyingi ambazo tunakusanya hapa kwetu huwa zinahifadhiwa nje ya nchi, kwa mfano kupitia *satellite*. Kwa hiyo, Sheria hii haijaweka chini ya malengo ya hii sheria, kwamba itaweka pia njia za kuhakikisha kwamba tunapata access ya hizi taarifa zetu ambazo zimehifadhiwa nje ya nchi kupitia *satellite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Tatu ni ufafanuzi katika eneo la moja ya malengo ya Sheria ni pamoja....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema, hebu ngoja kwanza. Hayo yote unayotiririka yapo kwenye kifungu cha 4?

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ni kwenye malengo ya Sheria.

MWENYEKITI: Sasa, huwa inabidi uwe na jambo moja tu, sasa sijui kati ya hayo yote umechagua lipi? Kwa ngazi hii hoja ni moja tu huwezi kuwa na hoja nyingi kwenye eneo moja.

MHE. NEEMA LUGANGILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hiki cha 4, basi naomba ufafanuzi kuhusiana na namna gani ambavyo Sheria hii

itahakikisha inalinda taarifa binafsi ambazo zinakusanywa na Serikali na Taasisi zake ambazo haziko chini ya Wizara hii.

MWENYEKITI: Sawa, hiki ni kifungu cha 4 ngapi?

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4(b).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kifungu cha 4(b).

WAZIRI YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Neema Lugangira juu ya Taasisi za Serikali ambazo haziko chini ya Wizara ambazo zinakusanya taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu hata katika Sheria tumeeleza kwamba Taasisi zote zikiwemo za Serikali zitasajiliwa na Tume. Tukaenda mbali zaidi tukasema kwa mujibu wa Sheria tuliyoileta hapa ni kwamba, taasisi zote za Serikali, Sheria hii itakaposainiwa zitahesabiwa kwamba zimesajiliwa *automatic* kwa sababu ni katika lengo hilo hilo la kuzilinda taarifa. Kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba, taarifa hii imelenga kila mkusanyaji na mchakataji wa taarifa *regardless* anatoka wapi, ni binafsi au Serikalini. Kwa hiyo, jambo lake analolisema limezingatiwa na Sheria tunayoipendekeza.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 5

Kifungu cha 6

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 7

Kifungu cha 8

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 9

Kifungu cha 10

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

1 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 22

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 23

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 24

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 29

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

1 NOVEMBA, 2022

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 37

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 38

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 41

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 42

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

1 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 56

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Jedwali la Muswada Kifungu cha Pili na cha Nne

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

NDG.EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA HABARI MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za

1 NOVEMBA, 2022

Bunge Toleo la mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Bill, 2022*) ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 (*The Personal Data Protection Bill, 2022*) kama ulivyopitishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe,

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana,

Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji waheshimiwa wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa mwaka 2022.

(Hojia iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO- KATIBU MEZANI.

Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa lengo la kuweka misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazo chakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi pamoja na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa Mara ya Tatu)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muswada umeshasomwa mara ya tatu na kwa hivyo kwa ngazi hii ya kuusoma muswada kwa mara ya tatu maana yake sisi kama bunge tumemaliza sehemu ya kutunga sheria inayohusu ulinzi wa taarifa binafsi na kwa sababu nilikuwa nimeshawahoji maana yake ni kwamba Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022 umepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu sheria hii ilikuwa inasubiriwa kwa muda mrefu

na sasa imefika wakati ambapo Serikali imefanya maamuzi ya kuleta muswada huu kwetu na sisi tumeshafanya kwa sehemu yetu na kama mlivyoona marekebisho mbalimbali ambayo Waziri na wataalamu wake walielewana na Kamati, kwa hiyo wakati nampongeza yeye pia niipongeze sana Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo imeifanya ya kuupitia muswada huu na kuhakikisha unakuwa mzuri zaidi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi za Watanzania, lakini pia na watu wengine ambao taarifa zao zinaweza kujikuta hapa nchini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote kwa kazi nzuri Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu na Wajumbe wote na Wabunge wengine ambao hampo kwenye hii Kamati lakini mlishiriki katika kutoa mawazo yenu pia tunawapongeza sana na tuwatakie kila lakheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yako yote wakati utakapofika Mheshimiwa Rais atakapo saina tunawatakia kila lakheri kwenye utekelezaji wa sheria hii. *(Makofi)*

Hili lingine sasa ni la jumla sasa nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania wote ambao huwa wanajitokeza Bunge linapotoa matangazo ya kwamba wadau wajitokeze ili kutoa mawazo yao kuhusu miswada mbalimbali ambayo huwa inajadiliwa na Bunge, kwa hiyo niwashukuru wadau wote ambao huwa wanajitokeza wakati mwingine tutapata nafasi ya kuwatambua ili wajue tunajua mchango wao katika utungaji wa sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo niwashukuru wadau wote na wananchi wote ambao huwa wanajitokeza wanapoitwa kwa wito wa kuja kutoa mawazo yao mbele ya Kamati. Nawashukuru wote. *(Makofi)*

Nitoe wito kwa wengine pia ambao pengine wakati mwingine hawajitokezi, lakini sasa Sheria ikishatungwa hivi ndo wanakuwa na maneno sehemu fulani kama vile hakupewa fursa, kwa sababu fursa iko wazi kwa hiyo ni vizuri tukawa sote Watanzania tunashirikiana kwenye hili zoezi ili inapofika wakati wa utekelezaji basi wote tunakuwa tumesikilizwa. Kwa hiyo na wao natoa wito ili tuendeleo kushirikiana lakini kwa ujumla wake ninwashukuru wale wote ambao huwa wanajitokeza wanapoitwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katiba yetu inataka hii miswada yote miwili tutaipeleka kwa Mheshimiwa Rais kama nilivyosema kabla ili Mheshimiwa Rais aweze kufanya kwa sehemu yake halafu zitakapokuwa sheria kamili tutawatangazia tutakapokutana tena.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili, la kwanza linahusu Kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, atakuwa ndiye anaye Kaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi

1 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea Dodoma, hilo ni tangazo la kwanza.
(Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili, siku ya jana tulitangaziana ratiba ya shughuli ambazo zitakuwa mbele yetu na ratiba kwa sababu tumeshaiweka kwenye vishikwambi vyenu na ninyi mliipitia tumefanya mabadiliko kidogo, sasa nalazimika kuwatangazia ili muendeleo kujiandaa kwa ajili ya michango ya jambo ambalo litakuwa linafuata hapo mbele.

Kwa ratiba ambayo tumefanya mabadiliko madogo Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa wote utajadiliwa siku ya ijumaa tarehe 11/11/2022 na kwa hiyo, siku ya kesho tutafanya muswada mmoja wa sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, lakini pia tutaanza mjadala wa Kamati.

Tutaanza mjadala wa Taarifa za Kamati zile tatu ambazo niliwatangazia jana, kwa hiyo tutaanza kesho badala ya kesho kutwa, nadhani tumeelewana, kwa hiyo mjiandae ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.32 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,
Tarehe 2 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*